# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

### Kikao cha Kumi na Nane – Tarehe 5 Mei, 2017

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae, Katibu.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MHE. JUMA S. NKAMIA (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka 2016/2017, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA - NAIBU MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, juu ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Katibu.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na.145

**Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Kuwabagua Wabunge wa Viti Maalum**

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR** aliuliza:-

Majukumu ya Mbunge kwa kuzingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 63(3) yameainisha kwa ujumla wake bila kubagua aina ya Ubunge; lakini Sheria Namba 16 ya mwaka 2009 iliyounda Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo *(CDCF)* imeonesha ubaguzi mkubwa kwa kumtambua Mbunge wa Jimbo pekee ambaye ndiye aliyetajwa na sheria hiyo kama Mwenyekiti wa Kamati ya Usimamizi wa Mfuko huo na kuwatenga Wabunge wa Viti Maalum licha ya kwamba Wabunge wote wanatekeleza majukumu sawa ya kuwatumikia wananchi.

Je, ni lini Serikali itarekebisha sheria hii ili ijumuishe Wabunge wote ikiwemo Wabunge wa Viti Maalum?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa

Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo ulianzishwa mwaka 2009 kwa Sheria Namba 16 ya mwaka 2009 iliyotungwa na Bunge. Fedha za Mfuko wa Jimbo hutolewa katika Majimbo yote ya uchaguzi Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kwa kuzingatia vigezo maalum vilivyopitishwa kisheria. Vigezo vinavyotumika kugawa fedha za Mfuko wa Jimbo ni idadi ya watu asilimia 45, mgao sawa *(pro-rata)* kila Jimbo asilimia 25, kiwango cha umaskini asilimia 20 na ukubwa wa eneo asilimia 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za Mfuko wa Jimbo huingizwa moja kwa moja katika *account* ya Halmashauri na zinasimamiwa kwa taratibu za Sheria ya Fedha isipokuwa Mbunge wa Jimbo ni Mwenyekiti wa Mfuko huo. Kimsingi sheria haina ubaguzi kwa Waheshimiwa Wabunge wa Viti Maalum kwa sababu fedha hizo za Serikali zinatumika kutekeleza miradi ya kipaumbele iliyoibuliwa na wananchi wenyewe kwenye Jimbo husika kwa kuzingatia mahitaji ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na malengo yaliyounda Sheria ya Mfuko wa Jimbo na vigezo vinavyotumika katika kupeleka fedha za Mfuko wa Jimbo, Serikali inaona sheria hiyo inajitosheleza kwa sasa kwa kuzingatia misingi ya uundwaji wake, labda Bunge ambalo ndilo lenye mamlaka ya kutunga sheria litakavyoamua vinginevyo.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu hayo ambayo hayajaniridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba sheria hii haina ubaguzi lakini mimi nasema ina ubaguzi. Kwa sababu iweje sheria ipingane na Katiba? Katiba imetutambua Wabunge wa Viti Maalum na

Wabunge wa Majimbo sote ni sawa, tuna haki sawa, tunafanya kazi sawa za kuiletea maendeleo nchi yetu hii iweje leo useme haina ubaguzi?

Je, ni lini sheria hii italetwa hapa Bungeni ili tuirekebishe tupate haki sawa sote, Wabunge wa Majimbo na Wabunge wa Viti Maalum, kwa sababu sote tunafanya kazi sawa?

Pili, kwa kuwa Wabunge wa Viti Maalum tunafanya kazi zaidi kwa sababu sisi tuna-*handle* mikoa, lakini Wabunge wa majimbo wanakuwa na majimbo. Jimbo liko ndani ya mkoa, Wabunge wa Viti Maalum tuko kwenye mkoa mzima tunafanya kazi za maendeleo, lakini tunatumia hela zetu za mfukoni tukipata posho, tukipata mshahara, ndiyo tunatumia Serikali haituhurumii?

Je, ni kitu gani chenye kigezo muafaka ambacho amekisema Naibu Waziri kati ya Jimbo na Mkoa upi wenye kigezo ambacho kinakubalika watu wengi, sijui Mkoa ni mkubwa kama alivyosema kuliko Jimbo...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Faida.

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR**: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anipe kigezo, bado hajaniambia kigezo.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri swali la msingi tunafanya kazi sahihi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nimesema kwa sababu sijasema mimi kama Jafo, nimesema kwa mujibu wa sheria. Bahati nzuri mnafahamu ndugu zangu kwamba sheria hii ilitungwa humu Bungeni na sheria hii ilipata msuguano mkubwa sana, ndiyo maana ukija kuangalia ni kwamba sheria hii hata suala la vile vigezo vilivyotengwa ndiyo maana inaitwa Sheria ya Mfuko wa Jimbo. Kwa hiyo, kama itaonekana kwamba nini kifanyike hayo sasa ni mawazo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu lazima tufahamu kuna Wabunge wa Majimbo, kuna Wabunge wa Viti Maalum kutoka Mikoa, kuna Wabunge wengine wanateuliwa na Rais maana yake wanazungumza karibu Tanzania nzima. Kwa hiyo, kama tukitaka tufanye tafakari hiyo na kutakuwa na Wabunge wengine ambao wao wanahudumu Tanzania nzima ndiyo maana nimesema Bunge hili ndiyo lenye dhamana ya kutunga sheria ikionekana jambo hilo linahitajika lifanyike, Bunge litafanya maamuzi sahihi. Tufahamu vilevile hata mkoa hauwakilishwi na Mbunge mmoja. Inawezekana mikoa mingine ina Wabunge wa Viti Maalum saba. Ndiyo maana nimesema jambo hili linatakiwa ifanyike *needs assessment* kwa ujumla wake kupata maamuzi kama Taifa. *(Makofi)*

**MWEYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa...

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS,TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Dada yangu Faida Bakar kuna sehemu ya pili alisema Wabunge wanatumia fedha zao. Naomba niwaambie hasa na Wabunge wa Majimbo, fedha za Mfuko wa Jimbo siyo fedha za kwenda kugawa kama zawadi. Fedha za Mfuko wa Jimbo zinapita katika akaunti maalum na zina Wajumbe maalum akiwepo Afisa Mipango ni Katibu wa Mfuko wa Jimbo, fedha ile inaingia mara moja kwa mwaka na Kamati inafanya maamuzi kutekeleza miradi, fedha ile siyo fedha ya kuingia mfukoni kwa mtu kwenda kutoa sadaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, niwatahadharishe Wabunge wa Majimbo kwamba mfahamu fedha hii inakwenda kujibu matatizo ya wananchi. Mlivyopita kuna mahitaji mbalimbali wananchi wameibua sasa katika vikao vyenu mnafanya maamuzi kwenda kujibu matatizo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri inatosha, ahsante. Waheshimiwa Wabunge, swali hili ni zito. Mheshimiwa Chenge, Mheshimiwa Ally Keissy, Mheshimiwa Mahawe, Mheshimiwa Paresso halafu tunaendelea.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chenge.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii, lakini pia niishukuru sana majibu ya Serikali kwa swali hilo, swali langu la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mgao wa mwisho wa fedha hizi za kuchochea maendeleo ya jimbo, baadhi ya majimbo nchini hapa likiwemo na Jimbo la Bariadi mgao wake wa kisheria ambao umetajwa na Mheshimiwa Waziri katika majibu yake, mgao wake haukuzingatiwa. Majimbo hayo likiwepo na la Bariadi walipewa fedha pungufu kinyume na vigezo hivyo. *(Makofi)*

Je, Serikali iko tayari kusahihisha dosari hiyo? Ahsante

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi. Swali lake mrekebishe hii kitu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wangu mwenye dhamana alitoa maelezo hapa katika nyakati mbalimbali suala zima baadhi ya majimbo fedha kuwa pungufu zaidi na hasa katika Mkoa wa Mwanza. Ninafahamu kwamba Mkoa wa Mwanza ulikuwa umeathirika kwa kiwango kikubwa sana lakini mgao ule kipindi kile ulitokea kwa sababu bajeti yetu ilikuwa inalenga bajeti ya majimbo ya mwanzo, kwa hiyo, majimbo mengine yalivyoongezeka kutoka Majimbo 189 mpaka 220 ikasababisha zile fedha zikawa na mgao mdogo, hata hivyo kulikuwa na makosa ya kimahesabu ambayo ofisi yetu ilitoa maelekezo kwa ma-*RAS* kwamba zile fedha ambazo baaadhi ya majimbo yaliongezewa zirudi kwa ma-*RAS* wa mikoa, lengo kubwa ni kufanya usahihisho kwa bajeti ile ya mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti yetu ambayo tumeipitisha juzi hapa mwaka 2017/2018 ninaamini

tumeshafanya marekebisho makubwa na Majimbo yote tarajieni katika bajeti ya mwaka huu unaokuja, imefanya mazingatio ya ongezeko la Majimbo mapya haya ambayo mimi nina imani hatutakuwa na shida tena huko tunakokwenda.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy, wajiandae Mheshimiwa Mahawe na Mheshimiwa Paresso.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza Mbunge aliyeuliza swali kwamba Wabunge wanatumia zile pesa, namshukuru sana Naibu Waziri alivyoeleza kuhusu zile pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa Wabunge hawashiki, pesa zinakwenda kwa Mkurugenzi, Mwenyekiti yeye ni Mwenyekiti tu. Kuna Afisa Mipango, kuna Madiwani wawili, kuna watendaji wawili ndipo utagawa zile pesa, hatugusi hata senti tano moja sisi kuweka kwenye mafuta.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu Mfuko wa Jimbo nimezungumza tangu mara ya kwanza una matatizo. Kuna majimbo mengine na tujimbo twingine.

**MBUNGE FULANI:** Ufutwe sasa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Huu mfuko hauwezi kufutwa kwa sababu kuna Wabunge wengine kama Viti Maalum, mzee wangu anasema Majimbo, Majimbo mengine yana watu 30, watu 40, mengine kata 10 Jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kama nilivyosema mara ya kwanza usimamishwe, wafanye tathmini upya, wagawe upya kutokana na idadi ya watu na ukubwa wa majimbo. Haiwezekani kuna majimbo mengine ni madogo wanapewa sawa na Jimbo kubwa haiwezekani. Ifanywe tathmini upya ili hela ziende kwa usawa bila ubaguzi wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majimbo ambayo hayana

vigezo, hayastahili kuapata mfuko wa Jimbo mkubwa, haiwezekani. Jimbo lako la Ilala kubwa lipate sawa na Jimbo...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuende na takwimu sahihi, haiwezekani.

Swali, Wabunge Viti Maalum hawaruhusiwi kupata Mfuko wa Jimbo na wasitegemee kuzipata, kwa sababu Mbunge wa Jimbo ndiyo anastahili kupata ule Mfuko wa Jimbo na ikiwezekana Wabunge wale wengine wachunguzwe walikotoka. Haiwezekani wewe uliyekuja kuzungumza hapa wakati ulikotoka wewe hauna hata wa...*(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi sana, Mheshimiwa Simbachawene.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Keissy ameuliza maswali ya nyongeza pia ametoa maelezo ya nyongeza. Hata hivyo katika maelezo yake kuna vitu vya msingi amevisema.

Kwanza ambacho ndicho nitakachokijibu vingine nitaviacha kwa sababu kwa mujibu wa Kanuni natakiwa kujibu swali moja. Ni kweli kwamba kuna vigezo vinavyotumika katika kugawa fedha hizi, vigezo hivi vimesemwa katika jibu la msingi. Kigezo cha kwanza ni idadi ya watu ambayo ni asilimia 45. Mgao sawa kwa kila Jimbo asilimia 25, kiwango cha umaskini asilimia 20, ukubwa wa eneo asilimia 10. Fedha yoyote itakayotengwa kwenye bajeti hapa itaingizwa katika hii *formula.*

Kwa hiyo, bahati mbaya sana kwa mwaka huu wa fedha, fedha iliyotengwa ilikua kidogo kwa sababu Hazina hawakutambua majimbo haya mapya, hatukuwa na mawasiliano mazuri. Nataka niwahakikishie kwamba kigezo

hiki sasa kwa mwaka huu wa fedha tumesahihisha hayo makosa yote na sasa majimbo yote yanahesabika, yaliyoongezeka na kosa hilo halitafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba kuna baadhi ya Majimbo yanapewa fedha kidogo kwa mujibu wa *formula* hii, hilo haliwezekani isipokuwa fedha zimeshuka tu kwa sababu zilikuwa kidogo na tulilazimika kuziingiza kwenye *formula* hii kama zilivyo, ndiyo maana ni tofauti na iliyotolewa nyuma na iliyotolewa sasa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya majibu haya, bado mnataka mjadala? Mheshimiwa Mahawe.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naitwa Mmasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu nimkumbushe Kaka yangu Jafo. Kaka yangu Mheshimiwa Naibu Waziri tulipokuja hapa Bungeni mimi na wewe tulikula kiapo kimoja, tofauti yetu ilikuwa kwenye majina. Mimi nilitamka Ester Michael Mmasi na wewe ukatamka jina lako kadri ilivyo kwenye kumbukumbu za Bunge hili. Mheshimiwa Naibu Waziri kwenye maslahi ya Kibunge hususani katika *payroll* ya Bunge sote tuna maslahi sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu hapa yametoka kwamba hawa wenzetu kupitia Mfuko wa Jimbo wanafanya kazi za wananchi, sisi ni akina nani na tunafanya kazi za nani? Hatufanyi kazi za familia zetu, tunafanya kazi za wananchi hawa hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia nchi ya Kenya, mathalani Wabunge...

**MWENYEKITI:** Uliza swali Mheshimiwa Mmasi.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Wabunge wa Kenya hili linafanyika. Nenda

tukaangalie Wabunge wa Kenya *(Woman MP's)* kwenye *county level* wana-*Capital Development Funds for women MP's,* kwa nini Tanzania ishindikane?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri majibu.

Sasa Mheshimiwa Waziri itabidi hebu kaa kwanza, kwa sababu nimeshaona hii kitu utasimama, utakaa acha tutumie utaratibu tofauti, Mheshimiwa Paresso. *(Kicheko)*

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Ubaguzi huu wa Wabunge kati ya Wabunge wa Viti Maalum na Wabunge wa Majimbo pamoja na kutokupewa Mifuko ya Jimbo, lakini pia hatuingii katika Kamati za Fedha kwenye Halmashauri zetu na jambo hili tumeshalisema muda mrefu, kwa nini Serikali inakuwa na kigugumizi kuruhusu Wabunge wa Viti Maalum katika Halmashauri tulizowapa tusiingie katika Kamati ya Fedha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge wa Viti Maalum ni hofu tu, tutawang'oa Majimboni. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ningependa nimuulize Mheshimiwa Waziri swali lifuatalo:-

Kwa kuwa fedha za Mfuko wa Jimbo pale ambapo zinaingizwa kwenye akaunti kwa upande wa Tanzania Bara, kwa upande wa Zanzibar zinachukua karibu miezi minne mpaka mitano kutokana na mlolongo mrefu ambapo fedha hizi zinaingizwa katika akaunti zetu za Majimbo ndani ya Wabunge wa Visiwa vya Unguja na Pemba.

Ningependa kumuuliza Mheshimiwa Waziri, je, ni sababu zipi za msingi zinazopelekea fedha zinapoingia katika

akaunti za Majimbo ya Tanznaia Bara zinachukua miezi sita kwa upande wa Tanzania Zanzibar. Je, nini kifanyike ili fedha hizi ziweze kufika kwa wakati kama ambavyo zinavyoingia upande huu? Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Munde. Jamani natumia Kanuni ya Tano kuendesha shughuli hii ya swali hili.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuuliza swali.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba pesa zile za Jimbo huwa zinakwenda kutumika kwa wananchi; na kwa kuwa Wabunge wa Viti Maalum wanafanya kazi na wananchi hao hao; na kwa kuwa tumelisema suala hili kuanzia mwaka 2011 mpaka leo hii na Serikali bado ina kigugumizi, bado inaona ugumu kuwapa pesa Wabunge wa Viti Maalum, huenda bajeti ya Serikali haiko vizuri.

Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari sasa kwa nia njema kabisa ya kusaidia Wabunge hawa wa Viti Maalum, walau kila Mbunge wa Jimbo husika kwa mfano kwangu mimi nina Majimbo 11, kila Mbunge wa Jimbo husika walau akakatwa asilimia 10 ya Mfuko wa Jimbo ikakaa kwa Mkurugenzi, *amount* ya pesa zile wakagaiwa Wabunge wa Majimbo siyo kugaiwa *cash*, zikakaa kwa Mkurugenzi labla mimi nikawa na milioni nne tu, nikaenda eneo fulani nikakuta hamna *gloves* nikawaambia zile milioni nne Mkurugenzi m-*deposit* kwa ajili ya kina mama? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, umeshaeleweka, Mheshimiwa Waziri sasa jibu.

Waheshimiwa Wabunge, swali hili limechukua dakika 20, tunaweza tukaamua tukaenda nalo hili moja tu leo. Mheshimiwa Waziri. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima

kubwa naomba kujibu swali ambalo nadhani litakuwa swali maarufu la mwaka na limeulizwa kwa staili ambayo haijawahi kufanyika, ninakupongeza Mwenyekiti kwa utaalamu wa kujua Kanuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali hili linahusu Mfuko wa Jimbo na Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Ester Mmasi, Mheshimiwa Munde Abdallah na wengine wengi Wabunge wa Viti Maalum wanataka na wao wapate mgao wa fedha za Mfuko wa Jimbo. Swali hili siyo kwamba linaulizwa kwa mara ya mwanzo leo, limekuwa likiulizwa na mara nyingi tumekuwa tukitoa majawabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu maarufu ambayo tumeyatoa kwamba tutakwenda kushughulikia tuone utaratibu wake, lakini kila tunaposhughulikia tunapata ugumu kwa sababu mfuko huu umezaliwa kwa mujibu wa sheria, sheria yenyewe inaitekeleza Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mfuko wenyewe unaitwa Mfuko wa Jimbo na kwa hiyo, kuupa jina linguine lolote lile ni kazi ngumu kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, humu ndani kuna Wabunge wa Majimbo, kuna Wabunge wa Viti Maalum, kuna Wabunge wa Mikoa, kuna Wabunge wanaoteuliwa na Mheshimiwa Rais. Bunge hili likitambua kwamba Wabunge wa aina hizi zote wapo, lilitunga Sheria ya Mfuko wa Jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwenye *instrument* yangu kwa mujibu wa sheria nilizopewa kuzisimamia nina sheria inayosema nitasimamia Mfuko wa Jimbo, haisemi vinginevyo. Ndiyo maana kwenye jibu letu la msingi nimesema kama Bunge litaona vinginevyo suala hilo linakuja kwa utaratibu mwingine, lakini kwa sasa mimi ninasimamia Mfuko wa Jimbo.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa Mheshimiwa Mwenyekiti.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wale

Wabunge waliokuwa wanadai sana mfuko huu, waliokuwa wa Viti Maalum, walipopata majimbo na wenyewe msimamo wao umebadilika, ni kwa sababu ya majukumu anayoyapata Mbunge wa Jimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali mengine yameulizwa na Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim ambaye ameuliza suala la fedha kuchelewa Zanzibar, hili tumelichukua, tunawasiliana na Ofisi ya Makamu wa Rais tuone utaratibu bora zaidi wa kuweza kufanya fedha hizo ziwafikie Wabunge wa Zanzibar, hasa tunatambua yapo mapendekezo ya kwamba bora zikapita katika Ofisi ya Bunge Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine dogo limeulizwa na Mheshimiwa Paresso kwamba Wabunge wa Viti Maalum hawaingii kwenye Kamati za Fedha. Kamati za Fedha zinatambua uwepo wa Madiwani na Mbunge unapoingia kwenye Halmashauri huwi Mbunge unakuwa Diwani, kule kwenye Kamati ya Fedha wanaoteuliwa kuingia kwenye Kamati ya Fedha huwa ni Madiwani. Sasa nadhani ni utaratibu wa Halmashauri zenu, kama wewe Mbunge kuteuliwa kuna baadhi ya Wabunge ambao wanaingia kwenye Kamati ya Fedha, lakini kule wameingia kwa tiketi ya Udiwani wao kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napata shida hapa kwa sababu la kwanza, kwamba kwa Majimbo ambayo yana Wabunge wengi wa Viti Maalum, na mfahamu kikao kile kina utaratibu wa gharama zake na mambo mengine. Ingawa gharama siyo hoja kubwa, lakini kwa Jimbo ambalo lina Wabunge wa Viti Maalum nane, 10, sijui hali itakuwaje kwa sababu gharama za uendeshaji wa Halmashauri zitakuwa kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ingelikuwa Wabunge labda ni mmoja au wawili pengine unaweza kuichukulia hili jambo likawezekana, lakini kwa hali ilivyo kuna tatizo kubwa sana na ninadhani ni vema hili jambo likabaki kama ilivyo na ndio utaratibu ulivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa tiketi ya Udiwani, Mbunge anaweza akateuliwa na Mwenyekiti kwa utaratibu ule akawa Mjumbe wa Kamati ya Fedha.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, baada ya muda huu tulioutumia vizuri sana na majibu na hoja, muendelee ku-*dialogue* ili kutazama kama mtafikia muafaka upi. Sasa sitaruhusu maswali ya nyongeza tena, muda wetu umekwenda.

Tunaendelea swali namba 146 Mheshimiwa Ahmed Salum kwa niaba yake Mheshimiwa Maige.

Na.146

**Serikali Kukamilisha Ujenzi wa Majengo ya Jimbo la Solwa**

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE (K.n.y MHE. AHMED A. SALUM)** aliuliza:-

Majengo mengi yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi katika Jimbo la Solwa kama vile vyumba vya madarasa, nyumba za walimu na zahanati yako katika hatua za mwisho kukamilika.

Je, kwa nini Serikali isione umuhimu wa kukamilisha majengo hayo ili yaweze kutoa huduma?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mbunge wa Solwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Solwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga wamejenga kwa nguvu zao vyumba vya madarasa 37,

nyumba za walimu 33 na zahanati 38 ambazo zipo katika hatua mbalimbali.

Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri imetenga jumla ya shilingi milioni 695.3 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa majengo yaliyoanza kwa nguvu za wananchi katika sekta ya elimu na afya. Hadi sasa Halmashauri imeshapokea shilingi 420,881,000 ambazo zimepelekwa katika ukamilishaji wa miundombiinu ya elimu na afya.

Vilevile Serikali imeongeza fedha za ruzuku ya maendeleo kutoka shilingi bilioni 1.2 zilizotengwa katika Halmashauri hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 hadi shilingi bilioni 1.7 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 sawa na ongezeko la asilimia 42 kwa ajili ya kutekeleza miradi kwa kuzingatia vipaumbele vya wananchi. Kulingana na muongozo wa asilimia 50 ya fedha hizo zinatakiwa kutumika katika miradi ngazi ya Halmashauri na asilimia 50 zinatakiwa kutekeleza miradi hiyo katika ngazi ya vijiji.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Pamoja na majibu hayo mazuri naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kwa wananchi wa Jimbo la Solwa, wananchi wa Jimbo la Msalala nao wameitikia vizuri sana wito wa Serikali kushiriki katika shughuli za maendeleo kwa kuchangia, hivi tunavyozungumza wameshakamilisha maboma 40 ya zahanati, maboma manne ya vituo vya afya na maboma zaidi ya 70 ya nyumba za walimu na vyumba vya madarasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maboma haya ni ya muda mrefu, fedha ambazo zimekuwa zikiletwa mara nyingi zinatosha asilimia 10 hadi 20 ya maboma haya. Nilitaka kujua kwa nini Serikali isiwe na mpango maalum wa kufanya tathmini ya maboma yote na kuleta fedha zinazoendana na maboma ambayo yamekwisha kukamilika ili yaweze kukamilishwa badala ya kuachwa yaanguke?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, moja ya tatizo kubwa ambalo Halmashauri zinapata ni ukosefu wa fedha hasa kutoka vyanzo vya ndani, Halmashauri nyingi za mikoani zimekuwa zikipata shida kupata ushuru wa huduma kutoka kwenye makampuni ya simu. Kwa mfano, Kampuni ya *Airtel* inalipa zaidi ya shilingi bilioni tano kwenye Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, wakati minara yake imetapakaa nchi nzima. Kwa nini Serikali isizisaidie Halmashauri kule ambako minara ipo, ushuru wa huduma ukalipwa kule ili Halmashauri ziweze kupata fedha za nyongeza kutekeleza miradi kama hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri jana, Mheshimiwa Chenge Kiti kilitoa maagizo *issue* hii iende kwenye bajeti. Kwa hiyo, jibu sahihi bila kuchukua muda mwingi lipokeeni, mnalifanyia kazi na Kamati ya Bajeti na Serikali inalifanyia kazi. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivyosema tunapokea, lakini nilitaka nimshukuru Mheshimiwa Maige kwa sababu kwao kule wamejenga maboma mengi sana lakini kwa kushirikiana na ile Kampuni ya Madini, wameendelea kujenga vituo vya afya. Hata hivyo, kipindi kirefu fedha zilikuwa haziji sasa kuanzia mwaka huu Wizara yetu imesimamia upatikanaji wa fedha na ndio maana mkiangalia kuna maboma mengi sana tunaanza kurekebisha. Bajeti ya mwaka huu tena kama mnakumbuka wakati tunapitisha bajeti hapa tumetenga fedha nyingine kuhakikisha kwamba maboma mbalimbali tunaweza kuyakamilisha katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwahakikishie kwamba katika mwaka wa fedha unaokuja kutakuwa na mabadiliko makubwa sana katika umaliziaji wa maboma haya, kwa sababu yote haya tumeshayafanya tathmini Wizara ya TAMISEMI.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Mwantum Dau, Wizara hiyo hiyo.

Na. 147

**Mabasi yaendayo Kasi**

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kuhusu huduma ya mabasi yaendayo kasi pale umeme unapokatika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakala wa mabasi yaendayo haraka umejipanga vizuri kwa kuweka jenereta moja katika kila kituo kikubwa, ambalo hutumika kama chanzo cha umeme pale umeme wa *TANESCO* unapokatika. Vituo vikuu vilivyowekewa jenereta ni vya Kimara, Ubungo, Morocco, Kivukoni, Gerezani na katika karakana iliyopo Jangwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia kupitia *DART* imeweka betri za kutunza umeme *(backup batteries)* katika vituo vyote vidogo 27 ili zitumike kama chanzo cha umeme, pale umeme wa *TANESCO* unapokatika.

**MHE. MWANTUMU D. HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri aliyoyajibu na naona yametosheleza hasa na wananchi huko watasikia jinsi walivyojipanga. Nina swali langu moja dogo tu la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itakamilisha mradi huu na kuondoa msongamano wa daladala ambazo nyingine ni za kizamani kabisa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mheshimiwa Mwantumu Dau, kwa sababu yeye ni Mjumbe wa Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambao wamekuwa wakifanya kazi kubwa sana mpaka kuanza kwa mradi huu.

Naomba niwahakikishie wakazi wa Dar es Salaam kwamba mradi huu awamu ya kwanza umekamilika na sasa tunajiandaa katika mradi wa awamu ya pili kuanzia Mbagala na mradi wa awamu ya tatu kuanzia Gongo la Mboto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmesikia Mheshimiwa Rais wakati anazindua *fly over* za Ubungo pale, kwamba fedha zimeshapatikana na muda wowote sasa kazi hii inaweza ikaanza. Lengo kubwa ni kuondoa foleni kabisa na kuondoa haya magari madogo katika Jiji la Dar es Salaam na Serikali kuwahudumia wananchi na kukuza uchumi wake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Haonga.

Na. 148

**Hitaji la Chuo cha Kilimo Wilaya ya Mbozi**

**MHE. PASCAL Y. HAONGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanzisha Chuo cha Kilimo Wilaya ya Mbozi ili kutoa fursa kwa wanafunzi wengi wanaohitimu kidato cha nne na cha sita Mkoa wa Songwe na maeneo mengine nchini ili waweze kupata mafunzo kwenye chuo hicho?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa

Kilimo, Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pascal Yohana Haonga, Mbunge wa Mbozi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo kwa Chuo cha Kilimo katika Wilaya, Mkoa na Taifa ni muhimu kwa kuwa kinasaidia kujenga nguvukazi wataalam na wakulima kifikra na kimtizamo katika kuongeza uzalishaji na tija katika nyanja ya kilimo kwenye eneo husika. Hivyo chuo cha kilimo kikianzishwa katika Wilaya ya Mbozi kinaweza kuchochea maendeleo ya uzalishaji na usindikaji wa mazao yanayozalishwa Wilayani hapo ikiwemo kahawa, mahindi, maharage na matunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kuanzisha chuo cha kilimo kuna gharama kubwa kwa ajili ya kujenga miundombinu, kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kuajiri rasilimaliwatu kwa ajili ya kazi za mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wakati huu vipo vyuo vitatu vya Serikali Mkoani Mbeya vinavyotoa mafunzo ngazi ya Stashahada na Astashahada. Vyuo hivi ni Uyole, Igurusi na Inyala vyenye uwezo wa kuwa na wanafunzi takribani 700 kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo *(ASDP II)* Wizara itaboresha Vyuo vya Kilimo vya Uyole, Igurusi, Inyala pamoja na vyuo vingine kwa kujenga miundombinu, kuongeza upatikanaji wa vifaa, kuongeza rasilimali watu na kadhalika ili viweze kudahili wanafunzi wengi zaidi wakiwepo wanaotoka Wilaya ya Mbozi.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa mpango wa Serikali kwa sasa ni kuelekea Tanzania ya viwanda na hakuna viwanda ambavyo tunaweza kuvipata bila kuboresha kilimo. Hii ni sawa na kwamba unapanda mchicha unategemea kuchuma machungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa pia hauwezi kuboresha kilimo bila kuwekeza kwenye vyuo vya kilimo. Je, Serikali ipo tayari kuboresha kituo cha mafunzo ya wakulima ambacho kipo kijiji cha Mbozi, kata ya Igamba, Jimbo la Mbozi ili kiwe chuo kamili, kwa maana tayari kituo hiki kipo na wakulima walishaanza kupata mafunzo pale tangu mwaka 2012?

Swali la pili, kwa kuwa vyuo vingi vya kilimo nchini kikiwepo Chuo cha Kilimo cha Uyole, vipo katika hali mbaya sana, Serikali imevitelekeza, miundombinu ni mibovu, havina wataalamu. Je, Serikali ipo tayari sasa kuboresha vyuo vyote vya kilimo nchini ili sasa tuweze kwenda na hii suala la nchi ya viwanda?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye majibu ya swali la msingi, Serikali ina nia ya kuendelea kuboresha vyuo vyetu vya kilimo, kuboresha kule ni zaidi tu ya kuviongeza idadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini kwamba tukiweza kuimarisha na kuboresha huduma zinazotolewa na vyuo vilivyopo sasa sio lazima kuongeza vyuo vingine. Kwa sasa nchini kwetu tuna vyuo 14 vya kilimo katika kanda sita za kilimo. Sasa tunachofanya ni kuendelea kuziboresha ili ziweze kutoa huduma nzuri zaidi badala ya kuelekea kujenga utiriri wa vyuo ambavyo havina *quality* nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge nimuelekeze tu kwamba kituo anachozungumzia wakati huko mbele tunaweza kufikiria kufanya chuo kamili lakini kwa sasa vyuo vitatu ambavyo vipo mkoa jirani wa Mbeya tutaendelea kuviimarisha na kuviboresha ili viweze kutoa huduma kwa watu wa Mbozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, jibu hilo pia linatumika kwa vyuo vyote nchini, kama nilivyoeleza

kwenye jibu la msingi. Serikali sasa inaanza kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Mifugo awamu ya pili ya *ASDP II,* moja kati ya matarajio katika kutekeleza mpango huu ni kuendelea kuboresha vyuo vyetu vya kilimo ikiwa ni pamoja na kuongeza kukarabati majengo, kuajiri rasilimali watu ya kutosha ili viweze kudahili wanafunzi wengi na kutoa elimu ya kilimo ambayo ni bora.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu.

Na.149

**Malipo ya Waliokuwa Watumishi wa Mashamba NAFCO**

**MHE. DKT. MARY M. NAGU** aliuliza:-

Watumishi wa yaliyokuwa mashamba ya *NAFCO* walishinda kesi yao ya madai dhidi ya Serikali na Mahakama kuiamuru Serikali kuwalipa mafao na madai yote lakini Serikali imeendelea kukaa kimya kwa muda mrefu na hivyo kuwanyima haki yao jambo ambalo linasababisha adha kubwa kwa familia zao.

Je, ni lini Serikali itawalipa haki yao waliokuwa watumishi wa mashamba ya *NAFCO* ikiwemo shamba la Murjanda?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu, Mbunge wa Hanang, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashamba ya kilimo yaliyokuwa chini ya Shirika la Taifa la Kilimo na Chakula *(NAFCO)* yaliajiri watumishi 314 kwa nyakati tofauti na kazi tofauti ambapo *NAFCO* kupitia makampuni hayo iliingia

mikataba ya hali bora na watumishi hao kwa lengo la kuboresha maisha yao. Utekelezaji wa mikataba hiyo ulitegemea ufanisi na utendaji wa taasisi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 16 Juni, 1996 *NAFCO* iliwekwa chini ya uangalizi wa *PSRC* kwa ajili kubinafsishwa kulingana na Sheria ya Mashirika ya Umma ya mwaka 1992. Aidha, baada ya zoezi la ubinafsishaji wa mashamba ya *NAFCO*, watumishi hao waliachishwa kazi kati ya mwaka 2003 na 2004 ambapo walilipwa malimbikizo ya mishahara yao na mafao mengine, bila kulipwa mafao yanayotokana na mikataba ya hali bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa baada ya kutolipwa madai yatokanayo mikataba ya hali bora, watumishi hao chini ya Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Mashambani Makao Makuu, walifungua kesi ya mdai Mahakama Kuu tarehe 5 Juni, 2004 dhidi ya *PSRC* na kushinda kesi hiyo ambayo ilichukua miaka minne mpaka mwaka 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi hao walistahili kulipwa mafao ya mikataba ya hali bora kama ifutavyo:-

Mishahara miwili baada ya notisi, magunia matatu ya ngano kwa kila mwaka waliofanyia kazi au fedha badala yake kwa bei ya wakati huo ilipofungwa mikataba, mwisho walipwe misharaha ya miezi minne kila mmoja kwa kila mwaka waliofanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ukweli kwamba madai haya yamepitia vyombo mbalimbali vya usimamizi wa Serikali, hata hivyo, kumekuwepo na madai yasiyo sahihi baada ya uhakiki wa kurudia.

Hivyo, napenda nichukue nafasi hii kuwataka wawasilishe madai hayo ofisi ya Msajili wa Hazina ambayo itashirikiana na Wizara ili tuweze kuyachambua na kujiridhisha ipasavyo iwapo wanastahili kulipwa na hivyo kuiomba Wizara ya Fedha na Mipango kuchukua hatua stahiki.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waingereza wanasema *justice delayed is justice denied,* na kwa vile imechukua muda. Je, Msajili wa Hazina, Hazina na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi watakuwa tayari sasa kukamilisha uhakiki huu na kuwalipa hao wanaodai ambao walikuwa wafanyakazi wa *NAFCO?*

Swali dogo la pili, ili tumalize migogoro iliyo kwenye mashamba ya *NAFCO,* je, Serikali iko tayali sasa kurudisha shamba la *Basutu plantantion* kwa wananchi ambao wana upungufu wa ardhi mapema inavyowezekana?

**MWENYEKIT:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba *justice delayed is denied*, vilevile *justice hurried is justice buried.* Kwa hiyo, katika mukhtadha huo tunaendelea na uhakiki ili haki itendeke pande zote, tunatambua kwamba imechelewa lakini haki katika hili ni pamoja na Serikali kuweza kulipa malipo ambayo ni stahiki kwa sababu tukiyaharakisha sana inawezekana hata baadhi ya wafanyakazi wale tukawapunja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jitihada zinaendelea na tunashirikiana na Wizara ya Fedha taratibu zikikamilika wananchi wake wa Hanang ambao anawasimamia vizuri sana watalipawa haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali la pili la *Basutu plantantion* ni kweli kabisa kama anavyosema Mheshimiwa Dkt. Nagu kwamba shamba lile baada ya kuwekewa utaratibu ambao Halmashauri wanakodisha kwa wananchi, tayari kuna malalamiko yametufika kwamba

utaratibu ule haujaweza kufanya lile ambalo lilitegemewa. Kuna malalamiko kwamba kuna wajanja wameingilia vilevile wale walengwa ambao walikuwa ni wananchi wa kawaida, maskini, wakulima wadogo wao inaelekea hawajanufaika katika mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara bado inaendelea kulichunguza suala hili na ikibainika kwamba lile lengo ambalo tulikusudia halifikiwi, Wizara itachukua utaratibu mwingine kuhusiana na shamba la *Basutu plantantion.*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mambo ya Ndani ya nchi Mheshimiwa Halima Ali Mohamed.

Na. 150

**Maafisa Usalama wa Kiume Kuwavua Wanawake Nikabu**

**MHE. HALIMA ALI MOHAMMED** aliuliza:-

Kwa mujibu wa Ibara ya 19(1) ya Katiba ya nchi, kila mtu anayo haki na uhuru wa kuamini dini aitakayo, lakini pia chini ya Ibara ya 15(1) na (2) ya Katiba ni lazima sheria zifuatwe.

Je, ni kwa nini wanawake wa kiislamu wanapovaa hijabu nikabu wanavuliwa na Maafisa Usalama wanaume?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Halima Ali Mohammed, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kweli kuwa wanawake wa kiislaamu wanapovaa hijabu na ama nikabu wanavuliwa na maafisa wanaume wa Jeshi la Polisi. Aidha,

Jeshi la Polisi linafanya kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zinazoliongoza Jeshi hilo na kwa mujibu wa *PGO* 103(1) ambayo inasema malalamiko yote dhidi ya Polisi lazima taarifa itolewe mara moja kwa Mkuu wa eneo na hatua za uchunguzi upelelezi ifanyike kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaombe wananchi hususani wanawake, pindi wanapofanyiwa vitendo kama hivyo, kupeleka malalamiko yao polisi au kwenye mamlaka nyingine husika ili sheria iweze kuchukua mkondo wake.

**MHE. HALIMA ALI MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu ambayo hayaridhishi aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri naomba sasa ni muulize maswali mawili ya nyongeza:

Kwa kuwa, wanawake wanaposafiri na kupitia bandarini kwenda Zanzibar au kutoka Zanzibar kuja Dar es Salaam wanavuliwa nikabu kuanzia katika geti la bandari, na kwa kuwa wanawake hawa wanapata manyanyaso na lugha za kejeli.

Je, ni muulize Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari sasa kupokea ushahidi?

Swali la pili, wapo wanaume wanaovaa mavazi na wakajipamba kujifananisha na wanawake, je, Serikali ina mpango gani wa kuwachukulia hatua wanaume hawa?*(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimezungumza katika jibu langu la msingi kwamba kama kuna matukio yoyote ambayo yameonekana kukiuka sheria za nchi ikiwemo hilo ambalo amelizungumza, kama ushahidi upo aulete tutaufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa nikiri kwamba kuna baadhi ya maeneo kwa mfano, tulifanya ziara katika bandari

ya Zanzibar tuliona utaratibu ambao unatumika katika kuwakagua abiria siyo mzuri na bahati nzuri tulikuwa na Naibu Waziri wa Miundombinu wa Zanzibar, hilo tumelizungumza na Serikali italifanyia kazi karibuni utaratibu ule utabadilika.Hata hivyo binafsi sikushuhudia wala kutokea malalamiko yoyote juu ya yale ambayo ameyazungumza Mheshimiwa Mbunge, lakini kama yapo na ushahidi upo basi tutafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la pili kwamba kuna wanaume wanavaa mavazi ya kike na wanawake wanavaa mavazi ya kiume. Tafsiri ya mavazi ya kiume na ya kike nayo ni tafsiri pana maana suruali ni vazi la kiume sijui tuliite la kike, mwanamke anavaa na mwanaume anavaa. Kwa hiyo, sidhani kama kuna tafsiri sahihi ya kusema hili ni vazi la kiume na ipi ni ya kike ili Serikali iingilie katika uhuru wa wananchi kuamua jinsi gani wanataka kuvaa ni uhuru wao Kikatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona swali lake hili linahitaji kwenda ndani kidogo, limekosa ufafanuzi kwa hiyo linakosa majibu ya wazi ya moja kwa moja. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate.

Na. 151

**Kuweka Kituo cha Uhamiaji katika Mpaka wa Tanzania na Msumbiji**

**MHE. DAIMU I. MPAKATE** aliuliza:-

Katika upande wa kusini mwa Jimbo la Tunduru Kusini wananchi takribani 200 wa Tanzania na Msumbiji huvuka Mto Ruvuma kila siku kutafuta mahitaji yao ya kila siku, upande wa Msumbiji wameweka Askari wa Uhamiaji ambao huwanyanyasa sana Watanzania kwa kuwapiga na kuwanyang'anya mali zao kwa kukosa hati ya kusafiria.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka Kituo cha Uhamiaji katika kijiji cha Makande Kazamoyo na Wenje ili kuwapatia Watanzania huduma ya uhamiaji?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikifanya juhudi za kuhakikisha kuwa inasogeza huduma karibu na wananchi ikiwa ni pamoja na huduma za Uhamiaji. Katika kutekeleza hilo Wilaya zilizo nyingi ikiwemo Tunduru zina Ofisi za Uhamiaji. Aidha, Serikali inatambua umbali mrefu wa takribani kilometa 90 uliopo kutoka vijiji vya Makando, Kazamoyo na Wenje kutoka Mjini Tunduru zilipo ofisi za Uhamiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua hilo na uhitaji wa huduma za uhamiaji katika vijiji hivyo ili kuwawezesha wanakijiji kuingia na kwenda nchini Msumbiji kihalali, tunafanya ufuatiliaji ili kujua gharama za kufungua ofisi za Uhamiaji katika kijiji cha Makando. Kwa kuanzia Ofisi hiyo itahudumia vijiji vya Kazamoyo na Wenje ili kuwawezesha kuvuka mpaka Kihalali. Tunawaomba wananchi na Mheshimiwa Mbunge kuwa na subira kwa kuzingatia kuwa suala hili linahitaji kutengewa fedha katika bajeti.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Serikali imetambua urefu mkubwa uliopo kutoka Ofisi ya Uhamiaji ilipo mpaka Wenje, Makande na Kazamoyo; na kwa kuwa wananchi hawa wa maeneo haya hawana uwezo mkubwa wa kuweza kufuata huduma hii ya uhamiaji zaidi ya kilometa 90 ziliko ofisi; na kwa kuwa Serikali inakosa mapato kutokana na tozo zinazotolewa kwenye hati

hizi ya kusafiria; je, kwa nini Serikali haioni umuhimu kwa sasa wa kuweza kutoa huduma hii kwa njia ya *mobile* ili wananchi hawa waweze kupata huduma hii kwa haraka?

Swali la pili, katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru Ofisi ya Uhamiaji ina gari ambalo kwa muda mrefu ni bovu halina huduma yoyote katika maeno yote yaliyopo. Je, Serikali ni lini itatoa gari kwa ajili ya kurahisisha huduma hii ili wananchi wale wahudumiwe kwa urahisi zaidi?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kukosa mapato Serikali si hoja ya kukosekana kituo karibu na mpaka. Kwa sababu kwa mujibu wa Sheria ya Uhamiji namba 54 pamoja na Kanuni zake mwaka 2015, inaeleza kabisa kwamba ili mtu aweze kuvuka kutoka nchi yetu na kwenda nchi nyingine anahitaji kuwa na nyaraka za aina tatu.

Nyaraka hizo aidha ni *passport* ama hati ya dharula ya kusafiria ama kibali maalum. Kwa hiyo, kwa mwananchi yoyote anahitaji kuvuka lazima apitie katika njia hizo *whether* ofisi ipo katika mpaka, ofisi ipo katika Wilaya ama ofisi iko katika Mkoa, kwa hiyo hiyo naona ni hoja ambayo siyo sahihi, ninaomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kuwasisitiza wananchi wake juu ya umuhimu wa kuweza kutii sheria za nchi yetu ili kuepusha uvukaji wa mipaka kiholela na kuikosesha Serikali mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusiana na gari, hili naomba Mheshimiwa Mbunge atuachie tulichukue, kwa sasa hivi hatuna gari za kutosha kwa Uhamiaji, pale ambapo gari zitapatikana tutaangalia na changamoto zingine za maeneo mengine na vipaumbele vilivyopo ili tuzingatie na kuchukua hatua stahiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Hasunga.

Na. 152

## Kufufua Elimu ya Watu Wazima kwa Vijana chini ya Miaka 40

**MHE. JAPHET N. HASUNGA** aliuliza:-

Kujua kusoma na kuandika ni nguzo muhimu sana katika maendeleo ya demokrasia na kudumisha umoja na amani nchini.

Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua elimu ya watu wazima kwa vijana wote walio chini ya miaka 40?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kujua kusoma na kuandika ni nguzo muhimu sana katika maendeleo ya demokrasia na kudumisha umoja na amani nchini. Takwimu za sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 kwa Tanzania Bara zinaonyesha kuwa watu wenye umri wenye umri wa miaka 15 na kuendelea ambao hawajui kusoma na kuandika ni asilimia 22.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa kujua kusoma na kuandika Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kutekeleza programu mbalimbali za kuwapatia vijana na watu wazima stadi za kujua kusoma, kuandika na kuhesabu.

Programu hizo ni pamoja na mpango wa uwiano kati ya elimu ya watu wazima na jamii (MUKEJA)unaojumuisha programu ya ndiyo ninaweza inayoendeshwa kama tarajali katika Wilaya tisa za majaribio ambazo ni Halmashauri za

Wilaya za Bagamoyo, Mwanga na Mkurunga, pamoja na Manispaa za Ilemela, Dodoma, Songea, Kinondoni, Temeke na Ilala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha elimu ya watu wazima na kuiwezesha jamii kuwa na stadi za KKK, Wizara yangu imeandaa miongozo ya wawezeshaji na vitabu ambavyo vimekwisha sambazwa katika Halmashauri zote nchini. Aidha, kila Mamlaka ya Serikali ya Mitaa imeelekezwa kutenga fedha katika bajeti zake kwa ajili ya kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia, kutoa mafunzo kwa wawezeshaji, kulipa honoraria kwa wawezeshaji, kufanya ufuatilia na kuhamasisha jamii ili watu wazima na vijana wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu wajiunge kwenye madarasa ya kisomo.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwa kuwa takwimu za mwaka 2016 zinaonyesha kwamba Watanzania ambao ni zaidi ya miaka 15 na ambao hawazidi miaka 54 wako takribani milioni 25 na kuendelea; na kwa kuwa asilimia 22.4 ni kubwa sana, maana yake ni kwamba karibu takribani watu 5,813,066 hawajui kusoma na kuandika.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kurudisha sasa vituo vya kufundishia kama ilivyokuwa zamani katika kila kijiji, kwa sababu tatizo hili ni kubwa sana na hasa katika Jimbo la Vwawa na maeneo mengine nchini?

Swali la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri umesema kwamba mmeziagiza Halimashauri kutenga fedha ili wahakikishe kwamba huo mfumo wa KKK unatekelezwa.

Je, mmeweka mkakati gani wa kuhakikisha kwamba kutakuwa na uwajibikaji na ufuatiliaji wa utekelezaji wa agizo hili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Hasunga kwa kuridhika na majibu yetu ya awali, pia kwa majibu yanayofuata ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi ni kwamba kila mahali kwenye taasisi ya elimu, iwe ni shule ya msingi, iwe ni sekondari, iwe ni chuo ni kituo halali cha watu wasiojua kusoma na kuandika kuweza kupata elimu au mahali pa kujifunza.

Vilevile Wizara baada ya kutembea na kuona kwamba eneo hilo bado lina uhitaji mkubwa, tumeshaweka mikakati ya kuona kwamba elimu ya watu wazima inapewa kipaumbele na kuona kwamba wananchi wetu wa Tanzania tupungue ikiwezekana angalau tufikie asilimia tano mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na ufuatiliaji katika Halmashauri ili kuhakikisha kwamba wanatimiza wajibu wao, niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa sisi sote ni Madiwani kwenye Halmashauri zetu, basi tuone umuhimu wa kutenga fedha kwa ajili ya shughuli hiyo ya kuhakikisha wenzetu wote wanajua kusoma, kuandika na kuhesabu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea tumesema hatuna maswali ya nyongeza kutokana na muda, tumetumia swali moja kwa nusu saa. Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Zainab Mussa Bakar.

Na. 153

**_Plate Number_ za Tanzania Bara Kutotumika Zanzibar**

**MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR** aliuliza:-

Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Je, ni kwa nini *plate number* za vyombo vya moto ambazo ni za Tanzania Bara hazitumiki au haziruhusiwi Zanzibar, na ni kosa ambalo linatozwa faini ya shilingi 300,000?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zainab Mussa Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Usalama Barabarani ambayo husimamia usajili wa vyombo vya moto siyo sheria ya Muungano. Kwa upande wa Tanzania Bara usajili wa vyombo vya moto unasimiwa na Sheria ya *The Road Traffic Act* ya mwaka 1973 na Kanuni ziitwazo *The Traffic Foreign Vehicles Rule* za mwaka 1973. Kwa upande wa Tanzania Bara sheria hizi zinasimamiwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na kwa upande wa Tanzania Zanzibar usajili wa vyombo vya moto unasimamiwa na Sheria *ya The Road Transport Act* namba 7 ya mwaka 2003. Majukumu ya usajili wa vyombo vya moto Zanzibar husimamiwa na Bodi ya Mapato Zanzibar tangu mwaka 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Usajili wa Vyombo vya Moto Tanzania Zanzibar *(The Road Transport Act No. 7)* ya mwaka 2003, chini ya kifungu cha 43, magari yasiyosajiliwa Zanzibar hutumika Zanzibar bila kufanyiwa usajili upya wa siku 90 pale ambapo magari hayo yanakibali cha kukaa na kutumika Zanzibar. Hata hivyo, baada ya kupita muda wa siku 90, mmiliki wa magari hayo hutakiwa kuomba kusajili magari yao kwa namba za Tanzania Zanzibar au kuomba muda zaidi wa kutumika Zanzibar bila usajili wa Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya kifungu cha 201 cha *The Road Transport Act* Namba 7 ya mwaka 2003, mmiliki wa chombo cha moto akishindwa kusajili chombo cha moto baada ya siku 90 na kushindwa kuomba kuongezewa muda

wa kutumia gari bila usajili, anakuwa amefanya kosa na faini yake ni dola za kimarekani 50 au shilingi zenye thamani ya dola hizi, na siyo shilingi 300,000.

**MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa mtu husajili namba kwa mujibu wa mahitaji yake na mahali alipo akiwa ni Tanzania Bara au Tanzania Zanzibar. Je, haiwezekani usajili huo kwa kuzingatia sayansi na teknolojia kuratibiwa pamoja?

Swali la pili, je, ni kitu gani kinachozuia mtu anayesajili namba zake Zanzibar kuweza kutumia namba hizo hizo akiwa Tanzania Bara kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi sheria hii siyo sheria ya Muungano na ndicho kitu kinachozuia namba za Tanzania Bara kutumika Tanzania Zanzibar na Tanzania Zanzibar kutumika Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili tumeliona kama Serikali na Kamati kikao cha pamoja kinachoshughulikia kero za Muungano kimeliona na kikao cha mwisho kimefanyika tarehe 13 Januari, 2017 chini ya Uenyekiti wa Makamu wa Rais na kimetoa maelekezo kushughulikia kero zote za Muungano ikiwa ni pamoja na hii ya usajili wa magari. Hivyo, kwa Serikali yetu tumeliona na tunaona kwa sababu tumepewa maelekezo Mawaziri wa pande zote mbili, Waziri wa Fedha wa Zanzibar, Waziri wa Fedha wa Tanzania pamoja na Waziri wa Mambo ya Ndani, tutakaa pamoja kuhakikisha kero hii inaondoka, lakini kwa mujibu wa sheria itakapokuwa tayari sheria hii italetwa ndani ya Bunge lako Tukufu ili kama Bunge lako litaridhia, tuweze kubadilisha utaratibu huo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Nswanzugwanko kwa niaba yake Mheshimiwa Zitto Kabwe.

Na. 154

**Utafiti wa Mafuta na Gesi – Mwambao wa Ziwa Tanganyika**

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO (K.n.y MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO)** aliuliza:-

Hivi sasa yapata miaka 11 utafiti wa mafuta na gesi katika mwambao wa Ziwa Tanganyika kwenye maeneo ya Kigoma, Rukwa na Katavi umefanyika au unaendelea kufanyika.

(a) Je, ni nini hali ya utafiti huo?

(b) Bonde la Mto Malagarasi nalo limefanyiwa utafiti wa mafuta na gesi; je, hali ya utafiti huo ikoje?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Nicodem Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mjini, lililoulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge wa Kigoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni ya *Beach Petroleum* ya nchini Australia ilianza kufanya utafiti wa mafuta na gesi Kusini mwa Ziwa Tanzanyika tangu mwaka, 2010. Kampuni hiyo ilifanya utafiti na kukusanya *data* ambazo kimsingi ziliwezesha kupatikana taarifa za uchunguzi pamoja na utafiti. Kampuni hiyo imeshindwa kuanza kuchimba gesi kwa sababu zifuatazo:-

Kwanza kabisa ni kwa sababu ya kupanda kwa gharama za uwekezaji, lakini pia kupanda na kushuka kwa bei za mafuta duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 10 Oktoba, 2016, Serikali za Tanzania na DRC ziliingia makubaliano ya *(MoU)*

ya kufanya utafiti wa mafuta na gesi pamoja katika Ziwa Tanganyika. Maeneo makubwa ambayo yamekubalika kufanyiwa kazi ni pamoja na kutathmini kwa pamoja *data* za kijiolojia pamoja na kijiofizikia ili kutambua ukubwa wa mashapo ambayo yatavuka mpaka, vilevile kuandaa jinsi zitakavyofanya kazi kwa ushirikiano. Nchi za Burundi na Zambia nazo zimeomba kuingizwa katika makubaliano hayo ili kufanya utafiti katika ziwa lote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya *Motherland Industries* ya nchini India iliingia ubia na Serikali kupitia *TPDC* kufanya utafiti wa mafuta na gesi asilia katika eneo la Bonde la Mto Malagarasi mwaka 2012. Kufuatia kushuka kwa bei ya mafuta duniani tangu wakati huo, kampuni imeshindwa kukamilisha majukumu yake ya kazi kama ilivyokubalika kwenye mkataba wa *Production Sharing Agreement*, kutokana na hatua hiyo, Serikali inakusudia sasa kurudisha eneo hilo kwa ajili ya utangazaji na wawekezaji wengine wapya.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2011 Serikali iliingia mkataba au ilikubaliana na Kampuni ya *Total* ya Ufaransa kwa ajili ya utafutaji wa mafuta katika *Lake Tanganyika North Block* baadae mazungumzo yakafa, mwaka 2014 Kampuni nyingine ya *Ras Al Khaimah* nayo pia ikawa imepewa zabuni ya utafutaji wa mafuta wa kitalu cha Kaskazini cha *Lake Tanganyika,* lakini mpaka sasa na kwenye majibu ya Mheshimiwa Waziri hakuna maelezo yoyote kuhusiana na hilo, kuna maelezo ya *block* ya Kusini peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2015 *TPDC* ilifanya *survey* katika eneo lote la ziwa na katika majibu ya Waziri hakuna matokeo yoyote ya utafiti kama jinsi ambavyo Mheshimiwa Nsanzugwanko alikuwa anataka kupatiwa taarifa.

Swali la kwanza, Serikali inaeleza nini *status* ya sasa hivi ya utafutaji wa mafuta katika eneo la Kaskazini mwa Ziwa Tanganyika ambapo Waziri hujalitolea maelezo kabisa?

Swali la pili, nini *status* ya umeme wa maporomoko ya Mto Malagarasi ambao ni tegemeo kubwa sana la uzalishaji wa umeme katika Mkoa wa Kigoma? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Zitto, nakumbuka tangu wakati wa uwekezaji katika Mto Malagarasi, wakati wa uwekezaji na ufadhili wa *MCC* alikuwa mbele sana kufuatilia umeme wa Kigoma, kwa hiyo nakupongeza sana kwa niaba ya wananchi wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana wananchi pia na Wabunge wa Kigoma wote Mheshimiwa Serukamba Mheshimiwa Nsanzugwanko kwa mshikamano wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijielekeze kwenye maswali mawili ya Mheshimiwa Zitto, *status* ya utafiti ikoje katika Ziwa Tanganyika. Kwanza kabisa pamoja na maswali ambayo yameulizwa na Mheshimiwa Zitto, kama alivyosema mwaka 2011 kampuni ya *Total* ilianza kufanya utafiti, lakini kulingana na gharama za uwekezaji ilishindwa na haikuendelea. Hata hivyo, taarifa zake zilitusaidia sana katika utafiti unaoendelea kwa sababu katika taarifa ambazo tulizipata, kampuni kwa kushirikiana na *TPDC* waliweza kuchora ramani za urefu wa kilometa 20,024 chini ya Ziwa Tanganyika ambazo zinatupa taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili walitathmini taarifa za utafiti za *Total* za miaka 80 iliyofanyiwa utafiti na makampuni ya nyuma, kwa hiyo, Kampuni ya *Total* iliacha lakini ilituachia taarifa Mheshimiwa Zitto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo *status* ikoje, ni kwamba baada ya utafiti huo *TPDC* mwaka 2014/2015 ilifanya *geo-survey* katika maeneo ya Ziwa Tanganyika na kwa kweli pesa kubwa sana zilitumika shilingi bilioni 6.96 kwa ajili ya utafiti huo na matokeo yake kwa kweli matarajio ya kupata mafuta katika Ziwa Tanganyika yapo. Hiyo ndiyo status Mheshimiwa Zitto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na mradi wa Malagarasi ni kati ya miradi muhimu sana katika ukanda wa Ziwa Tanganyika, maeneo ya Kigoma na maeneo ya jirani kwa sababu kwa sasa Mheshimiwa Zitto tumekamilisha upembuzi yakinifu na tumeshaanza majadiliano na wawekezaji pamoja na wafadhili wetu, tumepata fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika na mradi ule utagharimu dola milioni 149.5. Kwa hiyo, shughuli zitaanza mwezi wa saba mwakani na zitakamilika mwaka 2019/2020. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yetu yamekwisha sasa ni kipindi cha wageni.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe Mbunge, Waziri wa Habari Utamaduni, Sanaa na Michezo, wakiongozwa na Profesa Elisante Ole Gabriel - Katibu Mkuu, Ndugu Nuru Millao - Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Hassan Abbas - Mkurugenzi Idara ya Habari, Maelezo na Msemaji Mkuu wa Serikali, Dkt. Ayub Rioba - Mkurugenzi Mkuu Shirika la Utangazaji TBC. Pia wameambatana na Wenyeviti wa Bodi, Wakurugenzi Wakuu wa Taasisi, Idara, Vitengo na Maafisa mbalimbali kutoka katika Wizara hiyo. *(Makofi)*

Wageni wangine ni wasanii, wadau wa sanaa, wanahabari, utamaduni na wadau wa michezo. Pamoja na ujumbe kutoka *TFF* ambao wako hapa na Kitwana Manara *legend* wa mpira Tanzania yuko hapa. Maana ukizungumzia mpira Tanzania unamzunguzia Kitwana Manara, karibu sana, ulikosea tu kwenda huku. *(Makofi/ Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni mbalimbali Waheshimiwa Wabunge pamoja na wanafunzi waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. *(Makofi)*

Tuna mgeni maarufu Askofu Stephen Ngurumi Sanguda ambae anatoka Kanisa la *Tanzania Missionary Revival Church* na huyu ni mgeni wa Mheshimiwa Mbunge Kanyasu Constantine. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo dogo, mnatangaziwa kuwa Jumamosi tarehe 6 Mei, 2017, kwenye uwanja wa Jamhuri hapa Dodoma kutakuwa na mchezo wa kirafiki kati wa mpira wa miguu *(football)*, mpira wa pete *(netball)* pamoja na mpira wa kikapu *(basketball)* kati ya timu yetu ya *Bunge Sport Club* na Benki ya *NMB*. Mgeni rasmi katika michezo hiyo atakuwa Job Ndugai, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote mnaombwa kuhudhuria, na Mheshimiwa Ngeleja, Spika akiwa mgeni rasmi lazima mshinde. *(Makofi/Kicheko)*

Leo ni siku muhimu sana kwa Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina ni siku yake ya kuzaliwa, ana miaka 42, kwa hiyo hongera sana. *(Makofi)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**MWENYEKTI:** Kuna miongozo leo, Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba mwongozo wako kwa jambo ambalo limetokea mapema leo Bungeni wakati swali la kwanza lilivyokuwa linapatiwa majibu kuhusu Mfuko wa Jimbo, pamoja na maswali mengi ambayo Waheshimiwa Wabunge waliuliza, lakini kuna tatizo la Mfuko wa Jimbo kupunguzwa katika Majimbo yetu bila Wabunge kujulishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakurugenzi walivyokwenda kwenye bajeti, bajeti ambazo tumerudishiwa katika Halmashauri zetu, mimi nina kabrasha ambalo ni la Baraza la Madiwani jana Kamati ya Fedha imekaa Bajeti ya Mfuko wa Jimbo la Babati Mjini ilikuwa ni shilingi milioni 54, sasa ni shilingi milioni 39, inavyoonekana Serikali imepunguza hela za Mfuko wa Jimbo kwa Majimbo yote bila Wabunge kujua.

Naomba mwongozo wako ni kwa nini Serikali isituambie waziwazi Waheshimiwe Wabunge katika Majimbo

yetu, kwamba fedha hizi sasa zimepunguzwa na tujue, nasi tujipange kulingana na kiasi hicho ambacho kimepangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na utaratibu fedha zinaletwa halafu wanasema tuzirudishe Hazina, naomba mwongozo wako kwa nini Serikali isituambie waziwazi badala ya kutuchanganya na kuona fedha hizi zinapunguzwa badala ya kuongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wangu ni huo.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba mwongozo wako kwa mujibu wa ku-*top up* alichosema Mheshimiwa Gekul, kwamba Mfuko huu wa Jimbo tangu ulipoanzishwa fedha zile ambazo zilitamkwa wakati huo, ndiyo hizo hizo. Fedha ilishashuka thamani, lakini ni fedha hiyo hiyo imepita miaka nenda rudi.

**MWENYEKTI:** Mheshimiwa hebu kaa, mbona unadandia dandia tu miongozo. Tuendelee na Mheshimiwa Mchengerwa. *(Kicheko)*

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kuliona hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nakuomba uniruhusu nitoe pole kwa wananchi wangu wa Mkoa wa Pwani hususan Wilaya ya Mkuranga, Kibiti pamoja na Rufiji, kipekee kwa wananchi wa Rufiji kwa tukio la mauaji ya jana na kwa Mwenyekiti wetu wa *UWT* ambaye mumewe jana alipigwa risasi na majambazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira yangu ni kutoa pole tu kwa wananchi wangu na watambue kwamba ninawapigania sana. Kwa sababu wakati mwingine ninaponyamaza wanaona kabisa kwamba labda Mbunge wetu hatusaidii lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Kanuni ya 68(7), pia ninatambua jambo hili halijatokea muda huu ndani ya Bunge

lakini niombe huruma yako kwa kupitia Kanuni 5; ninatambua unayo mamlaka ya kuridhia ili nizungumze jambo hili, kwa sababu mijadala ya bajeti inaendelea na hili ni jambo jema kabisa kwa Waheshimiwa Wabunge ili waweze kutambua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mijadala ya bajeti inajadiliwa kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(b) ambayo Wabunge tunapata fursa ya kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa Bajeti. Pia wakati wa mijadala wakati wa kushika shilingi tunasimama kwa kupitia Kanuni ya 103(1) na zile Kanuni ambazo zinafuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba mwongozo wako ili niweze kufahamu, Mbunge anaposimama na akidhamiria kushika shilingi au mshahara zipo Kanuni ndogo ndogo ambazo zinafuata pale. Ukisoma Kanuni ya103(1) inazungumzia ufafanuzi wa jambo, Kanuni ndogo ya pili inazungumzia kutoa hoja shilingi; Kanuni ndogo ya tatu ni kutoridhika na hoja, na Kanuni ya nne inazungumzia utoaji wa dakika tano wakati wa kujadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kusimama kuomba kushika mshahara wa Waziri, tunatumia Kanuni ya 103, lakini huwezi kama Mbunge kuanza kuzizungumzia Kanuni ndogo zote zinazofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisimama hapa, nikashika mshahara lakini pia nikatumia Kanuni hii 103 bila kutaja Kanuni ndogo zinazofuata, nikiwa na maana kwamba hoja yangu kama haitajibiwa kwa ufasaha nipewe fursa kunyanyuka na kuweza kuipambanua vizuri ili Mheshimiwa Waziri aweze kunipatia majibu fasaha na kama atashindwa niendelee kushika shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati natoa hoja yangu katika mjadala wa Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi, Waziri hakunijibu inavyopaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hotuba ya

Mheshiwa Waziri kwa mujibu wa ukurasa 225 ilikiuka Ibara ya 2(2) na pia ilikiuka kifungu cha nne cha Sheria ya Uanzishaji wa Mikoa; Sura ya 367.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishwaji wa Mikoa na Wilaya ni Mamlaka ya Rais kama nilivyosema katika Ibara ya 2(2), lakini hotuba ya Mheshimiwa Waziri ilionyesha kabisa moja ya barabara ambayo ilipaswa kuwa katika Wilaya yangu imeondolewa na kupelekea katika Wilaya nyingine. Ukisoma ukurasa wa 225 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, tatizo lile limerejea zaidi ya mara mbili, ikimaanisha kwamba Wizara ilifanya makusudi kabisa kwenye hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine tunatoka katika Majimbo ambayo ni magumu yana matatizo makubwa, tunaposimama kwenye Bunge kuomba taarifa tunapaswa tujibiwe ipasavyo, sasa unapoona umejibiwa katika hoja ambayo ni ya msingi na haujapewa fursa ya kujieleza tunapata matatizo makubwa. Yapo maeneo yetu ambayo yana shida nyingi, tunasimama hapa kwa ajili ya wananchi, wakati mwingine hatuhitaji mzaha, tunataka tujibiwe kwa ufasaha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba nipatiwe mwongozo kutokana na hili, Waziri aniandikie kabisa kuthibitisha kwamba alifanya makosa kwenye jambo hili na siyo kuzungumza kwa maneno, kwa sababu taarifa ya Wizara imeandikwa kwa maandishi. Pia Mheshimiwa Waziri anielezee kuhusiana na barabara hii ambayo imeondolewa katika Wilaya yangu na ni Sera ya Serikali ina mpango gani, barabara yangu ya Nyamwage – Utete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaanza na wewe Mheshimiwa Mchengerwa kwanza pole kwa maafa yaliyokupata kwenye Jimbo lako, lakini Bunge linatambua namna unavyohangaikia wananchi wako.

Kuhusu mwongozo wako *rulling* yangu, kwanza umetumia kanuni ile 103 ambayo wala siyo mshahara wa Waziri ni Kanuni ambayo inataka kutaka vielelezo. Kanuni ya 101 ambayo ni mshahara wa Waziri ina masharti yake, ni lazima uulize swali la kisera, sasa vifungu vinavyofuata chini kama swali lako au hoja yako hai-*complement* sera, hoja yako inakuwa ni *redundant,* inakufa kabisa sababu haiendani na Kanuni.

Mheshimiwa Mbunge, kama ulivyosema kwa mujibu wa Kanuni ya tano huwezi ukamzuia Mbunge kuwa na hoja ya msingi ya Jimbo lake ukambana na Kanuni. Tukitumia Kanuni tu humu ndani yapo mambo inabidi Kanuni tuzisimamie, kuna mambo ya kibinadamu na kijamii lazima Kiti kiwe na *sense of compassionate. (Makofi)*

Kwa hiyo, *rulling* yangu namuagiza Waziri aliyehusika akae na wewe na mlijadili hili jambo na mlimalize kwa manufaa ya wananchi wako na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Pauline Gekul, hii ndiyo taabu ya kuingia Bungeni kwa kuchelewa. Swali la Mfuko wa Jimbo halikuwa swali la msingi kuhusu mapato ya Jimbo kupungua, swali la msingi ilikuwa ni ubaguzi kati ya Wabunge wa Viti Maalum na Wabunge wa Majimbo. Hivyo, huna mwongozo, kaa chini. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba tu kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge namna Bunge linavyoendeshwa, Kiti kikikaa hapa kuanzia Mheshimiwa Spika mpaka na sisi wengine hatuendeshi Bunge kwa maagizo ya familia zetu. Tunaendesha Bunge kwa Kanuni na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Waheshimiwa Wabunge, katika mijadala yetu yamejitokeza mambo mengi sana hapa kuwa uhuru ndani ya Bunge hakuna na wengi mna- *quote* Ibara ya 100 ya Katiba ambayo inasema, kutakuwa na uhuru wa mawazo majadiliano na utaratibu katika Bunge na uhuru huo hautavunjwa wala kuhojiwa na chombo chochote katika

Jamhuri ya Muungano au katika Mahakama au mahali pengine, nje ya Bunge. Pia Katiba hiyo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 89 utaratibu wa shughuli za Bunge, bila kuathiri masharti ya Katiba hii Bunge laweza kutunga Kanuni za kudumu kwa ajili ya kuweka utaratibu wa kutekeleza shughuli zake.

Waheshimiwa Wabunge, Erskine May ni mtaalam wa masuala ya Mabunge, nachukua muda kidogo niwaelimishe maana sitaki leo hapa malumbano yoyote humu ndani. Kadi ninazo mimi, filimbi ninayo mimi, *uniform* ninayo mimi, maana ninyi mmevaa nguo za kawaida.

*"The ancient and undoubted risk and privileges of Parliaments are claimed by the Speaker at the beginning of each new Parliament..."* Ndiyo hizi. *"The privileges are only codified in Erskine's May Parliamentary Practice and the House itself is the only judge of its own privileges. The House itself is the only judge of its own privileges."* Ndiyo tumetunga hizi Kanuni.

Nitatoa mfano mdogo, Mahakama ya Uganda imelizuia Bunge la Uganda kuunda Tume au Kamati kuchunguza bilioni sita zilizotolewa na *Tullow Oil against Heritage*. *Tullow Oil* walitoa *six billions* kama honoraria kwa watendaji wa Serikali ambao walisaidia *Tullow Oil* kupata hii, kwa hiyo Mahakama imekataza, sitakwenda mbali sana kwa sababu ni Mahakama.

Kwa hiyo, nataka kutoa mfano Bunge limesimamishwa na Mahakama kujadili au kuzungumzia suala hilo. Kwa hiyo, na sisi vilevile masharti yetu ambayo tunayo kwenye Kanuni zetu *issue* yoyote ambayo iko Mahakamani hairuhusiwi kuzungumziwa.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimeipitia taarifa ya Serikali, natoa tahadhari kwa Serikali, natoa tahadhari kwa Kamati ya Bunge ya Habari, natoa tahadhari kwa Kambi ya

Upinzani, yeyote atakayezungumza mambo ambayo Kanuni zetu zimekataza Kiti kitafanya kazi yake. Iwe Serikali, iwe Kamati, iwe Upinzani.

**MBUNGE FULANI:** Toa mfano.

**MWENYEKITI:** Subiri Sheikh*, the best is yet to come*. Sasa nimezipitia Kamati zote, taarifa zote, natoa *ruling* ya mazungumzo haya niliyoyasema *in advance* hatutaki kupoteza muda, muda wetu wa kukaa Bungeni ni mdogo, muda wa kufanya kazi za wananchi ni mwingi. Uamuzi wa Kiti kuondoa maneno kwenye Hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Kanuni ya 64(1)(c) inasema;

"Mbunge hatazungumzia jambo lolote ambalo lilijadiliwa na kutolewa maamuzi kwenye Mkutano uliopo au uliotangulia au ambao halikuletwa rasmi kwa njia ya hoja mahsusi na vilevile halitapinga uamuzi wowote uliofanywa na Bunge. Isipokuwa tu kwa kutoa hoja mahsusi inayopendekezwa kuwa uamuzi huo uangaliwe upya."

Katika Mkutano wa Saba, Msemaji wa Upinzani kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Katiba na Sheria, hotuba ilijitokeza malalamiko na ilionekana wazi kwamba hotuba hiyo ilisheheni maneno ya kuudhi dhidi ya Rais wa nchi. Maneno ambayo yanapeleka upotoshaji kwa umma *(wrong signal),* Kiti kiliamua maneno haya yote yaondolewe na yasiwe sehemu ya hotuba.

Baada ya kupitia hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ni wazi kuwa imerudia maneno yenye mwelekeo huo. Kanuni ya 61(1)(c) kwa ujumla wake inakataza kuzungumzia jambo lolote ambalo lilishatolewa uamuzi Bungeni. Hivyo basi, naagiza sehemu ya hotuba hiyo kwenye ukurasa wa 6 mpaka wa 10 na ukurasa wa 35 mpaka wa 47 ziondolewe kama nilivyosema hapo juu, kwa kuwa na maneno yenye maudhi hayo yaliyokwisha kutolewa uamuzi na Kiti kama nilivyoeleza hapo juu.

Kama kuna Mbunge yeyote wa Kambi yeyote anayeona maamuzi ya Kiti haridhiki nayo hutakiwi kupiga kelele wala kulalamika, nenda kwenye Kanuni ya 5(4)inakupa fursa kukilalamikia Kiti, tutakutana kwenye Kamati, kila mtu atakuja na Kanuni zake atasema. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Katibu.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwakawa Fedha 2017/2018 – Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo kwenye Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, sasa naomba kutoa hoja ya kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniteua kuisimamia Wizara hii yenye wajibu wa kuratibu na kuendeleza sekta ya habari, kudumisha na kuendeleza utamaduni, mila na desturi za Mtanzania, kuimarisha tija na kulinda kazi za sanaa na kuendeleza michezo katika Taifa letu. Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Rais utendaji bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Kaskazini kwa ushirikiano ambao

inaendelea kutoa kwa Wizara yangu. Kamati hii ilijadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka 2017/2018 tarehe 30 Machi, 2017 na kuyapitisha kwa kauli moja. Wizara yangu itazingatia ushauri uliotolewa na Kamati katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kuwapongeza Wabunge waliochaguliwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuliwakilisha Taifa letu katika Bunge la Afrika Mashariki, Mbunge mpya wa Viti Maalumu, Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Rwakatare na Wabunge wengine watano walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambao ni Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Alhaji Abdallah Majurah Bulembo, Mheshimiwa Profesa Palamagamba Mwaluko Kabudi, Mheshimiwa Juma Ali Juma na Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu mkubwa, naomba niwashukuru wananchi Jimbo la Kyela kwa upendo, imani na ushirikiano wanaonipa ambao umeniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya Ubunge kwa tija na ufanisi. Kupitia Bunge lako Tukufu, naomba niwahakikishie wananchi wa Kyela kuwa tutaendelea kushirikiana katika kuhakikisha Jimbo linapiga hatua kubwa za maendeleo. Aidha, naishukuru familia yangu hasa mke wangu Malkia wa Nguvu Linah kwa kunivumilia na kunitia moyo, nichape kazi pamoja na changamoto ya afya aliyonayo. Nimelelewa kumshukuru Mungu kwa kila jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yanayoonekana katika Wizara yangu yametokana na ushirikiano mkubwa na wa dhati ninaoupata kutoka kwa viongozi wenzangu na watumishi wote wa Wizara. Nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Anastazia James Wambura - Naibu Waziri, Profesa Elisante Ole Gabriel - Katibu Mkuu na Bi. Nuru Mrisho Millao - Naibu Katibu Mkuu kwa msaada mkubwa

wanaonipatia katika uongozi wa Wizara. Aidha, nawashukuru Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wakuu wa Vitengo, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, wataalamu na watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwa kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2016/2017, Bunge lako Tukufu lilipatwa na simanzi kubwa kwa kuondokewa na Mheshimiwa Samuel John Sitta aliyekuwa Spika Mstaafu wa Bunge la Tisa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Taifa liliondokewa na Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Dimani na Mheshimiwa Dkt. Elly Marko Macha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nchi yetu ilikumbwa na majanga mbalimbali na maafa yaliyosababisha vifo, majeruhi, uharibifu na upotevu wa mali ikiwa ni pamoja na tetemeko la ardhi lililotokea Mkoani Kagera. Naomba nitumie fursa hii kuwapa pole familia, ndugu, jamaa, marafiki na watanzania kwa ujumla kwa matukio hayo ya kusikitisha na kutia huzuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maandalizi ya hotuba hii, Wizara imezingatia maudhui ya hotuba ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka 2016/2017 na mwelekeo wa kazi za Serikali kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yangu imegawanyika katika sehemu saba, sehemu ya kwanza inahusu utangulizi, sehemu ya pili inazungumzia dira, dhima na majukumu ya Wizara, sehemu ya tatu ni mapitio ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa kipindi cha mwaka 2016/2017, na sehemu ya nne ni Mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, sehemu ya tano ni makadirio ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na sehemu ya sita ni maombi ya fedha kwa ajili ya kutekeleza mpango wa mwaka 2017/2018, sehemu ya saba ni shukrani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda naomba hotuba yangu nzima ambayo iko kwenye kitabu na inapatikana katika tovuti ya Wizara *www.habari.go.tz* iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dira, dhima na majukumu ya Wizara, ukurasa wa tano wa kitabu ambacho ninaamini mmeanza kugawiwa. Dira ya Wizara ni kuwa na Taifa linalohabarishwa vizuri, lililoshamirika kiutamaduni, lenye kazi bora za sanaa na lenye umahiri mkubwa katika michezo ifikapo mwaka 2025. Dhima ya Wizara ni kuendeleza utambulisho wa Taifa kwa kuwezesha upatikanaji stahiki wa habari, kukuza utamaduni, sanaa na michezo kwa lengo la kuleta maendeleo ya jamii kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa sera, sheria na mipango mbalimbali ya Serikali katika sekta za habari, utamaduni, sanaa na michezo, kuratibu na kusimamia shughuli za vyombo vya habari nchini pamoja na kuendeleza sekta ya utamaduni, sanaa na michezo. Aidha, Wizara inasimamia utekelezaji wa majukumu ya taasisi mbalimbali ambazo ziko chini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi hizo ni Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)*, Kampuni ya Magazeti ya Serikali *(TSN)*, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza *(TFB),* Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo *(TaSUBa)* na Baraza la Michezo la Taifa (BMT). Wizara pia inasimamia Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kupitia Idara ya Maendeleo ya Michezo. Aidha, Wizara inasimamia Kamati ya Maudhui

ambayo kimuundo ipo ndani ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa majukumu kwa kipindi cha mwaka 2016/2017. Mapato na matumizi ya Wizara ukurasa wa sita; kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ilipanga kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 820,005,000 kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato. Na kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2016 hadi Machi, 2017 ilipanga kukusanya jumla ya shilingi 627,505,000. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 jumla ya shilingi 455,305,309 zilikusanywa ambazo ni sawa na asilimia 56 ya lengo la makusanyo ya mwaka na asilimia 73 ya lengo la robo tatu yaani Julai, 2016 hadi Machi, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchanganuo wa makusanyo upo kwenye Kiambatisho namba moja ukurasa wa 66 hadi ukurasa wa 69.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2016/2017, taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ujumla wake zilipanga kukusanya shilingi 51,778,894,447 na kwa robo ya tatu zilipanga kukusanya shilingi 34,415,650,935. Kufikia Machi, 2017 shilingi 16,676,505,417 zilikuwa zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 33 ya lengo la mwaka na asilimia 49 ya lengo la robo ya tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara ilitengewa bajeti ya matumizi ya kawaida ya shilingi 17,326,176,000. Kati ya fedha hizo shilingi 13,437,270,000 ni mishahara ya Wizara na taasisi, ambapo shilingi 3,605,477,000 ni mishahara ya Wizara na shilingi 9,831,793,000 ni mishahara ya taasisi. Aidha, matumizi mengine ni shilingi 3,888,906,000 ambapo shilingi 3,380,323,000 ni za Wizara na shilingi 508,583,000 ni za taasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwezi Aprili, 2017 jumla ya shilingi 11,793,835,177 za matumizi ya kawaida zilipokelewa, ambazo ni sawa na asilimia 68 ya bajeti ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo matumizi mengineyo ni shilingi bilioni mbili, milioni mia moja arobaini na sita, mia tano arobaini na nne elfu, mia sita hamsini na mbili (Sh. 2,146,544,652) na mishahara ni shilingi bilioni tisa, milioni mia Sita arobaini na saba, mia mbili tisini elfu, mia tano ishirini na tano (Sh. 9,647,290,525).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Maendeleo, ukurasa wa nane. Kwa upande wa fedha za maendeleo, mwaka 2016/2017, Wizara ilitengewa shilingi bilioni tatu (Sh. 3,000,000,000) kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo iliyobainishwa katika aya ya 17 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Aprili, 2017 Wizara ilipokea shilingi bilioni moja, milioni mia moja tisini, mia tatu ishirini na nne elfu (Sh.1,190,324,000), sawa na asilimia 40 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika - Shilingi 30,324,000. Pili, ukarabati wa Chuo cha Sanaa Bagamoyo, shilingi 100,000,000. Tatu, eneo changamani la michezo la Taifa sh. 60,000,000 na nne, upanuzi wa usikivu wa *TBC* shilingi. 1,000,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka 2016/2017; Sekta ya Habari na Utangazaji ukurasa wa 9 hadi ukurasa wa 20. Katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Wizara iliendelea kusimamia kikamilifu Sekta ya Habari na Utangazaji nchini ili kuhakikisha vyombo vya habari vinatekeleza majukumu yake kwa umakini na kwa kuzingatia weledi ambapo mafanikio yaliyofikiwa ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Wizara iliratibu utugaji wa Sheria ya Kudumu ya Huduma za Habari Na. 12 ya Mwaka 2016 pamoja na Kanuni zake za Mwaka 2017. Sheria hiyo pamoja na mambo mengine inalenga kutatua

changamoto zilizokuwa zinaikabili Sekta ya Habari na Utangazaji Nchini ambazo zilitokana na upungufu wa kisheria hususan Sheria ya Magazeti ya Mwaka 1976 iliyokuwa inalalamikiwa na wadau wa habari kutokana na upungufu katika baadhi ya vipengele vya Sheria hiyo. Sheria hii imeanza kutumika rasmi tarehe 31 Desemba, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, magazeti na majarida mapya 20 yalisajiliwa Kiambatisho Na. II kinabainisha magazeti na majarida yaliyosajiliwa katika kipindi cha mwaka 2011 hadi 2016 ukurasa wa 70 wa kitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Wizara iliratibu kipindi maalum cha Tunatekeleza kinachorushwa na Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)* kila Jumatatu saa 1.00 usiku hadi saa 2.00 usiku, na Alhamisi saa 3.30 usiku hadi 4.30 usiku. Tayari vipindi 64 vimefanyika kati ya mwezi Agosti 2016 na Aprili 30, 2017 na kuhusisha Mawaziri 18, Katibu Mkuu Kiongozi na Makatibu Wakuu wote. Kupitia kipindi hiki watendaji wanapata fursa ya kuzungumza na wananchi kuhusu utekelezaji wa sera, mikakati, programu, miradi na mipango mbalimbali inayotekelezwa chini ya mamlaka zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, *TBC* inaendelea kuboresha usikivu wa redio za shirika hilo katika maeneo ya mipakani ya Kakonko/Kibondo, Nyasa, Longido, Rombo na Tarime kwa kufanya upembuzi yakinifu kubainisha maeneo itakapofungwa mitambo, kuandaliwa kwa hadidu za rejea na kutangaza zabuni ya kununua mitambo.

Mheshimiwa Mwwenyekiti, tano, *TBC* imefunga mitambo ya kupoozea studio za redio katika studio tano zilizoko barabara ya Nyerere. Aidha, vifaa vya mtambo wa kurusha matangazo ya redio na televisheni kwa njia ya *satellite (satellite Up-link)* vinatarajiwa kuingia nchini Mwezi Juni, 2017 kutoka Israel.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, *TBC* imefunga mitambo ya redio Mkoani Geita ili kuwezesha usikivu wa matangazo ya *FM*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba, Kampuni ya Magezeti ya Serikali *(TSN)* imeanzisha jukwaa la fursa za biashara ambalo kwa mara ya kwanza lilifanyika Mkoani Simiyu tarehe 13 Februari, 2017 ikiwa ni hatua ya kuyasogeza magazeti yake karibu na wananchi na vile vile kuwezesha kuibuliwa na kutangazwa kwa fursa mbalimbali za biashara na uwekezaji. *TSN* imeanzisha Mpango maalum wa kukuza lugha ya Kiswahili kwa kushirikiana na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) kwa kuchapisha makala za Kiswahili sanifu katika gazeti lake la habari leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tisa, *TSN* inakamilisha taratibu za kupata fedha kwa ajili ya kufunga mtambo wa uchapaji kibiashara *(Commercial Printing press)* kwa ajili ya kuchapa vitabu na nyaraka mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumi; Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA).* Imetoa leseni kwa vituo 23 vya redio na vituo sita vya televisheni katika kipindi hiki. Hata hivyo, tangu kuanzishwa kwa *TCRA* mwaka 2003 jumla ya vituo 148 vya redio na vituo 32 vya televisheni vimepewa leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kumi na moja, ili kusimamia ubora wa huduma za utangazaji *TCRA* iliendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye vituo vya utangazaji katika maeneo ya studio, vyumba vya kuandaa habari *(newsroom),* maktaba, utaratibu wa ndani wa kuandaa na kutangaza vipindi, sifa za watangazaji na waandishi wa habari na mikataba ya ajira. Moja ya mambo yaliyobainika katika kaguzi hizo ni kwamba asilimia 90 ya wafanyakazi hawana sifa stahiki katika taaluma ya uandishi wa habari na utangazaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili bado ni changamoto kubwa katika tasnia ya habari na utangazaji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Maendeleo ya Utamaduni, ukurasa wa 20 mpaka 26 wa kitabu. Katika Sekta ya Maendeleo ya Utamaduni, Wizara ilitekeleza yafuatayo

katika Mwaka 2016/2017. Kwanza, Wizara iliendelea kuhuisha Sera ya Utamaduni ya Mwaka 1997 kwa kufanya tathmini na kupokea maoni ya wadau kuhusu masuala ya kuzingatiwa katika Sera Mpya ya Utamaduni. Aidha, Wizara iliendelea kukusanya maoni ya wadau kwa ajili ya kuandaa Sera ya Lugha. Pili, Tanzania iliwasilisha Mkataba wa Ushirikiano *MOU* wa utamaduni kwa Serikali ya Kenya unaohusu kipengele cha *ENGIPAATA, EUNOTO* na *OLNG'ESHER* cha jamii ya Kimaasai ili kwa pamoja kiorodheshwe kwenye Orodha ya Dunia ya Urithi wa Utamaduni Usioshikika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii inalenga kuenzi, kulinda, kukuza na kuendeleza mila na desturi za Jamii ya Kimaasai kwa kizazi kilichopo na kijacho. Kuendeleza utambulisho wa jamii ya Kimaasai, Kitaifa na Kimataifa kama sehemu ya utamaduni na kuhamasisha utalii wa utamaduni wa jamii na kukuza soko la bidhaa za jadi, mavazi asili na vyakula vya asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Tanzania na China zilisaini Programu ya Utekelezaji wa Mkataba wa ushirikiano wa kiutamaduni kati ya nchi hizi mbili ya mwaka 2017 hadi 2020, ambayo pamoja na mambo mengine inajikita katika kujenga uwezo wa kitaalam katika uhifadhi na uendelezaji wa utamaduni, kuimarisha ushirikiano wa taasisi zinazohusika na usimamizi na uendelezaji wa utamaduni baina ya pande hizi mbili. Uhifadhi wa urithi wa kitamaduni pamoja na kuimarisha ushirikiano katika Sekta ya Habari na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, maeneo mbalimbali yenye historia ya ukombozi wa Bara la Afrika ikiwemo Majengo yalibainshwa katika Mkoa wa Dar es Salaam kwa ajili ya kukarabatiwa na kuhifadhiwa na ukarabati wa jengo dogo la ofisi ya muda ya Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika, Mkoani Dar es Salaam umeanza na kufikia hatua za mwisho kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, Wizara imeendelea kukusanya na kuhifadhi kwa njia ya upili taarifa za lugha za kijamii ambapo jumla ya maneno 150 ya nyimbo za kijamii

za jando na unyago kutoka katika jamii za Wazaramo, Wayao na Wamakonde yamefanyiwa utafiti na kuhifadhiwa kwa njia ya TEHAMA kwa minajili ya kulinda utambulisho wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, BAKITA ilianzisha mradi wa kuunda Kongoo ya Kiswahili ya Taifa inayotarajiwa kuwa na matini andishi yenye jumla ya maneno milioni mia moja. Aidha, kwa sasa tayari matini yenye jumla ya maneno milioni moja na nusu yamekusanywa na kuingizwa kwenye *computer* kwa njia ya ku-*scan* na kuhaririwa.

Mheshimiwa Mwenyeiti, saba; Baraza limeuza nakala 1,674 za kamusi yake mpya Kamusi Kuu ya Kiswahili kama njia ya kusambaza matumizi ya Kiswahili sanifu kwa watumiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nane, BAKITA imehariri kamusi ndogo za lugha tatu ambazo ni Kiswahili – Kiingereza – Kifaransa; Kiswahili – Kingereza – Kireno; na Kiswahii – Kingereza – Kiarabu pamoja na kudurufu toleo la kwanza la Kamusi Kuu ya Kiswahili kwa kuongeza maneno mapya 150 kwa ajili ya toleo la pili la kamusi hiyo ambalo lilitoka mwezi Februari mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tisa; ili kukifanye Kiswahili kuwa bidhaa, BAKITA imekamilisha maandalizi ya mafunzo ya Kiswahili kwa wageni na Miswada mitano ya kamusi ndogo ya lugha tatu kwa ajili ya soko la Afrika Mashariki na kwa Afrika kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa lugha ya Kiswahili imeendelea kukua na kuenea ndani na nje ya nchi. Kiswahili kwa sasa ni lugha ya kumi kati ya lugha 6,000 zinazozungumzwa na watu wengi duniani. Pia Kiswahili ni lugha ya pili inayozungumzwa na watu wengi katika Bara la Afrika. Aidha, lugha hiyo ni moja ya lugha rasmi za kufanyia kazi katika Umoja wa Afrika na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vile vile baadhi ya nchi za Afrika Mashariki tayari zimeanza kufundisha lugha hiyo kuanzia ngazi ya awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa raghba, uzalendo, jitihada, uungwana na kujivunia kutumia lugha la Kiswahili kama utambulisho wa Taifa na utamaduni wetu. Hii imeshadidisha matumizi ya lugha ya Kiswahili miongoni mwa viongozi na jamii kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Sekta ya Maendeleo ya Sanaa iko ukurasa wa 26 mpaka 32. Mafanikio yaliyofikiwa katika sekta hii katika mwaka 2016/2017, ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Wizara imeanza maandalizi ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Sanaa kwa kukusanya maoni ya Wadau wa sekta kuhusu masuala ya kuzingatiwa katika Sera hii. Aidha, kwa kushirikiana na Bodi ya Filamu Tanzania, Wizara iliendelea na zoezi la kuandaa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Filamu kwa kufanya tathmini ya sekta ya filamu nchini ili kuibua changamoto za kisera zinazoikabili sekta hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zinazoshughulika na urasimishaji imeandaa mkakati utakaowezesha kumtambua msanii kuanzia ngazi ya mtaa, kijiji hadi Taifa na aina ya sanaa anayofanya kabla ya kufanya urasimishaji wa fani zilizobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Wizara inaratibu uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Sanaa na Ubunifu ambapo rasimu ya awali ya andiko la kuanzisha mfuko huo imeandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, Bodi ya Filamu Tanzania ilipokea jumla ya Miswada ya kutengeneza filamu 170 ambapo baada ya kufanyiwa uchambuzi Miswada 166 ilipewa vibali na Miswada minne kutoka nje ya nchi haikuridhiwa kupewa vibali kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo pamoja na sababu za kimaadili, kiuhifadhi na kiusalama. Jumla ya vibali 122 vya utengenezaji wa filamu, nakala za filamu na picha jongevu vimekwishatolewa

vikiwemo 21 kwa kampuni za Kitanzania na 101 kwa kampuni za nje ya nchi. Kiambatisho namba tatu kinabainisha vibali vya kutengeneza filamu na picha jongevu vilivyotolewa katika kipindi cha mwaka 2011 hadi 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, Bodi ya Filamu imepanga na kutoa madaraja na ithibati kwa wataalam wa Sekta ya Filamu ikiwa ni pamoja na watayarishaji, waigizaji, wasambazaji, wahariri, watafuta mandhari, waongozaji, wapiga picha, waagizaji na wadau wengine ambao jumla ya wadau 19,809 na miundombinu 35 zikiwemo studio, majumba ya uzalishaji na majumba ya sinema vilipewa madaraja na ithibati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, ili kuimarisha weledi katika sekta ya filamu na michezo ya kuigiza, Bodi ya Filamu imeendesha warsha za kuwajengea uwezo wa kuzalisha filamu zenye ubora na kuimarisha weledi kwa watasnia 860 kutoka Mikoa ya Morogoro, Mwanza, Mara na waandishi wa miswada kutoka Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba, Wizara imeratibu na kuendesha operesheni kubwa mbili na za kawaida sita dhidi ya kazi za filamu zinazoingia sokoni bila kufuata taratibu, ambapo jumla ya kazi 2,394, 059 zilikamatwa, zikiwemo kazi za nje ya nchi 2,393,529 zenye thamani ya zaidi ya sh. 3,590,293,500 na za ndani 530 zenye thamani ya sh. 1, 590,000. Mitambo ya kufyatua kazi za filamu *(duplicators)* 19; *printer* za *CD, DVD* nane; *DVD writers* 31; *computer* tatu; *UPS 7* vilikamatwa katika operesheni hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hizo zinazoshukuliwa na Serikali kudhibiti uharamia yaani *piracy* katika kazi za filamu na muziki zimetafsiriwa visivyo na baadhi ya wadau kuwa Serikali inazuia kwa makusudi uingizwaji, usambazaji na uuzwaji nchini wa filamu za kigeni kinyume na matakwa ya soko huria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa hatua zinazochukuliwa ni kuhakikisha tu

kuwa kila mtu anayefanya biashara ya filamu nchini anafuata sheria zikiwemo; Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuingiza Na. 4 ya Mwaka 1976; Sheria ya Haki Miliki na Haki Shirikishi Na. 7 ya Mwaka 1999; Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa Na. 23 ya Mwaka 1984; Kanuni za Ushuru wa stempu kwa bidhaa za filamu na muziki za mwaka 2013; na Mkataba wa Kimataifa wa Berne *(Berne Convention)* kuhusu ulinzi wa kazi za sanaa wa mwaka 1886.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo lengo la Serikali si kumkandamiza mfanyabiashara yoyote wa bidhaa za filamu bali kuhakikisha sheria za nchi zinazingatiwa ili kuleta usawa kwenye ushindani wa kibiashara, kulinda maadili na maslahi ya wasanii wetu wa ndani na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) lilitoa ushauri kwa wasanii na wadau wa sanaa wapato 1572 kuhusu utaratibu na umuhimu wa kusajili kazi zao, masoko ya kazi za sanaa, maadili katika kazi za sanaa, Sheria na Uendeshaji wa matukio ya sanaa ikiwa ni pamoja na kupitia maandiko na shughuli mbalimbali za sanaa kutoka kwa wasanii na kuyaboresha.

BASATA vile vile iliratibu warsha ya siku tatu ya kuwajengea uwezo viongozi 30 wa Vyama vya Mashirikisho manne ya sanaa nchini ili kuboresha na kuimarisha utendaji wa Mashirikisho na Vyama vya Sanaa nchini. Aidha, kwa kushirikiana na Chama cha Waandishi wa Habari za Sanaa na Utamaduni (*CAJATz*), BASATA iliendesha semina kwa waandishi wa habari za sanaa wapatao 70 ili kuwajengea uwezo katika kuandika habari za sanaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) imedahili jumla ya wanachuo 224 (Wanaume 178 na Wanawake 46). TaSUBa iliandaa Tamasha la 35 la Sanaa na Utamaduni wa Mtanzania, ambalo lilifanyika kwa ufanisi na jumla ya vikundi 60 vilishiriki. Kati ya hivyo, vikundi 56 vya wasanii vilitoka ndani ya nchi na vikundi vinne vilitoka Kenya, Zimbabwe na Afrika Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TaSUBa vile vile ilinunua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwenye maeneo ya teknolojia ya sauti, muziki, ubunifu pamoja na uzalishaji wa picha jongevu vilivyogharimu shilingi millioni mia moja. Aidha, taasisi hiyo ilipata msaada wa vifaa vingine vya kufundishia (ala za muziki, vyombo vya sauti, kompyuta, kabati za kuhifadhia vifaa) vyenye jumla ya thamani ya Shilingi milioni mia moja kutoka Serikali ya Denmark.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inatambua changamoto zilizopo kwenye Sekta ya Sanaa ikiwa ni pamoja na ukosefu wa elimu, mitaji na weledi kwa baadhi ya wasanii. Wizara inaendelea kuzipatia ufumbuzi changamoto hizo kwa kuwashirikisha wadau wa Sekta za Umma na Sekta Binafsi ikiwa ni pamoja na kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Sanaa na Ubunifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Maendeleo ya Michezo ukurasa wa 37 mpaka 48. Mafanikio yaliyofikiwa katika Sekta ya Maendeleo ya Michezo katika mwaka wa 2016/2017, ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Wizara ilikamilisha maandalizi ya Rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Michezo ikiwa ni hatua ya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995. Kukamilika kwa mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995 kutawezesha pamoja na mambo mengine, kuifanyia marekebisho Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa, Na. 12 ya Mwaka 1967 na marekebisho yake Na. 6 ya Mwaka 1971 ili iendane na mahitaji ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hizi tunazichukua kuondokana na udhaifu tuliokuwa nao kwa muda mrefu wa kutegemea mafanikio bila kujenga mazingira stahili ya mafanikio. Miaka zaidi ya 30 sasa imepita toka Tanzania ing'are kimataifa katika medani za riadha kupitia wanariadha wake mashuhuri wakati huo, wakiwemo Francis Naali, Samson Ramadhan, Gidamis Shahanga, Juma Ikangaa, Suleiman Nyambui na Filbert Bayi ambaye aliweka

rekodi mpya ya dunia katika mbio za mita 1,500 mwaka 1974 huko Christchurch, New Zealand.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si kwenye riadha peke yake, lakini vilevile kwenye michezo mingine ukiwemo mpira wa miguu ambapo kwa kiasi kikubwa tulipotea kwenye ramani ya michezo duniani. Kwa mfano, ni miaka 37 imepita tangu nchi yetu ifanikiwe kufika ngazi ya fainali za *AFCON.* Mara zote tunaishia raundi ya kwanza sana sana raundi ya pili. Sababu ni ile ile niliyoelezea awali kwamba matarajio ya mafanikio bila kujenga mazingira stahili ya mafanikio. Sasa tumefungua ukurasa mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016/2017, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika michezo mbalimbali. Michezo hiyo ni pamoja na mashindano ya *Olympic* yaliyofanyika Rio de Janeiro, Brazil Agosti, 2016 ambapo Tanzania iliwakilishwa na wachezaji saba wa riadha kuogelea na Judo. Mwanariadha Alphonce Simbu aliweza kushika nafasi ya tano katika mashindano hayo upande wa mbio ndefu. Mapema mwaka huu Simbu aliweza kushinda na kupata medali ya dhahabu kwenye mashindano ya Mumbai *marathon*, India. Matokeo hayo ni matunda ya maandalizi na mazoezi ya kutosha kwa ufadhili wa kampuni ya *Multi Choice* Tanzania ambayo naipongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile mwanariadha Cecilia Ginoka Panga alikuwa mshindi wa kwanza kwenye mashindano ya Beijing *International Half Marathon* yaliyofanyika tarehe 16 Aprili, 2017. Pia mwariadha mwingine Bi Magdalena Chriprine Shauri alikuwa mshindi wa tano katika mashindano Hamburg Marathon yaliyofanyika tarehe 25 Aprili, 2017 yakijumuisha washiriki zaidi elfu 25 na kuvunja rekodi yake binafsi. Aidha Emmanuel Giniki Gisamoda alikuwa mshindi wa kwanza kwenye Shanghai *International Half Marathon* yaliyofanyika tarehe 23 Aprili, 2017. Wizara inaipongeza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa kuibua na kuendeleza vipaji vya michezo nchini kwani wanariadha wote niliowataja hao wapo JKT. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yalianza kujitokeza vile vile kwa upande wa mpira wa miguu ambapo timu ya Taifa ya vijana ya mpira wa miguu *(Serengeti Boys)* ilifuzu kucheza fainali za michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika *(AFCON)* kwa vijana wenye umri chini ya miaka 17 itakayofanyika Gabon mwezi huu. Serengeti Boys, mbali na kufuta historia hasi tulikuwa nayo ya miaka 37 ya timu zetu kushindwa kufika hata nusu fainali za *AFCON,* imeonesha weledi, nidhamu na uzalendo wa kujituma ya hali ya juu ambavyo vimeiwezesha timu hii kuzibwaga timu za U-17 toka nchi maarufu kisoka duniani zikiwemo Misri, Ghana, Gabon, India na Malasyia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, timu hii imeundwa kutokana na vijana walioonesha kipaji kikubwa kwenye mashindano ya UMISETA, UMITASHUMTA, *COPA COCACOLA* na *Airtel Rising Stars* miaka miwili iliyopita na tutaendelea kuilea ili iwakilishe nchi yetu kwenye mashindano ya Olympic ya mwaka 2020 kwa wachezaji wa umri chini ya miaka 23.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa kuwa mwaka 2019, Tanzania itakuwa mwenyeji wa Mashindano ya *AFCON* ya U17. Tayari *TFF* na kushirikiana na Wizara imeandaa timu maalum inayotokana na mashindano ya *youth under* 13 miaka miwili iliyopita ambayo inaendelea kuimarishwa kwenye moja ya *Sports Academies* hapa nchini. Kwa upande wa mchezo wa *tennis* kwa walemavu timu ya Tanzania ya mpira huo imeshinda ubingwa Afrika mwezi Aprili, mwaka huu Jijini Nairobi na kupata tiketi ya kuliwakilisha bara la Afrika katika mashindano ya kombe la dunia ya mchezo huo yatakayofanyika nchini Italia mwezi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanza maandalizi ya michezo ya UMISETA na UMITASHUMTA ambao Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI itakuwa wima kuangalia vijana wenye vipaji katika michezo mbalimbali ambao baadaye watahamishiwa kwenye shule teule 56 za kulea vipaji, hivyo katika michezo. Mbali na mikakati hiyo *TFF* inaandaa vituo vya ufundi vitakavyokuwa na vifaa stahiki kila mkoa kwa madhumuni ya kulea vipaji kwa njia mazoezi. Itapendeza

sana ikiwa kila Mheshimiwa Mbunge atahakikisha katika jimbo lake kuna angalau kuna kituo kimoja cha aina hiyo na vifaa stahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii kuwaomba wazazi nchini kuruhusu watoto wote bila kuwabagua kushiriki kwenye sanaa na michezo mbalimbali kwani michezo si tu ni afya bali vile vile ni ajira tena ajira ya uhakika kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuhiza maadalizi ya kutosha kwa timu zetu zinazoshiriki katika mashindano ya juu ya madola mwaka 2018 Serikali kupitia mahusiano ya diplomasia ya michezo inaendelea na mazungumzo na nchi za China, Cuba na Ethiopia ili kuwapeleka baadhi ya wanamichezo wetu kufanya mazoezi kwa michezo ya riadha, ngumi na mpira wa meza katika nchi hizo. Ni matumaini yetu kuwa mazungumzo yatakapokamilika timu zitakwenda katika nchi hizo ili kujiimarisha kwa ajili ya kushiriki katika mashindano ya Jumuiya ya Madola mwaka wa kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Morocco imeanza taratibu za ujenzi wa eneo changamani la michezo katika eneo la Nala mkoani Dodoma lenye ukubwa wa hekari 150. Naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt.John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake za kuimarisha michezo nchini kwani mradi huu ni matokeo ya ushirikiano mzuri baina yake na Mfalme wa Morocco.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya, kimeendelea kuendesha mafunzo ya stashahada ya ufundishaji michezo na utawala wa michezo ambapo jumla ya wanachuo 97 waliendelea na mafunzo. Jumla ya vyama, vilabu na vituo vya michezo 254 vimesajiliwa katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha ufanisi na tija katika ukusanyaji wa mapato yatokanayo na michezo,

Wizara imekamilisha ujezi wa mfumo wa kieletroniki wa ukusanyaji wa mapato yatokanayo na viingilio katika Uwanja wa Taifa na Uwanja wa Uhuru. Baraza la michezo la Taifa (BMT) liliendesha semina kwa maafisa michezo 49 wa mikoa na wilaya kutoka Mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Pwani, Morogoro, Lindi, Tanga, Singida, Dodoma, Manyara, Arusha na Kilimanjaro iliyolenga kuwajengea uwezo wa kusimamia utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya BMT na Uratibu wa Shughuli wa Michezo Katika Maeneo yao. Vile vile BMT ilisimamia uchaguzi wa vyama vya michezo vitano. Vyama hivyo ni Chama cha Judo Tanzania, Chama cha Riadha Tanzania, Kamati ya *Olympic* Tanzania, Chama cha Mashua Tanzania na Chama cha *Tennis* Tanzania. Vile vile kwa kushirikiana na *UNESCO BMT* iliendesha tamasha la kupinga matumizi ya madawa ya kusisimua misuli michezoni kwa wanafunzi kutoka shule 14 sekondari na msingi za Wilaya ya Temeke na wadau wengine wa michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu kulifanyika kulifanyika ligi kuu ya mpira wa miguu ya wanawake iliyohusisha timu 12 kutoka mikoa 12 ya Tanzania bara ambapo timu ya Mlandizi *Queens* iliibuka bingwa wa ligi hiyo, napenda kutumia fursa hii kumshukuru na kumpongeza mlezi wa timu hiyo Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, Mbunge wa kuteuliwa kwa kuiwezesha timu hiyo kufikia mafanikio hayo. Aidha, natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wengine kuiga mfao huo ili kuinua viwango vya michezo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge Wadau mbalimbali na wananchi kwa ujumla kwa kuichangia timu yetu ya Serengeti Boys ili iweze kufanya vizuri katika fainali za kombe za *under* 17 la *AFCON* na hatimaye kupata nafasi ya kushiriki kombe la dunia nchini India mwezi Novemba, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wadau mbalimbali na Watanzania

wote kwa ujumla kuendelaea kuwachangia timu yetu kwa hali na mali katika kufanikisha azma hii. Wizara imeunda Kamati ya watu 10 inayoongozwa na mtangazaji nguli nchini Bwana Charles Hilary kwa ajili ya kuhamasisha wananchi kuiunga mkono timu hii. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na *TFF* imefungua *Account* maalum iitwayo *TFF Football Development Fund* Na. 0086628003 *Diamond Trust Bank*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa kwa mchango wao mkubwa katika suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zilizojitokeza na hatua zilizokuchukuliwa, ukurasa 48 mpaka 51. Pamoja na mafanikio yaliyofikiwa katika mwaka 2016/2017, katika kipindi hicho Wizara ilikabiliwa na changamoto mbalimbali kama ilivyoainishwa katika aya ya 87, ukurasa 48 mpaka 51 wa hotuba yangu. Changamoto hizo ni pamoja na kutozingatiwa kwa maadili ya uandishi wa habari na utangazaji kwa baadhi ya vyombo vya habari, mmomonyoko wa maadili miongoni mwa jamii, sera na sheria za sekta utamaduni sanaa na michezo kutokidhi mahitaji ya sanaa, uchakavu wa mitambo wa Shirika la Utangazaji *(TBC)* na mwamko wa uelewa mdogo wa umuhimu wa jamii kushiriki kwenye michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imechukua hatua mbalimbali ili kuzipatia ufumbuzi changamoto zilizojitokeza kama nilivyoelezea kwa kina katika aya 87 ukurasa 48 mpaka 51 wa hotuba yangu; ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kuhusu uzingatiwaji wa sheria, kanuni na taratibu zinazosimia sekta za habari na utangazaji, utamaduni, sanaa na michezo pamoja na kuanza mapitio ya sera na sheria zinazokidhi mahitaji ya sasa. Aidha, Serikali imeendelea kuongeza bajeti ya Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)* ili kuboreshaji usikivu na uendeshaji wa Shirika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Sehemu d ya hotuba yangu ukurasa 51 mpaka 61 inaeleza kwa kina majukumu yaliyopangwa kutekelezwa na Wizara katika mwaka wa 2017/2018. Majukumu hayo kwa kifupi ni pamoja na, kwa kuanzia na sekta ya habari na utangazaji Wizara kupitia Idara ya Habari Maelezo itaendelea kuwa msemaji mkuu wa Serikali katika utekelezaji wa sera sheria, mikakati, *program* na miradi mbalimbali ya maendeleo. Kuratibu vitengo vya mawasiliano Serikalini na kusimamia utekekezaji wa Sheria Na. 12 ya Huduma za Habari ya Mwaka 2016 na kanuni zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, *TBC* itakarabati studio za redio *television* za Mikoani Dodoma na Dar es salaam, itanunua vifaa vya utangazaji wa redio na *television* na kuongeza ubora wa studio na mitambo. Kwa upande wa kampuni ya magazeti *TSN,* kampuni hiyo itaendelea kuimarisha ubora wa bidhaa na huduma zinazozitoa pamoja na kuongeza ufanisi katika uzalishaji na utendaji kazi. Aidha, Mamlaka ya Mawasiliano itaendelea kukamilisha zoezi la kutoa mafuzo kwa wakalimani wa lugha ya alama kutoka katika vituo vya *television* na kukamilisha mwongozo wa udhamini wa matangazo ya biashara kwa vituo vya utangazaji. Vile vile *TCRA* itaendelea kutoa elimu na mafunzo kwa vituo vya utangazaji ili kuhakikisha weledi wa kutayarisha na kutoa habari unazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya maendeleo ya Utamaduni. Katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kuratibu na kusimia ukusanyaji, uorodheshaji na usambazaji wa kumbukumbu za historia na urithi wa kiutamaduni, kuhuisha Sera ya Utamaduni ya Mwaka 97 na kuandaa Sera ya Lugha ya Taifa. Kufanya utafiti wa mila na desturi za jamii za Kitanzania kwa lengo la kuweka kumbukumbu. Kuhifadhi, kulinda, kuenzi na kuziendeleza na kufanya utafiti na kuhifadhi lugha za kijamii na kukuza misamiati ya lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Baraza la Kiswahili (BAKITA) litaandaa vipindi 52 vya Lugha ya Taifa kupitia redio ya *TBC* Taifa na *Cloud*s. Vipindi 52 vya kumepambazuka

kupitia *Redio One* na vipindi 52 vya Ulimwengu wa Kiswahili kupitia *Television* ya TBC. Kufanya tafsiri kwa asasi za Serikali mashirika ya umma na ya binafsi pamoja na watu binafsi; na kukusanya matini andishi ya Kiswahili yenye jumla ya maneno milioni mbili na kuyaingiza kwenye mfumo wa kusomeka kompyuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Maendeleo ya Sanaa. Katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kukamilisha uandaaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Sanaa, Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Filamu na Mfuko wa Maendeleo ya Sanaa na Ubunifu pamoja na kuratibu mkutano na matamasha mbalimbali ya kitaifa na kimataifa kuhusu masuala ya sanaa ya ubunifu. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji itafanya mapitio ya Sheria ya Haki Miliki na Haki Shirikishi na Namba Saba ya Mwaka 99 na kanuni zake ili kuimarisha utendaji wa *COSOTA* na kuboresha haki za wadau hususani wa Sekta ya Sanaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Bodi ya Filamu Tanzania itapitia miswada 205 ya kutengenezea filamu na makala za filamu na michezo ya kuigiza na kutoa vibali kwa watayarishaji na wapiga picha za filamu wa ndani nan je ya nchi, kuhakiki jumla ya kazi za filamu 1000; kuzipangia madaraja kuzitolea vibali kuendelea kubaini na kuwachukulia hatua wamiliki wa mitambo ya kutengeneza kazi za filamu zinazoingia sokoni kinyume na sheria na kuendelea kuwajengea uwezo wanatasinia wa filamu. Aidha, Bodi ya Filamu itafanya marekebisho ya Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza Na. 4 ya mwaka 1976.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa BASATA baraza litaendelea kuboresha ubunifu na kuibua na kukuza vipaji na kufanya tafiti mbalimbali za sanaa, kukuza soko la kazi la sanaa na kuwawezesha wasanii kutumia fursa za mitandao na teknolojia ya habari na mawasiliano katika kazi zao na kuhuisha na kuboresha Sheria Namba 23 ya mwaka 84 iliyoamzisha BASATA. Aidha, Taasisi ya sanaa na utamaduni

Bagamoyo (TaSUBa) itaendelea kujenga uwezo kwa wadau wa sekta ya sanaa na utamaduni kwa kutoa mafunzo ya stashahada na cheti na kozi fupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Maendeleo ya Michezo katika Mwaka wa Fedha 2017/2018. Wizara itaendelea kuisimamia maendeleo na michezo nchini kuboresha mfumo wa usimamizi wa Vyama vya Michezo nchini ikiwa ni pamoja na kuhuisha Sera ya Michezo na Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa Namba 12 ya mwaka 1967 na marekebisho yake Namba Sita ya mwaka 1971. Kuendelea na maandalizi ya kuwa mwenyeji wa mashindano ya mpira wa miguu ya *AFCON* 2019 kwa vijana wa chini wa umri wa miaka 17 na kutoa mafunzo ya michezo kupitia Chuo cha Michezo, Malya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa BMT, baraza hilo litaendelea kutekeleza mpango wa michezo kwa jamii kwa kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa Walimu wa shule ya sekondari na msingi. Kuhamasisha ushiriki wa jamii katika michezo mbalimbali ili kujenga na kuimarisha afya zao. BMT itaendelea kutoa elimu kwa wadau juu ya athari na matumizi ya dawa na mbinu haramu za kuongeza nguvu michezoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha utalii wa michezo na vile vile kuvitangaza vituo vya utalii vilivyopo nchini, mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki itahakikisha inawasiliana na Balozi zetu zilizopo nchini Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Italia, Uholanzi, Ubeligiji, Urushi, China, Japan, Jamhuri ya Korea, Canada na Marekani kwa lengo la kuzikaribisha *clubs* kubwa za mpira wa miguu za nchi hizo kuja nchini ili kutumia miundombinu yetu ya kisasa ya michezo na kutembelea vivutio mbalimbali vya utalii tulivyonavyo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tuna uzoefu wa ziara za aina hiyo ya wachezaji wa kimataifa wastaafu wa timu ya mpira wa miguu ya *Real Madrid* kutoka Hispania ambao

walicheza na wachezaji wastaafu wa timu yetu ya Taifa jijijni Dar es salaam mwaka 2014 na kupata fufsa ya kutembelea vivutio vyetu vya utalii. Ziara ya timu hiyo ilitangazwa dunia zima kupitia vyombo mbalimbali vya habari ikiemo pamoja ana *CNN, BBC* na *Super Sport.* Aidha, moja ya Timu iliyoko kwenye ligi kuu ya Uingereza *Everton FC* inatarajiwa kuja nchini mwezi Julai, 2017 kwa lengo la kucheza mechi moja ya kimataifa ya kirafiki na moja ya timu zetu kongwe zinazocheza ligi kuu nchini na kutembelea vivutio vyetu vya utalii. Dhamira ya *Everton FC* ni kucheza na timu itakayoshika katika mechi maalum ya kirafiki kati ya club ya Yanga na na Simba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujumbe wa timu hiyo umeshakuja Tanzania mara mbili ndani mwaka huu. Mara ya kwanza kujadiliana na Wizara na kukagua uwanja wa Taifa na miundombinu yake na mara ya pili kujiridhisha kuhusu ubora wa nyasi za uwanja wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Mapato Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018. Wizara kupitia Idara ya Habari Maelezo na Idara ya Maendeleo ya Michezo inakadiria kukusanya jumla ya sh. 855, 805,000 kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali vya mapato ikiwa ni ongezeko la asilimia 4.4 ikilinganishwa na sh. 820,005,000 ambazo ni makadirio ya mwaka 2016/2017. Aidha, taasisi zilizo chini ya Wizara zinatarajia kukusanya jumla ya sh. 36,912,939,000. Naomba muangalie kiambatisho Namba nne ukurasa wa 72 wa kitabu kuhusu mchanganuo wa makusanyo wa maduhuli kwa Taasisi za Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matumizi ya Kawaida. Katika mwaka 2017/2018, Wizara imetengewa bajeti ya sh. 21,892,695,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, matumizi mengine na mishahara. Fedha hizo zinajumuisha mishahara ya watumishi wa Wizara sh. 4,389,869,000. Mishahara ya Taasisi zilizo chini ya Wizara sh. 12,886,747,000, matumizi mengineyo ya Wizara sh. 3,405,783,000 na matumizi mengineyo ya Taasisi

sh.1,210,296,000; viambatisho namba tano, sita na saba vinafafanua zaidi kuhusu mgawanyiko wa bajeti hii ambao iko ukurasa wa 73 - 78 wa kitabu changu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Maendeleo. Katika mwaka 2017/2018, Wizara imetengewa jumla ya sh. 6,320,000,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi mitatu ya maendeleo ambayo ni *program* ya urithi wa ukombozi wa Bara la Afrika, maandalizi ya awali ya ujenzi wa eneo changamani la michezo Dodoma na upanuzi wa usikivu wa *TBC*, angalia kiambatisho namba nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha kwa ajili ya kutengeneza mpango wa mwaka 2017/2018. Ili Wizara iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ya mwaka wa fedha 2017/2018, naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe Jumla ya sh. 28, 212,695,000. Ambapo kati ya fedha hizo mishahara ni sh. 17,276,616,000 na matumzi mengineyo sh. 4,616,079,000 na miradi ya maendeleo ni sh. 6,320,000,000. Mchanganuo wa bajeti ya fedha hizo upo katika viambatanisho vilivyotajwa hapo awali ambavyo ni sehemu ya hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau mbalimbali wameshiriki katika kuiwezesha Wizara kufikia mafanikio mbalimbali katika 2016/2017, kama ilivyobainishwa awali. Napenda kutumia fursa hii kuwatambua na kuwashukuru baadhi ya wadau hao kama ifuatavyo:-

Serikali ya Jamhuri ya watu wa China, Finland, Uingereza, Denmark, Japan, Sweden, Norway, Jamhuri ya Kiislamu ya Watu wa Iran, Cuba, Jamhuri ya Korea, India, Misri, Uholanzi, Australia, Marekani, Ujerumani na Morocco.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nayatambua na kuyashukuru Mashirika ya Kimataifa kama ifuatavyo:-

Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu Sayansi na Utamaduni *(UNESCO).* Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP),* Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Japan

*(JICA),* Shirika la Kazi Duniani, *(ILO),* British Council na Umoja wa Ulaya *(EU). (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha niwatambue na kuwashukuru Washirika wote wa Maendeleo wa ndani ambao ni pamoja na *Star Times, NMB Bank, CRDB Bank, Tanzania Breweries Limeted, Serengeti Breweries Limited, TANESCO, TANAPA, NSSF, Multi Choice, Airtel, Tigo, Vodacom, Zantel* na wengine wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru wadau wa Wizara yangu wakiwemo waandishi wa habari, wanautamaduni, wasanii na wanamichezo kwa mchango wao uliowezesha Wizara kutekeleza majukumu yake. Aidha, naishukuru sana Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia *Press* A kwa kuchapa hotuba hii kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe tena shukrani zangu za dhati kwako na uongozi mzima wa Bunge letu Tukufu na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafikia

**MWENYEKITI:** Ahsante hoja imeungwa mkono.

## HOTUBA YA WAZIRI WA HABARI,UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO, MHE. DKT. HARRISON G. MWAKYEMBE (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2017/2018 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### A. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo kwenye Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, sasa naomba kutoa hoja ya kwamba Bunge lako

Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

2. ***Mheshimiwa Spika*****,** awali ya yote naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniteua kuisimamia Wizara hii yenye wajibu wa kuratibu na kuendeleza Sekta ya Habari; kudumisha na kuendeleza utamaduni, mila na desturi za Mtanzania; kuimarisha tija na kulinda kazi za sanaa nchini na kuendeleza michezo katika Taifa letu. Naomba kumhakikishia Mhe. Rais utendaji bora.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii chini ya Uenyekiti wa Mhe. Peter Joseph Serukamba (Mb.), Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kwa ushirikiano ambao imeendelea kutoa kwa Wizara yangu. Kamati hii ilijadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka 2017/2018 tarehe 30 Machi, 2017 na kuyapitisha kwa kauli moja. Wizara yangu itazingatia ushauri uliotolewa na Kamati katika utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya mwaka 2017/2018.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutumia fursa hii kuwapongeza Wabunge waliochaguliwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuliwakilisha Taifa letu katika Bunge la Afrika Mashariki, Mbunge mpya wa Viti Maalum, Mhe. Mch. Dkt. Getrude Rwakatare (Mb.) na Wabunge wengine watano (5) walioteuliwa na Mhe. Rais kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambao ni Mhe. Anne Killango Malecela (Mb.), Mhe. Alhaji Abdallah Majura Bulembo (Mb.), Mhe. Prof. Palamagamba Mwaluko Kabudi (Mb.), Mhe. Juma Ali Juma (Mb.) na Mhe. Salma Rashid Kikwete (Mb.).

5. ***Mheshimiwa Spika*****,** kwa unyenyekevu mkubwa, naomba niwashukuru wananchi Jimbo la Kyela kwa upendo, imani na ushirikiano wanaonipa ambao umeniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya ubunge kwa tija na ufanisi

mkubwa. Kupitia Bunge lako Tukufu naomba niwahakikishie Wana- Kyela kuwa tutaendelea kushirikiana katika kuhakikisha jimbo linapiga hatua kubwa za maendeleo. Aidha, naishukuru familia yangu hasa mke wangu Malkia wangu wa Nguvu Linah kwa kunivumilia na kunitia moyo nichape kazi pamoja na changamoto ya afya aliyonayo. Nimelelewa kumshukuru Mungu kwa kila jambo.

6. ***Mheshimiwa Spika*****,** mafanikio yanayoonekana katika Wizara yangu yametokana na ushirikiano mkubwa na wa dhati ninaoupata kutoka kwa viongozi wenzangu na Watumishi wote wa Wizara. Nitumie fursa hii kumshukuru sana Mhe. Anastazia James Wambura (Mb.), Naibu Waziri; Prof. Elisante Ole Gabriel, Katibu Mkuu; na Bi. Nuru Mrisho Millao, Naibu Katibu Mkuu kwa msaada mkubwa wanaonipatia katika uongozi wa Wizara. Aidha, nawashukuru Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wakuu wa Vitengo, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, wataalamu na watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwa kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2016/2017, Bunge lako Tukufu lilipatwa na simanzi kubwa kwa kuondokewa na Mhe. Samwel John Sitta, aliyekuwa Spika Mstaafu wa Bunge la Tisa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Taifa liliondokewa na Mhe. Hafidh Ally Tahir, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Dimani na Mhe. Dkt. Elly Marko Macha, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum. Vilevile, Nchi yetu ilikumbwa na majanga mbalimbali na maafa yaliyosababisha vifo, majeruhi, uharibifu na upotevu wa mali ikiwa ni pamoja na tetemeko la ardhi lililotokea Mkoani Kagera. Naomba nitumie fursa hii kuwapa pole familia, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania kwa ujumla kwa matukio hayo ya kusikitisha na kutia huzuni.

8. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika maandalizi ya hotuba hii, Wizara imezingatia maudhui ya Hotuba ya Mhe. Kassim M. Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2016/2017 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2017/2018.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba yangu imegawanyika katika sehemu Saba. Sehemu ya kwanza inahusu Utangulizi; sehemu ya pili inazungumzia Dira, Dhima na Majukumu ya Wizara; Sehemu ya Tatu ni Mapitio ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa kipindi cha mwaka 2016/2017, na sehemu ya Nne ni Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Aidha, Sehemu ya Tano ni Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na Sehemu ya Sita ni Maombi ya Fedha kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Mwaka 2017/2018. Mwisho, Sehemu ya Saba ni Shukrani.

## B. DIRA, DHIMA NA MAJUKUMU YA WIZARA

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** dira ya Wizara ni kuwa na Taifa linalohabarishwa vizuri, lililoshamirika kiutamaduni, lenye kazi bora za Sanaa na lenye umahiri mkubwa katika michezo ifikapo mwaka 2025.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** dhima ya Wizara ni kuendeleza utambulisho wa Taifa kwa kuwezesha upatikanaji stahiki wa habari, kukuza Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa lengo la kuleta Maendeleo ya jamii kiuchumi.

Majukumu ya Wizara

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina majukumu ya kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Mipango mbalimbali ya Serikali katika sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; kuratibu na kusimamia shughuli za Vyombo vya Habari nchini pamoja na kuendeleza Sekta ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Aidha, Wizara inasimamia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi mbalimbali zilizopo chini yake. Taasisi hizo ni Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN), Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza (TFB), Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) na Baraza la Michezo la Taifa (BMT). Wizara pia inasimamia Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kupitia Idara ya Maendeleo ya Michezo. Aidha, Wizara

inasimamia Kamati ya Maudhui ambayo kimuundo ipo ndani ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

## C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA KIPINDI CHA MWAKA 2016/2017

### C1. MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA

**13.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2016/2017, Wizara ilipanga kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi Milioni Mia Nane Ishirini, na Elfu Tano (Sh. 820,005,000) kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato. Kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Wizara ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi Milioni Mia Sita Ishirini na Saba, Mia Tano na Tano Elfu (Sh. 627,505,000). Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 jumla ya Shilingi Milioni Mia Nne Hamsini na Tano, Mia Tatu na Tano Elfu, Mia Tatu na Tisa (Sh. 455,305,309) zilikusanywa ambazo ni sawa na asilimia 56 ya lengo la makusanyo ya mwaka na asilimia 73 ya lengo la robo ya tatu (Julai, 2016 hadi Machi, 2017). Mchanganuo wa makusanyo upo kwenye *Kiambatisho Na.I.*

**14.** ***Mheshimiwa Spika*****,** kwa Mwaka 2016/2017 Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ujumla wake zilipanga kukusanya Shilingi Bilioni Hamsini na Moja, Milioni Mia Saba Sabini na Nane, Mia Nane Tisini na Nne Elfu, Mia Nne Arobaini na Saba (Sh. 51,778,894,447) na kwa robo ya tatu (Julai, 2016 hadi Machi, 2017) zilipanga kukusanya Shilingi Bilioni Thelathini na Nne, Milioni Mia Nne Kumi na Tano, Mia Sita Hamsini Elfu, Mia Tisa Thelathini na Tano (Sh. 34,415,650,935). Kufikia Machi, 2017 Shilingi Bilioni Kumi na Sita, Milioni Mia Sita Sabini na Sita, Mia Tano na Tano Elfu, Mia Nne Kumi na Saba (Sh. 16,676,505,417) zilikuwa zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 33 ya lengo la mwaka na asilimia 49 ya lengo la robo ya tatu.

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Wizara ilitengewa bajeti ya Matumizi ya Kawaida ya Shilingi Bilioni Kumi na Saba, Milioni Mia Tatu Ishirini na Sita,

Mia Moja Sabini na Sita Elfu (Sh. 17,326,176,000). Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni Kumi na Tatu, Milioni Mia Nne Thelathini na Saba, Mia Mbili Sabini Elfu (Sh. 13,437,270,000) ni Mishahara ya Wizara na Taasisi, ambapo Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Sita na Tano, Mia Nne Sabini na Saba Elfu (Sh. 3,605,477,000) ni Mishahara ya Wizara na Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Nane Thelethini na Moja, Mia Saba Tisini na Tatu Elfu (Sh. 9,831,793,000) ni Mishahara ya Taasisi. Aidha, Matumizi Mengineyo ni Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Nane Themanini na Nane, Mia Tisa na Sita Elfu (Sh. 3,888,906,000) ambapo Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Tatu Themanini, Mia tatu Ishirini na Tatu Elfu (Sh. 3,380,323,000) ni za Wizara na Shilingi Milioni Mia Tano na Nane, Mia Tano Themanini na Tatu Elfu (Sh. 508,583,000) ni za Taasisi.

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi mwezi Aprili, 2017 jumla ya Shilingi Bilioni Kumi na Moja, Milioni Mia Saba Tisini na Tatu, Mia Nane Thelathini na Tano Elfu, Mia Moja Sabini na Saba (Sh. 11,793,835,177) za Matumizi ya Kawaida zilipokelewa ambazo ni sawa na asilimia 68 ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo Matumizi Mengineyo ni Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Moja Arobaini na Sita, Mia Tano Arobaini na Nne Elfu, Mia Sita Hamsini na Mbili (Sh. 2,146,544,652) na Mishahara ni Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Sita Arobaini na Saba, Mia Mbili Tisini Elfu, Mia Tano Ishirini na Tano (Sh. 9,647,290,525).

## Miradi ya Maendeleo

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa fedha za maendeleo, Mwaka 2016/2017, Wizara ilitengewa Shilingi Bilioni Tatu (Sh. 3,000,000,000) kwa ajili ya kutekeleza Miradi ifuatayo ya Maendeleo:

a) Programu ya Ukombozi wa Bara la Afrika - Sh. 700,000,000;
b) Ujenzi wa Ukumbi wa Wazi wa Maonyesho ya Sanaa (BASATA)- Sh. 800,000,000;
c) Ukarabati wa Chuo cha Sanaa Bagamoyo- Sh. 300,000,000;

d) Eneo Changamani la Michezo - Sh. 100,000,000;
e) Habari kwa Umma - Sh. 100,000,000; na
f) Upanuzi wa Usikivu-TBC Sh. 1,000,000,000

**18.** ***Mheshimiwa Spika*****,** hadi kufikia mwezi Aprili, 2017 Wizara ilipokea Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Moja Tisini, Mia Tatu Ishirini na Nne Elfu (Sh.1,190,324,000) sawa na asilimia 40 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ifuatayo:

a) Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika - Sh. 30,324,000;
b) Ukarabati wa Chuo cha Sanaa Bagamoyo - Sh. 100,000,000;
c) Eneo Changamani la Michezo la Taifa - Sh. 60,000,000; na
d) Upanuzi wa Usikivu – TBC Sh.1,000,000,000

## C2. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA 2016/2017

### Sekta ya Habari na Utangazaji

**19.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Wizara iliendelea kusimamia kikamilifu Sekta ya Habari na Utangazaji nchini ili kuhakikisha Vyombo vya Habari inatekeleza majukumu yake kwa umakini na kuzingatia weledi. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) imeendelea kuratibu ushiriki wa Vyombo vya Habari katika matukio mbalimbali ya Kiserikali. A i d h a , Wizara imeendelea kuweka mazingira mazuri kwa Sekta ya Habari ili kuiwezesha kukua na kufanya shughuli zake kwa uhuru na haki kwa mujibu wa Ibara ya 18 na 30 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Ibara ya 19 ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa mwaka 1966 ambao Tanzania imeridhia.

**20.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika Mwaka 2016/2017, Wizara iliratibu utungaji wa Sheria ya Huduma za Habari Na. 12 ya Mwaka 2016 pamoja na Kanuni zake za Mwaka 2017. Sheria hiyo pamoja na mambo mengine, inalenga kutatua

changamoto zilizokuwa zinaikabili Sekta ya Habari na Utangazaji nchini zilizotokana na upungufu wa Kisheria hususan Sheria ya Magazeti ya Mwaka 1976 iliyokuwa inalalamikiwa na Wadau wa Habari kutokana na upungufu katika baadhi ya vipengele vya Sheria hiyo. Sheria hii imeanza kutumika rasmi tarehe 31 Desemba, 2016. Aidha, katika hatua ya kukuza Sekta ya Habari nchini, jumla ya magazeti na majarida mapya 20 yalisajiliwa katika kipindi hiki na Vitambulisho vya Waandishi wa Habari 326 vilitolewa. Mwelekeo wa usajili wa Magazeti na Majarida katika kipindi cha mwaka 2011 hadi 2016 ni kama inavyoonekana katika *Kiambatisho Na. II.* Pia, katika kipindi hiki jumla ya magazeti na majarida 473 yalifutiwa usajili kutokana na kutochapishwa kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo kinyume na taratibu za usajili.

**21. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara kupitia Idara ya Habari-MAELEZO imeendelea kuratibu programu ya kujenga uwezo wa Vitengo vya Mawasiliano Serikalini katika Wizara, Mikoa, Serikali za Mitaa, Wakala wa Serikali na Taasisi nyingine za Umma ili ziweze kusemea na kutoa ufafanuzi kwa weledi na umahiri katika masuala yanayohusu Taasisi zao. Kwa mwaka 2016/2017 Idara iliratibu Mkutano wa Maafisa Habari na Mawasiliano uliofanyika Dodoma mwezi Machi, 2017 na kuhudhuriwa na Maafisa Habari 230. Katika

Mkutano huo, Maafisa Habari walipata fursa ya kubadilishana uzoefu na kujenga uwezo wa utendaji na uboreshaji wa kazi. Maafisa hao pamoja na mambo mengine, wameazimia malengo ya kitaifa ya utoaji wa taarifa kwa Umma kuhusu shughuli zinazotekelezwa na mafanikio yake kupitia Vyombo vya Habari na kufanyiwa tathmini. Aidha, kufuatia uzinduzi wa Tovuti za Halmashauri zote nchini uliofanyika tarehe 27 Machi, 2017 mjini Dodoma, Idara ya Habari – MAELEZO ina jukumu la kusimamia uhuishaji wa Tovuti hizo. Usimamizi madhubuti wa Tovuti hizo utaimarisha mawasiliano ya karibu zaidi kati ya Serikali na wananchi.

**22.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara vile vile kupitia Idara ya Habari-MAELEZO iliratibu kipindi maalum cha **"TUNATEKELEZA"** kinachorushwa na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) kila Jumatatu saa 1:00 usiku hadi saa 2:00 usiku, na Alhamisi saa 3:30 usiku hadi 4:30 usiku. Ni azma ya Wizara kuhakikisha kuwa mawasiliano kati ya Serikali na wananchi yanaimarishwa na kuwa endelevu/kudumu. Tayari vipindi 64 vimefanyika kati ya mwezi Agosti 2016 na Aprili 30, 2017. Jumla ya Mawaziri 18, Katibu Mkuu Kiongozi, na Makatibu Wakuu wote, walipata fursa ya kuzungumza kupitia kipindi hiki. Watendaji Wakuu wa Mashirika/Taasisi/ Wakala na Idara zinazojitegemea wanaendelea kuutaarifu umma kuhusu utekelezaji wa Sera, Mikakati, Programu, Miradi na Mipango mbalimbali inayotekelezwa chini ya mamlaka zao.

Aidha, kipindi hiki kimewawezesha wananchi kupata suluhisho la changamoto zinazowakabili kwa kutoa maoni yao, kuuliza maswali na kupatiwa majibu papo kwa papo. Kipindi hiki cha "TUNATEKELEZA" kinadhaminiwa na TANAPA, TANESCO na NSSF na Wizara inatoa rai kwamba wadhamini wengi zaidi wajitokeze ili kipindi hiki kirushwe mara nyingi zaidi kupitia vyombo vingi zaidi ili kuwahabarisha wananchi kikamilifu.

## Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2016/2017, Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) liliendelea kuboresha usikivu wa Redio za Shirika katika maeneo ya mipakani mwa nchi yetu ambayo ni: Kakonko/Kibondo, Nyasa, Longido, Rombo na Tarime. Hadi sasa hatua zilizofikiwa ni: wataalam kufanya Upembuzi Yakinifu, kubainisha maeneo itakapofungwa mitambo na kuandaliwa kwa Hadidu za Rejea. Aidha, Shirika limeshawasilisha maombi ya masafa (*frequencies*) katika Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa ajili ya maeneo hayo. Zabuni kwa ajili ya kununua mitambo ilitangazwa tarehe 4 Februari, 2017 na kazi ya kufunga mitambo inatarajiwa kukamilika mwaka huu wa fedha.

**24. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, TBC ilianza kutekeleza mradi wa mfumo wa kupoza studio za redio zilizopo Barabara ya Nyerere kwa kufunga mitambo mipya ya kupoozea. Tayari studio zote tano (5) za redio zimefungwa mitambo hiyo na kufanyiwa majaribio na mfumo unafanya kazi ipasavyo. Aidha, kwa upande wa televisheni, TBC ilianza kutekeleza mradi wa kufunga vifaa vipya vya mtambo wa kurusha matangazo ya redio na televisheni kwa njia ya satelaiti *(satellite Up-link)* ambapo Mkataba na Mzabuni ulisainiwa tarehe 20 Desemba, 2016 na vifaa husika vinatarajiwa kuingia nchini Mwezi Juni, 2017 kutoka Israel.

***25. Mheshimiwa Spika,*** Katika Mwaka 2016/2017 TBC imefunga mitambo ya redio Mkoani Geita ili kuwezesha usikivu wa matangazo ya FM kwenye masafa ya 87.7MHz TBCTaifa na 89.7MHz TBCF na mitambo hiyo ilianza kufanya kazi tarehe 25 Februari, 2017. Utafiti umefanyika na kubaini kuwa maeneo ambayo yanapata matangazo kutoka kutoka kituo hiki cha Geita ni pamoja na: Geita Mjini (Nzela – 24km, Kasamwa – 23km, Katoro – 30km na Nkome – 34km); Bukombe (Ushirombo mjini – 50km, Lunzewa – 70km); Chato (Chato mjini – 50km na Muganza – 65km) na Kahama (Kahama mjini – 60km na Kakora – 30km)

**26. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi hiki, TBC iliandaa vipindi mbalimbali vya kuelimisha umma kuhusu Nyanja za maendeleo, utamaduni, sanaa, afya, uchumi, kilimo biashara, siasa na nyinginezo. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 TBC Taifa iliandaa na kutangaza jumla ya vipindi 2,604, ambapo vipindi 1,548 vilihusu elimu, utamaduni, sanaa, afya uchumi, kilimo na biashara na vipindi 1,056 vilihusu burudani.

**27. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 TBC ilirusha matangazo mbashara 62 ya shughuli mbalimbali za kitaifa zikiwemo zilizomhusu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Bunge letu Tukufu, Idara ya Mahakama na mikutano mingine ya kitaifa na kimataifa. Aidha, TBC iliendesha msimu wa tatu wa kipindi cha *Club*

*Raha Leo show* ambacho kililenga zaidi kuibua na kukuza vipaji vya vijana na hatimaye kupewa mafunzo ya muziki na Chuo Kikuu Huria (OUT) na Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) ili kuimarisha vipaji vyao. Kipindi hiki kilileta mvuto mkubwa na hamasa kwa wasikilizaji na watazamaji wa TBC kwa ujumla na ni matumaini yetu kitaendelea kuboreshwa zaidi katika siku zijazo.

**Kampuni ya Magezeti ya Serikali (TSN)**

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya Magezeti ya Serikali (TSN) ina jukumu la msingi la kuhabarisha, kuelimisha na kuburudisha jamii kupitia magazeti yake ya Daily News, Sunday News, HabariLeo na SpotiLeo, Majarida mbalimbali, tovuti zake na mitandao ya jamii. Katika mwaka 2016/2017 TSN iliendelea kuboresha Magazeti ya Serikali kimaudhui na kimuonekano ili kuvutia wasomaji na matangazo ya biashara na hivyo kuimarisha mapato ya Kampuni. Kutokana na hatua hii TSN imeendelea kuongoza kwa uwiano wa matangazo sokoni (market share) hasa kwa gazeti lake la Daily News kwa asilimia 31. Aidha, katika kipindi hiki, Kampuni iliweza kuongeza idadi ya matangazo kwa kupata wateja wapya 25 zikiwemo kampuni kubwa 2 za wakala wa matangazo.

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki TSN ilianzisha utaratibu wa kushirikiana na wadau mbalimbali kuandaa Jukwaa la Fursa za Biashara katika Mikoa ya Tanzania Bara na Zanzibar. Kupitia jukwaa hilo TSN inatoa fursa kwa Mikoa na wadau wengine wanaoshiriki kuibua na kutangaza fursa za biashara na uwekezaji. Aidha, utaratibu huu unayasogeza magazeti ya Kampuni karibu na wananchi na kuchangia maendeleo yao kwa kusaidia kubainisha na kutangaza fursa mbalimbali za biashara katika Mikoa husika. Jukwaa la Biashara la kwanza lilifanyika Mkoani Simiyu tarehe 13 Februari, 2017 kwa ushirikiano na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Mhe. Anthony Mtaka na lilihudhuriwa na wajumbe zaidi ya 160 na kushirikisha wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Benki za TIB, NMB, Mamlaka ya Mapato Tanzania na Baraza la Biashara la Taifa.

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2016/2017 TSN iliimarisha Kitengo cha machapisho kupitia njia ya mtandao. Aidha, Kampuni ilianzisha Dawati la habari digitali (Multimedia Desk) ambalo limeendelea kuimarishwa kwa kuongezewa watendaji na vitendea kazi hatua ambayo imeliwezesha Dawati hilo kukusanya na kusambaza habari kwa njia ya picha, maandishi, na video kwa kutumia mtandao. Kwa sasa, mitandao inayotumika ni tovuti za magazeti husika na mitandao ya jamii. Aidha, Kampuni imeweza kusambaza magazeti yake kwa kupitia mitandao ya M-Paper, Bongo Papers na Sim-Gazeti.

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** ikiwa ni hatua ya kuelimisha jamii, TSN ilitoa machapisho maalum kuhusu matukio mbalimbali ya kitaifa na kimataifa kama vile maadhimisho ya sikukuu ya wakulima - Saba Saba; Nane Nane; Uhuru wa Tanganyika; Mapinduzi ya Zanzibar; Siku ya Ukimwi Duniani; Siku ya Malaria Duniani; Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi). Aidha, TSN imeanzisha Mpango maalum wa kukuza lugha ya Kiswahili kupitia gazeti lake la HabariLeo ambapo kwa sasa Kampuni hiyo imeingia makubaliano na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) ya kuchapisha makala za Kiswahili sanifu katika gazeti hilo. Lengo pia ni kulifanya gazeti hili ambalo sasa linauzwa na kusomwa nchini Kenya kuwa nyenzo ya kufundishia na kueneza Kiswahili katika Ukanda wa Afrika Mashariki. TSN iko kwenye mazungumzo na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ili kuwezesha utekelezaji kwa upana zaidi wa azma hii.

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki TSN iliendelea na taratibu za kupata fedha kwa ajili ya kufunga mtambo wa uchapaji kibiashara (commercial printing press) kwa ajili ya kuchapa vitabu na machapisho mengine kama vile taarifa mbalimbali, shajara, kalenda, majarida na vipeperushi. Kampuni imeendelea kukamilisha taratibu za kibenki za kupata mkopo wa Shilingi Bilioni 2.4 kutoka Benki ya TIB (Development) ambao ni pamoja na kuwasilisha andiko jipya la mradi baada ya lile la awali kuwa limepitwa na wakati. Aidha, Kampuni iliendelea kuimarisha ofisi yake

ya Dodoma ikiwa ni pamoja na kuongeza Waandishi wa Habari katika Ofisi hiyo ili kukabiliana na ongezeko la mahitaji ya huduma zake kufuatia Serikali kuhamia rasmi Dodoma.

## Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

**33.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inawajibika pia katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo katika eneo la Maudhui na Usajili wa Vyombo vya Habari na Utangazaji. Kwa mujibu wa Sheria Na. 12 ya TCRA ya mwaka 2003 Kifungu cha 27 (1) na Kifungu cha 174 cha Sheria ya Mawasiliano ya Ki-elektroniki na Posta (EPOCA) ya mwaka 2010, kazi za Kamati ya Maudhui ni pamoja na kumshauri Waziri wa Sekta kuhusiana na Sera ya Utangazaji, kusimamia na kufuatilia maudhui ya vituo vya utangazaji, kushughulikia malalamiko kutoka kwa Watangazaji na watumiaji wa huduma za utangazaji, na kusimamia na kuhakikisha kuwa Kanuni za Utangazaji zinafuatwa.

**34.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Wizara kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imetoa leseni kwa vituo 23 vya Redio na vituo Sita (6) vya Televisheni. Aidha, jumla ya vituo 148 vya redio na vituo 32 vya Televisheni vimepewa leseni tangu kuanzishwa kwa TCRA mwaka 2003.

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kusimamia ubora wa Huduma za Utangazaji *(Broadcasting Quality of Service)* kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye Vituo vya Utangazaji kwa lengo la kuhakiki vitendea kazi na ubora wa huduma zinazotolewa na vituo hivyo. Maeneo yaliyohakikiwa ni pamoja na studio, vyumba vya kuandaa habari *(Newsroom),* maktaba, utaratibu wa ndani wa kuandaa na kutangaza vipindi, sifa za Watangazaji na Waandishi wa Habari na Mikataba ya Ajira. Vituo vyote vilivyokaguliwa vimeonyesha ubora katika kutoa huduma kwa wasikilizaji wake katika maeneo husika ikiwa ni pamoja na ubora wa usikivu ambao hauna miingiliano ya sauti, ubora wa vitendea kazi katika

vituo, uelewa wa Taratibu na Sheria za utangazaji kwa wafanyakazi, pamoja na uwezo wa kituo katika kutimiza haki na maslahi ya wafanyakazi wake. Aidha, katika ukaguzi uliofanywa, asilimia 90 ya wafanyakazi wamebainika hawana sifa stahiki katika taaluma ya uandishi wa Habari na Utangazaji.Hii bado ni changamoto kubwa katika tasnia ya Habari na Utangazaji.

**Sekta ya Maendeleo ya Utamaduni**

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2016/2017, Wizara iliendelea kuhuisha Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997 kwa kufanya tathmini na kupokea maoni ya Wadau kuhusu masuala ya kuzingatiwa katika Sera Mpya ya Utamaduni. Aidha, Wizara iliendelea kukusanya maoni ya Wadau kwa ajili ya kuandaa Sera ya Lugha.

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania imefanikiwa kuwasilisha Mkataba wa Ushirikiano (MoU) wa Utamaduni kwa Serikali ya Kenya unaohusu kipengele cha ENGIPAATA, EUNOTO na OLNG'ESHER cha jamii ya Kimaasai ili kwa pamoja kukiorodhesha kwenye Orodha ya Dunia ya Urithi wa Utamaduni Usioshikika. Azma hii inalenga kuenzi, kulinda, kukuza na kuendeleza mila na desturi za jamii ya kimaasai kwa kizazi kilichopo na kijacho; kuendeleza utambulisho wa jamii ya kimaasai kitaifa na kimataifa kama sehemu ya utamaduni na kuhamasisha utalii wa utamaduni wa jamii na kukuza soko la bidhaa za jadi, mavazi ya asili na vyakula vya asili.

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua ya kuimarisha ushirikiano wa Kimataifa katika uendelezaji wa utamaduni, Tanzania na China zilisaini Programu ya Utekelezaji wa Mkataba wa Ushirikiano wa Kiutamaduni wa mwaka 2017-2020. Programu hiyo pamoja na mambo mengine, inajikita katika kujenga uwezo wa kitaalam katika uhifadhi na uendelezaji wa utamaduni, kuimarisha ushirikiano wa Taasisi zinazohusika na usimamizi na uendelezaji wa utamaduni baina ya pande hizi mbili, uhifadhi wa urithi wa kitamaduni pamoja na kuimarisha ushirikiano katika Sekta ya Habari na Michezo.

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taifa letu linakabiliwa na changamoto ya mmomonyoko wa maadili unaotokana hasa na kutozingatiwa kwa malezi na makuzi mema ya Mtanzania, athari za mwingiliano wa tamaduni za kigeni na mitandao ya kijamii. Katika kukabiliana na changamoto hii Wizara inaendelea kufanya mijadala ya kitaifa kuhusu maadili ya Mtanzania ambapo katika kipindi hiki kupitia Programu ya "*Wadau Tuzungumze*" uliendeshwa mjadala kuhusu Maadili ya Mtanzania. Aidha, Wizara ilishiriki katika Tamasha la Maadili kwa Vijana na Watoto kupitia asasi ya kidini ya Tumaini Jipya. Jitihada hizi zinalenga kuenzi, kutunza, kurithisha na kuendeleza maadili, mila na desturi nzuri za Mtanzania.

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaratibu utekelezaji wa Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika yenye jukumu la kukusanya, kuweka kumbukumbu, kuhifadhi na kukumbuka nakshi ya urithi wa Bara la Afrika tangu harakati za kupigania Uhuru wa Afrika, hadi Bara zima lilipokombolewa. Katika kipindi hiki, maeneo mbalimbali yenye historia ya ukombozi wa Bara la Afrika ikiwemo majengo yalibainishwa katika Mkoa wa Dar es Salaam kwa ajili ya kukarabatiwa na kuhifadhiwa.

Aidha, kwa kuwa Programu hii ni mtambuka, katika kipindi hiki iliundwa Kamati ya Wataalam ya kufuatilia utekelezaji wa kazi za Programu ambayo imekuwa ikikutana mara kwa mara na kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa Programu. Vilevile, katika kipindi hiki, ukarabati wa Jengo dogo la Ofisi ya muda ya Programu hii Mkoani Dar es Salaam umeanza na kufikia hatua za mwisho kukamilika.

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukuza na kuendeleza Lugha ya Kiswahili na fasihi zake, Wizara imeendelea kuhamasisha utunzi wa riwaya na tamthilia, na uundwaji wa vyama vya fasihi ambapo vyama viwili (2) vilizinduliwa. Vyama hivyo ni Chama cha Lugha na Fasihi ya Kiswahili Tanzania (CHALUFAKITA) na Chama cha Umoja wa Waandishi wa Riwaya Wenye Dira (UWARIDI).

Aidha, Wizara ilishiriki katika Makongamano ya Vyama vya Kiswahili vya Afrika Mashariki ambavyo ni Chama cha Kiswahili Afrika Mashariki (CHAKAMA) na Chama cha Wanafunzi Afrika Mashariki (CHAWAKAMA). Vilevile, katika kipindi hiki utafiti wa lugha za ulumbi pamoja na katuni zilizotumika wakati wa kipindi cha Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2015 ulifanyika kwa njia ya upili ambapo jumla ya maneno 250 na Katuni 50 vilikusanywa kwa lengo la kukuza misamiati ya lugha ya Kiswahili.

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki Wizara imeendelea kukusanya na kuhifadhi taarifa za upili za lugha za kijamii ambapo jumla ya maneno 150 ya nyimbo za kijamii za jando na unyago kutoka katika jamii za Wazaramo, Wayao na Wamakonde yamefanyiwa utafiti na kuhifadhiwa kwa njia ya TEHAMA kwa minajili ya kulinda utambulisho wake. Tafiti zimebaini Maktaba hai ambayo ni wazee wanatumia lugha za kiasili kutolea mafunzo. Wizara kwa kushirikiana na wadau inaendelea kuhifadhi tafiti za lugha za kijamii kwa njia ya TEHAMA.

**Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA)**

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) iliandaa na kurusha hewani vipindi 46 vya "Lugha ya Taifa" kupitia TBCTaifa na Clouds, vipindi 461 vya "Kumepambazuka" kupitia Radio One na vipindi 47 vya "Ulimwengu wa Kiswahili" kupitia televisheni ya TBC . Vipindi hivi hulenga kuelimisha umma wa Watanzania juu ya makuzi na maendeleo ya lugha ya Kiswahili, vikiwemo msamiati na sarufi. Aidha, Baraza lilipitia na kutoa Ithibati miswada 29 ya vitabu vya taaluma.

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kujenga mazingira ya kuwezesha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika maendeleo ya Kiswahili, BAKITA imeanzisha Mradi wa kuunda Kongoo ya Kiswahili ya Taifa inayotarajiwa kuwa na matini andishi yenye jumla ya maneno milioni mia moja (100,000,000). Hivi sasa tayari Matini yenye jumla ya

maneno milioni moja na nusu yamekusanywa na kuingizwa kwenye kompyuta kwa njia ya kuskani na kuhaririwa.

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza pia limeratibu na kutoa huduma za tafsiri na ukalimani kwa Asasi na Mashirika mbalimbali, watu binafsi pamoja na mikutano ya Kimataifa. Hali kadhalika, limefuatilia matumizi ya Kiswahili na kubaini makosa mbalimbali yaliyofanywa na Vyombo vya Habari na watumiaji wengine wa Kiswahili na kuyasahihisha kwa kutoa ushauri wa matumizi stahiki. Aidha, katika kueneza matumizi sahihi ya Kiswahili, Baraza limeingia mkataba na Gazeti la Serikali la HabariLeo wa kueneza Kiswahili fasaha. Vilevile, Baraza limeuza nakala 1,674 za Kamusi yake mpya (Kamusi Kuu ya Kiswahili) kama njia ya kusambaza matumizi ya Kiswahili sanifu kwa watumiaji.

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki BAKITA ilikusanya Istilahi 300 za magonjwa ya mimea kwa ajili ya Kamusi ya magonjwa ya mimea; kuhariri kamusi ndogo za lugha tatu ambazo ni Kiswahili-Kiingereza-Kifaransa, Kiswahili-Kiingereza-Kireno na Kiswahili- Kiingereza-Kiarabu; kudurusu toleo la kwanza la Kamusi Kuu ya Kiswahili kwa kuongeza maneno mapya 150 kwa ajili ya toleo la pili la Kamusi hiyo ambalo lilitoka mwanzoni mwa mwezi Februari, 2017.

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua ya kukifanya Kiswahili kuwa bidhaa, BAKITA imekamilisha maandalizi ya mafunzo ya Kiswahili kwa wageni na Miswada mitano (5) ya Kamusi Ndogo ya Lugha tatu (3) kwa ajili ya soko la Afrika Mashariki na Afrika.

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa lugha ya Kiswahili imeendelea kukua na kuenea ndani na nje ya nchi. Kiswahili kwa sasa ni lugha ya 10 kati ya lugha 6,000 zinazozungumzwa na watu wengi duniani na ni lugha ya pili inayozungumzwa na watu wengi katika Bara la Afrika. Aidha, lugha hiyo ni moja ya lugha rasmi za kufanyia kazi katika Umoja wa Afrika na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vilevile, baadhi ya nchi za Afrika Mashariki zinafundisha lugha hiyo kuanzia ngazi za awali.

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** nachukuwa fursa hii kumpongeza Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa raghba, uzalendo, jitihada, uungwana na kujivunia kutumia lugha ya Kiswahili kama utambulisho wa Taifa na Utamaduni wetu. Hii imeshadidisha matumizi ya Lugha ya Kiswahili miongoni mwa Viongozi na Jamii kwa ujumla.

**Sekta ya Maendeleo ya Sanaa**

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki Wizara imeanza maandalizi ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Sanaa kwa kukusanya maoni ya Wadau wa Sekta kuhusu masuala ya kuzingatiwa katika Sera hiyo. Aidha, katika kuhakikisha kazizotezaSanaazinarasimishwa, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zinazoshughulika na urasimishaji imeandaa Mkakati utakaowezesha kumtambua msanii kuanzia ngazi ya Mtaa/ Kijiji hadi Taifa na aina ya sanaa anayofanya kabla ya kufanya urasimishaji wa fani zilizobaki. Utambuzi huu utahitaji msanii kujiorodhesha kupitia mfumo wa kieletroniki utakaowekwa au kupitia Maafisa Sanaa/Utamaduni.

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaratibu uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Sanaa na Ubunifu ambapo rasimu ya awali ya andiko la kuanzisha Mfuko huo imeandaliwa. Aidha, Wadau wa Sekta ya Sanaa 1,130 wamewasilisha maoni yao yanayolenga kuboresha rasimu ya Andiko ili Mfuko huo uweze kuzingatia kikamilifu changamoto zinazoikabili Sekta ya Sanaa nchini hususan changamoto za kimitaji. Vilevile, katika kipindi hiki, Wizara iliratibu matamasha mbalimbali yanayolenga kutangaza kazi za Wasanii nchini na nje ya nchi. Matamasha hayo ni pamoja na maandalizi ya Tamasha la tatu (3) la Sanaa na Utamaduni la Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAMAFEST) lililoratibiwa kwa kushirikiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki na Tamasha la Wasanii litakalofanyika mwezi Julai, 2017 katika kijiji cha wasanii Mwanzega kwa lengo la kuwaleta wasanii pamoja ili kujifunza mambo mbalimbali ikiwemo ujasiriamali na kuandaa mikakati ya kupinga matumizi ya madawa ya kulevya.

**Bodi ya Filamu Tanzania**

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Filamu imeendelea na zoezi la kuandaa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Filamu ambapo katika kipindi hiki Tathmini kuhusu Sekta ya Filamu nchini ilifanyika kwa lengo la kuibua changamoto za Kisera zinazoikabili Sekta hiyo. Tathmini hiyo ilihusisha kupata maoni ya wadau wa Filamu 1,162 ambapo wadau 326 walitoka Mkoani Dar es salaam na wadau 836 kutoka Mikoani. Aidha, rasimu ya Sera imeandaliwa na wadau 1,233 wa Sekta ya Filamu (waigizaji, waongozaji, wasambazaji, wapiga picha, walimu na watayarishaji wa filamu) wamepata fursa ya kutoa maoni yao katika rasimu hiyo ikiwa ni hatua ya kuhakikisha Sera inayotungwa inazingatia kikamilifu matakwa na mahitaji ya Kisera katika Sekta ya Filamu nchini.

Vilevile, kupitia kipindi cha "Wadau Tuzungumze," wawakilishi wa Shirikisho la Filamu na Vyama vinavyounda Shirikisho wamepata fursa ya kutoa maoni yao katika rasimu ya Sera husika. Sera hii pamoja na mambo mengine itajikita katika kutatua changamoto za kimitaji zinazowakabili wanatasnia ya Filamu nchini kwa kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Filamu. Wizara pia ilikutana na Wasanii wanawake ili kubaini changamoto zinazowakabili kwa lengo la kuzipatia ufumbuzi. Pamoja na maoni yao kutumika katika kuandaa Rasimu ya Sera, Wizara iliwahimiza waendelee kuwa Mabalozi wazuri wa maadili katika tasnia ya Sanaa.

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendelea kusimamia kikamilifu utengenezaji wa kazi za picha jongevu nchini, Bodi ya Filamu imeendelea kupitia miswada ya kutengeneza filamu na kutoa vibali kwa watayarishaji na wapiga picha kutoka ndani na nje ya nchi. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 jumla ya miswada 170 ilipokelewa na kufanyiwa uchambuzi ambapo miswada 166 iliridhiwa na Miswada Minne (4) kutoka nje ya nchi haikuridhiwa kupewa vibali kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na za kimaadili, kihifadhi na kiusalama. Jumla ya vibali 122 vya utengenezaji wa filamu, makala za filamu na picha jongevu vimetolewa vikiwemo

21 kwa Kampuni za Kitanzania na 101 kwa Kampuni za nje ya nchi. Aidha, Vibali 44 vipo katika hatua ya ukamilishaji wa malipo. Hii ni sawa na asilimia 114 ya miswada inayotakiwa kushughulikiwa kwa mwaka 2016/2017. *Kiambatisho Na. III* kinabainisha vibali vya kutengeneza Filamu na picha jongevu vilivyotolewa katika kipindi cha mwaka 2011 hadi 2016.

**54. *Mheshimiwa Spika,*** ili kupanua wigo wa soko la kazi za filamu nchini na kusogeza huduma kwa wananchi, Bodi imedhamiria kurasimisha maeneo yote yasiyokuwa rasmi ya kuoneshea kazi za filamu pamoja na maktaba za kazi hizo. Hivyo, hadi kufikia Machi, 2017, jumla ya vibanda na maktaba 3,726 sawa na asilimia 75 ya lengo la vibanda na maktaba 5,000 vilibainishwa kutoka Wilaya/Mikoa ya Dodoma, Manispaa Mtwara, Mara, Mwanza, Arusha, Sengerema, Manyoni, Tarime Mjini, Tarime Vijijini, Chato, Kilwa, Misenyi, Muheza, Kakonko, Tanga, Lushoto, Kilindi, Serengeti, Rorya, Tabora, Kigoma, Katavi, na Geita.

Aidha, kanzi data ya watayarishaji, waigizaji, wasambazaji, wahariri, watafuta mandhari, waongozaji, wapiga picha, wasambazaji, waagizaji, wamiliki wa studio, majumba ya uzalishaji na majumba ya sinema imeendelea kuhuishwa. Vilevile, Bodi imeendelea kuhamasisha wadau kuendelea kupanua wigo wa soko ambapo kwa sasa kumekuwa na ongezeko la uoneshaji wa Filamu za kitanzania katika kumbi za sinema, mauzo kwa njia ya mtandao (online platforms) na wengine kuanzisha chaneli maalum kwa ajili ya kuuza kazi za filamu.

**55. *Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Bodi ya Filamu imepanga na kutoa madaraja na ithibati kwa wataalam wa Sekta ya Filamu ikiwa ni pamoja na watayarishaji, waigizaji, wasambazaji, wahariri, watafuta mandhari, waongozaji, wapiga picha, waagizaji na wadau wengine ambapo jumla ya wadau 19,809 na miundombinu 35 zikiwemo studio, majumba ya uzalishaji na majumba ya sinema vilipewa madaraja na ithibati.

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** weledi ni suala muhimu katika Sekta ya Filamu na Michezo ya Kuigiza ili kuinua ubora na kuimarisha ushindani wa kazi zinazozalishwa. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali katika kipindi hiki imeendesha warsha za kuwajengea uwezo wa kuzalisha filamu zenye ubora na kuimarisha weledi kwa wanatasnia 860 kutoka mikoa Mitatu (3) ya Morogoro (194) Mwanza (312), Mara (230) na waandishi wa Miswada kutoka Dar es Salaam (124). Warsha/mafunzo yalijikita katika maeneo yafuatayo: Uandishi wa Miswada na Utafiti, Uongozaji Michezo ya kuigiza na Filamu, Taaluma ya Upigaji Picha katika uzalishaji wa filamu bora, kujitangaza na kutengeneza jina la bidhaa *(branding, trademarks and film promotion and management),* matumizi sahihi ya mtandao katika Sekta ya Filamu, uhusiano kati ya Mtunzi, Muongozaji na Muigizaji na umuhimu wa weledi na taaluma katika Filamu. Wizara itaendelea kuwajengea uwezo wasanii wetu ili kazi wanazozalisha ziwe na ubora unaostahili ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi.

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kudhibiti na kusimamia usambazaji wa kazi za filamu nchini, zilifanyika operesheni kubwa mbili (2) na za kawaida sita (6) dhidi ya kazi za filamu zinazoingia sokoni bila kufuata taratibu. Katika operesheni hizo, hadi kufikia Machi, 2017, jumla ya kazi 2,394,059 zilikamatwa zikiwemo kazi za nje ya nchi 2,393,529 zenye thamani ya zaidi ya shilingi 3,590,293,500 na za ndani 530 zenye thamani ya shilingi 1,590,000. Aidha, mitambo ya kufyatua kazi za Filamu (Duplicators) (19), Printers za CD/ DVD (8), DVD writers (31), Kompyuta (3), UPS (7) vilikamatwa katika operesheni hizo. Vilevile, uhuishaji wa leseni za uendeshaji shughuli za filamu umekamilika na wadau wanaendelea kuwasilisha maombi ili kuhuisha leseni zao.

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** hatua zinazochukuliwa na Serikali kudhibiti uharamia (piracy) katika kazi za filamu na muziki zimetafsiriwa visivyo na baadhi ya wadau kuwa Serikali inazuia kwa makusudi uingizwaji, usambazaji na uuzwaji nchini wa filamu za kigeni kinyume na matakwa ya soko huria. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hatua

zinazochukuliwa ni kuhakikisha kila mtu anayefanya biashara ya filamu nchini anafuata Sheria zikiwemo: Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza Na. 4 ya mwaka 1976; Sheria ya Haki Miliki na Haki Shiriki Na.7 ya mwaka 1999; Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa Na. 23 ya Mwaka 1984; Kanuni za Ushuru wa Stempu kwa Bidhaa za Filamu na Muziki za mwaka 2013 na Mkataba wa Kimataifa wa Berne kuhusu Ulinzi wa Kazi za Sanaa wa mwaka 1886. Kwa hiyo lengo la Serikali sio kumkandamiza mfanyabiashara yoyote wa bidhaa za filamu, bali kuhakikisha Sheria za nchi zinazingatiwa na kila mdau; tozo stahiki zinalipwa na maadili ya nchi yanalindwa na hivyo kuleta usawa kwenye soko na kulinda maslahi ya wasanii wetu wa ndani.

**Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA)**

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2016/2017, Baraza la Sanaa la Taifa lilitekeleza majukumu yafuatayo: kuendesha zoezi la usajili na ufuatiliaji wa wadau kwa ajili ya kuhuisha vibali vyao ambapo jumla ya wasanii binafsi, kumbi, vikundi vya sanaa, wakuzaji na wadau wa Sanaa wapatao 809 walipewa usajili na vibali; kwa kushirikiana na Chama cha Waandishi wa Habari za Sanaa na Utamaduni (CAJATz), BASATA iliendesha midahalo 34 ya jukwaa la sanaa ambapo wasanii na wadau wa sanaa wapatao 3,399 walishiriki. Aidha, Baraza lilitoa ushauri kwa wasanii na wadau wa sanaa wapatao 1,572 kuhusu taratibu na umuhimu wa kusajili kazi zao, masoko ya kazi za sanaa, maadili katika kazi za sanaa, Sheria na uendeshaji wa matukio ya sanaa ikiwa ni pamoja na kupitia maandiko ya shughuli mbalimbali za sanaa kutoka kwa wasanii na kuyaboresha. Vilevile, Baraza liliratibu warsha ya siku 3 ya kuwajengea uwezo viongozi 30 wa vyama na mashirikisho Manne (4) ya Sanaa nchini ili kuboresha na kuimarisha utendaji wa Mashirikisho na Vyama vya Sanaa nchini. Baraza pia kwa kushirikiana na Chama cha Waandishi wa Habari za Sanaa na Utamaduni (CAJATz) liliendesha semina kwa waandishi wa habari za sanaa wapatao 70 ili kuwajengea uwezo katika kuandika habari za sanaa.

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia changamoto zilizojitokeza mwaka 2016 katika uendeshaji wa Shindano la Urembo maarufu kama "Miss Tanzania," zikiwemo taratibu za kuwapata washiriki na uendeshaji na utoaji wa zawadi, BASATA imebaini uwepo wa udhaifu mkubwa wa maandalizi na uendeshaji wa shindano hilo. Wizara imeielekeza BASATA kusitisha leseni ya Kampuni ya "*Lino International Agency Ltd*" iliyoendesha shindano hilo hadi hapo itakapotimiza ahadi zote zilizotolewa katika shindano hilo. Aidha, Wizara imeielekeza BASATA kuhakikisha kuwa inaingia mikataba ya kisheria na wale wenye nia ya kuendesha mashindano ya aina hiyo ili kuondokana na ubabashaji wa aina yoyote katika tasnia hii.

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** ikiwa ni hatua ya kuibua vipaji na kurithisha Sanaa zetu kwa vizazi vijavyo, Baraza liliendesha warsha ya siku Tano (5) katika fani ya upigaji na uchezaji wa ngoma na midundo ya asili kwa watoto wa shule za msingi Wilayani Kisarawe Mkoa wa Pwani ambapo jumla ya Watoto100 na Walimu wa Sanaa Sita (6) kutoka shule 5 za msingi walishiriki. Aidha, Baraza lilitoa tuzo kwa wanafunzi 7 waliofanya vizuri katika masomo ya Muziki, Sanaa za ufundi na Sanaa za Maonyesho katika mtihani wa Kidato cha Nne wa mwaka 2015 kutoka shule za Loyola na Azania-Dar es salaam, Darajani – Kilimanjaro, Arusha Sekondari-Arusha na Bukoba Sekondari-Kagera.

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza lilijadili maombi ya Wakuzaji Sanaa waliosajiliwa na kutoa vibali 58 vya kuingiza wasanii kutoka nje ya nchi. Aidha, BASATA kwa kushirikiana na Kampuni ya Haak Neel Production iliendesha maonyesho ya Siku ya Msanii katika Ukumbi wa Kijiji cha Makumbusho Kijitonyama tarehe 24 Machi, 2016, ambapo wasanii na vikundi mbalimbali walipata fursa ya kuonyesha na kuuza sanaa zao.

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatambua changamoto zilizopo kwenye sekta ya Sanaa ikiwa ni pamoja na ukosefu wa mitaji, elimu stahili na weledi kwa baadhi ya wasanii. Wizara inaendelea kuzipatia ufumbuzi

changamoto hizo kwa kuwashirikisha wadau wa Sekta za Umma na sekta binafsi ikiwa ni pamoja na kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Sanaa na Ubunifu.

**Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa)**

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** TaSUBa inatoa mafunzo ya stashahada, cheti na kozi fupi katika maeneo ya Sanaa za Maonyesho, Sanaa za Ufundi, Filamu na Televisheni, na Ubunifu wa Muziki. Katika kipindi hiki, TaSUBa imedahili jumla ya wanachuo 224 (Wanaume 178 na Wanawake 46). Aidha, jumla ya wanachuo 85 (Wanaume 50 na Wanawake 35) walihitimu mafunzo katika kipindi hicho. Vilevile, Taasisi iliandaa Tamasha la 35 la Sanaa na Utamaduni wa Mtanzania, ambalo lilifanyika kwa ufanisi na jumla ya vikundi 60 vilishiriki. Kati ya hivyo, vikundi 56 vya wasanii vilitoka ndani ya nchi na vikundi Vinne (4) vilitoka Kenya, Zimbabwe na Afrika Kusini.

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** TaSUBa imekamilisha utafiti wa soko na ajira kuhusu uandaaji wa mtaala unaohusu masomo ya uigizaji, filamu, ngoma, DJ, sarakasi, muziki na uchoraji ili kupata ithibati ya VETA. Rasimu ya mtaala huo imewasilishwa VETA kwa ajili ya kupata maoni ya kitaalamu ili kukamilisha kazi hiyo. Aidha, ili kuwezesha utambuzi wa vyanzo vya mapato yatokanayo na utamaduni unaoshikika na usioshikika, TaSUBa iliendesha semina ya siku Tano (5) kwa maafisa utamaduni toka halmashauri Kumi na Tano (15) za Bagamoyo, Mkuranga, Igunga, Uyui, Arumeru, Mbinga, Mtwara–Mikindani, Njombe, Ifakara Sumbawanga, Kaliua, Mpanda, Kishapu, Tabora na Nanyumbu. Vilevile, ikiwa ni hatua ya kuendeleza ushirikiano na wadau wa Sanaa wa nje ya nchi, katika kipindi hiki TaSUBa ilishirikiana na vikundi pamoja na vyuo mbalimbali kutoka nje ya nchi kama vile HiOA (Sweden), Zulker (Marekani), Jean Performance Troupe (China), ASEDA (Ujerumani), St Sig-frids Folk High School (Sweden), Finn Threartre Works (Ujerumani) na wengine wengi.

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, TaSUBa kupitia mradi wa Ukarabati wa Chuo cha Sanaa Bagamoyo

ilinunua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwenye maeneo ya teknolojia ya sauti, muziki, ubunifu pamoja na uzalishaji wa picha jongevu. Vifaa hivi vimegharimu Shilingi millioni 100. Aidha, TaSUBa imepokea msaada wa vifaa vingine vya kufundishia (ala za muziki, vyombo vya sauti, kompyuta, kabati za kuhifadhia vifaa) vyenye jumla ya thamani ya Shilingi milioni 100 kutoka Serikali ya Denmark. Kupatikana kwa vifaa hivi kutaongeza tija katika utoaji wa mafunzo katika Taasisi hiyo kwa kuimarisha utoaji wa mafunzo kwa vitendo.

**Sekta ya Maendeleo ya Michezo**

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** michezo ni nyenzo muhimu katika kuzalisha ajira na kukuza pato la Taifa, kuimarisha afya, kulitangaza Taifa na kuliongezea heshima nje ya Nchi pamoja na kuimarisha umoja, undugu, uelewano, mshikamano na ushirikiano ndani na nje ya Nchi. Michezo inatumika pia kama nyenzo ya kuelimisha jamii katika masuala mbalimbali ikiwemo masuala ya afya, elimu na utunzaji wa mazingira na inatumika pia katika kuimarisha vivutio vya utalii.

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2016/2017, Wizara ilikamilisha maandalizi ya Rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Michezo ikiwa ni hatua ya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995. Rasimu hiyo ilijadiliwa katika ngazi za awali za kuidhinishwa na Serikali na kutolewa maoni mbalimbali yanayohitaji kuzingatiwa ambapo Wizara inaendelea kuzingatia maoni hayo. Kukamilika kwa mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995 kutawezesha pamoja na mambo mengine, kuifanyia marekebisho Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa Na. 12 ya Mwaka 1967 na marekebisho yake Na. 6 ya Mwaka 1971 ili iendane na mahitaji ya sasa.

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** hatua hizi tunazichukua kuondokana na udhaifu tuliokuwa nao kwa muda mrefu wa kutegemea mafanikio bila kujenga mazingira stahili ya mafanikio. Miaka zaidi ya 30 sasa imepita toka Tanzania ing'are kimataifa katika medani za riadha kupitia

wanariadha wake mashuhuri wakati huo, wakiwemo Francis Naali, Samson Ramadhan, Gidamis Shahanga, Juma Ikangaa, Suleiman Nyambui na Filbert Bayi ambaye aliweka rekodi mpya ya dunia katika mbio za mita 1,500 mwaka 1974 huko Christchurch, New Zealand. Siyo kwenye riadha peke yake, bali vilevile kwenye michezo mingine ukiwemo mpira wa miguu ambapo kwa kiasi kikubwa tulipotea kwenye ramani ya michezo duniani. Kwa mfano, ni miaka 37 imepita tangu nchi yetu ifanikiwe kufika ngazi ya nusu fainali za AFCON: mara zote tunaishia raundi ya kwanza au ya pili. Sababu ni ileile niliyoelezea awali: matarajio ya mafanikio bila kujenga mazingira stahili ya mafanikio. Sasa tumefungua ukurasa mpya.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2016/2017, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika michezo mbalimbali. Michezo hiyo ni pamoja na mashindano ya Olimpiki yaliyofanyika Rio de Janeiro, Brazil (Agosti, 2016) ambapo Tanzania iliwakilishwa na wachezaji saba (7) wa riadha, kuogelea na judo. Mwanariadha Alphonce Simbu aliweza kushika nafasi ya Tano (5) katika mashindano hayo kwa upande wa mbio ndefu. Mapema mwaka huu, Simbu aliweza kushinda na kupata medali ya dhahabu kwenye mashindano ya Mumbai Marathon, India. Matokeo hayo ni matunda ya maandalizi na mazoezi ya kutosha kwa ufadhili wa Kampuni ya MultiChoice Tanzania ambayo naipongeza sana.

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, mwanariadha Cecilia Ginoka Panga alikuwa mshindi wa kwanza kwenye mashindano ya Beijing International Half Marathon yaliyofanyika tarehe 16 Aprili, 2017. Pia, mwanariadha mwingine Bi. Magdalena Crispin Shauri alikuwa mshindi wa Tano katika mashindano ya Hamburg Marathon yaliyofanyika tarehe 23 Aprili, 2017 yakijumuisha washiriki zaidi ya 25,000 na kuvunja rekodi yake binafsi. Aidha, Emmanuel Giniki Gisamoda alikuwa mshindi wa kwanza kwenye Shanghai International Half Marathon yaliyofanyika tarehe 23 Aprili, 2017. Wizara inaipongeza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa kwa kuibua na kuendeleza vipaji vya michezo nchini kwani wanariadha wote hao Wanne wapo JKT.

**72. *Mheshimiwa Spika,*** mafanikio yalianza kujitokeza vilevile kwa upande wa mpira wa miguu ambapo Timu ya Taifa ya Vijana ya Mpira wa Miguu, Serengeti Boys, ilifuzu kucheza fainali za michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) kwa vijana wenye umri chini ya miaka 17 itakayofanyika Gabon, Mei, 2017. Serengeti Boys, mbali na kufuta historia hasi tuliyokuwa nayo ya miaka 37 ya timu zetu kushindwa kufika nusu fainali za AFCON, imeonyesha weledi, nidhamu na uzalendo wa kujituma wa hali ya juu ambavyo vimeiwezesha timu hii kuzibwaga timu za U-17 toka nchi maarufu kisoka duniani zikiwemo: Misri, Ghana, Gabon, India na Malaysia.

Timu hii imeundwa kutokana na vijana waliooneshа kipaji kikubwa kwenye mashindano ya UMISSETA, UMITASHUMTA, Copa Coca-Cola na Airtel Rising Stars miaka 2 iliyopita na tutaendelea kuilea ili iwakilishe nchi kwenye mashindano ya Olympic ya mwaka 2020 kwa wachezaji wenye umri chini ya miaka 23. Aidha, kwa kuwa mwaka 2019 Tanzania itakuwa mwenyeji wa Mashindano ya AFCON ya U-17, tayari TFF kwa kushirikiana na Wizara imeandaa timu maalum inayotokana na mashindano ya U-13 miaka 2 iliyopita ambayo inaendelea kuimarishwa kwenye moja ya "*Sports Academies*" hapa nchini.

**73. *Mheshimiwa Spika,*** tumeanza maandalizi ya michezo ya UMISSETA na UMITASHUMTA ambayo Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI, itakuwa wima kuangalia vijana wenye vipaji katika michezo mbalimbali ambao baadaye watahamishiwa kwenye shule teule 56 za kulea vipaji hivyo katika michezo. Mbali na mikakati hiyo, TFF inaandaa vituo vya ufundi vitakavyokuwa na vifaa stahiki kila mkoa kwa madhumuni ya kulea vipaji kwa njia ya mazoezi. Itapendeza sana ikiwa kila Mbunge atahakikisha kuwa katika jimbo lake vilevile kuna angalau kituo kimoja cha aina hiyo na vifaa stahili. Naomba kutumia fursa hii kuwaomba wazazi nchini kuruhusu watoto wote bila kuwabagua kushiriki kwenye sanaa na michezo mbalimbali, kwani michezo siyo tu ni afya bali vilevile ni ajira, tena ajira ya uhakika kwelikweli.

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kuhimiza maandalizi ya kutosha kwa Timu zetu zitakazoshiriki katika mashindano ya Jumuiya ya Madola ya mwaka 2018, Serikali kupitia mahusiano ya diplomasia ya michezo inaendelea na mazungumzo na nchi za China, Cuba na Ethiopia ili kuwapeleka baadhi ya wanamichezo wetu kufanya mazoezi kwa michezo ya Riadha, Ngumi na Mpira wa Meza katika nchi hizo. Ni matumaini yetu kuwa mazungumzo yatakapokamilika timu zitakwenda katika nchi hizo ili kujiimarisha kwa ajili ya kushiriki katika mashindano hayo.

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa tunakuwa na miundombinu bora ya michezo na yenye hadhi ya Kimataifa, Serikali inaendelea kushirikiana na Wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi ili kuboresha iliyopo na kujenga miundombinu mipya. Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Morocco imeanza taratibu za ujenzi wa eneo changamani la michezo katika eneo la Nala Mkoani Dodoma lenye ukubwa wa ekari 150. Kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, zimeundwa Kamati mbalimbali za Wadau wa mradi huo pamoja na Wataalam kwa ajili ya pamoja na mambo mengine, kuandaa wananchi na eneo husika la mradi huo. Aidha, Wataalam kutoka Morocco wameshatembelea eneo husika na kupata taarifa muhimu kwa ajili ya tathmini na makadirio ya gharama za utekelezaji wa mradi huo.

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake za kuimarisha michezo nchini kwani mradi huu ni matokeo ya ushirikiano mzuri baina yake na Mfalme wa Morocco.

**77.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kimeendelea kuendesha mafunzo ya Stashahada ya ufundishaji michezo na utawala wa michezo ambapo jumla ya wanachuo 97 wanaendelea na mafunzo ya Stashahada za fani mbalimbali za michezo. Aidha, Chuo kimetoa mafunzo ya wiki mbili yanayohusu

Ufundishaji, Uongozi na Utawala wa Michezo kwa Walimu wa Shule za msingi na Sekondari. Ili kuibua na kukuza vipaji vya michezo mbalimbali, Wizara na Ofisi ya Rais, TAMISEMI tupo katika mazungumzo ya kuhakikisha kuwa Chuo hiki kinaboreshwa na walimu wa michezo wanakwenda kupatiwa elimu stahiki ya michezo ili wawe chachu ya maendeleo ya michezo katika nchi yetu.

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Wizara iliendelea na kazi ya Usajili, ambapo hadi mwezi Machi, 2017 jumla ya Vyama, Vilabu na Vituo vya Michezo 258 vilisajiliwa katika kipindi hiki. Usajili huu unaviwezesha Vyama na Vilabu vya Michezo kutambulika na kuendesha shughuli zao kwa mujibu wa Sheria za nchi.

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ufanisi na tija katika ukusanyaji wa mapato yatokanayo na michezo, Wizara imekamilisha ujenzi wa mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato yatokanayo na viingilio katika Uwanja wa Taifa na Uwanja wa Uhuru. Mfumo huu pamoja na kulenga kupunguza upotevu wa mapato ya Serikali yatokanayo na viingilio katika viwanja hivyo, unaimarisha pia uwazi katika mgawanyo wa mapato hayo. Ni matumaini ya Wizara kuwa wamiliki wa viwanja vingine wataiga mfumo huu ili kuongeza ufanisi na uwazi katika ukusanyaji wa mapato yatokanayo na viingilio katika viwanja hivyo. Katika mwaka 2016/2017 Wizara imeendeleza mahusiano mema ndani na nje ya nchi ili kutafuta washirika wa maendeleo kwa ajili ya ugharamiaji wa shughuli mbalimbali za Maendeleo ya Michezo.

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, Wadau mbalimbali na wananchi kwa ujumla kwa kuchangia Timu yetu ya Serengeti Boys ili iweze kufanya vizuri katika fainali za kombe la U-17 la AFCON na hatimaye kupata nafasi ya kushiriki Kombe la Dunia nchini India Mwezi Novemba, 2017. Aidha, natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge, wadau, mbalimbali na Watanzania wote kwa ujumla kuendelea kuichangia Timu yetu kwa hali na mali.

Katika kufanikisha azma hii wizara imeunda Kamati ya watu Kumi (10) inayoongozwa na Mtangazaji Nguli nchini Bw. Charles Hilary kwa ajili ya kuhamasisha wananchi kuiunga mkono Timu hii. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na TFF imefungua akaunti maalum iitwayo "TFF Football Development Fund No. 0086628003, Diamond Trust Bank" kwa ajili ya kuchangia timu yetu ya Serengeti Boys.

Napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim M. Majaliwa kwa mchango wao mkubwa katika suala hili.

**Baraza la Michezo la Taifa (BMT)**

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017 Baraza la Michezo la Taifa (BMT) liliendesha semina kwa maafisa michezo 49 wa Mikoa na Wilaya kutoka Mikoa ya Dar- es-salaam, Mtwara, Pwani, Morogoro, Lindi, Tanga, Singida, Dodoma, Manyara, Arusha na Kilimanjaro. Mafunzo haya yalilenga kuwajengea uwezo wa kusimamia utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Michezo, Sheria ya BMT na uratibu wa shughuli za michezo katika maeneo yao. Aidha, Baraza liliandaa mkutano wa wadau wa Michezo ambao ulibainisha upungufu uliopo katika Sheria ya BMT unaoifanya Sheria hiyo kutoendana na mahitaji ya sasa ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Baraza pia limeendelea kupokea maoni ya wadau mbalimbali wa michezo kuhusu maeneo yanayohitaji kuboreshwa katika Sheria ya BMT ili Sera itakapokamilika Sheria hiyo iweze kuhuishwa mapema.

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2016/2017 BMT ilisimamia chaguzi za vyama vya michezo vitano. Vyama hivyo ni Chama cha Judo Tanzania (JATA), Chama cha Riadha Tanzania (RT), Kamati ya Olimpiki Tanzania (TOC), Chama cha Mashua Tanzania (TSA) na Chama cha Tenisi Tanzania (TTA). Aidha, BMT iliendelea kuhamasisha ushiriki wa wanawake na watu wenye ulemavu katika michezo na kugombea nafasi mbalimbali za uongozi wa Vyama na

Mashirikisho ya Michezo. Katika vyama vya Michezo Vitano (5) vilivyofanya uchaguzi kwa mwaka 2016/2017, Wanawake 13 walijitokeza kugombea nafasi mbalimbali na kati yao 11 walishinda. Aidha, Baraza linaendelea kuimarisha Chama cha Michezo cha Wanawake ambacho kitakuwa na jukumu la kusimamia, kuhamasisha na kuratibu ushiriki wa wanawake kwenye michezo.

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** ikiwa ni hatua ya kuimarisha utendaji wa Vyama vya Michezo na kupunguza migogoro katika tasnia ya michezo nchini, BMT iliendesha mikutano na wadau wa Michezo na viongozi wa vyama vya michezo katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Kilimanjaro, Manyara na Lindi. Aidha, BMT iliendelea kuhamasisha vyama na wadau mbalimbali wa michezo kuibua na kuwaendeleza wachezaji ili kufanya vizuri katika mashindano ya kimataifa na kuliletea sifa Taifa letu.

Katika mwaka 2016/2017 Timu ya Taifa ya Wanawake chini ya miaka 20 (Kilimanjaro Queens) ilishinda na kutwaa Kikombe cha Afrika Mashariki na Kati. Aidha, kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu, katika kipindi hiki kulifanyika Ligi Kuu ya Mpira wa Miguu ya Wanawake iliyohusisha timu 12 kutoka Mikoa 12 ya Tanzania Bara ambapo timu ya Mlandizi Queens iliibuka bingwa wa Ligi hiyo. Napenda kutumia fursa hii kumshukuru mlezi wa Timu hiyo Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mbunge wa Kuteuliwa kwa kuiwezesha Timu hiyo kufikia mafanikio hayo. Aidha, natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wengine kuiga mfano huo ili kuinua viwango vya michezo nchini.

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** BMT iliendelea kuhamasisha na kutoa elimu ya kupinga matumizi ya madawa ya kusisimua misuli michezoni. Kwa kushirikiana na UNESCO, Baraza limeendesha Tamasha la Kupinga Matumizi ya Madawa ya Kusisimua Misuli Michezoni ambalo lilifanyika Uwanja wa Taifa tarehe 18 Februari 2017 na kuhudhuriwa na wanafunzi kutoka shule 12 za Sekondari na Msingi za Wilaya ya Temeke na wadau wengine wa michezo.

**Utawala na Rasilimaliwatu**

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua ya kuimarisha utendaji wa watumishi, mwaka 2016/2017 Wizara iliwezesha watumishi 19 kuhudhuria mafunzo mbalimbali ya muda mrefu. Aidha, Wizara imeendelea kuimarisha Utawala Bora kwa kuwashirikisha Watumishi katika maamuzi mbalimbali sehemu za kazi ambapo vikao mbalimbali vya Watumishi wa Wizara vilifanyika na kutoa fursa kwa Watumishi kuchangia katika kuboresha na kuimarisha utendaji kazi.

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, Wizara iliendelea na juhudi za kupambana na maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) mahala pa kazi, kwa kutoa huduma ya lishe kwa watumishi waliojitokeza kuwa na VVU/UKIMWI. Aidha, Wizara imeendelea kuhamasisha watumishi kujitokeza kwa ajili ya kupima afya zao na hivyo kuwezesha wale watakaobainika kuwa na mahitaji kuweza hudumiwa kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

**C3. CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA**

**87.** ***Mheshimiwa Spika*****,** pamoja na mafanikio yaliyofikiwa katika mwaka 2016/2017, katika kipindi hicho Wizara ilikabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo na hatua zilizochukuliwa ni kama ifuatavyo:

a) Sera na Sheria za Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo kutokidhi mahitaji ya sasa. Kama ilivyobainishwa awali, Wizara inafanya mapitia ya Sera na Sheria husika ili kukabiliana na changamoto hii.

b) Kutozingatiwa kwa maadili ya uandishi wa habari na utangazaji kwa baadhi ya vyombo Vyombo vya Habari. Kama ilivyobainishwa katika Hotuba hii, Wizara iliendelea kutoa elimu kuhusu uzingatiwaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia Sekta ya Habari na Utangazaji

pamoja na kukutana na Vyombo husika kwa majadiliano na mashauriano.

c) Uchakavu wa mitambo ya Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC). Katika hatua ya kuimarisha mitambo ya TBC ili iendane na teknolojia ya kisasa katika Sekta ya Utangazaji, Serikali imeendelea kuongeza bajeti ya Maendeleo ya Shirika hilo na kufikia Sh. 3,000,000,000 ikiwa ni ongezeko la Sh. 2,000,000,000. Aidha, ili kuimarisha zaidi uwezo wa TBC wa kugharamia uendeshaji na uwekezaji katika Teknolojia ya Utangazaji na vilevile kuzifikia Wilaya takribani 84 ambazo hazipati matangazo ya TBC kikamilifu, TBC imewasilisha Serikalini ombi la kupatiwa chanzo cha mapato kwa njia ya Tozo kwenye visimbuzi, utaratibu ambao unatumika katika nchi nyingi Duniani.

d) Kuwepo kwa mmomonyoko wa maadili miongoni mwa jamii kutokana na mambo mengine, kutozingatiwa kwa malezi na makuzi ya asili ya kitanzania, kutozingatia mila na desturi za mtanzania na athari za utandawazi. Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kutoa elimu kuhusu uzingatiaji wa maadili ya mtanzania pamoja na kuwa na mjadala kuhusu maadili kupitia Programu ya Wadau Tuzungumze. Wizara inatoa wito kwa Watanzania kuendelea kuenzi mila, desturi na tamaduni zetu chanya kwani Taifa lisilo na utamaduni wake ni kama Taifa mfu.

e) Wadau wa tasnia ya Sanaa kutozingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za kuendesha shughuli za Sanaa nchini. Wizara kwa kushirikina na taasisi zake inaendelea kuwaelimisha wadau kupitia njia mbalimbali zikiwemo warsha na mikutano mbalimbali. Mathalan Bodi ya Filamu Tanzania inaendelea kuendesha warsha kwa wadau wa Filamu. Vilevile, Baraza la Sanaa la Taifa kupitia Jukwaa la Wasanii linaelimisha wasanii watambue umuhimu wao katika maendeleo ya Jamii na wajibu wao kuzingatia weledi.

f) Eneo la Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo kumegwa na bahari. Taasisi ya Sanaa na

Utamaduni Bagamoyo iliandaa Andiko lililoelezea changamoto hiyo na kuomba msaada wa Kitaalam kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais–Mazingira. Aidha, Wataalam kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira wametembelea eneo hilo na kufanya tathmini ya kitaalam na taarifa ya tathmini hiyo imewasilishwa Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira. Taarifa hiyo inabaisha gharama za kutatua changamoto hiyo ambazo ni Shilingi Milioni 138. Taasisi kwa sasa inaendelea kutafuta wafadhili kwa ajili ya kutekeleza mapendekezo ya Taarifa ya Wataalam.

g) Mwamko na uelewa mdogo wa umuhimu wa jamii kushiriki kwenye Michezo. BMT inaendelea kuhamasisha jamii kushiriki katika michezo mbalimbali ili kujenga na kuimarisha afya zao kupitia mabonanza na matamasha ya Michezo na uratibu wa mazoezi kila Jumamosi ya pili ya kila mwezi. Wizara inatoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kuhamasisha Wananchi katika maeneo yao kushiriki kikamilifu katika shughuli za michezo ili pamoja na mambo mengine kujenga na kuimarisha afya zao. Nichukuwe fursa hii kumshukuru Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake za kuhamasisha Wananchi kushiriki kikamilifu katika mazoezi ya viungo na michezo kwa ajili ya pamoja na mambo mengine, kuimarisha afya zetu.

## D. MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### Sekta ya Habari na Utangazaji

***88. Mheshimiwa Spika*,** Wizara katika mwaka 2017/2018 itatekeleza yafuatayo: kuendelea kuwa Msemaji Mkuu wa Serikali katika utekelezaji wa Sera, Sheria, Mikakati, Programu na Miradi mbalimbali ya Maendeleo; kuratibu Vitengo vya Mawasiliano Serikalini ikiwa ni pamoja na kufuatilia na kutathmini utendaji wa Maafisa Mawasiliano Serikalini katika Wizara, Wakala na Idara za Serikali zinazojitegemea, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za Umma kwa lengo la kuimarisha Vitengo

hivyo; na kusimamia utekelezaji wa Sheria Na. 12 ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 na Kanuni zake. Aidha, Wizara itaendelea kuwa kiungo muhimu cha mtiririko wa habari nchini kwa kuratibu na kusimamia njia mbalimbali za upashanaji habari.

**Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)**

***89. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018 TBC itakarabati studio za Redio na Televisheni za Mkoani Dodoma na Dar es Salaam; itanunua vifaa vya utangazaji wa redio na televisheni; itaongeza ubora wa studio na mitambo na kununua vitendea kazi muhimu kwa ajili ya shughuli za utangazaji na ufundi.

**Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN)**

***90. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) itatekeleza majukumu yafuatayo: kuimarisha ubora wa bidhaa na huduma inayotolewanaKampuni kwakutumiamikakati na mbinu za kisasa pamoja na teknolojia bora ili kumudu ushindani katika soko; kuimarisha utendaji kazi wa rasilimaliwatu kwa kuboresha miundombinu, vitendea kazi, na kuimarisha Kanuni, Sera na Taratibu za utendaji kazi ili kuongeza motisha, uwajibikaji na ufanisi na ushindani wa Kampuni katika soko na kujenga na kuimarisha uhusiano na ushirikiano na wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa maendeleo na ustawi wa Kampuni na Taifa kwa ujumla. Aidha, Kampuni itaendelea kuboresha utawala bora kwa kuongeza uwazi katika uendeshaji wake na kukuza lugha ya Kiswahili ndani na nje ya nchi kwa kutumia gazeti la Habari Leo.

**Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)**

***91. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania(TCRA) itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria na Kanuni za Utangazaji kwa kuhamasisha utengenezaji na uzalishaji *(content creation and*

*production)* wa maudhui ya ndani; kukamilisha zoezi la kutoa mafunzo kwa wakalimani wa lugha ya alama kutoka kwenye vituo vya televisheni na kukamilisha mwongozo wa udhamini wa matangazo ya Biashara *(Code of advertisement and sponsorship)* kwa vituo vya utangazaji. Aidha, TCRA itakamilisha Waraka wa mashauriano na wadau wa jinsi ya kuanzisha utangazaji wa Redio unaotumia mfumo wa dijitali *(Digital Sound Broadcasting);* na kushauriana na wadau kuhusu vigezo vya kupata kituo bora cha utangazaji, kipindi bora na mtangazaji bora kwa kila mwaka. TCRA itaendelea pia kutoa elimu na mafunzo kwa vituo vya utangazaji ili kuhakikisha weledi wa kutayarisha na kutoa habari unazingatiwa.

### Sekta ya Maendeleo ya Utamaduni

***92. Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia ukusanyaji, uorodheshaji na usambazaji wa kumbukumbu za historia na urithi wa utamaduni; kuratibu mjadala wa kitaifa unaohusu maadili na uzalendo; kuhuisha Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997 na kuandaa Sera ya Lugha ya Taifa; kufanya utafiti wa mila na desturi za jamii za Kitanzania kwa lengo la kuweka kumbukumbu, kuhifadhi, kulinda, kuenzi na kuziendeleza na kufanya utafiti na kuhifadhi lugha za kijamii na kukuza misamiati ya lugha ya Kiswahili. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha na kutekeleza makubaliano mbalimbali ya ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa katika nyanja ya utamaduni pamoja na kuratibu maadhimisho, makongomano, matamasha na mikutano ya Kitaifa na Kimataifa kuhusu Lugha na Utamaduni.

### Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA)

***93. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) litaandaa vipindi 52 vya lugha ya Taifa kupitia redio ya TBC$_{\text{Taifa}}$ na Clouds, vipindi 52 vya Kumepambazuka kupitia redio 1 One na vipindi 52 vya Ulimwengu wa Kiswahili kupitia televisheni ya TBC . Aidha, Baraza litatoa huduma ya tafsiri kwa Asasi za Serikali,

Mashirika ya Umma na ya binafsi pamoja na watu binafsi na kujenga uwezo polepole wa ukalimani kutoka lugha ya Kiswahili kwenda lugha mbalimbali za kigeni na lugha za kigeni kwenda Kiswahili; kutoa ithibati ya vitabu vya kiada na ziada pamoja na kuchapisha vitabu na majarida ya Kiswahili na kusanifisha Istilahi 300 mpya. Vilevile, BAKITA itakusanya matini andishi ya Kiswahili yenye jumla ya maneno milioni mbili na kuyaingiza kwenye mfumo wa kusomeka kikompyuta. Baraza pia litafanya Kongamano la kuadhimisha miaka 50 ya BAKITA.

**Sekta ya Maendeleo ya Sanaa**

***94. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kukamilisha uandaaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Sanaa na Mfuko wa Maendeleo ya Sanaa na Ubunifu pamoja na kuratibu mikutano na matamasha mbalimbali ya kitaifa na kimataifa kuhusu masuala ya Sanaa na Ubunifu. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji itafanya mapitio ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya mwaka 1999 na Kanuni zake ili kuimarisha utendaji wa COSOTA na kuboresha haki za wadau hususani wa sekta ya Sanaa.

**Bodi ya Filamu Tanzania**

***95. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Bodi ya Filamu imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo: kukamilisha Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Filamu; Kuhuisha Mpango Mkakati wa Bodi ya Filamu; kupitia miswada 205 ya kutengeneza filamu, makala za filamu na michezo ya kuigiza na kutoa vibali kwa watayarishaji na wapiga picha za filamu wa ndani na nje ya nchi; kununua eneo Mkoani Dodoma kwa ajili ya Ofisi za Bodi; kuhakiki kazi za filamu 1,000, kuzipangia madaraja na kuzitolea vibali; kuwajengea uwezo wanatasnia wa filamu, vyombo vya wadau (Shirikisho na Vyama) kwa kuendesha warsha, vikao na mijadala katika Mikoa yote nchini kwa awamu hadi ifikapo mwaka 2020.

*96. Mheshimiwa Spika,* majukumu mengine yatakayotekelezwa na Bodi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, ni pamoja na: kuendelea kubaini na kuwachukulia hatua wamiliki wa mitambo ya kutengeneza kazi za filamu zinazoingia sokoni kinyume na Sheria; kuendelea kubaini makampuni ya filamu, studio na watendaji katika sekta ya filamu na kuwapa leseni za uendeshaji na vitambulisho vya ithibati pamoja na kuhuisha torwi; kuendelea kubainisha na kurasimisha vibanda 5,000 vya filamu; kusimamia majumba ya sinema 15 na kufanya ukaguzi wa majumba hayo; kuendelea kuimarisha urasimishaji wa Sekta ya Filamu; Kutoa Elimu kuhusu masuala ya Sekta; kuhamasisha wadau kushiriki matamasha, tuzo na maonesho ya bidhaa za filamu kitaifa, kikanda na kimataifa; kuratibu na kuendesha tuzo moja ya Kitaifa pamoja na kuendelea kuimarisha Bodi kwa kununua vifaa vya kiufundi na vitendea kazi vingine muhimu. Aidha, Bodi itaanza kutengeneza ramani ya masuala ya filamu *(film sector mapping),* kufanya tafiti, tathmini na ufuatiliaji. Vilevile, Bodi itafanya marekebisho ya Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza Na. 4 ya Mwaka 1976.

**Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA)**

***97. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, BASATA itaendelea kuboresha ubunifu, kuibua na kukuza vipaji na kufanya tafiti mbalimbali za Sanaa; kukuza soko la kazi za sanaa na kuwawezesha wasanii kutumia fursa za mitandao na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika kazi zao; kutambulisha na kuitangaza sekta ya sanaa kwa kuendesha matamasha, maonesho na maadhimisho ya Sanaa na kuhuisha na kuboresha Sheria Na. 23 ya mwaka 1984 iliyoanzisha BASATA. Aidha, Baraza litaendelea kuboresha, kuimarisha na kuongeza vyanzo vya mapato yake pamoja na kudhibiti, kusimamia na kuboresha maadili katika sekta ya Sanaa.

**Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa)**

***98. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, TaSUBa itatekeleza majukumu yafuatayo: kuandaa wakuzaji

wa sanaa, wasanii waendeshaji na wasimamizi wa shughuli za sanaa kwa sekta za umma na binafsi; kuandaa watafiti na washauri wa sanaa kwa ngazi ya taifa na kimataifa; kukuza viwango vya sanaa na moyo wa kupenda mila na desturi za Mtanzania; na kukuza mwamko wa matumizi ya sanaa katika mapambano ya matatizo mbalimbali kama vile kukabiliana na umasikini, maradhi, rushwa, uharibifu wa mazingira, unyanyasaji wa jinsia na watoto.

**Sekta ya Maendeleo ya Michezo**

***99. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kusimamia maendeleo ya michezo nchini; kuboresha mfumo wa usimamizi wa Vyama vya Michezo nchini ikiwa ni pamoja na kuhuisha Sera ya Michezo na Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa No. 12 ya Mwaka 1967 na marekebisho yake Na. 6 ya Mwaka 1971 pamoja na kuratibu ushiriki wa timu za Taifa katika Michezo ya Jumuiya ya Madola inayotarajiwa kufanyika nchini Australia mwezi Aprili, 2018. Aidha, Wizara itaendelea na maandalizi ya kuwa mwenyeji wa Mashindano ya Mpira wa Miguu (AFCON 2019) kwa vijana wenye umri chini ya miaka 17. Vilevile, Chuo cha Michezo Malya kitaendelea kudahili wanafunzi na kuendesha mafunzo ya utaalamu wa fani mbalimbali za michezo. Wizara pia itaendelea kutoa huduma ya Kinga na Tiba kwa Wanamichezo na kuboresha mifumo ya usimamizi wa Sekta ya Michezo nchini pamoja na kuboresha miundombinu ya michezo.

***100. Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha utalii wa michezo na vilevile kuvitangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini, mwaka 2017/2018 Wizara kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki itahakikisha inawasiliana na Balozi zetu zilizopo nchini Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Italia, Uholanzi, Ubelgiji, Urusi, China, Japan, Jamhuri ya Korea, Canada na Marekani kwa lengo la kuzikaribisha Klabu kubwa za mpira wa miguu za nchi hizo kuja nchini ili kutumia miundombinu yetu ya kisasa ya michezo na kutembelea vivutio mbalimbali vya utalii tulivyo navyo. Tayari tuna uzoefu wa ziara ya wachezaji wa Kimataifa

Wastaafu wa timu ya mpira wa miguu ya Real Madrid ya Hispania ambao walicheza na wachezaji wastaafu wa Timu yetu ya Taifa, jijini Dar es Salaam mwaka 2014 na kupata fursa ya kutembelea vivutio vyetu vya utalii.

Ziara ya Timu hiyo ilitangazwa dunia nzima kupitia vyombo mbalimbali vya Habari ikiwa ni pamoja na CNN, BBC na Supersport. Aidha, moja ya Timu kubwa iliyoko kwenye ligi Kuu ya Uingereza, Everton FC inatarajiwa kuja nchini mwezi Julai, 2017 kwa lengo la kucheza mechi moja ya Kimataifa ya Kirafiki na moja ya timu zetu Kongwe zinazocheza Ligi Kuu nchini na kutembelea vivutio vyetu vya Utalii. Dhamira ya Evaton FC ni kucheza na timu itakayoshinda katika mechi maalum ya kirafiki kati ya klabu ya Yanga na Simba. Ujumbe wa Timu hiyo umeshakuja Tanzania mara mbili ndani ya mwaka huu, mara ya kwanza kujadiliana na Wizara na kukagua uwanja wa Taifa na miundombinu yake na mara ya pili kujiridhisha kuhusu ubora wa nyasi za uwanja huo.

**Baraza la Michezo la Taifa (BMT)**

***101. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, BMT itatekeleza majukumu yafuatayo kuendeleza Mpango wa Michezo kwa jamii kwa kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa walimu wa shule za Msingi na Sekondari; kuhamasisha ushiriki wa jamii katika michezo mbalimbali ili kujenga na kuimarisha afya zao na kuratibu zoezi la ushiriki wa Wananchi katika mazoezi ya kila Jumamosi ya pili ya kila mwezi ili kuondokana na magonjwa yasiyoambukiza. BMT itaratibu chaguzi za vyama vya Michezo vitakavyofanya chaguzi kwa mujibu wa Katiba zao na kutekeleza programu za kuongeza ushiriki wa Wanawake na watu Wenye ulemavu katika Michezo; kuendesha mafunzo ya utawala bora katika michezo. Vilevile, BMT itatoa elimu kwa wadau juu ya athari za matumizi ya dawa na mbinu haramu za kuongeza nguvu michezoni.

**Utawala na Rasilimaliwatu**

***102. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara inatarajia kuajiri watumishi 60 na

kupandisha vyeo watumishi 108 ambao watatimiza vigezo kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za utumishi wa umma. Aidha, Wizara itaendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI ya mwaka 2001 pamoja na kukabiliana na magonjwa nyemelezi yasioambukiza kwa watumishi. Vilevile, Wizara itaendelea kuimarisha Utawala Bora kwa kuendesha vikao mbalimbali vya watumishi, kutoa elimu kwa watumishi juu ya kujiepusha na rushwa pamoja na kuboresha nyaraka mbalimbali ikiwa ni pamoja na Mkataba wa Huduma kwa Mteja. Wizara pia itaendelea kuwajengea uwezo watumishi ikiwa ni pamoja na kuimarisha mazingira ya utendaji kazi kwa kuwapatia vitendea kazi stahiki.

## E. MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### Mapato

***103. Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara kupitia Idara ya Habari-MAELEZO na Idara ya Maendeleo ya Michezo inakadiria kukusanya jumla ya Shilingi Milioni Mia Nane Hamsini na Tano, Mia Nane na Tano Elfu (Sh. 855, 805,000) kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali vya mapato ikiwa ni ongezeko la asilimia 4.4 ikilinganishwa na Shilingi Milioni Mia Nane Ishirini, na Elfu Tano (Sh. 820,005,000) ambayo ni makadirio ya mwaka 2016/2017.

***104. Mheshimiwa Spika*,** ni matarajio ya Wizara kuwa makusanyo haya yataongezeka zaidi mara baada ya kukamilika kwa taratibu za kuanzisha vyanzo vipya vya mapato kupitia Idara ya Habari –MAELEZO kufuatia kuanza kutekelezwa kwa Sheria ya Huduma za Habari Na.12 ya mwaka 2016 na Kanuni zake ambapo Shilingi Milioni Mia Saba Hamsini (Sh.750, 000,000) zinatarajiwa kukusanywa katika mwaka 2017/2018.

***105. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2017/2018, Taasisi zilizo chini ya Wizara zinatarajia kukusanya jumla ya Shilingi Bilioni Thelathini na Sita, Milioni

Mia Tisa Kumi na Mbili, Mia Tisa Thelathini na Tisa Elfu (Sh.36,912,939,000). Kiambatisho Na. IV kinabainisha makadirio ya makusanyo haya.

**Matumizi ya Kawaida**

***106. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2017/2018, Wizara imetengewa bajeti ya Shilingi Bilioni Ishirini na Moja, Milioni Mia Nane Tisini na Mbili, Mia Sita Tisini na Tano Elfu (Sh. 21,892,695,000) kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Matumizi Mengineyo na Mishahara). Fedha hizo zinajumuisha Mishahara ya Watumishi wa Wizara, Shilingi Bilioni Nne, Milioni Mia Tatu Themanini na Tisa, Mia Nane Sitini na Tisa Elfu (Sh. 4,389,869,000), Mishahara ya Taasisi zilizo chini ya Wizara Shilingi Bilioni Kumi na Mbili, Milioni Mia Nane Themanini na Sita, Mia Saba Arobaini na Saba Elfu (Sh. 12,886,747,000), Matumizi Mengineyo ya Wizara Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Nne na Tano, Mia Saba Themanini na Tatu Elfu (Sh. 3,405,783,000) na Matumizi Mengineyo ya Taasisi Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Mbili Kumi, Mia Mbili Tisini na Sita Elfu (Sh. 1,210,296,000). Mchanganuo wa makadirio ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara na Taasisi ni kama inavyoonekana katika *Kiambatisho Na. V*. Aidha, *Kiambatisho Na. VI* ni mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida kwa Wizara pekee yake na *Kiambatisho Na. VII* ni kwa upande wa Taasisi zilizo chini ya Wizara.

**Miradi ya Maendeleo**

***107. Mheshimiwa Spika*****,** katika Mwaka 2017/2018, Wizara imetengewa jumla ya Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Tatu Ishirini (Sh. 6,320,000,000) kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo mitatu, ambayo ni Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika, maandalizi ya awali ya Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dodoma na Upanuzi wa Usikivu TBC. Mchanganuo upo katika *Kiambatisho Na. VIII*.

## F. MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA KUTEKELEZA MPANGO WA MWAKA 2017/2018

***108. Mheshimiwa Spika,*** ili Wizara iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ya Mwaka wa Fedha 2017/

2018, naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi Bilioni Ishirini na Nane, Milioni Mia Mbili Kumi na Mbili, Mia Sita Tisini na Tano Elfu (Sh. 28,212,695,000) ambapo kati ya fedha hizo, Mishahara ni Shilingi Bilioni Kumi na Saba, Milioni Mia Mbili sabini na Sita, Mia Sita Kumi na Sita Elfu (Sh.17,276,616,000) na Matumizi Mengineyo Shilingi Bilioni Nne, Milioni Mia Sita Kumi na Sita, na Sabini na Tisa Elfu (Sh. 4,616,079,000) na Miradi ya Maendeleo ni Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Tatu Ishirini (Sh. 6,320,000,000). Mchanganuo wa bajeti ya fedha hizo upo katika viambatisho vilivyotajwa hapo awali ambavyo ni sehemu ya Hotuba hii.

## G. SHUKRANI

***109. Mheshimiwa Spika*,** Wadau mbalimbali wameshiriki katika kuiwezesha Wizara kufikia mafanikio mbalimbali katika mwaka 2016/2017 kama ilivyobainishwa awali. Napenda kutumia fursa hii kuwatambua na kuwashukuru baadhi ya Wadau hao kama ifuatavyo: Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, Finland, Uingereza, Denmark, Japan, Sweden, Norway, Jamhuri ya Kiislam ya Watu wa Iran, Cuba, Jamhuri ya Korea, India, Misri, Morocco, Uholanzi, Australia, Marekani na Ujerumani. Aidha, nayatambua na kushukuru Mashirika ya Kimataifa kama ifuatavyo: Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Japan (JICA), Shirika la Kazi Duniani (ILO), British Council na Umoja wa Ulaya (EU). Aidha, niwatambue na kuwashukuru washirika wote wa maendeleo wa ndani ambao ni pamoja na StarTimes (T), NMB Bank, CRDB Bank, Tanzania Breweries Limited (TBL), Serengeti Breweries Limited (SBL), TANESCO, TANAPA, NSSF, Multi Choice (T), AIRTEL, TiGo, Vodacom (T), Zantel, na wengine wengi.

***110. Mheshimiwa Spika*,** napenda kuwashukuru Wadau wa Wizara yangu wakiwemo Waandishi wa Habari, Wanautamaduni, Wasanii na Wanamichezo kwa mchango wao uliowezesha Wizara kutekeleza majukumu yake. Aidha,

ninaishukuru sana Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi "Press A" kwa kuchapa hotuba hii kwa wakati.

***111.*** ***Mheshimiwa Spika,*** nitoe tena shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya: **www.habari.go.tz**

***112.*** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii.

**MHE. JUMA S. NKAMIA (K. n. y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa fasili ya (7) (1)(a) ya Nyongeza ya Nane, imetaja majukumu ya Kamati ya Kisekta ikiwemo kushughulikia Bajeti ya Wizara. Aidha, Kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane (6)(5)(c) iliyo chini ya Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 Kamati imepewa jukumu la kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa

Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti za Wizara hii kwa mwaka wa fedha unaoishia ili kulinganisha kuhusu makadirio ya matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaohusika

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti na uzingatiwaji wa Maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Katika eneo hili Kamati itaeleza kuhusu namna ukusanyaji wa maduhuli ulivyokuwa, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati pamoja na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Fungu 96 ilipanga kukusanya sh. 820,005,000/=. Hadi kufikia Februari 2016 wizara imekusanya sh. 418,580,116 sawa na asilimia 51 ya makadirio ya makusanyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Idara ya Habari kwa makusanyo makubwa na ina imani kuwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 makadirio ya makusanyo kwa idara hii yataongezeka. Aidha, Kamati pia inatarajia kuwa asilimia 49 ya ukusanyaji wa maduhuri itakamilika ifikapo mwisho wa mwaka huu wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Upatikanaji wa Fedha Kutoka Hazina kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo iliidhinishiwa shilingi bilioni 20.326 ambapo kati ya fedha hizo shilingi bilioni 17.3 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Februari 2017, Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni 10.67 sawa na asilimia 52.48 ya bajeti hiyo. Kati ya fedha hizo, Wizara imepokea shilingi bilioni 10.4 sawa na asilimia 60 ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge, kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi milioni 190.32 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo ni sawa na asilimia 6.3 ya fedha

iliyoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Rejea kielelezo Namba mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Aprili 2017 Kamati ilijulishwa na Wizara kupitia Barua yenye Kumb. Na. CDA.7/238/01E/33 ya tarehe 12 Aprili, 2017, kuwa tayari Serikali imetoa kiasi cha shilingi bilioni tatu kwa Wizara hii. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni moja ni kwa ajili ya Mradi wa Maendeleo wa Upanuzi wa Usikivu –*TBC* ambazo zilikuwa zimeidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kiasi cha shilingi bilioni mbili ambacho hakikupangwa katika Bajeti ya Mwaka wa 2016/2017, kimetolewa kwa ajili ya kutatua changamoto mbalimbali zinazoikumba *TBC* ikiwemo kulipa malimbikizo ya madeni ya muda mrefu ya watoa huduma mbalimbali na wafanyakazi wa *TBC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha kwa *TBC* kwani Shirika hilo liko katika hali mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kama zilivyo Kamati nyingine za Kisekta, ilifanya ziara ya kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Miradi miwili kati ya sita ilikaguliwa, miradi ambayo ni pamoja na Mradi wa Upanuzi wa Usikivu wa *TBC* (Mradi Namba 4279).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitembelea mradi huu mnamo tarehe 16 Machi, 2017. Kabla ya kutembelea mradi huu Kamati ilitembelea kituo cha kurusha matangazo cha Azam ili kuweza kujionea hali ya uwekezaji iliyofanyika ili kuwa na picha halisi ya ulinganishi wakati wa kujadili suala la uwekezaji katika kituo cha kurushia matangazo cha Taifa cha *TBC*. Ziara hii iliwapa uelewa mpana Wajumbe wa Kamati na iliwajengea uwezo wa kujua ni nini iishauri Serikali na iwekeze kwa kiasi gani ili kuwa na tija katika Mradi wa Usikivu wa *TBC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ukweli kwamba *TBC* ndilo Shirika pekee la Taifa la Utangazaji nchini lakini Kamati iliona hali mbaya ya miundombinu na teknolojia kwa maana ya mitambo duni ya kurushia matangazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/2017, *TBC* ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni moja kwa ajili ya kuboresha usikivu kutokana na kukosekana kwa mawasiliano kwa takribani Wilaya 81 nchini. Hadi Kamati inatembelea *TBC* hakuna hata senti moja iliyokuwa imetolewa. Aidha, mnamo mwezi Aprili Kamati ikiwa imeshachambua bajeti ya Wizara hii ilipokea barua kutoka Wizara ya Habari ambayo tayari nimeshaelezea kuhusu utoaji wa shilingi bilioni tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Habari inahitaji uwekezaji kama ambavyo Azam *TV* ilivyofanya kwani imetumia takribani dola za kimarekani milioni arobaini ambayo ni sawa na shilingi bilioni tisini za Kitanzania. Aidha, kwa ajili ya kuondokana na hali duni ya shirika hili la *TBC*, *TCB* ilishawahi kuandaa andiko lenye kuonesha mahitaji muhimu ya kuweza kuinusuru, ambapo inakadiriwa zaidi ya shilingi bilioni 80 zinahitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Ukarabati wa Chuo cha Sanaa Bagamoyo. Tarehe 17 Machi, 2017, Kamati ilitembelea Chuo cha Sanaa Bagamoyo ili kukagua mradi tajwa. Katika taarifa yake, Mkurugenzi alieleza kuwa, mradi huu ulianza katika Mwaka wa Fedha 2010/2011 ukiwa na malengo makuu matatu ambayo ni kuimarisha miundombinu na vifaa ili kuboresha mazingira ya ufundishaji na kujifunza, kuimarisha miundombinu na vifaa ili kuboresha mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira yenyewe ni pamoja na mazingira ya utendaji kazi na kuimarisha miundombinu ili kulinda usalama wa wafanyakazi, wanachuo na mali za taasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makadirio ya miradi yalikuwa ni shilingi bilioni 8.54. Hata hivyo, tangu kipindi hicho mradi umekuwa ukipangiwa fedha chache ambazo pia zimekuwa hazitolewi. Kwa kipindi chote hicho cha miaka takribani sita mradi umetengewa shilingi bilioni 1.785 na hadi sasa fedha iliyotolewa ni shilingi milioni 100 kati ya shilingi milioni 300 zilizotengwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii imeisikitisha Kamati kwa kuwa inatambua thamani ya mradi huu kwa maendeleo ya Sekta ya Sanaa na Utamaduni nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni ya Jumla Kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo yafuatayo kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2015/2016:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kutoa shilingi bilioni moja kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Upanuzi wa Usikivu wa *TBC* mwezi April 2017 bado kiasi hiki ni kidogo. Serikali kama ina nia ya dhati ya kuiona *TBC* inafanya vizuri ni vyema sasa ikaamua kuwekeza kwa kutenga fedha za kutosha kama makampuni mingine yanavyofanya, ikiwemo AZAM**.** *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Chuo cha Sanaa Bagamoyo ni moja kati ya taasisi nyingine tatu zilizoteuliwa kuwa vituo vyenye ubora uliotukuka *(Centres of Excellence)* na hususan kwenye ufundishaji katika nyanja za utamaduni na sanaa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki *(East African Community Centre of Excellence in Culture and the Arts*) Serikali haina budi kutenga fedha za kutosha kwa taasisi hii ili iweze kutekeleza miradi yake ambayo inaendana na hadhi iliyopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati**.** Kuhusu utekelezaji wa maoni ya Kamati yaliyotolewa wakati wa uwasilishaji wa bajeti ya Wizara hii, Wizara imetekeleza kwa kiasi fulani na kwa yale ambayo

hayajatekeleza Kamati inaeleza na inaendelea kuiomba Serikali kuendelea kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Pili, Uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo inatarajia kukusanya sh. 855,000,000 ikiwa na nyongeza ya shilingi milioni 35.8 ya sh. 820,000,000 kilichokadiriwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017**.** Kati ya Fedha hizo sh. 147,000,000 ambayo ni sawa na asilimia 17 ni kutoka Idara ya Habari na sh. 708,000,000 ambayo ni sawasawa na asilimia 82 kutoka Idara ya Maendeleo ya Michezo kama inavyooneshwa kwenye kielelezo namba tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu yake**,** katika mwaka huu wa Fedha 2017/2018, Wizara inaomba kuidhinishiwa sh. 28,212,695,000/=. Kati ya fedha hizo matumizi ya kawaida ni sh. 21,892,695,000/= sawa na asilimia 71.1. Aidha, kwa upande wa miradi ya maendeleo sh. 6,320,000,000/= sawa na asilimia 28.8 zinaombwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi hiki cha fedha kinachoombwa ni sawa na nyongeza ya sh. 7,000,000,000 ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge katika mwaka wa fedha 2016/2017. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza bajeti ya Wizara hii na hususan miradi ya maendeleo ambayo imepata nyongeza ya shilingi bilioni 3.2 sawa na asilimia 52.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu; Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati. Naomba kuchukua nafasi hii kuwasilisha Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti, pamoja na Serikali kuongeza bajeti ya Wizara hii kwa asilimia 22, Kamati inaona bado bajeti ya Wizara hii haikidhi mahitaji na hususan fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo. Kamati inaishauri Serikali

kuhakikisha inaongeza Bajeti ya Wizara hii na inatoa fedha kwa wakati kama zilivyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Utangazaji la Tanzania *(TBC).* Sekta ya Habari inahitaji uwekezaji mkubwa ili kutoa matokeo chanya. *TBC* inafanya kazi kubwa, lakini kazi zake zinakwamishwa na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Aidha, kwa ajili ya kuondokana na hali duni ya shirika hili, *TBC* ilishawahi kuandika andiko lenye kuonesha mahitaji muhimu ya kuweza kulinusuru shirika ambapo fedha zinazohitajika inakadiriwa kuwa ni sh. 80,000,000,000. Kutokana na hali hii, kamati inashauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna imani Serikali ina nia ya dhati ya kuifanya *TBC* kuwa Shirika la Utangazaji la Taifa, hivyo, tunashauri basi iwekeze vya kutosha kwa kutenga bajeti nzuri ikiwa ni pamoja na kupeleka fedha za tozo za ving'amuzi *TBC* kama yanavyofanya mashirika mengine makubwa ya Utangazaji Duniani ikiwemo *BBC*, *VOA* na hata *DW*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imeshahamia Dodoma sasa na hivyo ile dhana ya Makao Makuu ya nchi ni Dodoma imeanza kuonekana; Kamati inashauri Serikali iiwezeshe *TBC* ili ijenge studio ya kisasa Dodoma kwani hali ya studio iliyopo sasa Dodoma ni mbaya na haiendani ya hadhi ya Makao Makuu ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBC* itumie maeneo yake ya Mwenge na Pugu kutafuta wabia wa kujenga majengo ya kisasa na kukodisha ili kuweza kuongeza kipato cha Shirika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Sanaa Bagamoyo (TaSuBa) ni moja kati ya miradi ambayo Kamati iliitembelea mnamo mwezi Machi 2017. Kwa ujumla hali ya taasisi hii siyo nzuri ikilinganishwa na hadhi yake ya kuwa taasisi yenye ubora

uliotukuka kwenye ufundishaji katika Nyanja za Utamaduni na Sanaa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (*East African Community Centre of Excellence in Culture and the Arts*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ulianza katika mwaka wa fedha 2010/2011 na ulipaswa kuwa umepokea jumla ya shilingi bilioni 1.78 zilizoidhinishwa na Bunge, hata hivyo ni shilingi milioni 100 tu sawa na asilimia 5.6

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imesikitishwa sana kuona kwa kipindi chote hiki, TaSuBa imepokea kiasi kidogo tu cha fedha. Kamati inaishauri Serikali kuangalia Taasisi hii kwa jicho la pekee na kuhakikisha inaitengea fedha za kutosha ili kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Kwa kuanzia, Kamati inaitaka Serikali kutoa kiasi cha shilingi milioni 200 kilichobaki kati ya shilingi milioni 300 zilizoidhinishwa na Bunge katika mwaka huu wa fedha unaomalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Magazeti ya Serikali *(TSN)*. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga shilingi bilioni 2.4 kwa ajili ya Kampuni ya Kampuni ya Magazeti ya Serikali kununua mitambo mipya na ya kisasa ya uchapaji. Aidha, Kamati inashauri mashine ya zamani ifungwe Dodoma ili isaidie kufikisha magazeti katika mikoa ya jirani na Dodoma kama Tabora, Mwanza, Iringa na kwingineko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu. Mwenendo wa timu ya mpira wa miguu ya Tanzania si nzuri hata kidogo. Kamati inatambua thamani ya mpira katika maendeleo ya nchi na hivyo basi inashauri Serikali iiangalie timu hii kwa kuangalia namna gani inaweza kuwezeshwa ili iweze kufanya vizuri katika mashindano mbalimbali kwani ndiyo timu inayowakilisha nchi yetu katika mataifa mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Viwanja vya Michezo. Katika taarifa yake ya maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kuhusu bajeti ya Wizara katika mwaka wa fedha 2016/2017, Kamati ilishauri Serikali iwekeze katika ujenzi wa viwanja vingine vya michezo nchini hasa

katika Majiji ya Arusha, Mwanza na kadhalika. Katika taarifa yake ya utekelezaji nwa maoni ya Kamati, tulijulishwa kuwa Serikali imefanya ukarabati wa viwanja kadhaa vya michezo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inarudia tena ushauri wake kwa Serikali iwekeze kwenye ujenzi wa viwanja vipya vyenye hadhi ya uwanja wa Taifa na siyo kuishia kufanya ukarabati tu. Aidha, Kamati inashauri ikiwezekana kila Halmashauri kuwe na viwanja vya michezo ili kuinua michezo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kazi za Wasanii**.** Tatizo la wizi wa kazi za Wasanii ni tatizo la muda mrefu na Kamati imekuwa ikilisemea mara kwa mara. Kamati bado inaendelea kuliongelea suala hili na kuwataka wale wote wanaohusika katika wizi huu kuacha. Aidha, Kamati inawashauri wasanii waboreshe kazi zao na hususan filamu kutokana na maendeleo ya teknolojia ili ziweze kuteka soko la ndani na nje ya nchi kuwa bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kazi za Wasanii. Tatizo la wizi wa kazi za wasanii ni tatizo la muda mrefu na Kamati imekuwa ikilisemea mara kwa mara. Kamati bado inaendelea kuliongelea suala hili na kuwataka wale wote wanaohusika katika wizi huu kuacha. Aidha, Kamati inawashauri wasanii waboreshe kazi zao na hususan filamu kutokana na maendeleo ya teknolojia ili ziweze kuleta soko la ndani na nje ya nchi kuwa bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgogoro Kuhusu Uingizwaji wa Filamu za Nje ya Nchi. Kamati inatambua na kuthamini kazi kubwa inayofanywa na wasanii wa filamu hapa nchini. Hivi karibuni kumeibuka mgogoro baina ya wasambazaji wa filamu na wasanii wa filamu hapa nchini. Imebainika kuwa chanzo cha mgogoro huu ni uingizwaji wa filamu za nje nchini hali ambayo imekuwa ikizorotesha soko la filamu za hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa uingizwaji huu wa filamu za nje hapa nchini umechochewa na kushuka kwa ubora wa filamu za hapa nchini na hivyo kutokuwa na mvuto kama ulivyokuwepo hapo awali. Kutokana na hali hii Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Serikali ikutane na pande hizi zote mbili ili kuweza kufikia suluhu ya suala hili;

(b) Kamati inatoa rai kwa wasanii wa filamu nchini kuboresha kazi zao ili kuvutia watazamaji wengi wa ndani na nje ya nchi kama ilivyokuwa hapo awali.

(c) Wananchi waendelee kununua kazi wa wasanii wa filamu nchini ili kuweza kukuza sanaa hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Upungufu wa Sheria Haki Miliki. Sheria ya Haki Miliki Namba 7 ya Mwaka 1999 imekuwa na upungufu mwingi ikiwemo kupitwa na wakati, hali ambayo imekuwa ikiwakosesha wasanii mapato, lakini pia Serikali. Kwa mujibu wa Utafiti uliofanywa na *Rulu Art Promoters* unaonesha kuwa sekta ya muziki pekee inaweza kuchangia kwenye Pato la Taifa zaidi ya asilimia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua umuhimu wa kazi za wasanii hapa nchini ikiwemo kutoa ajira kwa vijana; lakini wamekuwa hawanufaiki ipasavyo kutokana na kazi ya jasho lao. Kamati inaitaka Serikali kuifanyia marekebisho Sheria hii ili wasanii waweze kunufaika lakini pia Serikali iweze kupata mapato stahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rasimu ya Kanuni za Urushaji wa Matangazo ya Dijitali na Leseni. Kamati imebaini kuwa pendekezo la Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi

kuhusu Kanuni za Urushaji wa Matangazo ya Digitali na Kanuni za Leseni itakuwa na athari mbaya katika sekta ya urushaji wa matangazo hapa nchini. Rasimu ya kanuni inazuia uwepo wa *channel* za umma katika vifurushi vya Matangazo ya *DHT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Ikumbukwe kuwa, watumiaji wa mfumo wa *DTH* huonesha *channel* za umma kama *channel* za nyongeza kwa wateja ili kuboresha vifurushi vyao na hivyo kusaidia wananchi wengi kuona *channel* hizo za umma. Kuziondoa *channel* hizi kutalazimisha wateja kuwa na ving'amuzi zaidi ya kimoja ili kuona chaneli za umma. Huu ni mzigo kwa wateja lakini pia changamoto kwa warusha matangazo wa *DTH*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu lakini pia Kamati imebaini kuwa rasimu hiyo itataka kuzuiwa kwa mapato yatokanayo na matangazo ya biashara pamoja na kuongezwa kwa ada ya leseni kutoka asilimia 0.8 ya pato la jumla la mwaka la mmiliki wa leseni hadi asilimia moja, kiasi ambacho ni kikubwa na si rafiki. Kamati inashauri Rasimu hizi ziangaliwe upya ili kuleta usawa na kutodhoofisha sekta hii muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hitimisho. Napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuliongoza vyema Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipekee zaidi, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa utendaji kazi wao mzuri na umahiri waliouonesha wakati wa kuchambua bajeti ya Wizara hii. Kwa kuwa, muda unatosha, napenda kuwatambua; kwanza Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mwenyekiti, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako hautoshi. Mheshimiwa Nkamia, toa hoja tu, maliza tu.

**MHE. JUMA S. NKAMIA (K.n.y. MHE. PETER J. SERUKAMBA - MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Harrison Mwakyembe, Mbunge, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mbunge, Naibu Waziri, Profesa Elisante Ole-Gabriel Katibu Mkuu, Nuru Milao Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano walioupatia Kamati katika muda wote ambao Kamati ilikuwa ikitekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Katibu wa Bunge Dokta Thomas Kashililah kwa utendaji kazi wake ambao unawezesha Kamati kutekeleza majukumu kwa ufanisi. Namshukuru pia, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Dickson Bisile, Makatibu wa Kamati, Agnes Nkwera na Pamela Pallangyo na msaidizi wao Gaitana Chima na watumishi wote wa Bunge kwa ushauri wao makini uliowezesha kutekeleza majukumu ya Kamati na kuwasilisha taarifa hii kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naliomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Fungu 96, sh. 28,212,695,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Umesoma vizuri sana.

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII KUHUSU MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI JUU YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 PAMOJA NA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

---

### 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, niwasilishe Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati juu ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Fasili ya (7) (1) (a) ya Nyongeza ya Nane, imetaja Majukumu ya Kamati za Kisekta ikiwemo la kushughulikia Bajeti ya Wizara hii. Aidha, Kwa mujibu wa Nyongeza ya nane (6) (5) (c) iliyo chini ya Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1-2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 Kamati imepewa jukumu la kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha unaoishia ambao ni 2016/2017 pamoja na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Bajeti za Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha unaoishia ili kufanya ulinganisho kuhusu

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha unaofuata wa 2017/2018.

## 2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIWAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

### 2.1 Uchambuzi wa Mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** katika eneo hili Kamati itaeleza kuhusu namna ukusanyaji wa maduhuli ulivyokuwa, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati pamoja na upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

#### 2.1.1Uchambuzi wa Taarifa kuhusu ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (**Fungu 96**), ilipanga kukusanya **shilingi 820,005,000/=.**Hadi kufikia Februari, 2016 Wizara ilifanikiwa kukusanya **shilingi 418,580,116/=** sawa na asilimia **51** ya makadirio ya makusanyo***. (Rejea Kielelezo Na. 1)***

**Kielelezo Na. 1 MAKUSANYO YA MADUHULI 2016/2017**

| IDARA | HABARI | MAENDELEO YA MICHEZO | JUMLA |
|---|---|---|---|
| MAKADIRIO YA MAKUSANYO | 140,003,000 | 680,002,000 | 820,005,000 |
| MAKUSANYO HALISI | 151,168,664 | 267,411,452 | 418,580,116 |
| **ASILIMIA** | **108** | **39** | **51.05** |

**Chanzo: Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2016/2017**

***Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Idara ya Habari kwa Makusanyo makubwa na ina imani kuwa katika Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 Makadirio ya Makusanyo kwa Idara hii yataongezeka. Aidha, Kamati pia inataraji kuwa asilimia 49 ya ukusanyaji wa maduhuli itakamilika ifikapo Mwisho wa Mwaka huu wa Fedha wa 2016/2017***.

**2.1.2Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017**


**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo **(Fungu 96)** iliidhinishiwa shilingi **Bilioni 20.326** ambapo kati ya fedha hizo shilingi **Bilioni 17.3** zilikuwa ni kwaajili ya matumizi ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Mwezi Februari 2017, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi **Bilioni 10.67** tu sawa na **asilimia 52.48** ya Bajeti hiyo.Kati ya Fedha hizo, Wizara ilipokea kiasi cha shilingi **Bilioni 10.4 (sawa na asilimia 60 ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi **Milioni 190.32** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo (**Sawa na asilimia 6.3 ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya utekeleza Miradi ya Maendeleo**). ***(Rejea kielelezo Na. 2)***

**Mheshimiwa Spika**, mnamo mwezi Aprili 2017, Kamati ilijulishwa na Wizara kupitia Barua yenye **Kumb. Na. CDA.7/238/01E/33** ya tarehe 12 Aprili, 2017, kuwa tayari Serikali imetoa kiasi cha shilingi **Bilioni 3** kwa Wizara hii. Kati ya Fedha hizo, shilingi **Bilioni 1** kwaajili ya Mradi wa Maendeleo wa Upanuzi wa Usikivu –TBC ambazo zilikuwa zimeidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Aidha, kiasi cha shilingi **Bilioni 2** ambacho hakikupangwa katika Bajeti ya Mwaka 2016/2017, kimetolewa kwaajili ya kutatua changamoto mbalimbali zinazoikumba TBC ikiwemo kulipa malimbikizo ya madeni ya muda mrefu ya watoa huduma mbalimbali.

***Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha kwa TBC kwani Shirika hilo lilikuwa katika hali mbaya sana kifedha.***

**Kielelezo Na. 2 UPATIKANAJI WA FEDHA KUTOKA HAZINA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/20147**




**uzi wa**

endeleo
ya ziara
ha kwa
(2) kati
liwa na

**(Mradi**

adi huu
a Mradi

**Chanzo: Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2016/2017**

huu Kamati ilitembelea Kituo cha kurusha matangazo cha Azam ili kuweza kujionea hali ya uwekezaji iliyofanyika ili kuwa na picha halisi ya ulinganisho wakati wa kujadili suala la uwekezaji katika kituo cha kurusha matangazo cha taifa cha TBC. Ziara hii iliwapa uelewa mpana Wajumbe wa Kamati na iliwajengea uwezo wa kujua ni nini ishauri Serikali au iwekeze kwa kiasi gani ili kuweza kuwa na uwekezaji wenye tija katika Mradi wa Usikivu wa TBC.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na ukweli kwamba TBC ndiyo Shirika pekee la Taifa la Utangazaji nchini lakini Kamati iliona hali mbaya ya miundombinu na teknolojia kwa maana ya mitambo duni, vidukuzi mpakato (*Computer*) vilivyochoka, vyumba vya kurushia matangazo (*Studio*) vidogo na visivyovutia, hata ukumbi wa kufanyia vikao ni mdogo ukilinganisha na ukubwa wa Shirika hilo la Utangazaji, viti, meza vilivoharibika katika Taasisi hiyo vinavyoondoa morali ya kufanya kazi kwa weledi kwa watumishi wa Taasisi ya TBC.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/ 2017 TBC ilitengewa kiasi cha shilingi **Bilioni 1** kwa ajili ya kuboresha Usikivu kutokana na kukosekana kwa mawasilinao kwa takribani Wilaya 81 nchini. Mpaka Kamati inatembelea TBC hakuna hata senti moja iliyokuwa imetolewa. Aidha, mnamo mwezi Aprili Kamati ikiwa imeshachambua Bajeti ya Wizara hii ilipokea barua kutoka Wizara ya Habari ambayo ilieleza kuwa Mradi huu umepewa Fedha za Serikali kiasi cha shilingi **Bilioni 1** kilichoidhinishwa na Bunge. Kamati I naipongeza Serikali kwa hatua hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Habari inahitaji uwekezaji kama ambavyo AZAM TV imefanya kwani imetumia takribani **dola za kimarekani milioni 40** ambayo ni sawa na takribani shilingi **Bilioni 90 za Kitanzania.** Aidha, kwa ajili ya kuondokana na hali duni ya shirika hili, TCB ilishawahi kuandika andiko lenye kuonesha mahitaji muhimu ya kuweza kulinusuru Shirika ambapo inakadiriwa kiasi cha shilingi **Bilioni 80** zinahitajika.

### 2.2.2 Mradi wa Ukarabati wa Chuo cha Sanaa Bagamoyo (Mradi Namba-4353)

**Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 17 Machi, 2017, Kamati ilitembelea Chuo cha Sanaa Bagamoyo ili kukagua mradi tajwa. Katika Taarifa yake, Mkurugenzi alieleza kuwa,Mradi huu ulianza katika Mwaka wa Fedha 2010/2011 ukiwa na malengo makuu 3 ambayo ni Kuimarisha miundombinu na vifaa ili kuboresha mazingira ya ufundishaji na kujifunza, kuimarisha miundombinu na vifaa ili kuboresha mazingira ya utendaji kazi na kuimarisha miundombinu ili kulinda usalama wa wafanyakazi, wanachuo na mali za Taasisi. Makadirio ya Mradi yalikuwa ni shilingi **Bilioni 8.54.** Hata hivyo tangu kipindi hicho Mradi umekuwa ukipangiwa fedha kidogo ambazo pia zimekuwa hazitolewi. Kwa kipindi chote hicho cha miaka takribani 6 Mradi umetengewa jumla ya shilingi **Bilioni 1.785** na mpaka sasa kiasi kilichotoka ni shilingi milioni **100** kati ya shilingi **Milioni 300** kilichotengwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018.

***Mheshimiwa Spika, Hali hii imeisikitisha sana Kamati kwa kuwa inatambua thamani ya Mradi huu kwa maendeleo ya Sekta ya Sanaa na Utamaduni nchini.***

### 2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yafuatayo kuhusu utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016:-

a) Pamoja na Serikali kutoa kiasi cha shilingi Bilioni 1 kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Upanuzi wa Usikivu wa TBC mwezi April 2017, bado kiasi hiki ni kidogo. Serikali kama ina nia ya dhati ya kuiona TBC inafanya viuzuri ni vyema sasa ikaamua kuwekeza kwa kuitengea fedha za kutosha kama Makampuni mingine yanavyofanya ikiwemo AZAM**.**

b) Kwa kuwa Chuo cha Sanaa Bagamoyo ni moja kati ya Taasisi zingine 3 zilizoteuliwa kuwa vituo vyenye ubora uliotukuka (*Centres of Excellence*) na hususan kwenye

Ufundishaji katika Nyanja za Utamaduni na Sanaa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (*East African Community Centre of Excellence in Culture and the Arts*) Serikali haina budi kutenga fedha za kutosha kwa Taasisi hii ili iweze kutekeleza Miradi yake ambayo itaendana na hadhi iliyopewa.

### 2.3.1Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Kuhusu utekelezaji wa Maoni ya Kamati yaliyotolewa na Kamati wakati wa uwasilishaji wa Bajeti ya Wizara hii Wizara imetekeleza kwa kiasi fulani na kwa yale ambayo haijayatekeleza Kamati itayaeleza tena kwenye Taarifa hii na hususan masuala ya kibajeti.

## SEHEMU YA PILI

---

### 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### 3.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018


**Mheshimiwa Spika,** Katika kikao chake kilichofanyika tarehe 30 Machi, 2017, Kamati ilichambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kama ifuatavyo:-

### 3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (**Fungu 96)** inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi **855,805,000/= (Milioni 855.805)** ikiwa na nyongeza ya shilingi **milioni 35.8** ya kiasi cha shilingi **820,005,000/=** (**Milioni 820)** kilichokadiriwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017**.** Kati ya Fedha hizo Shilingi **147,003,000/=** (**Milioni 147 sawa na asilimia 17)** ni kutoka Idara ya Habari na Shilingi **708,802,000/ =** (**Milioni 708 sawa na asilimia 83)** kutoka Idara ya

Maendeleo ya Michezo kama inavyoonesha kwenye ***Kielelezo Na. 3.***

**Kielelezo Na. 3: MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018**




**Chanzo: Randama ya Wizara, Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2017/2018**


### 3.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika,** ili kuwezesha utekelezaji wa Majukumu yake**,** katika Mwaka huu wa Fedha 2017/2018, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **28,212,695,000/= (Bilioni 28.21)**. Kati ya fedha hizo, hizo Matumizi ya Kawaida yanaombewa shilingi **21,892,695,000/=** (**Bilioni 21.89)** sawa na **asilimia 71.1.** Aidha, kwa upande wa Miradi ya Maendeleo shilingi **6,320,000,000/= (Bilioni 6.32)** sawa na **asilimia 28.8** zinaombwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kiasi hiki cha fedha kinachoombwa ni sawa na nyongeza ya shilingi **Bilioni 7** (**sawa na asilimia 27.9**) ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge katika Mwaka wa Fedha 2016/2017. **Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza Bajeti ya Wizara hii na**

**husussan Miradi ya Maendeleo ambayo imepata nyongeza ya shilingi Bilioni 3.2 sawa na asilimia 52.5.**

**Kielelezo Na. 4: ULINGANISHO WA BAJETI 2016/2017 NA 2017/2018**




***Chanzo: Taarifa ya Wizara kuhusu Bajeti ya 2016/2017 na 2017/2018***

## SEHEMU YA TATU

## 4.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua nafasi hii kutoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (**Fungu 96**) kama ifuatavyo:-

### 4.1 Bajeti

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na Serikali kuongeza Bajeti ya Wizara hii kwa **asilimia 22,** Kamati inaona bado Bajeti ya Wizara hii haikidhi mahitaji na hususan fedha za kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

***Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaongeza Bajeti ya Wizara hii na inatoa kwa wakati fedha hizi zote zitakazoidhinishwa na Bunge lako Tukufu***.

### 4.2 Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC)

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Habari inahitaji uwekezaji mkubwa ili kutoa matokeo mazuri. TBC inafanya kazi kubwa sana lakini kazi zake zinakwamishwa na ufinyu wa Bajeti. Kwa mfano; Kamati ilipata fursa ya kutembea Kampuni ya Utangazaji ya AZAM TV ambayo imefanya uwekezaji mkubwa wa takribani **dola za kimarekani milioni 40** ambayo ni sawa na takribani **shilingi Bilioni 90.** Aidha, kwa ajili ya kuondokana na hali duni ya shirika hili, TCB ilishawahi kuandika andiko lenye kuonesha mahitaji muhimu ya kuweza kulinusuru Shirika ambapo inakadiriwa kiasi cha shilingi **Bilioni 80** zinahitajika. Kutokana na hali hii, Kamati inashauri:-

***a) Kama kweli Serikali ina nia ya dhati ya kuifanya TBC kuwa Shirika la Utangazaji la Taifa basi iwekeze vya kutosha kwa kutenga Bajeti nzuri ikiwa ni pamoja na kupeleka fedha za tozo za ving'amuzi TBC kama yanavyofanya Mashirika makubwa ya Utangazaji Duniani ikiwemo BBC. Fedha hizi ni muhimu ziwe 'ring fenced' ili zisiweze kutumika kwa matumizi mengine.***

***b) Kwa kuwa Serikali imeshahamia Dodoma na hivyo ile dhana ya Makao Makuu ya Nchi ni Dodoma imeanza kuonekana; Kamati inashauri Serikali iiwezeshe TBC ili ijenge Studio ya Kisasa Dodoma kwani hali ya studio iliyopo ni mbaya na haiendani ya Hadhi ya Makao Makuu ya Nchi.***

***c) TBC itumie maeneo yake ya Mwenge na Pugu kutafuta Wabia wa kujenga majengo ya kisasa na kukodisha ili kuweza kuongeza kipato cha Shirika.***

### 4.3 Taasisi ya Sanaa Bagamoyo (TaSuBa)

**Mheshimiwa Spika**, Taasii ya Sanaa Bagamoyo (TaSuBa) ni moja kati ya Miradi ambayo Kamati iliitembelea mnamo mwezi Machi 2017. Kwa ujumla hali ya Taasisi hii siyo

nzuri sana ikilinganishwa na hadhi yake ya kuwa Taasisi yenye ubora uliotukuka kwenye Ufundishaji katika Nyanja za Utamaduni na Sanaa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (*East African Community Centre of Excellence in Culture and the Arts*).

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu ulianza katika Mwaka wa Fedha 2010/2011 na ulipaswa kuwa umepokea jumla ya shilingi **Bilioni 1.78** zilizoidhinishwa na Bunge, hata hivyo ni shilingi **Milioni 100 tu sawa** na **asilimia 5.6 tu** ndiyo zimetolewa katika Mwaka huu wa Fedha 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imesikitishwa sana kuona kwa kipindi chote hiki, TaSuBa imepokea **Milioni 100** tu. ***Kamati inaishauri Serikali kukiangalia Taasisi hii kwa jicho la pekee na kuhakikisha inaitengea fedha za kutosha ili kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Kwa kuanzia, Kamati inaitaka Serikali kutoa kiasi cha shilingi Milioni 200 kilichobaki kati ya shilingi Milioni 300 zilizoidhinishwa na Bunge katika Mwaka huu wa Fedha wa 2016/2017.***

### 4.4 Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga kiasi cha shilingi **Bilioni 2.4** kwa ajili ya Kampuni ya Magazeti ya Serikali kununua Mashine mpya na za kisasa za uchapaji. ***Aidha, Kamati inashauri mashine ya zamani ifungwe Dodoma ili isaidie katika kufikisha magazeti katika Mikoa ya jirani na Dodoma kama Tabora, Mwanza, Iringa n.k.***

### 4.5 Timu ya Taifa

**Mheshimiwa Spika,** Mwenendo wa Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu siyo mzuri sana. Kamati inatambua thamani ya Mpira katika Maendeleo ya nchi na hivyo basi inashauri ***Serikali iiangalie Timu hii na iiwezeshe ili iweze kufanya vizuri katika Mashindano mbalimbali kwani ndiyo Timu inayowakilisha Nchi yetu.***

### 4.6 Ujenzi wa Viwanja vya Michezo

**Mheshimiwa Spika**, katika Taarifa yake ya Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara hii katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Kamati ilishauri Serikali iwekeze katika ujenzi wa Viwanja vingine vya michezo nchini hasa katika Majiji ya Arusha, Mwanza n.k. Katika Taarifa yake ya utekelezaji nwa Maoni ya Kamati, tulijulishwa kuwa Serikali imefanya ukarabati wa Viwanja vya Michezo vikiwemo Sokoine, Nyamagana.

***Mheshimiwa Spika, Kamati inarudia ushauri wake kuwa Serikali iwekeze kwenye Ujenzi wa Viwanja vipya vyenye hadhi ya Uwanja wa Taifa (UHURU) na siyo kuishia kufanya Ukarabati tu. Aidha, kama itawezekana kila Halmashauri kuwe na viwanja vya michezo ili kuinua michezo nchini.***

### 4.7 Kazi za Wasanii

**Mheshimiwa Spika,** tatizo la wizi wa kazi za Wasanii ni tatizo la muda mrefu na Kamati imekuwa ikilisemea mara kwa mara. ***Kamati bado inaendelea kuliongelea suala hili nakuwataka wale wote wanaohusika katika udhalimu huu kuacha. Aidha, Kamati inawashauri wasanii waboreshe kazi zao na hususan filamu kutokana na maendeleo ya Teknolojia ili ziweze kuteka soko la ndani na nje ya nchi.***

### 4.8 Mgogoro kuhusu uingizwaji wa filamu za nje ya nchi

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua na kuthamini kazi kubwa inayofanywa na wasanii wa filamu hapa nchini. Hivi karibuni kumeibuka mgogoro baina ya wasambazaji wa filamu na wasanii wa filamu hapa nchini. Imebainika kuwa chanzo cha mgogoro huu ni uingizwaji wa filamu za nje nchini hali ambayo imekuwa ikizorotesha soko la filamu za hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa uingizwaji huu wa filamu za nje hapa nchini umechochewa na kushuka

kwa ubora wa filamu za hapa nchini na hivyo kutokuwa na mvuto kama uliokuwepo hapo awali.

***Kutokana na hali hii Kamati inashauri yafuatayo:-***

***a) Serikali ikutane na pande hizi zote mbili ili kuweza kufikia suluhu ya suala hili.***

***b) Kamati inatoa rai kwa wasanii wa filamu nchini kuboresha kazi zao ili kuweza kuvutia watazamaji wengi ndani na nje ya nchi kama ilivyokuwa awali.***

***c) Wananchi waendelee kununua kazi wa wasanii wa filamu nchini ili kuweza kukuza sanaa hii muhimu***

### 4.9 Mapungufu ya Sheria Hakimiliki

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Hakimiliki Na. 7 ya Mwaka 1999 imekuwa na mapungufu mengi ikiwemo kupitwa na wakati hali ambayo imekuwa ikiwakosesha wasanii mapato lakini pia Serikali. Kwa mujibu wa Utafiti uliofanywa na Rulu Art Promoters unaonesha kuwa Sekta ya Muziki pekee inaweza kuchangia kwenye pato la Taifa zaidi ya asilimi moja.

***Kamati inatambua umuhimu wa kazi za wasanii hapa nchini ikiwemo kutoa ajira kwa vijana wengi lalkini wamekuwa hawanufaiki ipasavyo kutokana na kazi ya jasho lao, Kamati inaitaka Serikali kuifanyia marekebisho Sheria hii ili wasanii waweze kunufaika lakini pia Serikali iweze kupata mapato stahiki.***

### 4.10 Rasimu ya Kanuni za Urushaji wa Matangazo ya Digitali na Leseni

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa Pendekezo la Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuhusu Kanuni za Urushaji wa Matangazo ya Digital na Kanuni za Leseni itakuwa na athari mbaya katika Sekta ya Urushaji wa matangazo hapa nchini. Rasimu ya Kanuni inazuia

uwepo wa chaneli za Umma katika vifurushi vya Matangazo ya DHT. Ikumbukwe kuwa watumiaji wa mfumo wa DTH huonyesha chaneli za Umma kama chaneli za nyongeza kwa wateja ili kuboresha vifurushi vyao na hivyo kusaidia wanannchi wengi kuona chaneli hizo za Umma. Kuziondoa chaneli hizi kutalazimisha wateja kuwa na ving'amuzi zaidi ya kimoja ili kuweza kuona chaneli za Umma. Huu ni mzigo kwa wateja lakini pia changamoto kwa warusha matangazo wa DTH.

**Mheshimiwa Spika**, siyo hivyo tu, lakini pia Kamati imebaini kuwa rasimu hiyo inataka kuzuiwa kwa mapato yatokanayo na matangazo ya biashara pamoja na kuongezwa kwa ada ya leseni kutoka asilimia 0.8 ya pato la jumla la Mwaka la mmiliki wa leseni hadi asilimia 1 kiasi ambacho ni kikubwa na siyo rafiki .

***Kamati inashauri Rasimu hizi ziangaliwe upya ili kuleta usawa na kutodhoofisha Sekta hii muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.***

## 5 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuliongoza vyema Bunge letu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kipekee zaidi**,** napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa utendaji kazi wao mzuri na umahiri waliouonyesha wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara hii. Napenda kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Peter Joseph Serukamba, Mb, Mwenyekiti
2. Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb M/Mwenyekiti
3. Mhe. Hussein Mohamed Bashe, Mb Mjumbe
4. Mhe. Peter Ambrose Paciece Lijualikali, Mb jumbe
5. Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi, Mb Mjumbe
6. Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mb Mjumbe
7. Mhe. Kasuku Samson Bilago, Mb Mjumbe

| | | |
|---|---|---|
| 8. | Mhe. Lucia Ursula Michael Mlowe, Mb | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Dkt. Jasmine Tiisekwa, Mb | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Ahmed Ally Salum, Mb | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Susan Anselm Lyimo, Mb | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Juma Selemani Nkamia, Mb | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Selemani Said Bungara, Mb | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Zitto Zuberi Ruyagwa Kabwe, Mb | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Boniphace Mwita Getere, Mb | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Bernadetha Kasabango Mushashu, Mb | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mb | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Savelina Sylvanus Mwijage, Mb | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Sikudhani Yassin Chikambo, Mb | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Grace Victor Tendega, Mb | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Juma A. Juma, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** namshukuru Mhe. Harrison G. Mwakyembe (Mb) Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Anastazia J. Wambura (Mb) Naibu Waziri, Prof. Elisante Ole Gabriel Katibu Mkuu, Ndg. Nuru Milao Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano waliotupatia katika muda wote ambao Kamati ilikuwa ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, namshukuru sana Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashillilah kwa utendaji kazi wake ambao unawezesha Kamati kutekeleza majukumu kwa ufanisi. Namshukuru pia Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman B. Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Dickson M. Bisile, Makatibu wa Kamati hii Ndg. Agnes Nkwera na Ndg. Pamela Pallangyo na msaidizi wao Ndg. Gaitana Chima na Watumishi wote wa Bunge kwa ushauri wao makini uliotuwezesha kutekeleza majukumu ya Kamati na kuwasilisha Taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, sasa naliomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo **(Fungu 96)** shilingi **Bilioni Ishirini na nane, Milioni mia mbili na kumi na mbili, Laki sita na tisini na tano elfu. (28,212,695,000/=).**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono Hoja.

Peter J. Serukamba, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII**
5 MEI, 2017

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Msemaji Mkuu Kambi ya Upinzani, kuhusu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii, lakini naomba nitambue wageni wangu, wanafunzi 57 kutoka Chuo Kikuu cha *UDOM* ambao ni Wanachama wa CHADEMA, ambao wamo humu ndani na ni wageni wangu, lakini hawakutambulishwa inavyopaswa. Wanafunzi 57 Wanachama wa CHADEMA, *UDOM,* karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nisome hotuba; Utangulizi. Kwa mujibu wa Kanuni Namba 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha katika Wizara hiyo, mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijawasilisha maoni hayo, naomba kutumia fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama hapa kufanya kazi hii muhimu kwa Taifa na kuhakikisha misingi ya kikatiba ya kulinda na kuenzi haki na uhuru wa kutoa na kupata habari inalindwa na kuenziwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani kwa Naibu Waziri Kivuli wa Wizara hii, Mheshimiwa Devota Minja (Mb) kwa ushirikiano mkubwa anaonipa, lakini kipekee kwa kutumia taaluma yake kama Mwanahabari, kutoa ushauri wa kitaalam ambao umesaidia sana katika maandalizi ya hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia fursa hii kuwapongeza wanahabari na wasanii wote nchini, kwa uvumilivu na ujasiri wao wa kufanya kazi bila woga licha ya changamoto na vikwazo vingi vinavyowakabili kipindi hiki. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapongeza timu za michezo mbalimbali na wanamichezo wote ambao kwa nyakati tofauti wanaipatia nchi yetu heshima kubwa kwa kushiriki na kutuwakilisha katika mashindano mbalimbali ya ndani na ya kimataifa yaliyofanyika katika mwaka huu wa fedha unaomaliza muda wake pamoja na kuwa msaada wa Serikali ni kidogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia haitanielewa kama sitatambua mchango mkubwa wa Wanambeya ambao umenifanya niwe nilivyo leo kisiasa. Sitasahau heshima kubwa ya Wanambeya waliyonipa ya kunifanya kuwa Mbunge wa kwanza Tanzania Bara na Visiwani kupata kura nyingi kuliko Mbunge yeyote katika Bunge hili na katika uchaguzi Mkuu wa 2015. *To cut the story short Mr. Chairman, I am the most voted MP in this house and I am proud of that.* Nasema ahsanteni sana Wanambeya kwa heshima hii kubwa mliyonipa na kazi hii ninayoifanya hapa ni mojawapo ya ishara kwamba, naitendea haki heshima mliyonipa na inshallah 2020 nitakuwa *the most voted MP in Africa. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya salamu hizo za utangulizi, naomba sasa nianze kuzungumzia masuala ya kisera na kibajeti katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Uhuru wa Kujieleza na Kutoa Maoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uhuru wa Kujieleza na Kutoa Maoni. Wakati tarehe 3 Mei, wiki hii Dunia imeadhimisha Siku ya Uhuru wa Habari Duniani, tasnia ya habari Tanzania inapita

katika majaribu makubwa kuliko wakati wowote katika historia ya nchi yetu. Uhuru wa kupata na kutoa habari hapa nchini umeporomoka kwa kasi ya kutisha hasa baada ya Serikali ya Awamu ya Tano kuingia madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ripoti ya *The Freedom Press* ya mwaka 2017 iliyochapishwa katika Gazeti la *The Citizen* la tarehe 3 Mei, 2017 ni kwamba; Tanzania haina uhuru kamili wa habari na kwamba imeshuka kwa alama tatu kutoka alama 61 mwaka 2016 hadi 58 mwaka huu wa 2017. Kushuka huko kumeifanya Tanzania kushika nafasi ya 122 kati ya nchi 198 duniani zilizofanyiwa utafiti kuhusu uhuru wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu kubwa ya Tanzania kushuka katika viwango vya uhuru wa habari ni kutungwa kwa sheria zinazodhibiti uhuru wa habari yaani Sheria ya Makosa ya Kimtandao *(Cyber Crimes Act)* ya mwaka 2015 na Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari *(Media Services Act)* ya mwaka 2016 pamoja na kushtakiwa na kufungwa kwa waandishi wa habari na wamiliki wa mitandao ya kijamii *(bloggers)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ripoti hiyo ya *The Freedom Press*, inasema kwamba, pamoja na Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, kuendelea kuendesha kampeni kubwa ya kupambana na rushwa, lakini Serikali yake imekuwa haina uvumilivu *(tolerance)* ya kukosolewa na vyombo vya habari na mitandao ya kijamii. Ripoti hiyo inaonesha kwamba, mwishoni mwa mwaka 2016 takriban watu 10 walikuwa wameshtakiwa kwa kilichodaiwa kumkashifu Rais chini ya sheria ya makosa ya kimtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mwanzilishi mwenza wa Mtandao wa *Jamii Forums*, **Maxence Melo**, naye alikamatwa na kushtakiwa chini ya sheria hiyo. Matukio haya ya ukamataji, kuwashtaki na kuwafunga watu ambao wametumia haki yao ya Kikatiba ya kutoa maoni yao,

kumeipotezea nchi sifa katika medani za kimataifa na kutuweka katika orodha ya nchi zinazokandamiza uhuru wa habari duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkutano Mkuu wa kwanza wa Umoja wa Mataifa wa mwaka 1946 uliazimia na kueleza yafuatayo kuhusu uhuru wa habari, na ninaomba ninukuu, *quote*:-

*"Freedom of information is a fundamental human right and the touchstone of all the freedom to which the United Nations is consecrated."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa tafsiri isiyo rasmi ni kwamba, uhuru wa kupata taarifa ni msingi wa haki zote za binadamu. Tamko la Umoja wa Mataifa linafafanua kuwa kila mmoja ana haki ya kujieleza na kutoa maoni ikiwa ni pamoja na haki ya kutoa maoni bila kuingiliwa na ikijumuisha pia kutoa na kupokea taarifa kutoka kwenye chombo chochote cha habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 18 inakazia Tamko hilo la Umoja wa Mataifa ambapo inaeleza kuwa, naomba kunukuu:-

*"kila mtu:- (a)..."*

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu!

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** *"...anao uhuru wa maoni ya kueleza fikra zake.*

*(b)..."*

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu!

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** *...Anayo haki ya kutafuta, kupokea na kutoa habari bila... mipaka ya nchi,*

*(c)Anao uhuru wa...*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sugu, hebu subiri kwanza. Mheshimiwa nani, hoja yako ni ipi?

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna hotuba hiyo anayoisoma.

**MWENYEKITI:** Vitabu vinaletwa, viko njiani.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa endelea.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 18, inakazia Tamko hilo la Umoja wa Mataifa, ambapo inaeleza kuwa, naomba kunukuu:-

*18.Kila mtu-*

*(a)Anao uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake;*

*(b)Anayo haki ya kutafuta, kupokea na kutoa habari bila ya kujali mipaka ya nchi;*

*(c)Anao uhuru wa kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake; na*

*(d)Anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na kuhusu masuala muhimu kwa jamii.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tamko hili la Umoja wa Mataifa linaonekana kuwa kitendawili kisichokuwa na majibu kwa Serikali ya Awamu ya Tano. Hii ni kutokana na matukio kadhaa yanayoashiria kukiuka misingi ya uhuru wa habari na haki ya kutoa maoni ndani ya nchi kutokana na matukio kadhaa nitakayoeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja; kupotea kwa Ben Saanane na kukamatwa na kuteswa kwa wananchi... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sugu, Kiti kilishatoa *Rulling* na wewe ni Mbunge mzoefu, umeshinda kura nyingi sana; na Kiti kikishatoa *Rulling,* sasa nakuongoza uende kwenye Ukurasa wa 12(3).

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** *(Hakusikika vizuri)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sugu, usibishane na Kiti.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** *(Hakusikika vizuri)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sugu...

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** *(Hakusikika vizuri)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sugu, *Microphone* yake haiwezi kuwaka.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** *(Hakusikika vizuri)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sugu!

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** ...ku-*discuss* na Mheshimiwa Waziri...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sugu!

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Amesema ataweka *commitment* ya kulishughulikia suala la Ben Saanane. Tumetoka kwenye Kikao, mimi kama Waziri Kivuli wa Habari, Mheshimiwa Lema...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sugu!

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Lema, kama Waziri Kivuli wa Mambo ya Ndani; nilitarajia...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sugu! Mheshimiwa Sugu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Sugu! Mtu akikuheshimu na wewe mheshimu. Mimi nafanya kazi ya Kanuni, hakuna tofauti na Jaji na wanasheria wengi mko hapa, sidhani kama Jaji anajibiwa hivi mkiwa mahakamani. Nimesema, kama kuna mtu anaona *Rulling* zangu zimekwenda kinyume, tumieni Kanuni ya 5(4); *very simple.* Sasa acha hayo yako nenda kwenye ukurasa wa 12(3).

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitaachaje haya maneno?

**MWENYEKITI:** Sasa *Rulling* ndio ya Kiti ndiyo hiyo.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** ...Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** *Matches* zinakuudhi, lakini *Rulling* ya Kiti *I have to be very firm.*

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hi ni *dictatorship* mnayoifanya.

**MWENYEKITI:** Sasa, ndio nasema usiende nikaku-*charge* kwenye Kanuni ya 74 ya Kudharau Mamlaka ya Kiti.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** ...Na kupelekwa maadili?

**MWENYEKITI:** Mimi nakuomba nenda, Hotuba yako iko vizuri, nenda ukurasa wa 12, sisi wote tunayo hapa, wale ambao hawajapata Makatibu, naomba vitabu hivyo vitolewe wagawiwe Waheshimiwa Wabunge kabla hajamaliza Hotuba yake. Nenda kwenye ukurasa wa 12.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kupotea kwa Ben Saanane...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sugu, usitake tufanye vitu ambavyo si vizuri.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** *(Hapa hakusikika)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sugu! Nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Lissu!

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako na naomba Mwongozo wako kuhusu hiki ambacho kimefanyika sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni hizi za Bunge Kuhusu Utaratibu wa Majadiliano ziko wazi. Mbunge atazungumza halafu ndipo ataambiwa umekosea, kama amesema uongo huyu anayedai amesema uongo atatoa ukweli wake, halafu huyu anayedaiwa kutoa uongo ataambiwa athibitishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu utaratibu wa hotuba za Upinzani kuchukuliwa na Serikali kabla hazijasomwa, halafu Serikali inaamua Wapinzani waseme kipi na wasiseme kipi maana yake ni kwamba, basi afadhali huyu *Chief Whip* wa Serikali akae kwenye Kiti hicho tujue kwamba, Bunge hili linaendeshwa na Serikali. Huu utaratibu ambao Serikali, Bungeni ndiyo inaamua kitu gani kisemwe, huu utaratibu unaua Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kama kuna utaratibu wowote wa kikanuni unaoruhusu Kiti chako kutoa maamuzi ya namna hii kabla hotuba haijasomwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Asante. Mheshimiwa Jenista! Jiandae Mheshimiwa *AG!*

**MBUNGE FULANI:** Aaaa! Hajaomba

**MWENYEKITI:** Ameshaniomba. Subiri Mheshimiwa Ester, utapewa nafasi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwelewa sana Mheshimiwa Tundu Lissu, Mnadhimu wa Kambi ya Upinzani Bungeni, lakini na mimi naomba tu nitoe taarifa kwenye Bunge hili na Mwongozo wako wewe utatuongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapofanya shughuli hizi za uendeshaji wa shughuli Bungeni, kama *Chief Whip* wa *Opposition* alivyo na majukumu ya ku-*whip* jambo lolote ambalo lintakiwa liwe *whipped* kwa maana ya misingi ya utendaji bora wa shughuli za Bunge ndani ya Bunge kwa kufuata Kanuni, wajibu huo ndivyo ulivyo kwenye upande huu wa pili, kwangu mimi kama *Chief Whip* wa Serikali ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu sina mamlaka yoyote ya kikanuni ya kukwambia wewe Mwenyekiti ufanye nini, lakini ninayo mamlaka ndani ya Bunge hili, kama Mbunge yeyote ya kuhakikisha kwamba, Kanuni tulizojiwekea zinafuatwa na zinaendelea kuheshimika ndani ya Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshikmiwa Mwenyekiti, wewe umetoa mwongozo na mwongozo hakutolewa na *Chief Whip.* Kwa kumbumkumbu zangu za Bunge miongozo ikitolewa ndani ya Bunge anayefanya maamuzi kwa mujibu wa kanuni ni Kiti; lakini historia ya jambo hili imejitokeza katika hotuba kadhaa. Sisi kama viongozi wote ndani ya Bunge, hotuba hizi zimekuwa zikija kwenye meza zetu mapema. Katika jambo hili la leo ambalo naendelea kulitolea ushauri wa kina, baada ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni kuliondoa toka siku ya kwanza, jambo ambalo nimeendelea kushauri katika Bunge hili; moja, vyombo ambavyo vinahusika na jambo hili viendelee kufanyia kazi jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, kwa mujibu wa kanuni tulizonazo haitukatazi pia Mbunge kuzitumia kanuni hizi kuleta jambo hili kwa namna nyingine. Tatu, tunao uwezo pia wa kambi hizi zote mbili kukutana katika utaratibu mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kutumia busara tu na busara itaongozwa na kiti chako. Vilevile viongozi wa kambi zote mbili tunatakiwa tufike mahali busara ituongoze katika kuliangalia jambo hili na kulitekeleza na kulisimamia kwa misingi ambayo itatusaidia zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tu nitoe taarifa katika Bunge hili na kukuomba wewe utuongoze kwa mfano kanuni hizi zimesomwa kwenye kifungu cha 64 zinaeleza kabisa utaratibu wa majadiliano ndani ya Bunge nini kinaruhusiwa na nini hakiruhusiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba, kwanza usimamie kanuni, lakini la pili, kama jambo lenyewe linaonesha kwamba linahitaji tukutane pande hizi zote mbili, halina sababu ya kuendelea kuliweka katika mazingira ambayo yanaashiria kuvunjwa kwa kanuni zaidi ya kufuatilia kanuni ambazo tumejiwekea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bulaya.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama kuna muda watu wanaamua kunyamaza kimya si kwamba hawana maumivu. Hii tabia imekuwa ikijirudia kwa Serikali kutuchagulia Kambi Rasmi ya Upinzani ambayo kwa mujibu wa Katiba na Kanuni ndiyo kazi yetu kuishauri Serikali; wao wanataka sasa kutuamulia mpaka katika hotuba zetu tuseme nini. Hilo haliwezi likaruhusiwa, tukitoka mnasema, tukibaki ndani mnatunyanyasa kwa kutumia wingi wenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufanye nini? kwa nini mnatuonea? Leo mpo madarakani kesho hamtakuwepo...

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** ...lazima tuweke misingi ya kuheshimiana, lazima tuweke misingi ya kupendana kwa

dhati, si kila wanacho kitaka Serikari ndio sisi tuseme, sisi ni *watchdog* wa Serikali.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Ester kaa chini.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Wewe ndiyo hutarudi ndani ya Bunge.

**MWENYEKITI:** Ahsante kaa chini. Waheshimiwa, nafikiri Mheshimiwa Lissu ulikuwa umechelewa. Nilitoa maelezo marefu sana. Kwanza niwahakikishie jambo moja, kwamba Kiti hiki hakiongozwi na Serikali. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI**: Nikisema hivyo, kanuni zetu hizi ukienda Kanuni ya Nane...

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ni kiini macho tu.

**MWENYEKITI:** Labda, Mheshimiwa Msigwa sikiliza. Kanuni zetu ukienda Kanuni ya Nane Kiti hiki hakina mlengwa Serikali wala wa Vyama.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** ...si imeandikwa hapa? Umeona bwana! Hilo moja sasa...

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mtuache tuseme.

**MWENYEKITI:** Mimi nilishatoa *ruling, ruling* yangu ilishatoka. Mheshimiwa Lissu wewe ni Mwenyekiti, *President* mtaalam mkubwa sana wa Sheria. *Ruling* zangu hazihojiwi hapa. *Rulling* zangu zinahojiwa kwa kutumia kanuni ya tano...

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haijawahi kutokea...

**MWENYEKITI: ...** ndiyo nasema *ruling* yangu haijadiliwi hapa...

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inajadiliwa wapi?

**MWENYEKITI:** Kanuni ya tano fasihi ya nne...

**MHE. TUNDU A. LISSU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wapi inatakiwa kujadiliwa?

**MWENYEKITI:** Kanuni ya Tano Fasili ya Nne

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakijawahi kutokea hiki kitu.

**MWENYEKITI:** ... kwa sababu hamjakata rufaa. Kanuni ya Tano kusaidia na umma ambao wako humu ndani wajue kuwa hamwonewi na Serikali wala haihoji kiti.

Mbunge yeyote, ambaye hataridhika na uamuzi wa Spika anaweza kuwasilisha sababu za kutoridhika kwake kwa Katibu wa Bunge ambaye atawasilisha malalamiko hayo kwa Spika.

Kwa hiyo Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Sugu twende kwenye ukurasa 12(3) endelea kuna mambo mengi endelea. Njoo usomee hapa, ukitaka kusoma hapo *its up to you* lakini njoo usomee hapa, ili Mbunge uliyepata kura nyingi uonekane hapa.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *I hope* muda wangu umelindwa.

**MWENYEKITI:** Muda wako umelindwa wala usipate tabu. Fuata tu Kiti kinavyosema mambo yako yatakwenda vizuri tu humu ndani. Twende ukurasa wa 12(3).

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti**,** toka mwanzoni wa Novemba, 2016 ambapo ni takriban miezi sita sasa Msaidizi wa Mwenyekiti wa Chadema Taifa Benny Saa Nane hajulikani aliko. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sugu! Mheshimiwa Sugu! Mheshimiwa Sugu! *Don't test my patience,* kama unafikiri huwezi acha usiseme. Huwezi kuhitimisha kurasa ulizokatazwa.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja nihitimishe.

**MWENYEKITI:** Huwezi kuhitimisha maneno ambayo hayako kwenye Kiti changu.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuhitimisha.

**MWENYEKITI:** *No no no,* Sugu *I am doing my job here.* Kama ipo kwenye hotuba soma, kama haipo kwenye hotuba usisome.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti nahitimisha kwa namna hii. Kama Bunge hili limeamua kukumbatia masuala ya kidikteta katika Taifa hili...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sugu...

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tunashuhudia…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sugu, acha hayo mambo Mheshimiwa Sugu…

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, WASANII NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashuhudia…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sugu, usibishane na mamlaka ya Kiti. Mheshimiwa Sugu hitimisha, huna cha kuhitimisha funga *file* yako ukakae.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nahitimisha.

**MWENYEKIT:** *No no no*, hayo maneno hayapo kwenye ripoti yako. Funga file yako kakae.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mkiwa mna redio…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa vituo vya redio wala havikukatazwa. Mheshimiwa Sugu! Mheshimiwa Sugu! Mheshimiwa Sugu!

*(Hapa Mheshimiwa Joseph O. Mbilinyi aliendelea kuzungumza hata baada ya kuzuiliwa na Mwenyekiti)*

**MWENYEKITI:** Basi kakae. Ahsante kaka kakae, ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa na hayo makofi yamesaidia usisikike kabisa. Kwa hiyo...

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO MHE. JOSEPH O. MBILINYI KUHUSU BAJETI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, naomba kuwasilisha mbele ya bunge lako maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Wasanii na Michezo kwa mwaka wa fedha 2016/17 na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha katika Wizara hiyo, mwaka wa fedha 2017/18.

**Mheshimiwa Spika,** kabla sijawasilisha maoni hayo, napenda kutumia fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema, na kuniwezesha kusimama hapa kufanya kazi hii muhimu kwa taifa, ya kuhakikisha misingi ya kikatiba ya kulinda na kuenzi haki na uhuru wa kutoa na kupata habari inalindwa na kuenziwa katika nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kutoa shukrani kwa Naibu Waziri Kivuli wa Wizara hii, Mheshimiwa Devota Minja (Mb) kwa ushirikiano mkubwa anaonipa, lakini kipekee kwa kutumia taaluma yake kama mwanahabari, kutoa ushauri wa kitaalam ambao umesaidia sana katika maadnalizi ya hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,** napenda pia kutumia fursa hii kuwapongeza wanahabari na wasanii wote nchini, kwa uvumilivu na ujasiri wao wa kufanya kazi bila woga licha ya changamoto na vikwazo vingi vinavyowakabili kipindi hiki. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazipongeza timu za michezo mbalimbali na wanamichezo wote ambao kwa nyakati tofauti wanaipatia nchi yetu heshima kubwa kwa

kushiriki na kutuwakilisha katika mashindano mbalimbali ya ndani na ya kimataifa yaliyofanyika katika mwaka huu wa fedha unaomaliza muda wake pamoja na kuwa na msaada kidogo kutoka serikalini.

**Mheshimiwa Spika,** dunia haitanielewa kama sitatambua mchango mkubwa wa Wana Mbeya ambao umenifanya niwe nilivyo leo. Sitasahau heshima kubwa wana mbeya waliyonipa ya kunifanya kuwa Mbunge wa kwanza Tanzania Bara na Visiwani kupata kura nyingi kuliko Mbunge yeyote katika Bunge hili katika uchaguzi Mkuu wa 2015. *To cut the story short Mr. Speaker, I am the most voted Mp in this house and I am proud of it.* Nasema asanteni sana wana Mbeya kwa heshima hii kubwa mliyonipa, na kazi hii ninayoifanya hapa ni mojawapo ya ishara kwamba; naitendea haki heshima mliyonipa.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya salamu hizo za utangulizi, naomba sasa nianze kuzungumzia masuala ya kisera na kibajeti katika Wizara hii ya Habari, Utamaduni, Wasanii na Michezo.

## 2. UHURU WA KUJIELEZA NA KUTOA MAONI

**Mheshimiwa Spika**, Wakati tarehe tatu Mei wiki hii dunia imeadhimisha siku ya uhuru wa habari, tasnia ya habari Tanzania inapita katika majaribu makubwa kuliko wakati wowote katika historia ya nchi yetu. Uhuru wa kupata na kutoa habari hapa nchini umeporomoka kwa kasi ya kutisha hasa baada ya Serikali hii ya awamu ya tano kuingia madarakani.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Ripoti ya The Freedom Press ya mwaka 2017 iliyochapishwa katika gazeti la The Citizen la tarehe 3 Mei,2017 ni kwamba; Tanzania haina uhuru kamili wa habari, na kwamba imeshuka kwa alama tatu kutoka alama 61 mwaka 2016 hadi 58 mwaka huu wa 2017. Kushuka huko kumeifanya Tanzania kushika nafasi ya 122 kati ya nchi 198 duniani zilizofanyiwa utafiti kuhusu uhuru wa habari.

**Mheshimiwa Spika,** sababu kubwa ya Tanzania kushuka katika viwango vya uhuru wa habari ni kutungwa kwa sheria zinazodhibiti uhuru wa habari yaani Sheria ya Makosa ya Kimtandao (Cyber Crimes Act) ya mwaka 2015; Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari (Media Services Act) ya mwaka 2016 pamoja na kushtakiwa na kufungwa kwa waandishi wa habari na wamiliki wa mitandao ya kijamii (bloggers).

**Mheshimiwa Spika,** ripoti hiyo ya The Freedom Press, inasema kwamba pamoja na Rais wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kuendesha kampeni kubwa ya kupambana na rushwa lakini Serikali yake imekuwa haina uvumilivu (tolerance) wa kukosolewa na vyombo vya habari na mitandao ya kijamii. Ripoti hiyo inaonyesha kwamba mwishoni mwa mwaka 2016 takriban watu 10 walikuwa wameshtakiwa kwa kilichodaiwa kumkashifu Rais, chini ya sheria ya makosa ya kimtandao. Aidha, mwanzilshi mwenza wa mtandao wa Jamii Forums Maxence Melo, naye alikamatwa na kushtakiwa chini ya sheria hiyo. Matukio haya ya ukamataji, kuwashtaki na kuwafunga watu ambao wametumia haki yao ya kikatiba ya kutoa maoni yao, kumeipotezea sifa nchi yetu katika medani za kimataifa na kuiweka katika orodha ya nchi zinazokandamiza uhuru wa habari duniani.

**Mheshimiwa Spika**, Mkutano Mkuu wa kwanza wa Umoja wa Mataifa wa mwaka 1946 uliazimia na kueleza yafuatayo kuhusu uhuru wa habari, naomba kunukuu;

***"Freedom of information is a fundamental human right and……the touchstone of all the freedom to which the United Nations is consecrated"***

**Mheshimiwa Spika**, kwa tafsiri isiyo rasmi ni kwamba, uhuru wa kupata taarifa ni msingi wa haki zote za binadamu.

**Mheshimiwa Spika**, Tamko la Umoja wa Mataifa linafafanua pia kuwa kila mmoja ana haki ya kujieleza na kutoa maoni ikiwa ni pamoja na haki ya kutoa maoni bila

kuingiliwa na ikijumuisha pia kutoa na kupokea taarifa kutoka kwenye chombo chochote cha habari.

***"Everyone has the right to freedom of opinion and expression, this right includes freedom to hold opinions without interference and to seek, receive and impart information and through any media and regardless of frontiers".***

**Mheshimiwa Spika,** Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ibara ya 18 inakazia tamko hilo la Umoja wa Mataifa ambapo inaeleza kuwa; naomba kunukuu;

"kila mtu-

(a) Anao uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake;

(b) Anayo haki ya kutafuta, kupokea na kutoa habari bila ya kujali mipaka ya nchi;

(c) Anao uhuru wa kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake; na

(d) Anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na kuhusu masuala muhimu kwa jamii.

**Mheshimiwa Spika**, tamko hili la Umoja wa Mataifa linaonekana kuwa kitendawili kisichokuwa na majibu kwa serikali ya awamu ya tano. Hii ni kutokana na matukio kadhaa yanayoashiria kukiuka misingi ya uhuru wa habari na haki kutoa maoni ndani ya nchi kutokana na matukio kadhaa nitakayoeleza.

***[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]***

### 3. SERIKALI KUINGILIA VYOMBO VYA HABARI

#### i. Kuvamiwa kwa Kituo cha Clouds TV na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 17 mwezi Machi mwaka 2017 Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Paul Makonda

ambaye inasemekana jina lake halisi ni Daudi Albert Bashite, alivamia kituo cha luninga cha Clouds kinachomilikiwa na Kampuni ya Clouds Media Group akiwa ameambatana na askari wenye silaha za moto na kuingia moja kwa moja kwenye chumba cha habari (news room).

**Mheshimiwa Spika**, imeelezwa na kuripotiwa na vyombo vya habari kuwa lengo la uvamizi huo lilikuwa kuwatisha na kuwalazimisha watangazaji wa kipindi cha "Weekend Chat Show" maarufu kama **Shilawadu**. Kitendo hicho cha Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ni cha kulaaniwa na watu wote wanaopenda na kujali misingi ya uhuru wa habari.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hatua za serikali kupitia kwa aliyekuwa Waziri wa Habari wa wakati huo Mheshimiwa Nape Nnauye kuunda kamati ya uchunguzi na kamati hiyo kuwasilisha taarifa yake Serikalini, badala ya kuchukua hatua dhidi ya Mkuu huyo wa Mkoa, ikaamua kumfukuza kazi na kutupa kapuni taarifa ya Kamati pamoja na juhudi alizochukua Mheshimiwa Nape Nnauye kulinda maslahi mapana ya uhuru wa vyombo vya habari.

**Mheshimiwa Spika**, kitendo alichofanya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam si tu kinakiuka uhuru wa vyombo vya habari bali kinakiuka misingi ya utawala bora na kimeonesha kuwa Mkuu huyo wa Mkoa hana chembe ya maadili ya uongozi wa umma kwa mujibu wa kiapo alichokula kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya mwaka 1995.

**Mheshimiwa Spika**, ikumbukwe kuwa pamoja na kuwa Mkuu wa Mkoa ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa kwa mujibu wa Sheria lakini hana mamlaka ya kuamuru namna ya askari wa Jeshi la Polisi, Magereza au Uhamiaji kufanya kazi zao. Kwa namna inavyoonekana hata Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam CP Simon Sirro hana haja ya kuwepo kwa sababu Mkuu wa Mkoa ndiye amekuwa akiagiza askari kufanya majukumu yao kinyume kabisa na Sheria ya Jeshi la Polisi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inaunga mkono kauli na uamuzi wa Jukwaa la Wahariri wa vyombo vya habari kususia kuripoti taarifa zinazomhusu Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ili iwe fundisho kwa viongozi wengine ambao kwa namna moja ama nyingine wamekuwa wakiwanyanyasa waandishi wa habari wakati wanapotekeleza majukumu yao.

**ii. Kuvamiwa kwa Waandishi wa Habari na Wafuasi wa Prof. Lipumba**

**Mheshimiwa Spika,** Tarehe 22 Aprili 2017 katika Hoteli ya Vina iliyopo Mburahati, Manispaa ya Kinondoni Jijini Dar es Salaam lilitokea tukio la kusikitisha ambapo waandishi wa habari walivamiwa wakati wakitekeleza majukumu yao kwenye mkutano wa waandishi wa habari ulioandaliwa na kiongozi wa Wilaya wa Chama cha Wananchi CUF.

**Mheshimiwa Spika**, waandishi wa habari walipigwa na kuumizwa na kikundi kilichoratibiwa na Prof. Ibrahim Lipumba ambaye amekuwa chanzo cha mgogoro ndani ya Chama ambacho alitangaza hadharani kuachia ngazi zake wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2015.

**Mheshimiwa Spika**, mmoja wa wanakikundi cha Prof. Lipumba Ndugu Abdul Kambaya alikiri hadharani kuwa vijana waliowavamia waandishi wa habari ni vijana wanaotokana na genge lao. Cha kushangaza zaidi ni kuwa toka, matamshi hayo ayatoe hadharani amekaa muda mrefu mtaani bila kuchukuliwa hatua yoyote hali inayoonesha kuwa serikali inajua vema uwepo wa watu hao ambao wamewaumiza waandishi wa habari.

**Mheshimiwa Spika**, Baadhi ya waandishi wa habari kama vile Asha Bani wa gazeti la Mtanzania na Fredy Mwanjala wa kituo cha runinga cha Channel ten, ni miongoni mwa waandishi ambao wameumizwa na kikundi hicho cha Prof. Lipumba.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawashauri waandishi wa habari kutotoa taarifa zinazomhusu Prof, Lipumba na watu wake kama wambavyo wamefanya kwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kwamba huo ni mkakati wa serikali wa kutaka kuvigombanisha vyombo vya habari na vyama vya Upinzani nchini hasa Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA). Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inalaani matukio yote yanayoashiria kuvuruga amani ya nchi yetu.

### iii. Kukamatwa kwa Waandishi wa Habari kwa amri za Wakuu wa Wilaya

**Mheshimiwa Spika**, ukiacha Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, yupo Mkuu wa Wilaya ya Arumeru Alexander Mnyeti ambaye naye amekuwa akiwanyanyasa waandishi wa habari. Tarehe 21 Desemba 2016 aliamuru Mwandishi wa habari wa ITV/Radio One Ndugu Halfan Lihundi kukamatwa na kuwekwa ndani kwa saa 24 kwa sababu ya kutoa na kuripoti taarifa mbalimbali zinazohusu matatizo ya wananchi hasa migogoro ya ardhi na tatizo la Maji bila kuishirikisha au kupata kibali cha Serikali ya Wilaya.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa zinaonesha kuwa Halfan Lihundi alihojiwa na Jeshi la Polisi na kufunguliwa jalada la uchochezi. Baada ya kelele za wadau ilipofika tarehe 22 Desemba 2016 mwandishi huyo wa habari aliachiwa huru na Jeshi la Polisi bila masharti yoyote. Huu ni uonevu ndani ya Taifa letu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza itaacha lini uonevu wa kiasi hiki? Aidha, Serikali sasa iwapatie semina elekezi wakuu wa Mikoa na Wilaya ili watekeleze majukumu yao kwa kuzingatia sheria.

**Mheshimiwa Spika**, Kama hiyo haitoshi tarehe 7 Februari, 2017 waandishi wa habari wawili walikamatwa na kuhojiwa katika Kituo cha Polisi cha Usa River mkoani Arusha, kwa amri ya Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Alexander Mnyeti. Waandishi waliokamatwa ni Bahati Chume wa gazeti la Mwananchi Mkoa wa Kilimanjaro na Dorine Alois kutoka kituo cha Sunrise Radio cha jijini Arusha.

**Mheshimiwa Spika,** Waandishi hao walikamatwa walipokuwa wakifuatilia habari ya mgogoro kwenye machimbo ya kokoto katika Kijiji cha Kolila mpakani mwa Wilaya za Arumeru na Hai. Baadaye waliandika maelezo juu ya madai kuwa waliingia katika kijiji hicho bila taarifa ya mkuu wa Wilaya Mnyeti.

**Mheshimiwa Spika**, ikumbukwe pia kuwa ni Mnyeti na Makonda ambao wote kwa nyakati tofauti wamenukuliwa wakitoa maneno ya kulidharau Bunge kinyume na Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge na wameshakwisha kuhojiwa na Kamati ya Bunge ya masuala hayo na Bunge kuazimia kuwasamehe.

**Mheshimiwa Spika,** Naye Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Mkoani Tanga Godwin Gondwe ambaye ni Mwandishi wa habari wa siku nyingi na anayetambua kazi za habari, aliamuru Jeshi la Polisi kuwakamata na kuwaweka ndani waandishi wa habari wawili waliokuwa wakifuatilia tukio la kufukuzwa kwa wachimbaji wadogo 3,000 eneo la mlima wa Mazigamba, Kijiji cha Nyasa Wilayani Handeni.

**Mheshimiwa Spika**, Tukio hilo lilitokea tarehe 5 Novemba 2016, majira ya saa 8 mchana ambapo mwandishi wa Clouds Tv Salehe Masoud na mwadishi wa Star Tv MacDonald walikamatwa na kuwekwa mahabusu kwa saa 8 huku mwandishi wa gazeti la Tanzania Daima, Nasra Abdallah akifanikiwa kutoroka.

**Mheshimiwa Spika,** Agizo la Gondwe kutaka waandishi hao wakamatwe lilitokea baada ya wanahabari hao kufika katika eneo la mgodi na kupata picha ambako nyumba za wakazi wa eneo hilo zimechomwa moto na baadhi ya mali kuteketea.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya wanahabari kufika eneo hilo Polisi waliwaamuru kuzima Kamera zao kutokana na kupewa amri ya Mkuu wa Wilaya. Mmoja wa Askari Polisi alihoji waandishi hao kwanini wamekwenda kwenye eneo

hilo bila ruhusa ya Mkuu wa Wilaya, hivyo kutaka waondoke kwakuwa hawana kibali wala taarifa za ujio wao.

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo, waandishi hao waliwaeleza Polisi kuwa hawalazimiki kuwa na vibali kufika kwenye matukio ya aina hiyo na kwamba wamekwenda ili kufahamu tukio hilo kwa undani, kwani kuna taarifa kuwa baadhi ya wananchi wameuawa kwenye operesheni hiyo na maiti zao bado hazijaondolewa.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya mabishano kama dakika 45 ndipo mmoja wa mapolisi hao aliwaongoza waandishi kwa Mkuu wa Operesheni ambapo nae alikataa kuzungumza chochote na kuwataka waende kwa Mkuu wa Polisi kituo cha Handeni.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kwamba waandishi hao waliomba kupiga picha kwanza ndipo waende huko, lakini walikataliwa ambapo Polisi huyo aliwaamuru waliopo chini yake kuwaondoa waandishi eneo hilo huku wakiwasindikiza na mitutu ya bunduki na wengine wakiendelea kupiga mabomu.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kukamatwa waandishi hao walipelekwa kituo cha polisi Handeni ambapo walikaa huko kuanzia saa 8 mchana hadi saa 3 usiku ambapo walitolewa kutokana na juhudi za wahariri akiwemo Katibu wa Jukwaa la wahariri Neville Meena kuzungumza na Gondwe.

**Mheshimiwa Spika,** Wakuu wa Wilaya wanaonekana kutumia madaraka yao vibaya kunyang'anya uhuru wa waaandishi wa habari na kuwanyima wananchi haki ya kujua kinachoendelea nchini. Matumuzi mabaya ya madaraka yanawafanya baadhi ya wakuu wa Wilaya kuwa wahariri kwenye vyombo vya habari na papo hapo, kuwa walalamikaji na waamuzi ambao wanaweza kuamua mtu kuswekwa ndani kwa amri zao.

**Mheshimiwa Spika**, viongozi hawa na wengine wenye tabia kama hizi hawafai kuwepo katika utumishi wa umma. Ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa serikali kuwachukulia hatua ikiwemo kuwafukuza kazi kwa sababu wametenda makosa ya kukiuka uhuru wa vyombo vya habari, kutumia madaraka yao vibaya pamoja na kukiuka Maadili ya Viongozi wa Umma.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuileta Bungeni Sheria inayowapa wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya uwezo wa kuwaweka rumande raia kwa masaa 48 ili sheria hiyo tuifute kwa kuwa haina maslahi kwa Taifa na hutumiwa na Serikali kukandamiza haki za kiraia ndani ya Taifa. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe maelezo ni wapi Askari Polisi wametoa mamlaka ya kuwazuia waandishi wa habari kufanya shughuli zao za kutafuta habari ambazo huzifanya kwa mujibu wa Katiba ya Nchi na sheria zilizopo.

### iv. Kufungiwa kwa Magazeti na Stesheni za Radio

**Mheshimiwa Spika,** Katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa mwaka wa fedha 2016/2017 tulieleza masikitiko yetu kufuatia uamuzi wa serikali kupitia Gazeti la serikali namba 03 juzuu ya 97 wa kufuta gazeti la Mawio katika orodha ya magazeti nchini bila hata kusikiliza wamiliki na waendeshaji wa gezeti hilo. Hata hivyo, mwezi Machi mwaka huu 2017, Mahakama Kuu Masjala ya Dar es Salaam ilikosoa uamuzi wa Serikali wa kulifungia gazeti hilo. Mmoja wa wanaharakati wa haki za binadamu alinukuliwa akisema kuwa uamuzi wa Serikali kulifungia gazeti la Mawio ni mwendelezo wa falsafa ya *“Nyonga kwanza kusikiliza baadae”.*

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kauli ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kulaani Serikali kulifungia gazeti la Mawio, bado Serikali ikalifungia gazeti la Mseto kwa miezi 36 na mpaka sasa bado lipo kifungoni na waandishi wa habari wa gazeti hilo kuendelea kuripoti Makao Makuu ya Jeshi la Polisi.

**Mheshimiwa Spika**, vituo vya radio navyo havijawa salama kutoka kwenye mkono wa Serikali, kwa sababu tarehe 29 Agosti mwaka 2016 vituo vya radio Five na Magic FM vilifungiwa na Waziri mwenye dhamana ya habari ili kuchunguzwa na Kamati ya Maudhuo ya TCRA. Kitendo cha kuvifungia vituo hivyo vya radio kwa sababu za jumla kuwa vimekuwa vikitangaza habari za uchochezi, ni kitendo cha uonevu na mwendelezo wa falsafa ile ile ya nyonga kwanza sikiliza baadae.

### v. Utekaji nyara na Ukamataji holela wa Wasanii Nchini

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 26 Machi, 2017 Msanii Emmanuel Elibariki alias 'Ney wa Mitego' alikamatwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za uchochezi kwa kuueleza umma ukweli juu ya kukosekana kwa uhuru wa kujieleza kupitia wimbo wake maarufu ***"WAPO"*.** Kutokana na hali hiyo, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) liliamua kupiga marufuku wimbo wa WAPO usichezwe mahali popote. Hata hivyo, baadaye serikali iliruhusu wimbo huo upigwe bila kutoa sababu za kuukataza katika hatua ya kwanza. Jambo hili linaifanya Serikali kuonekana kufanya mambo bila mpangilio na hivyo kuifanya kutoaminika katika maamuzi yake.

**Mheshimiwa Spika,** Utamaduni wa kuwakamata wasanii haukuishia kwa Msanii Ney wa Mitego. Msanii Roma Mkatoliki alitekwa na kurejeshwa kwa namna ya utatanishi sana ambayo mpaka sasa kuna maswali mengi ambayo hayajapatiwa majibu.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo ya kina juu ya watekaji wa ROMA Mkatoliki na Jeshi la Polisi liwasake na kuwakamata watu wote waliohusika na utekaji huo ili wafikishwe Mahakamani kujibu mashtaka dhidi yao. Ni vema sasa serikali ikachukua hatua ya kuwakamata watekaji hao kuonesha kwamba kweli ina mkono mrefu.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha Kambi Rasmi ya Upinzani tunampa ujasiri ROMA atoke mbele ya jamii aeleze kwa uwazi yaliyomkuta na aliyofanyiwa, hii itasaidia katika kutambua ni kikundi gani kinafanya vitendo hivyo na kujua kuwa wanafanya hivyo kwa niaba ya nani.

### vi. Bunge Live bado Kizungumkuti

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 27 Januari 2016 serikali kupitia Waziri wa Habari wakati huo Mheshimiwa Nape Moses Nnauye ilitoa kauli hapa Bungeni kuwa imezuia Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) kurusha moja kwa moja vipindi vya Bunge kutoka Dodoma.

**Mheshimiwa Spika,** sababu kubwa iliyotolewa wakati huo ilikuwa ni gharama kubwa ya kurusha matangazo hayo kwa sababu Serikali ilikuwa imeamua kubana matumizi na kupeleka fedha kwenye miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kauli wadau kadhaa ikiwemo Kampuni ya Uhai Media na asasi zingine binafsi zilijitokeza na kuonesha nia ya kurusha matangazo ya Bunge moja kwa moja, serikali ilikuja na sababu nyingine kwamba wananchi wanashindwa kufanya kazi kutokana na kuangalia mijadala ya Bunge, hivyo imesitisha matangazo hayo ili wananchi wapate nafasi ya kufanya kazi.

**Mheshimiwa Spika,** niliihoji serikali kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika hotuba yangu ya mwaka wa fedha uliopita, kuwa kama tatizo ni fedha ni kwa nini hawaruhusu mashirika binafsi kurusha matangazo ya Bunge? Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kusisitiza kuwa, uamuzi wa kutorusha matangazo ya Bunge sio unawakosesha wananchi haki yao kwa mujibu wa ibara ya 18 (d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, bali pia inarudisha nchi yetu nyuma kwa kuondoa utamaduni tuliokwisha kujijengea kwa muda mrefu wa wananchi kuona namna wawakilishi wao wanavyotekeleza majukumu yao na serikali ikiwajibika kwao kupitia Bunge lako tukufu.

**Mheshimiwa Spika,** badala ya vyombo vya habari vya umma kurusha matangazo ya moja kwa moja ya Bunge, ili wananchi waweze kufuatilia vikao vya Bunge, tena kwa kipindi hiki muhimu cha kujadili Bajeti ya Serikali, sasa hivi vyombo hivyo vimekuwa vikirusha matangazo yanayomuonesha Mkuu wa nchi na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Paul Makonda. Ni dhahiri kuwa sasa kuna watu katika nchi hii wanaona wana sifa za pekee kuliko Mhimili wa Bunge na hivyo ni wao tu ndio wanastahili kuonekana moja kwa moja wakitekeleza majukumu yao. Huu ni ubaguzi na ubinafsi wa hali ya juu kufanywa na viongozi wakubwa wa nchi.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa zinaonesha kuwa tayari Bunge limepata leseni ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuruhusu Channel yake kufanya kazi ya kurusha matangazo. Kwa kuwa ilionekana ni gharama kulitumia Shirika la Utangazaji Tanzania, na kwa sasa kama nilivyoeleza channel ya Bunge imepata leseni na ithibati kutoka TCRA ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kupitia kwa Kamisheni ya Bunge kwa kushirikiana na wadau kurudisha utaratibu wa kurusha matangazo ya moja kwa moja ya Bunge ili wananchi waendelee kupata haki yao ya kuona na kujua kinachoendelea Bungeni.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani ina uhakika kwamba Bunge kwa kurusha mubashara matangazo yake, wadhamini wengi watajitokeza na hivyo channel hiyo itakuwa inafanya biashara nzuri na hivyo miradi mingi ya Maendeleo ya Bunge ambayo ilikuwa imesimama kwa ukosefu wa fedha itaweza kuendelea.

## 4. KUYUMBA KWA UCHUMI NA ATHARI ZAKE KATIKA TASNIA YA HABARI

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na serikali ya awamu ya tano ambazo kwa namna moja ama nyingine zimekuwa na athari katika ukuaji wa sekta binafsi. Hii ni pamoja na uamuzi wa kuondoa au

kupunguza matangazo ya serikali kwenye vyombo vya habari vinavyomilikiwa na watu binafsi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hayo kufungwa kwa biashara nyingi katika miji na majiji nchini kumepunguza matangazo mbalimbali ya biashara katika vyombo vya habari hali inayopelekea vyombo vingi vya habari kuyumba kimapato. Hii si ishara njema katika sekta ya habari nchini, Kambi Rasmi ya Upinzani inadhani kuwa huu ni mkakati wa serikali kuviua vyombo vya habari binafsi ili kuendelea kutumia vyombo vya habari vya umma pekee.

**Mheshimiwa Spika,** ukisoma taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka fedha 2016/2017, moja ya sababu zilizochangia Mashirika ya TBC (Shirika la Utangazaji Tanzania) na TSN (Kampuni ya Magazeti ya Serikali) kushindwa kukusanya maduhuli pamoja na mambo mengine, serikali inakiri yenyewe kuwa ni kushuka kwa biashara sokoni kutokana na baadhi ya biashara kufungwa na makampuni mengi kubana matumizi na kupunguza bajeti.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuangalia namna bora ya kuhakikisha kuwa pamoja na kupenda sana matumizi ya vyombo vya habari inatoa sera na kodi ambazo ni rafiki katika ukuaji wa sekta hii ikiwemo na vyombo vinavyomilikiwa na serikali. Kambi ya Upinzani inapenda kutoa tahadhari kuwa, kama hatua hazitachukuliwa, tutarajie vyombo vingi vya habari kufunga shughuli zao na waaandishi wengi wa habari pamoja na waajiriwa wengine wa sekta ya habari kusimamishwa kazi kutokana na ukata.

**Mheshimiwa Spika**, ni lazima serikali itambue kuwa sekta ya habari inategemea ukuaji wa uchumi na sekta binafsi kwa upande mwingine, hivyo ni lazima kwa mwaka ujao wa fedha Bunge liangalie namna bora ya kuishauri serikali kwenye masuala ya kodi na ukuaji wa biashara ili kuweza kuchochea ukuaji wa sekta ya habari.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bunge inaitaka serikali kuhakikisha kuwa inavipa bajeti ya kutosha vyombo vinavyomilikiwa na umma na kuacha kuviingilia ili viwe na ubunifu wa namna bora ya kuhimili ushindani wa soko kwa sababu moja ya changamoto katika vyombo hivyo ni kushindwa kuhimili soko la habari. Haishangazi kuona Rais anawasiliana kwa karibu na vyombo vya habari binafsi na sio mashirika ya habari ya umma kwa sababu ya kukosa weledi na ubunifu katika utekelezaji wa majukumu yao. Kambi ya Upinzani haishangai kuona TBC wakitangaza habari za uongo zilizopikwa mitandaoni bila kufanya tafiti za kina kabla ya kuzitoa kwa umma. Ni lazima TBC ijitathmini kuacha ushabiki wa kisiasa na kuegemea kwenye taaluma.

## 5. WIZI WA KAZI ZA WASANII

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa serikali ya awamu ya nne nilizungumza kwa kirefu namna ya kulinda kazi za wasanii nchini. Moja ya pendekezo ambalo baadae lilichukuliwa na serikali ni kutumia stika maalumu ambazo zitatoa utambulisho wa kazi halisi za wasanii kuzuia wizi wa kazi za wasanii. Pamoja na serikali kutumia stika za Mamlaka ya Mapato (TRA) bado tatizo hili halikupata ufumbuzi. Hii ni kutokana wizi wa kazi za wasanii kuendelea kuwepo.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na kuwa sisi Kambi Rasmi ya Upinzani ndio chanzo na msingi wa hoja ya matumizi ya stika katika kulinda kazi za wasanii, napenda kusisitiza na kuieleza serikali na Bunge lako tukufu kuwa kwa sasa dunia imekwenda mbele zaidi kwa sababu kwa sasa biashara ya muziki na filamu inafanyika kwa kutumia mitandao zaidi na wasanii duniani kote sasa wanafanya biashara ya muziki kwa kutumia mitandao kama vile Youtube, iTune na mitandao mingine kusambaza na kuuza kazi zao.

**Mheshimiwa Spika**, kwa hapa nchini wasanii wanaojitambua wamekuwa wakitumia mtandao maarufu wa MKITO, Blogs, Websites zingine na biashara zao kuendelea na kuwanufaisha kiuchumi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeshangazwa na kauli na hatua za kipropaganda

anazofanya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam baada ya kutangaza kuwa anazuia kazi za wasanii wa filamu kutoka nje ya nchi, hii inatokana na kutokufahamu kuwa kuzuia filamu za nje sio kinga ya kuzuia wizi wa kazi za wasanii au hata kuboresha soko la kazi zao bali njia pekee ni kuhakikisha kuwa wanaboresha kazi zao kwa kuongeza ubunifu na kutumia njia za kisasa kuuza na kutangaza kazi zao.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuacha kuitazama mitandao ya kijamii kwa jicho hasi na badala yake waione kama sehemu ya ajira kwa wasanii wetu ili kuwasaidia kukuza kipato chao na kujitangaza kimataifa. Aidha Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawaasa wasanii kutotumika kisiasa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ambaye hata hivyo amesusiwa na vyombo vya habari kutokana na matendo yake yasiyokuwa ya kimaadili na matumizi mabaya ya madaraka yaliyopitiliza.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kulieleza Bunge lako tukufu kuhusu agizo la Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam la kazuia kazi za wasanii wa nje kuingia nchini kama ndio msimamo wa serikali au ni kwa Mkoa wa Dar es Salaam pekee na kama anayo mamlaka kisheria kutoa agizo alilotoa au ni kujitaftia umaarufu baada ya kukataliwa na tasnia ya habari.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa wasanii nchini kuimarisha vyama vyao vilivyopo kama vile TUMA, CHAMUDATA, BONGO MOVIE! Na vingine ili kusimamia maendeleo yao halisi na sio kutumika kisiasa na watu ambao hawana uelewa wa kazi ya sanaa na zaidi ya kutaka kujipa umaarufu wa kisiasa. Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kusisitiza kuwa kazi za sanaa na sheria zinazosimamia hati miliki ni za kitaifa na kimataifa na katika masuala hayo Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ametoa agizo ambalo hajui athari zake katika kazi ya sanaa hasa kwenye mikataba ya kimataifa.

## 6. SEKTA YA MICHEZO

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza hoja yake kwa mwaka uliopita kuwa, ili tuweze kuendeleza michezo ni lazima serikali iwekeze katika michezo. Serikali haiwezi kutegemea mafanikio katika michezo kama fedha za maendeleo kwenye Wizara mpaka Februari 2017 imetolewa kwa asimili 6 pekee.

**Mheshimiwa Soika,** Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikisisitiza mara kwa mara kuwa michezo kwa kiwango kikubwa Duniani ni biashara na sio burudani kama ambavyo hapa Tanzania inavyochukuliwa.Kwa dhana hiyo ya michezo ni biashara, ni lazima tufanye uwekezaji, kwani biashara yoyote ile, ili iende vizuri ni lazima uwekezaji wa maana ufanyike.

**Mheshimiwa Spika,** katika uwekezaji huo ni lazima uanzie kwenye ngazi ya chini, kwa kuwatayarisha watoto wetu kuwa wachezaji wazuri wa michezo mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika, katika hilo naomba kunukuu ushauri uliotolewa na Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani, kwa Ofisi ya Rais- TAMISEMI kuhusu nini kifanyike ikiwa ni mwanzo wa uwekezaji katika michezo;**

*“**Mheshimiwa Spika**, Shughuli za Michezo na utamaduni katika halimashauri zinakuwa chini ya idara ya Elimu ya Msingi ambayo ina majukumu makubwa sana ya kushughulikia elimu ya Msingi na sehemu kubwa ya bajeti yake ya matumizi ya kawaida inatoka serikali kuu. Kitengo cha Michezo na utamaduni kinakuwa kimemezwa na shughuli za Elimu ya Msingi hivyo kushindwa kutimiza majukumu yake kwa ufanisi.*

***Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri serikali kuunda idara mpya ya Michezo na utamaduni katika halimashauri hapa nchini ili kuinua na kuhamasisha shughuli za Michezo na utamaduni katika nchi yetu kwavile zitalazimisha serikali kuu na Halimashauri*

*kutenga fedha za kutosha katika bajeti kwa ajili ya idara hiyo ya Michezo na utamaduni".*

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka uliopita, tulisisitiza kuwa ni lazima tuhakikishe kuwa Viwanja vya Michezo vinaboreshwa ili kukidhi mahitaji ya sekta ya michezo. Aidha tunapenda kurudia kuwa, ni lazima viwanja vyote vilivyopokwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) huku wakijua kuwa ni mali ya wananchi wote kwa kuwa vilipatikana kabla ya mfumo wa vyama vingi kuanza. Ni lazima baadhi ya Halmashauri na Serikali Kuu ivichukue viwanja vya CCM kwa kuwa Chama hicho kimeshindwa hata kuviendeleza.

## 7. SEKTA YA UTAMADUNI

**Mheshimiwa Spika,** serikali hii bado haijaona umuhimu wa kuendeleza sekta ya utamaduni nchini. Ieleweke kuwa utamaduni si tu ni utambulisho wa utaifa bali pia sekta hiyo ikiboreshwa vizuri inaweza kuwa chanzo cha mapato kwa kuvutia watalii wa nje na ndani.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa awamu ya nne serikali iliunda Kamati iliyokuwa inaratibu na kukamilisha mchakato wa vazi la taifa. Kamati hiyo ilitumia fedha lakini hatujaweza kujulishwa kama mchakato huo ulikamilika..Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza mbele ya Bunge hili mchakato wa vazi la taifa umefikia wapi na nini hatma yake.

## 8. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara hii ilitengewa shilingi bilioni 3 kwa ajili ya miradi ya maendeleo, hadi kufikia Februari mwaka huu Wizara ilipokea shilingi 190,324,000 sawa na asilimia 6 pekee. Hii ina maana kwamba, bajeti ya maendeleo haijatekelezwa kwa asilimia 94.

**Mheshimiwa Spika,** kutotekeleza bajeti ya maendeleo katika wizara hii kwa asilimia 94, ni dharau na kunaonyesha

jinsi Serikali isivyothamini sekta ya habari, michezo na utamaduni. Ikumbukwe kwamba Chama cha Mapinduzi na Serikali yake ndio wanufaikaji wakubwa wa sekta hii hasa kipindi cha kampeni za uchaguzi kinapofika. Kipindi cha kampeni utaona jinsi CCM inavyojikomba kwa wasanii na kuwatumia katika kampeni zao, lakini uchaguzi unapopita wanawasahau wasanii na wanamichezo kwa ujumla. Kutenga bajeti ndogo kwa sekta hii na mbaya zaidi kutoitekeleza kwa asilimia 94 ni majibu tosha kwamba sekta hii sio kipaumbele kwa Serikali. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawatahadhariha wasanii na wanamichezo wote nchini, kuwa makini na ulaghai unaofanywa na CCM na serikali yake kwa kuwapa vijizawadi kipindi cha kampeni kuonyesha kwamba inawajali, lakini *'deep down'* haina mpango nao kabisa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwendo huu wa utoaji fedha za miradi ya maendeleo ni ishara kuwa serikali haina nia ya kuendeleza sekta zilizopo ndani ya Wizara hii.

## 9. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba nimalizie hotuba yangu kwa kumnukuu msomi na mwanafalsafa wa fasihi andishi wa nchini Marekani, Jill McCorkle aliyesema: ***"By limiting or denying freedom of speech and expression, we take away a lot of potential. We take away thoughts and ideas before they even have the opportunity to hatch. We build a world around negatives – you can't say, think, or do this or that"***

**Mheshimiwa Spika,** kwa tasfiri isiyo rasmi ni kwamba, kwa kuminya uhuru wa habari na kujieleza tunaondoa mambo mengi yenye faida. Tunatupilia mbali mawazo na fikra kabla hata hayajafikia hatua ya kuzaliwa. Tunajenga mazingira katika ulimwengu hasi ambapo huwezi kusema chochote, huwezi kufikiri, huwezi kufanya hiki wala kile. Kwa maneno mengine Mheshimiwa Spika, ni kama uko kwenye ulimwengu wa giza, na kwa hali hiyo hakuna hatua yoyote ya maendeleo inaweza kupigwa.

***[Baadhi ya Aya zimeondolewa kwa Maelekezo ya Kiti]***

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Joseph Osmund Mbilinyi (Mb)
**WAZIRI KIVULI NA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, KATIKA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, WASANII NA MICHEZO**
5 Mei, 2017

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mwongozo wa Mwenyekiti

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaamini kwenye upande wa Kanuni.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mwongozo wa Mwenyekiti

**MWENYEKITI:** Mlinga kaa, hatuna miongozo sasa hivi. Tunaanza uchangiaji na Mheshimiwa Juma Nkamia ajiandae Cosato Chumi.

**MBUNGE FULANI:** Huu ni mpunga wa Ulanga.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie kwa uchache tu, kuhusu Wizara hii ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu *Subhana wataala* kwa kunipa afya njema na kusimama leo mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kuchangia machache kwa lengo la kuisaidia Serikali kuboresha pale ambapo naamini inaweza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayoifanya. Mimi simpongezi tu Mheshimiwa Rais hivi hivi bali nampongeza kwa kuzingatia vigezo vitatu vya *leadership.* Kwanza ujasiri, pili, uthubutu na tatu kujiamini kwake. Katika falsafa za kiongozi bora akiwa na misingi hii mitatu, anakuwa kiongozi bora. Ndivyo ambavyo Mheshimiwa Rais anafanya, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu wake pamoja na Serikali yote kwa ujumla. Nampongeza sana Mheshimiwa Harrison Mwakyembe, Naibu wake na Watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kweli Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ibara ya 18 na hata Sera ya habari ya 1993 inazungumza juu ya kwamba kila mtu ana haki ya kupata habari. Sina haja ya kwenda mbali sana, lakini haki ya kupata habari pamoja na wajibu wa kupata habari vyote hivi vinategemeana. Haki bila wajibu haiwezi kwenda. Si kwa sababu tu Katiba inatamka na Tanzania imeridhia matamko ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika, watu wavunje sheria tu kwa makusudi kwa sababu Katiba imetaka hivyo. Sidhani kama hiyo ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti Waadishi wa habari wa nchi hii wanafanyakazi kubwa sana. Vyombo vya habari vinavyafanya kazi kubwa sana, lakini kuna kitu kimoja ambacho sisi waandishi tunasahau. Mwandishi wa habari ni *sub-soldier,* hili lazima ulielewe. Hakuna nchi yoyote duniani, mimi siamini na sijawahi kuona kwamba vyombo vya habari vinaweza vikaamka tu magazeti yanatunaka tu watu wakaa kimya. Ndiyo maana ya kuwa na *state. State* maana yake ni ku- *protect citizen* wake katika Taifa lile. Ndivyo ambavyo kazi inafanya. Nawashukuruni sana Mheshimiwa Waziri endeleana na moyo huo huo, chapa kazi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nizungumzie kidogo kuhusu michezo. Mpira wa miguu ndio mchezo unaopendwa kuliko yote duniani kwa sasa hivi. Naipongeza sana timu yetu ya Serengeti *boys* na viongozi wa *TFF*. Hata hivyo, timu za

vijana hazijengwi na *TFF,* zinajengwa na vilabu. Hili lazima *TFF;* na nashukuru rais wa *TFF*, Rais anayemaliza muda wake yuko hapa; ninachosema lazima Vilabu viakikishiwe kwamba kweli vina wachezaji wa timu za vijana. Tusijidanganye tukasema *TFF* ama Serikali inaweza kuwa na *academy* yake kuwatengeneza wachezaji, hiyo haijatokea duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti ni imani yangu kwamba Mheshimiwa Waziri na bahati nzuri sasa kwamba *FIFA* imetoa *room* kwa Serikali ku-*interfere* pale ambapo wanaona mashirikisho ya mpira na michezo mingine hayafanyi vizuri tofauti na ilivyokuwa wakati wa *Blatter.* Kwa hiyo Mheshimiwa Mwakyembe *you have the room,* ukiona hapaendi vizuri *FIFA* imetoa hiyo. Jitahidi sana, lazima tuhakikishe vilabu hivi vinakuwa na timu za vijana zilizo imara ili tupate *national* timu inayoweza kwenda kushindana. *Otherwise* tutapiga kelele miaka nenda, miaka rudi, hatuwezi kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nidhamu pia kwa wachezaji, wachezaji wasipokuwa na nidhamu; hata hapa ndani ya Bunge ndiyo maana tunatunga hizi kanuni ili tuwe na nidhamu. Kama hawana nidhamu hatuwezi kufanya vizuri katika michezo, hili lazima tuliangalie. Sitaki kuzungumzia rafiki zangu hapa wananiambia *point* za Kagera nasema hizo nawachia *TFF* watajua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kidogo kuhusu Shirika la Utangazaji Tanzania. Mimi kwa maono yangu na kwa mtazamo wangu na kwa *analysis* nzuri tu kwamba uanzishwaji wa Redio Tanzania kubadilishwa kuwa Shirika la *TBC* lazima kuna makosa yalifanyika. Hili shirika ni shirika la habari, lakini halina tofauti kimuundo na *TANESCO,* halina tofauti kimuundo na bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo *TBC* pale kuna Wakurugenzi zaidi ya 10, mameneja 14 wakati pale wanahitajika viongozi wanne tu. Mkurugenzi Mkuu, Mkuu wa vipindi, *CP,* Meneja wa Ufundi, umemaliza. Mheshimiwa Waziri angalieni Muundo wa lile Shirika ndiyo maana leo wanapata tabu sana. Lile ni *broadcasting house* siyo Shirika la Uzalishaji,

hapo ndipo tatizo linapotokea. Leo Ryoba anapata tabu sana pale kwa sababu anashindwa kuendesha lile shirika limekuwa ni kama shirika la uzalishaji na si *broadcasting house. Angalieni hilo. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna matatizo ya vifaa, hata ile *studio* ambayo ilitengenezwa wakati ule wa *TVT* ndiyo studio inahusika kuzalisha matangazo yaende huko nje. Usikivu umekuwa duni. Leo ukienda huko Pangani wapi unasikia *KBC* Kenya. Hapa Chemba ukienda kwa Mtoro ndiyo hatusikiki kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko Mlalo ndio kabisa wanasikia Kenya. Ukienda huko Tanganyika huko wanasikiliza Kongo. Lazima tufanye *investment* ya kutosha. Hata *live coverage* ni aibu kabisa kwa Shirika kubwa kama lile kwenda kuazima chombo cha kurushia matangazo kutoka kwa mtu binafsi. Kabisa! Ni aibu! Juzi Rais anakwenda Mtwara wameazima chombo kwa mtu binafsi Benjamin, pale wanalipa sijui dola mia sita sijui ngapi ni aibu. Msaidieni Ryoba yule, vinginevyo atashindwa. *(Makafi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hii tunayotumia hapa Bunge imetengenezwa tu *amplifier lakini pia zile flyways zina life Span.* Nunueni vingine na nimefurahi kusikia Mheshimiwa Waziri kwamba mwezi wa sita vitakuja vingine. Wazee sisi wengine tumekulia pale kama siyo *TBC* tusingekuwa hapa. Mimi mtoto wa mfinyanga vyungu naingia Bungeni, kama si *TBC* tusingekuwa hapa leo. Kwa hiyo, isaidieni sana *TBC* hasa kwenye vifaa lakini na muundo wake. Mheshimiwa Mwakyembe nakujua fanyakazi yako angalia ile shirika vizuri badilisha *style* irudi kuwa *broadcasting house* na siyo shirika la uzalishaji. Weka viongozi wanne tu Mkurugenzi Mkuu, wa Ufundi, *Control programs* umemaliza unasonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Sixtus Mapunda jiandae. Mheshimiwa Cosato Chumi.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa na mimi nafasi ya kuchangia kwenye Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Naomba nichangie kwenye maeneo mawili, eneo la kwanza nitachangia eneo la michezo na eneo la pili nitachangia kwenye eneo la utamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kuu inayoikabili Wizara hii katika kukuza sekta ya michezo, sekta ya habari, sanaa na Utamaduni nchini ni changamoto fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 161 cha Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 - 2020 kinasema yafuatayo:-

*"Katika kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa Ilani hii, Serikali itaimarisha sekta ya michezo nchini kwa kuifanya sekta ya michezo kutoa fursa ya ajira hususan kwa vijana kwa kupanua wigo wa vyanzo endelevu vya fedha za uendeshaji na ugharimishaji wa maeneo ya michezo hapa nchini kwa kuanzisha bahati nasibu ya michezo." (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo ilikuwa *commitment* ambayo tuliitarajia sasa, baada ya miaka miwili ya kuwa madarakani Wizara ingekuja na mkakati wa kuanzisha hicho chombo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri ufuatao; badala ya Serikali kwenda kuanzisha chombo kingine cha bahati nasibu, ni vyema sasa ingetumika hii Bodi ya Bahati Nasibu ya sasa, isipokuwa iboreshwe kidogo. Sasa inafanya kazi zake ikiwa chini ya Wizara ya Fedha na ukiangalia kwa ujumla wake, Wizara ya Fedha ina majukumu mengi, haiwezi ikafanya kazi vizuri na ikaifanya hii Bodi ya Bahati Nasibu ikaleta mapato yale tunayoyatarajia ukilinganisha na nchi nyingine waliyowahi kufanya mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara ya Fedha na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, mkae

mkubaliane ihame huku ije kwenye Wizara ya Michezo. Nasema hivyo kwa sababu nne zifuatazo:-

Kwanza, msingi mkuu wa kuhamisha majukumu kuyapeleka kwenye Wizara ya Habari ulishaainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi; la pili, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ina miundombinu inayojitosheleza ya kuifanya ikafanya kazi vizuri kuliko ikikaa kwenye Wizara ya Fedha. Kwa sababu ili bahati nasibu ilete mapato mazuri inahitaji hamasa. Wizara ya Fedha haina *room* ya hamasa, ila kwenye michezo kuna hamasa. Tukiiweka hii italeta picha nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya tatu, wanaocheza hii michezo wana uhusiano wa moja kwa moja na michezo, kwa hiyo, ukiiweka kule kwenye Wizara ya Fedha inakuwa ime-*hang,* umeweka kitu kama mtoto mkiwa hana baba wala mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne na la mwisho, *the best practice* kutoka nchi nyingine, kuna nchi zimefanikiwa kwa kuweka hii kwenye Wizara ya Michezo na wakapata pesa nyingi za kuendesha Wizara. Brazil wanafanya hivyo, Australia wanafanya hivyo, Uingereza wanafanya hivyo na hata majirani zetu Kenya wanafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiombe Serikali isipate kigugumizi, isianzishe Bodi nyingine ya Bahati Nasibu, isipokuwa hii iliopo iondoke Wizara ya Fedha ikasimamiwe chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nataka kulichangia ni kuhusu utamaduni. Taifa lolote duniani linatambulika kutokana na utamaduni wake na hata kama zile nchi zilizokuwa na utamaduni wa pamoja unaoeleweka kama nchi yetu Tanzania tukiongea kiswahili tunaeleweka kama Watanzania, nchi nyingine zina alama nyingine

zinazotambulisha mataifa yao. Nchi yetu ukiondoa lugha ya kiswahili, ina mambo mengine ambayo yanalitambulisha Taifa letu.

Jambo la kwanza, ni Bendera ya Taifa; jambo la pili, Wimbo wa Taifa; jambo la tatu, Mwenge wa Uhuru na jambo la nne ni Ngao ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Mheshimiwa Dkt. Suleiman Ally Yussuf alikwenda mbali sana katika kuchangia, alifika hatua ya kusema Mwenge wa Uhuru uondolewe upelekwe kwenye makumbusho. Naomba nichukue fursa hii kuyasema yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzito wa Mwenge wa Uhuru ni ule ule, sawa sawa na Wimbo wa Taifa; uzito wa Mwenge wa Uhuru ni ule ule sawa sawa na Ngao ya Taifa, uzito wa Mwenge wa Uhuru ni ule ule sawa sawa na wimbo wa Taifa. Kwa nini nasema haya? Hayo mambo yote ni *package* moja.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

## T A A R I F A

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa mzungumzaji taarifa kwamba tofauti na Mwenge wa Uhuru; Bendera ya Taifa, Ngao ya Taifa, Wimbo wa Taifa vyote kwa pamoja vinaitwa *National Emblems* na vimetungiwa sheria mahususi na Bunge hili inayoitwa *National Emblems Act. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenge wa Uhuru haujawahi kutungiwa sheria na kwa hiyo, huwezi ukaulinganisha kwa vyovyote vile na kile kitu kinachoitwa Nembo za Taifa ambazo zinatambulika kisheria kwa sababu zimetungiwa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo taarifa yangu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Amekuelewa. Mheshimiwa Sixtus.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba unilindie muda wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa lolote duniani na mifumo yoyote ya sheria duniani inatokana na mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo sheria inayotungwa inaweza ikatokana na *the best practice.* Jambo hili limefanyika katika jamii kwa muda gani? Limekubalika katika jamii kwa muda gani? Hapo ndipo linapopelekea kwenye kutunga sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie kitu kimoja, mila na desturi za Taifa lolote lile zinatokana na historia yake. Huwezi ukauondoa Mwenge wa Uhuru kwenye historia ya Taifa letu. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kweli!

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwakumbushe kidogo, mwaka 1961 tulipopata uhuru tulikuwa na ajenda mahususi, tulisema mambo yafuatayo: "Sisi tunataka kuuwasha mwenge na kuuweka juu ya Mlima Kilimajaro umulike hata nje ya mipaka yetu ulete tumaini pale ambapo hapana matumaini, ulete upendo pale ambapo pana chuki na ulete heshima pale ambapo pana dharau."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hebu mniambie haya mambo yote mazuri, hivi kweli yapotee hewani! Huo ndiyo msingi wa historia ya utu wa Watanzania. Kwa hoja hiyo ninashangaa, kwa nini Mwenge wa Uhuru haukuwahi kutungiwa sheria! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo lilinikwaza jana, kuuita Mwenge wa Uhuru ni ibada. Kila jambo tukilifanyia ibada hatutafanya hata moja. Mwaka 2016 nilikuwa Jimboni, mwananchi mmoja akaniambia, Mheshimiwa Mbunge kwa nini mkiingia Bungeni mnafanya ibada? Nikamuuliza ibada gani? Akasema, ninyi mkifika si kwanza siwa mnaliinamia, hamfanyi kitu bila siwa na mkiondoka kama Bunge kwenda kwenye Kamati, siwa mnaifunika ndani, mkirudi wote mnasimama mnafanya ibada ya siwa. Jamani, wote tungesema hizi ni imani, tungefika? Kitu kimoja ninachotaka kusema, nchi yoyote unaitambua kwa vitu vingi; alama ni moja ya ishara ya kuitambua nchi. Ninamshangaa sana ndugu yangu, Mheshimiwa Tundu Lissu, amesema Ngao ya Taifa imetungiwa sheria, lakini hakujipa muda wa kutosha kuangalia Ngao ya Taifa imeundwa na nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambieni, kwenye Ngao ya Taifa ina mambo yafuatayo, kuna bibi na bwana, kuna pembe za ndovu mbili zikichunguliana, kuna mwenge wa uhuru umekaa katikati, chini yake kuna bendera, sasa sioni kipya hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo tunaweza tukafika sehemu tukaelewana, jambo ambalo tunaweza tuka-*discuss* tukaelewana kuhusu mwenge wa uhuru ni *modality* ya kuukimbiza mwenge wa uhuru. Hili liko *open to discussion. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuupeleka mwenge wa uhuru kwenye makumbusho, ni kuipeleka historia ya Taifa la Tanzania kwenye makumbusho. Haya mambo anayeweza kuyafanya ni yule ambaye sio mzalendo wa Taifa hili, ni yule ambaye hajui mambo matatu yanayoongelewa katika moto wa mbio za Mwenge ndiyo unayotengeneza utu wetu? Nani anapenda dharau humu ndani? Nani anapenda chuki humu ndani na nani ambaye hapendi heshima humu ndani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaombe ndugu zangu, mwenge wa uhuru ni jambo jema sana, ni jambo ambalo inabidi tulienzi, tuliheshimu, tukiudharau mwenge tutapata shida. Mimi najua kwa nini wanadharau mwenge. Siku zote historia ni nzuri hata kama aliyeandika ile historia... *(Makofi/ Vigelegele)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chumi, ajiandae Mheshimiwa Sugu.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na laiti ningejua Mheshimiwa Mapunda angekuwa na maneno mazito hivi, ningeridhia kumpa muda wangu, lakini kwa sababu ameshamaliza ngoja niendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuunga mkono hoja na kwa sababu muda unaweza ukaniwia mchache, nina mambo machache ya kuzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuzungumza kuhusu mchezo wa mpira ambao ndiyo unapendwa kuliko mchezo wowote. Katika kuzungumzia suala la mchezo wa mpira, napenda kuzungumzia umuhimu wa timu yetu ya Taifa kujiweka katika mazingira ambayo inaweza ikawa inapata nafasi za kushiriki katika mashindano ya Kombe la Dunia na mashindano ya *AFCON.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nina takwimu, katika takwimu za viwango vya *FIFA* mpaka mwezi Machi sisi Tanzania tulikuwa wa 157 wakati Afghanistan walikuwa wa 156, unaweza kupata picha ina maana hata Afghanistan wametuzidi sisi. Kwa nini inatokea hivi? Viwango vya *FIFA* vinapangwa kulingana na idadi ya mechi unazocheza zilizopo kwenye kalenda ya *FIFA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo letu sisi, wasimamizi wa mpira ambao ni *TFF* hawalizingatii hilo na matokeo yake tunacheza mechi chache sana kufuatana na kalenda ya *FIFA* kitu ambacho kingeweza kutupa sisi *points* za kupanda kwenye viwango vya *FIFA.* Sasa unapokuwa chini ya viwango vya *FIFA* maana yake ni nini? Hata unapopangiwa kwenye mashindano ya ku-*qualify* kwenda *AFCON* au kwenda *World Cup* unajikuta kwamba uko kwenye *pot four,* maana yake ni kwamba *pot one* wanaingia wale ambao ni vigogo kadhalika *pot two* na *pot three.* Sasa kila mara utakuta wewe unapangiwa na timu ambazo ni vigogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mashindano ya ku-*qualify* kwenda Kombe la Dunia, sisi mechi ya kwanza tulipangiwa na Malawi tukashinda, lakini mechi ya pili tukajikuta tunaangukia kwa Algeria. Kilichotupata wote mnajua, goli saba kwa mbili. Kwa sababu gani? Kwa sababu sisi hatushiriki ipasavyo mechi za Kimataifa kulingana na kalenda ya *FIFA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano, katika mwaka 2016 Tanzania imeshiriki mechi tatu tu ambazo ziko kwenye kalenda ya *FIFA* ukilinganisha na wenzetu, kwa mfano Rwanda wamecheza mechi 11, Uganda mechi 13, Kenya mechi 10, hata hao Afghanistan wenye matatizo, walicheza mechi sita; sisi tumecheza mechi tatu tu, utawezaje kupanda kwenye viwango vya *FIFA?*

**MBUNGE FULANI:** Haiwezekani.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama vile haitoshi, nimechukua takwimu za miaka mitatu iliyopita na miaka mitatu tuliyomo; katika kipindi cha miaka mitatu kutoka mwaka 2014 mpaka 2016 sisi tumecheza mechi za *FIFA* 24 tu ukilinganisha na Rwanda mechi 26, Uganda mechi 43, Kenya mechi 27, hata Afghanistan mechi 29. Sasa kuna watu hapa wanamkumbuka Leodgar Tenga, ni kwa sababu ya mambo kama haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha uongozi wa *TFF* ya sasa hivi tumecheza takribani mechi 24 tu; kwa kipindi kama hicho, wakati wa Tenga tumecheza mechi 47.

Sasa takwimu hizi ndiyo zitakupeleka kwenye viwango bora vya *FIFA* na ili ujihakikishie kuwa kwenye ushindani unaoweza kukupeleka kushiriki Kombe la Dunia au *AFCON,* lazima uwe kwenye viwango bora vya *FIFA* angalau namba moja mpaka 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kutoshiriki mechi hizi athari yake ni nini? Athari yake kama nilivyosema, unajikuta unapangiwa na vigogo kama Algeria. Kuonesha kwamba ushiriki wa mechi za *FIFA* ni muhimu, baada ya kucheza mechi zilizopo kwenye kalenda ya *FIFA* na Burundi na Botswana, ukienda kwenye takwimu za *FIFA World Rankings* zilizotoka jana, tarehe 4 Mei, sasa hivi kutoka 157 tumefika 135. Kwa hiyo, kuna umuhimu sana wa *TFF* kujikita katika kuhakikisha kwamba inahakikisha kuwa Timu ya Taifa inacheza mechi nyingi kulingana na kalenda ya *FIFA. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu mmoja tunataniana hapa, tulikuwa tunaangalia kirefu cha *TFF - Tanzania Football Federation,* lakini inaanza kugeuka sasa inakuwa *Tanzania Football Fungiafungia.* Maana yake sasa tazama watu wanafungiwa, hata hapa Bungeni mtu akikosea anaitwa anapata haki ya kusikilizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016 kutokana na ile waliyosema kupanga matokeo, kuna wachezaji wamefungiwa miaka kumi katika soka. Hata dunia ya akina Messi na akina Ronaldo, huwezi ukacheza *maximum of more than ten years.* Unapomfungia mtu miaka kumi, si umeua kipaji chake. Maana yake ni nini? Lazima tuwe *considerately. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *TFF* isijikite tu kwenye mambo haya ya usimamizi wa nidhamu ikajikuta inaacha kusimamia mambo ambayo yangetufanya sisi tupande katika viwango vya *FIFA. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nizungumzie soka letu. Nilisema hata mwaka 2016, kwa nini tusi-*commercialize* mpira wetu? Uingereza timu yao ya Taifa inasuasua, lakini hakuna mahali ambapo kuna biashara kama katika soka ya *EPL.* Je, Serikali, Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, wewe ni mwanasheria, naamini unaweza ukatusaidia, kwa nini tusi-*commercialize* mpira wetu na sisi ikawa ni chanzo kikubwa cha kutupa mapato?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika dunia ya sasa hivi, soka ni uchumi ndugu zangu. Usione watu wanamnunua Ronaldo au Messi kwa mamilioni ya pesa, yanarudi kwa namna nyingi tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaishauri Serikali, hebu tufikirie, kama sisi sasa hivi tuna soko huria, kwa nini pia katika soka tusi-*commercialize* hii ikawa *professional football? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi pia katika vilabu; siwezi kuisema tu *TFF* peke yake, hata vilabu vyetu vikubwa Simba na Yanga; hivi wewe unajiita Rais wa Klabu, majengo toka walivyojenga akina Marehemu Tabu Mangala, mnashindwa hata kujenga viwanja vya michezo vya mazoezi? Unaenda kila siku kuazima uwanja *Boko Veteran*! Wewe Rais wa Simba au Rais wa Yanga, unaacha *legacy* gani katika klabu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyakati hizi kuna fursa nyingi sana za kuweza kupata wadhamini, watu wa kuwekeza; Azam wamekuja juzi tu tumeona. Sasa lazima tujisifu kwamba ni viongozi wa vilabu ambao kweli tunaacha *legacy* katika vilabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Nkamia amesema lazima soka ianzie kwenye timu za vijana, lakini mimi nataka niende mbele zaidi, hata Serikali Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe peke yako huwezi, lazima ushirikiane na

Wizara ya Elimu, lazima ushirikiane na TAMISEMI na Wizara ya Ardhi kutenga maeneo na kuyapima kwa ajili ya michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimesoma Malangali sekondari, ilikuwa ni shule yenye mchepuo wa kilimo. Tulikuwa tuna shule kama Shycom cha mchepuo wa biashara, lazima kama tuko *serious* tunataka tuvune kutoka michezo tuanzishe shule ambazo zitakuwa na michepuo ya michezo, tutaziwekea miundombinu ya kimichezo, lakini lazima pia ziwe na walimu kutoka Chuo cha Walimu wa Michezo kule Malya, *otherwise* Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe tutakuja tuta-*table* hapa bajeti tutachangia, tutaondoka 2020 itafika, *World Cup* tutaishia kuiona kwenye *tv, AFCON* tutaishia kuiona kwenye *tv. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, kama *seriously* tunataka kuwekeza kwenye michezo, ni lazima tufanye mambo hayo. Kwa sababu gani? *In connection* na michezo, moja, kwanza unatangaza Taifa. Tumeona Alphonce Simbu amekwenda kule *London Marathon.* Kitendo cha kuwa mtu wa tano tu, tayari sisi umeshavutia idadi kadhaa ya watalii, umeongeza mapato katika Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapopiga kelele kuhusu michezo, siyo kwa ajili ya kuburudika, hapana, ni kwa sababu michezo ni chanzo kikubwa sana cha mapato na hivyo itakuwa na mchango mkubwa katika uchumi wa Taifa letu. Marekani leo hii, *entertainment and sports industry* mchango wake katika Pato la Taifa la uchumi wa Marekani siyo chini ya asilimia saba. Kwa hiyo, hatuzungumzii kuhusu tu kuji-*entertain. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, lazima nizungumzie pia wasanii. Juzi hapa kumetokea mvutano kwamba Serikali izuie picha kutoka nje, hapana. Ninachosema Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, filamu zinazotoka nje ikiwa msanii wa ndani lazima alipie *COSOTA,* lazima alipie BASATA, lazima alipie Bodi ya Filamu kukaguliwa

picha zake; ni lazima pia na hizi filamu zinazotoka nje tuweke utaratibu ziweze kulipia mapato katika Taifa hili. Sasa filamu kutoka nje inanunuliwa shilingi 1,000, filamu ya ndani inanunuliwa shilingi 2,500 lakini hii ya nje haijapitia mfumo wowote ambao utahakikisha kwamba inalipia kodi. Kwa hiyo, tunaposema haya tunazungumzia mapato katika Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nizungumze pia kuhusu wasanii na wenyewe wafanye kazi ambazo zina mvuto, isiwe kama tunavyoona kwenye mitandao ya kijamii, dhihaka imejaa sana. Kwa hiyo, nao wafanye kazi kadri inavyotakiwa. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niliambiwa nitapewa dakika tano za Mheshimiwa Mwamoto.

**MWENYEKITI:** Hapana, huo siyo utaratibu. Dakika tano ni zako na za mwingine, lakini hamna tano, kumi hapana. Tuendelee.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, umenipa tano?

**MWENYEKITI:** Maliza tu. Unga mkono hoja.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema pale mwanzo, naunga mkono hoja lakini lazima tuoneshe *seriousness* kwa vitendo katika suala zima la michezo kwa sababu za kiuchumi na kimapato. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, nilipokuwa natangaza majina ya wageni, kulikuwa hakuna majina rasmi ya watu wa *TFF;* nilimwona tu Kitwana Manara ndio nikamtaja. Kwa bahati mbaya nilikuwa sikumwona *President* wa *TFF,* Ndugu Malinzi. Sasa nitangaze rasmi kuwa

Ndugu Malinzi yupo Bungeni na amekuja kwenye Wizara hii na ni mtu muhimu kwenye masuala ya mpira. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Katunyang'anya *point* huyo!

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimia Sugu na Mheshimiwa Lissu ajiandae.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi sasa ya kuchangia baada ya kususia hotuba kutokana na kubanwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze sijui na Mwenyekiti, sijui Katibu, ni Naibu Katibu, Kiongozi Mstaafu wa UVCCM anayesema kwamba tukiudharau mwenge tutapata taabu sana. Ninyi mmemdharau Mwalimu Nyerere na bado mna-*survive,* itakuwa sisi kuudharau mwenge! Mmedharau misingi mingi sana ya Mwalimu Nyerere ambayo aliiweka katika nchi hii. Mnalinda mwenge badala ya kulinda Azimio la Arusha ambalo lilikuwa na misingi mizuri kabisa kwa ajili ya kuwa na viongozi bora wa nchi hii. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mtu anayesimama kwenye Bunge hili, hata wewe uliyekuwa kiongozi wa UVCCM, sijawahi kusikia hata siku moja unamkumbuka Seth Benjamin, shahidi wa Azimio la Arusha. Mnatetea vitu vyepesi vyepesi tu, mnasimama humu ndani. Unasema lazima tukimbize mwenge kwa sababu upo kwenye ngao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ile ngao kuna jembe na nyundo na pembe ya ndovu. Sasa tuvichengue vyote kuwe na *route* ya pembe, jembe na kuwe na *route* ya shoka nazo viwe na mbio zake kwa sababu tu zenyewe nazo zipo kwenye Ngao ya Taifa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, alichokizungumza Mheshimiwa Lissu ni kitu cha msingi sana. Nembo za Taifa zinaeleweka na tunatakiwa tuziheshimu, tusipotoshe kama tulivyopotosha mambo mengine huko nyuma. *(Makofi)*

Mhesimiwa Mwenyekiti, huu mwenge ndiyo maana hata sijauzungumzia kwenye hotuba yangu, hauna hata shughuli ya kufanya; wanavizia miradi. Mbeya Mjini mathalani toka uhuru kulikuwa hakujajengwa madaraja yanayounganisha Jiji la Mbeya na kata za pembezoni kuelekea Mbeya Vijijini, kunazunguka mto. Leo hii chini ya Meya wa CHADEMA, Mheshimiwa Mwashilindi katika kipindi kisichozidi miaka miwili, tumejenga zaidi ya madaraja kumi kuunganisha Jiji la Mbeya na pembezoni. Huko nyuma chini ya Meya wenu hamkujenga, sisi tumejenga halafu eti mnakuja kuleta mwenge kuzindua, ndiyo maana wananchi hawakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi humu ndani pia tunawakilisha wananchi, hatuwezi kuja humu ndani kuzungumza kitu ambacho ni *unpopular* huko nje. *Only people* ambao wanaweza kufanya hivyo ni ninyi kwa sababu mnazozijua wenyewe. Mnajua kabisa hiki kitu hakitakiwi na wananchi, lakini mna-*impose,* mnalazimisha. *That is you,* sisi hatutafanya hivyo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasanii, ifike sehemu sasa sisi wasanii tuache kutumika. Unaangalia *move* kama ya hawa watu wa filamu ya hivi karibuni, wanaitwa na Bashite. Bashite kakataliwa na jamii zote, mpaka masela wa *hip hop* wamemkataa, washikaji zake ambao alikuwa nao anafanya naye *gym* huwaoni tena, wamemkimbia; ameenda kuchukua wanyonge wa bongo filamu, anawakumbatia, anatoa matamko ya ajabu baada ya kukataliwa na vyombo vya habari *(media)*. Wasanii tunaachaje ku-*support* vyombo vya habari wakati ni wadau wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyombo vya habari ni wadau wetu. Bila wao sisi hatuwezi kufanya sanaa. Ukiona wapo katika *movement* fulani kudhibiti kitu fulani chenye manufaa kwa nchi, ni lazima sisi wasanii tuunge mkono wanahabari. Wanahabari wamemsusia Bashite, sisi tunaenda tu kukaa pale kwenye makochi ya Serikali kumsaidia kujisafisha na kumnasua. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema wanasiasa tuache kutumia wasanii vibaya, tuache ku-*abuse* wasanii. Mpaka Wabunge, juzi anasimama humu Mheshimiwa Keissy, huwa na namwita mzee, lakini simwiti mzee, anasimama anasema Msanii Roma kamtukana Rais. Hamjui hata Roma, hajawahi kumwona. Kwanza yeye ni sala tano anavyotuambia, anajuaje mambo ya *hip-hop?* Hamjui Roma, hajawahi kumwona, anatoka anasema, Roma kamtukana Rais. Wapi? *(Kicheko)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwakyembe ulienda kukaa na mtu aliyemtukana Rais wako pale kwenye *press?* Halafu watu mnapiga makofi, mnashangilia. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema, mtu kama Mheshimiwa Keissy nampuuza. Kwanza Bunge lililopita miaka mitano yote alikuwa anatetea bangi humu ndani; nashangaa hajaulizwa. Miaka mitano yote alikuwa anatetea bangi. Alinifuata mimi, bwana tutetee hoja ya bangi; nikamwambia bwana, mimi hayo mambo siyajui, wala sijawahi kuyagusa. Utajijua mwenyewe huko. *(Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namtaka Roma Mkatoliki, msanii wa muziki ambao nimeuasisi, atoke sasa aongee kwa uwazi, *in details* kilichomkuta ni nini? *Public* ikishajua, inaweza ikasaidia kujua ni nani waliomteka yeye na wenzake na walitumwa na nani, *full stop.* Vinginevyo tutaendelea kuwa na *debate* kama za Ben Saanane hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ripoti ya Nape, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujibu atuambie kabisa kiuweledi *what made you deny* ripoti ya Waziri aliyekutangulia Mheshimiwa Nape? Huyu mtu Bashite ameenda kuvamia kituo cha redio na *tv* mpaka *studio* na watu wana bunduki, *machineries,* polisi wamesema hawawajui wale watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nani wale watu walioenda kuvamia kituo cha *Clouds fm?* Kuna watu wananiambia, Sugu ulikuwa na bifu na *Clouds* miaka yote, sasa hivi unawatetea. Nilikuwa na bifu na *Clouds* kwa sababu ya haki. Haki ni haki, iwe dhidi yangu, iwe ni dhidi ya *Clouds* na mtu yeyote, nitatetea. Hata kama ninyi huko nikiona Waziri yeyote hatendewi haki, nitamtetea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu mtu ripoti imewekwa wazi kwamba amefanya makosa, kwa nini analindwa? Analindwa kwa maagizo ya nani Bashite? Maagizo ya nani yanafanya eti waseme hatuwezi kuchukua hatua kwa sababu Bashite hakusikilizwa? Hakusikilizwa wakati Tume imeenda imekaa ofisini kwake masaa matano, sita, saba, nane, akatokea mlango wa uani! Sasa yeye ni bingwa wa kuwaambia watu tukutane *central police,* tukutane mahakamani; yeye anaitwa kwenye vyombo halali vya sheria, chombo kilichoundwa na Waziri, anaingia mitini, *he is a coward.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Bashite is a coward,* ni jambazi, *thug,* ni *criminal* ni *fraud.* Bashite ni *fraud* kwa sababu ame-*forge* vyeti. Halafu Serikali inatoka inasema ooh, hatukuwagusa wanasiasa. Ma-*RC* na ma-*DC* siyo wawakilishi wa wananchi. Sisi hapa ndiyo tunaweza kuingia kwenye uongozi kwa kusoma na kuandika, lakini siyo *RC* wala *DC.* Wale wanatakiwa lazima wawe na *level* fulani ya elimu na hili suala linajulikana wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi, suala la Bashite siyo kwamba ana elimu gani? Suala ni ku-*forge. He is a fraud!* Amefanya *forgery,* anatakiwa kusimama mahakamani, ndipo sehemu anapotakiwa kusimama. Sasa kinachomfanya azuiwe asichukuliwe hatua hizo ... *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu, Mheshimiwa Sugu, subiri kidogo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68(1), Mheshimiwa Mbunge anayezungumza amemtaja Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam...*(Kicheko)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Kwani huyo ndio Bashite? Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ni Makonda. *(Makofi/ Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama anayetajwa ni Bashite, basi naahirisha kuomba utaratibu kwa sababu anayetajwa ni Bashite ambaye huyo Bashite hana mamlaka yoyote na wala sijui ana-*exist* wapi na huyo Bashite hahusiki Serikalini wala hayupo Serikalini. *(Kicheko)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Yupo Kolomije! Ume-*panic* Mheshimiwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Sugu. *(Kicheko)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Waziri ame-*panic!*

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sasa Serikali kupitia Waziri wa TAMISEMI inaanza kutupa mwanga wa Bashite ni nani, kwa sababu inaleta mjadala sana katika Taifa hili*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huyu mtu ni *fraud.* Tunaonea watu wadogo, watu wanalazwa, watu wanazimika, eti nchi hii wanasema dereva wa Mkuu wa Mkoa anatakiwa awe na cheti cha *form four,* lakini Mkuu wa Mkoa hata kama ameishia darasa la pili, akiweza kusoma na

kuandika *that is a big joke!* Ilibidi mje na maelezo yanayonyooka. Tanzania hii nawaambia kila siku, watu wameamka, siyo kama Tanzania ile ya zamani unaamka tu unasema kwamba kiongozi fulani fikra zake zimeota; ameota au amefanya nini ndiyo maono sahihi kwa asilimia mia moja. Hata wakati huo, kulikuwa na mijadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge la wakati ule mimi nikiwa mdogo, tulikuwa hatuoni kwenye *tv,* tunasikiliza kwenye redio, kuna watu walikuwa wanaitwa akina Tuntemeke Sanga na Mohamed Nandonde, huwaoni kwa sura lakini lazima usikilize Bunge ukisia kwamba anadai barabara ya Mtwara wakati ule. Halafu sasa hivi mnakuja mnasema tu tumefanya hivi, tumefanya hivi, mnasahau watu waliofanya kazi, mnamsahau Rashid Kawawa na Mwalimu Nyerere. Hata mtoto wa Kawawa juzi mmemnyima Ubunge hapa wa Afrika Mashariki, halafu mnajidai mnaenzi watu. Mtoto wa Nyerere pia mmemnyima Ubunge wa *East Africa* hapa, halafu mnasema mnaenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *cybercrime* naona imeanzishwa kwa ajili ya UKAWA tu. Wakati vijana wa UKAWA kutoka akina Mdude Nyagali kutoka Mbozi mpaka hao tunaozuiwa tusiwataje, akina Ben Saanane wanapata matatizo, wanakamatwa na kunyanyaswa kwa kutoa maoni yao kwenye mitandao, vijana wa CCM wanatukana Viongozi wa Upinzani mpaka matusi ya nguoni lakini hakuna mtu ambaye anawakamata wala kuwachukulia hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitu hivi mnaweza mkaona ni vitu vyepesi sana, lakini niwambieni mna... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lissu. Mheshimiwa Lissu samahani kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo dogo la wachezaji wote wa *volleyball* saa 7.00 mchana mkutane kantini. Endelea.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naomba nianze kwa kuzungumzia moja ya vitu ambavyo ni *omission* sijui ni nini kwa kiswahili, lakini kuna vitu ambavyo vinashangaza kwa jinsi ambavyo tumejisahau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Katiba ya Kenya ya sasa hivi, vile vifungu vya mwanzo kabisa vimezungumzia nembo za taifa la Kenya; wimbo wa Taifa na maneno yake; *court of arms* na nembo nyingine za Taifa la Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Tanzania huu utakuwa ni mwaka wa 66 tangu tupate uhuru. Mheshimiwa Waziri utakapokuja kuzungumza hapa hebu waeleze Wabunge hawa kama kwa sheria za Tanzania (sizungumzii Katiba), kama Wimbo wetu wa Taifa unatambuliwa kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu miaka kumi baada ya kupata uhuru mwaka 1971 Bunge hili lilitunga sheria inayoitwa Sheria ya Nembo za Taifa na sheria ile inazungumzia Bendera ya Taifa na ile Bibi na Bwana *(court of arms).* Wimbo wa Taifa (Mungu Ibariki Afrika) siyo nembo ya Taifa kwa mujibu wa sheria za Tanzania. Mheshimiwa Waziri, atakapokuja kuzungumza hebu aje atuelezee usahaulifu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, miaka 48 iliyopita kuanzia mwaka 1969 mpaka 1971 kilikuwa kipindi ambacho nchi yetu iliua uhuru wa vyombo vya habari kwa kutaifisha vyombo vya habari vya binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili gazeti la *Daily News* lilitokana na kutaifishwa kwa *The Standard.* Magazeti mengi yalikuwa *nationalized.* Tukaingia kwenye utawala wa kiimla kwa maneno ya Mheshimiwa Waziri hapa, kwenye vitabu vyao, nimekuja na *copy* hapa. Tukaingia kwenye dola la kiimla

ambalo halikuwa linatambua uhuru wa habari na tumeenda na uimla huo mpaka 1984 tulipopata *Bill of Rights* kwenye Katiba yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Bill of Rights* hii ni muhimu sana kwenye masuala ya uhuru wa vyombo vya habari. Tofauti na haki nyingine, haki ya kupata habari imeondolewa kile kitu kinaitwa *clawback clauses,* haina *clawback clauses*. Uhuru wa kupata na kusambaza habari, hautegemei sheria kwa mujibu wa Katiba hii. Ukienda kwenye nyingine inasema kwa mujibu wa sheria, kwa kufuatana na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Article* 18 ya Katiba imeondoa *clawback clauses,* lakini unashangaa Mheshimiwa Rais anawaambia watu hadharani kwamba msifikiri mna uhuru wa habari wa aina hiyo.

**MBUNGE FULANI:** *Not to that extent. (Makofi)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** *Not to that extent. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba yetu imeondoa mipaka ya uhuru wa habari. Kwenye haki ya habari *there are no clawback clauses*. Mheshimiwa Waziri atakapokuja hebu tunaomba atusaidie, haya maneno anakuwa ameshauriwa au anakuwa anajisemea tu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii katika awamu hii, kama kuna kipindi ambacho uhuru wa habari unakabiliwa na tishio kuliko kipindi kingine chochote ni tangu mwaka 2015. Silaha za *choice,* kuna Sheria inaitwa *Electronic and Postal Communications Act,* imetumika kukamata watu wengi sana kwa sababu ya ku-*execise* uhuru wao wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Makosa ya Mtandao na Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari; hizo sheria tatu ndiyo zinazotengeneza utatu haramu kwenye masuala ya uhuru wa vyombo vya habari. *They constitute the biggest threat on press freedom in this country.* Ndiyo maana polisi wanatembea *all over* kwenye *cyber space.*

Ukiisema Serikali vibaya, ndani! Ukimkosoa Rais au Waziri, ndani! Nani aliyewaambia katika nchi hii kwamba *the President is above the law? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nani aliyesema kwa mujibu wa sheria gani kwamba Rais hawezi akasemwa vibaya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mheshimiwa mmoja aliwahi kuwa Jaji Mkuu wa nchi hii, alisema hiyo dhana kwamba Rais yupo juu ya sheria yenyewe ina-*undermine* Katiba. Mheshimiwa Jaji Mkuu Samata!

Sasa Bunge hili lina wajibu, msifikirie hii ni kelele ya wapinzani, Bunge hili lina wajibu wa kulinda uhuru wa habari. Mkinyamaza kimya ninyi mlio wengi, leo ni sisi, kesho ni Mheshimiwa Nape na keshokutwa ni wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza wakati tunapitisha Sheria ya Vyombo vya Habari, nilinukuu maneno ya baba wa Rais wa sasa wa Ghana wakati Nkurumah anapitisha sheria ya kuweka watu kizuizini, anamtumia Waziri wa Mambo ya Ndani anaitwa Tawia Adamafio. Wakamwambia Tawia Adamafio, angalia unatengeneza mtego wa panya, utakukamata wewe. Kweli Tawia Adamafio alikuwa mtu wa kwanza katika historia ya Ghana kuwekwa kizuizini kwa sheria aliyoipitisha mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhalini Waheshimiwa Wabunge, hizi sheria; haya mambo mabaya ambayo yanafanyika nchi hii halafu mnayalinda yasisemwe, mnatuziba sisi mdomo mnafikiria mtashughulikia sisi; mnashughulikia Bunge hili na mkishalishughulikia hili Bunge, mtashughulikiwa ninyi wenyewe na hakutakuwa na mtu wa kuwapigieni kelele; hakutakuwa na mtu wa kuwasemea kwa sababu wengine wote tutakuwa tumenyamazishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kuhusu wasanii wetu! Kuna kitu kinaitwa *artistic freedom.* Wasanii

wanapotunga nyimbo, wana-*exercise their freedom of speech as well*. Ukiwakamata, ukawateka nyara na kuwatesa, una-*violate their artistic freedom*, una-*violate their freedom of speech.* Sasa hatujawahi kuona katika vipindi vingine vyote katika uhuru wa nchi hii wasanii wakitekwa nyara kwa sababu ya nyimbo zao, tumeiona kwa ... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, jioni tutaanza na Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Zaynabu Vulu, Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mheshimiwa Salum Rehani, Mheshimiwa Amina Mollel na Mheshimiwa Martha Mlata.

Kwa taarifa tu, maana tuna wageni wengi humu ndani, wengine wa Mheshimiwa Sugu, msifikirie maamuzi yanayofanywa hapa ni kukandamiza. Mmeona mchango wa Mheshimiwa Lissu na mchango wa Mheshimiwa Sugu hakuna mtu yeyote aliyewaingilia. Ndivyo vitu ambavyo haviingiani wala havikinzani na Kanuni ya 64. Tunakwenda na kanuni. Hakuna chochote tulichozuia kwa sababu ilikuwa ni uhuru wao. Kwa hiyo, nataka wageni muelewe, msitoke hapa mkafikiri...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Habari ndio hiyo! Naahirisha Bunge mpaka saa 11.00 jioni. *(Makofi/Kicheko)*

*(Saa 7. 00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea kama tulivyotangaza, mchangiaji wetu wa kwanza ni Venance

Mwamoto; Mheshimiwa Zaynabu Vulu na Mheshimiwa Rashid Shangazi, wajiandae.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii jioni hii ya leo. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe kwa kazi nzuri ambayo anaifanya na ameonyesha kwamba yeye ni mwanamichezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nachukua nafasi hii kumpongeza sana Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Ndugai kwa kutupa ushirikiano mkubwa, hasa timu yetu ya *Bunge Sports Club.* Pia nimpe pongezi nyingi Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu yeye siyo tu kutupa ushirikiano, amekuwa ni mchezaji mahiri ambaye anapokosekana, basi inatupa shida. Kwa nafasi hii pia, nawapongeza sana timu yetu ya *Lipuli Sports Club* ya Iringa ambayo imepanda daraja. Naomba Mungu awajalie ili wahakikishe kwamba tunaendelea na tuweze kuchukua ubingwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kuchangia sana sana leo nitajikita kwenye kutoa ushauri zaidi, kwa sababu tumekuwa tukichangia mara nyingi kwenye Wizara hii ambayo kwa kweli ina wapenzi wengi kuliko Wizara nyingine. Kwa sababu wanamichezo wapo wengi kuliko wanachama wa vyama vyetu vya kisiasa, lakini bado haijatendewa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ambayo Wizara hii imepitishiwa ni shilingi bilioni kama 28. Fedha hii haitoshi kwa sababu Wizara hii imebeba mambo mengi. Wizara hii mwaka 2016 tofauti na mwaka 2015 ambapo walipata fedha nyingi kuliko mwaka huu; sasa mimi sina hakika kama tuna dhamira ya kutaka kweli kupambana na mambo ya michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba tutawalaumu *TFF* kwamba hatufiki mbali, tutawalaumu michezo mingine lakini Serikali bado haijaamua kwa dhati kwamba tumeamua sasa michezo iwe kazi. Sasa hivi bado michezo ni baada ya kazi, lakini ingekuwa ni kazi, basi ingetengewa bajeti ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja niliuliza swali hapa Bungeni kwamba kwa nini michezo isifutwe? Wengi hawakunielewa, wengi walifikiria kwamba huyu jamaa vipi, amechanganyikiwa? Wengine wakafikiria labda sijui nafikiria kitu gani, lakini nilikuwa na maana tu kwamba kama kweli tunataka kuendeleza michezo kwa bajeti hii, hatutafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe ushauri kwamba kama kweli tumedhamiria kuisaidia Wizara hii na Mheshimiwa Mwakyembe na Naibu wake waonekane wamefanya kazi, basi tuhakikishe Bodi ile ya Michezo ya Kubahatisha inahamia kwenye Wizara hiyo. Mheshimiwa Waziri wa Fedha bila kufanya hivyo Mheshimiwa Mwakyembe hutafanya lolote, utaondoka hutafanya chochote ambacho unaweza ukajivunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri kwa sababu sheria inasema, fedha ambayo inatoka kwenye Bodi hiyo ni ile ya mchezo wa Bahati Nasibu ya Taifa, lakini kwenye Bodi ile kuna michezo mingi kama *betting*, kuna *casino* ambazo zinaingiza fedha nyingi. Zile zinakwenda Wizara ya Fedha, inayokwenda pale ni kutoka kwenye mchezo wa Bahati Nasibu ya Taifa ambao unachezwa mara moja au mara nyingine hauchezwi kabisa kwa mwaka. Kwa hiyo, nafikiri tuhamishe Bodi hiyo iende iwe chini ya Wizara ya Michezo, kutakuwa kuna fedha ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tuvunje Baraza la Michezo la Taifa (BMT) ma tuanzishe kitu kinaitwa Shirikisho la Michezo la Taifa. Ukishaweka shirikisho, maana yake itakuwa ni rahisi kutafuta vyanzo vya pesa; lakini leo Baraza la Michezo

wako hoi, hawana kitu chochote. Na mimi nilikuwa Mjumbe wa Baraza na najua yaani hapo unawasukuma tu, lakini hatuna dhamira ya kweli ya kuinua michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri tutoke. Mwaka 2016 nilishauri nikasema niko tayari mkitaka niwasaidie kuandika kitu hicho kizuri, kwa sababu nilishafanya utafiti, ninazo nondo za kutosha, hamtakwama. Msiogope kupata ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye *TFF. TFF* nawaomba pamoja na kuwa fedha ambazo mnapata ni kidogo, lakini hebu wekeni mambo vizuri, kwa sababu malalamiko kwa *TFF* sasa hivi yamekuwa ni makubwa, vilabu havifanyi chaguzi, Mabaraza ya *TFF* mikoani imekufa, ni migogoro. Kwa hiyo, tusitegemee kama tutakuwa na timu nzuri. Kwa hiyo, nashauri hebu jikiteni kwa wanachama wenu, wapeni uelewa waweze kuelewa wapi tunatoka na wapi tunakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tumekuwa tunafanya vibaya na timu yetu ya Taifa. Ukiangalia ligi ya Tanzania kwa Afrika Mashariki ndiyo ligi bora sawa sawa na Uingereza. Ligi bora kwa sababu gani? Kanuni za mchezo wa miguu kwa nchi yetu zinaruhusu kuwa na wachezaji wengi kwenye vilabu. Kwa hiyo, unakuta timu ya Taifa ligi ni nzuri, lakini unapokwenda kuchangua timu ya Taifa huwezi kupata wachezaji wazuri, kwa sababu wachezaji wale wengi ni wa nje ya nchi yetu kama ambavyo ligi ya Uingereza ilivyo. Ligi ya Uingereza ni nzuri, lakini hawana timu ya Taifa nzuri. Kwa hiyo, naomba warekebishe hizo kanuni ili tuweze kupata timu nzuri ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu *academy.* Tunasisitiza kwamba kila timu iwe na *academy* na watu binafsi waanzishe *academy,* lakini kuanzisha ni gharama kubwa. Kwa hiyo, nafikiria tujikite zaidi kwenye mashindano ya UMISHUMTA, UMISETA, SHIMIWI na michezo mingine, zile ndiyo *academy* zetu ambazo sisi wengine tumetokea huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia ni ndogo tu, wachezaji wa mpira wa Tanzania wana chama chao, nami bahati nzuri ndio nilikuwa Rais wa kile chama kinaitwa *SPUTANZA.* Kupitia *SPUTANZA* wangeweza kupata wachezaji wale ambao wamestaafu wakagawanywa kwenye mashule yote.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI anasikia pale, mkashirikiana wale wachezaji wakagawanywa shule zote Tanzania, hata kwa posho ndogo, ungeona mabadiliko ambayo yangetokea kwenye michezo, lakini leo hii ni taabu kwa sababu huwezi kuwaajiri na fedha hazipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Chuo cha Michezo kiko Malya. Chuo kile kinapata kila mwaka bajeti ndogo. Sasa kuna haja ya kuanzisha Chuo kingine hasa Mikoa ya Nyanda za Juu ya Iringa, Mbeya, Rukwa tukawa na chuo kingine kule. Kile chuo watu hata hawakitambui, hata Makete tungeweza kuanzisha kwa sababu ya hali ya hewa nzuri, lakini sehemu inayofaa kabisa ni Kilolo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii niwapongeze sana wachezaji wa zamani. Leo Kitwana Manara amewawakilisha wote hapa. Hebu niseme, tuweke utaratibu wa kuwaenzi hawa watu. Leo hii kuna mtu kama Jela Mtagwa, amewekwa mpaka kwenye *stamp* ya nchi hii, lakini leo ukimwona unaweza ukatoa machozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtu kama Athuman Chama, anaugua pale anakosa hata pesa, hivi kwa nini sasa Serikali, Mheshimiwa Mwakyembe usifanye mpango wakapata hata bima ya afya tu? Tutakuwa tumewaenzi wachezaji wote wa zamani, kitu ambacho kiko ndani ya uwezo wako. Kwa sababu haiwezekani ukawa unashangilia wakati anafanya vizuri, wakati akishachoka na yeye tunashindwa kumsaidia, kwa hiyo tuwasaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo yuko Sambu ametufanyia vitu vizuri, tumtunuku hata Bima ya Afya. Inawezekana hata Bima ya Afya yule hana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa kweli nisingependa kuchukua muda mrefu, niseme tu Mheshimiwa Mwakyembe na Mheshimiwa Naibu wako, hebu zungumzeni na wadau wa michezo kwenye mikoa, wanawahitaji. Piteni pale mzungumze nao, wanaweza wakashauri kitu kizuri. Tuko wapi? Tumetoka wapi? Tunatakiwa kwenda wapi? Kwa sababu wameachwa, hawana watu wa kuwasikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Zaynabu Vulu, hayupo; Mheshimiwa Rashid Shangazi, hayupo; Mheshimiwa Salum Rehani, hayupo; Mheshimiwa Amina Mollel na Mheshimiwa Martha Mlata ajiandae.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na naomba tu kwanza kabisa ni-*declare interest* kabisa kwamba na mimi ni mwanahabari, kwa hiyo, Wizara hii ni ya kwangu na inanihusu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kutupa afya na kuweza kujumuika hapa. Kwanza kabisa nampongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi nzuri anayoifanya. Pili, nampongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri, dada yangu pamoja na Mheshimiwa Mwakyembe kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia masuala mawili. Kwanza nianze na *TBC* kwa sababu ndiyo ambayo imenifanya mimi nikawa Amina hapa nilipo. Nimefanya kazi *TBC* kwa miaka nane. Shirika la Utangazaji *TBC* lina hali mbaya kiasi ambacho jitihada zinahitajika kwa kweli ili kuona ni kwa jinsi gani tunawasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBC* ni chombo cha umma, ni shirika pekee la habari la umma katika nchi hii na ndiyo chombo cha Serikali na siku zote wanasema kwamba ni vyema ukaanza na nyumbani kwako. Huwezi kwenda kwingine pasipo kuanza na nyumbani kwako. Inatia uchungu unapoangalia vyombo vingine vya habari vina hali nzuri wakati sisi chombo chetu kina hali mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali halisi naijua sana *TBC,* mitambo yake imechoka mno, inahitaji siyo kufanyiwa marekebisho, bali inahitajika mitambo mingine mipya ili kuweza kwenda na wakati huu uliopo. Hata kama hao wafanyakazi, kwa kweli wakati mwingine ile *morally* ya kazi inashuka. Siku moja mjitolee tu mwangalie hata wanapokuwa katika matukio mbalimbali ambayo wao wanahusika muone ni kwa jinsi gani wanavyojitoa katika kuhakikisha kwamba jahazi linakwenda, lakini ndani yake maumivu na mateso wanayopata kwa mitambo ilivyo chakavu, inatia uchungu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba na nina imani sana na Serikali na nina imani sana na Mheshimwa Dkt. Mwakyembe. Kwanza yeye ana taaluma hiyo ya habari lakini vilevile ni mwanasheria. Kwa maana hiyo, ni matarajio yangu makubwa sana kwa Serikali na wewe pamoja na dada yangu mpendwa Mheshimiwa Anastazia kwamba mtaliangalia kwa jicho la huruma na kwa jicho la pekee Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba maslahi ya wafanyakazi wa *TBC* yaangaliwe. Wana miezi saba hawana posho na kama mnavyojua, watu wanategemea kwa kiasi kikubwa sana hizo posho. Mishahara mara nyingi tunakopa; na kama umekopa mshahara, unategemea ile posho ndiyo iweze kukusaidia. Sasa kama hata hiyo posho hupati miezi saba! Juzi juzi wamelipwa posho ya miezi minne na bado wanadai posho ya miezi saba. Jamani hebu tuwe na huruma tuwafikirie wafanyakazi hawa wa *TBC* ambao wanajitoa. Kwanza hawa ni wazalendo wa hali ya juu ambao

wanahakikisha kwamba *TBC* inasimama na kwenda, pamoja na changamoto zote zilizopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind up* atuambie hivi tangu *StarTimes* wameingia ubia na *TBC* mpaka leo ni miaka mitano tayari imepita na nilijua ule mkataba ni wa miaka mitano, lakini kumbe unakwenda mpaka miaka kumi. Naomba Mheshimiwa Waziri aje atuambie kwamba *TBC* tangu imeingia ubia na *StarTimes* imefaidika nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wako pale, wanatumia eneo lile la *TBC* pamoja na kwamba tunawahitaji sana wawekezaji, lakini hatuhitaji wawekezaji ambao wanakuja kutunyonya. Tunataka wawekezaji ambao na sisi tutafaidika. *StarTimes* kama kweli katika yale makubaliano ya Mkataba wao wangetimiza vyema, leo hii Shirika hili la Utangazaji la *TBC* lisingekuwa na shida iliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi sana kwamba Mkurugenzi wa *TBC* ataweza ku-*perform* vizuri endapo mtamwezesha. Tido alipoingia alikuta *TBC* ina shilingi bilioni sita ndiyo maana *TBC* ikapanda juu kwa haraka sana, lakini ameingia Mkurugenzi wa sasa, hakuna fedha, madeni chungu mzima, atawezaje ku-*perform?* Mimi nawaomba sana mhakikishe kwamba mnaisaidia *TBC* ili iweze ku-perform vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namwomba kaka yangu Rioba, kwa upande mwingine ni shemeji yangu, dada yangu ameolewa huko Ukuryani huko Musoma, Mara. Namuamini sana na nina matarajio makubwa sana naye, lakini pia kaka yangu Rioba punguza ukali. Umekuwa mkali mno kiasi kwamba hata wafanyakazi wakikuona wanakukimbia kama panya. Punguza ukali tushirikiane. *(Makofi)*

Mfano, hata sisi huku tunafanya kazi vizuri sana na Spika. Ukiweka ukaribu vizuri na wafanyakazi, pamoja na kwamba ndiyo huo ukaribu uwe na mipaka ili muweze kushirikiana na kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naomba kujibu baadhi ya hoja kuhusu uhuru wa habari; na mimi hapa nitanukuu tu mambo machache. Kwa mfano, tofauti na mawazo ya wenzetu ambao wanasema kwamba nchi hii haina uhuru wa vyombo vya habari, naomba ninukuu kwa kusema kwamba nchi hii ina idadi ya vyombo vya habari na njia nyinginezo za mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Tanzania ina magazeti na majarida 428, redio 148, televisheni 32 na watumiaji wa *internet* wapatao milioni 20, yaani nusu ya nchi; na kuna *lines* za simu zilizosajiliwa na zinazotumika zipatazo milioni 41; robo tatu ya idadi ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ripoti mbalimbali duniani, Tanzania iko juu duniani na Afrika. Ukiacha jinsi ambavyo wanazungumza hapa, Tanzania kwa mfano, taarifa ya mwaka huu ya Chama cha Wanahabari Wasio na Mipaka *(Reporters Without Borders)* ambayo inasema kwamba, kwa mujibu wa ripoti hiyo, Tanzania ni miongoni mwa nchi 20 bora katika uhuru wa habari Afrika. Ya kwanza katika Afrika Mashariki ikiwa ni ya 83 duniani ambapo Kenya ni ya 95, Uganda ni 112, Sudan Kusini 145, Congo-DRC ni ya 154, Rwanda ya 159 na Burundi iko katika nafasi ya 160. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa ripoti hii, Tanzania Kimataifa pia imezizidi baadhi ya nchi kubwa ya huko Ulaya. Katika nchi hizo mfano, Marekani na Asia katika uhuru wa kujieleza na habari; Tanzania imezidi nchi za Ugiriki, Israel, Brazil, Paraguay, Uganda, Falme za Kiarabu, Cameroon, Tunisia na Guinea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ambayo ilitungwa mwaka 2016 hapa ya Huduma ya Habari namba 12 ya 2016 ni sheria ambayo imeleta mageuzi makubwa sana katika kutetea uhuru wa habari kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, imebainika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Martha Mlata, ajiandae Mheshimiwa Rashid Shangazi.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia. Wakati naongea, naomba ni-*declare* kwamba mimi pia ni msanii wa nyimbo za injili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu mwaka 2005 nilichaguliwa kuingia ndani ya Bunge hili na nilipoingia ndani ya Bunge hili, hapakuwa panazungumzwa habari za sanaa ndani ya nyumba hii, lakini mpaka sasa hivi ni hatua kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka wakati huo kabla sijawa Mbunge tulikuwa tumeanzisha uanaharakati kwa ajili ya kutetea haki za wasanii. Kwa hiyo, nilipoingia kwa kweli niliendeleza na ndiyo maana mpaka leo hii tunamshukuru Mheshimiwa Rais ambaye ameweza kugundua umuhimu na kuingiza sanaa kwamba ni mojawapo ya Wizara maalum kabisa. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Mawaziri, Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe pamoja na dada yangu kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya na Katibu Mkuu. Tumeiona kwa sababu sisi tunaelewa tulipotoka mpaka hapa tulipo. Kwa hiyo, nawatia moyo muendelee kufanya kazi pamoja na kwamba bajeti yenu kwa kweli hairidhishi, lakini ninaamini kwa utendaji wenu mzuri hakika mta-*perform* vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi Singida. Naomba nichukue nafasi hii kupongeza sana timu yangu ya *Singida United* ambayo imeweza ku-*perform* vizuri na kuweza kuingia ligi kuu. Nampongeza sana Rais wa *Singida United,* Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Mwenyekiti wa *Singida United,* Ndugu yetu Yusuph Mwandami na viongozi wote wa *Singida United* walioisaidia ikafikia hapa ilipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe tahadhari na tangazo moja kubwa sana kwamba Dar es Salaam tunaomba mjiandae, nyang'anyaneni kombe hili, yoyote atakayepata tutunzieni. Singida sisi tunaenda kubaki na kombe hili, hamtaliona tena huko. Natoa salamu hizo.

**MBUNGE FULANI:** Ni la Singida!

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Yah, lazima libaki Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nishukuru sana *TFF.* Namshukuru Rais wa *TFF,* Ndugu Malinzi, Katibu Ndugu Mwesiga na Ndugu Salum Madadi ambao wamekuwa karibu sana na sisi kutusaidia na kutuelekeza ni namna gani tunajenga uwanja wetu uweze ku-*qualify* ili mechi iweze kucheza Singida. Na sisi Chama cha Mapinduzi tumejipanga, naipongeza Kamati yangu ya Siasa ya Mkoa ya Chama ambayo wamesimama kidete kuhakikisha uwanja ule unakamilika. Nawapongeza sana, *big up* sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wadau tushirikiane kwa sababu Kanda ya Kati hakuna timu nyingine ya Ligi kuu zaidi ya *Singida United*, tuisaidie ili kombe liendelee kubaki Makao Makuu ambayo ni Kanda ya Kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, pia nisisahau kumpongeza Alphonce Simbu, kijana ambaye anatoka Singida, ametupa heshima kubwa sana kwa kazi nzuri aliyoifanya na kupata medali ya dhahabu na alipoenda

*London Marathon* ameshika nafasi ya tano, tunamtia moyo, ame-*improve,* tunaamini mwakani atashika nafasi nzuri na tumtakie heri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze, nimesha-*declare interest,* nataka niseme kuhusu jambo moja ambalo lipo mitaani sasa hivi, hasa kwenye tasnia ya filamu. Vijana wapo mitaani hawana kazi, filamu zao ambazo wamezicheza zimebaki kwenye makabati, siyo kwamba hazina ubora, lakini kuna tatizo kubwa sana ambalo nashukuru sana Wizara ilishaanza kushughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana muelewe wazi kwamba taratibu zinazotumika siyo sahihi kwa sababu ushindani umekuwa ni mkubwa. Kazi za nje zinazoingia ndani, tena zinatafsiriwa kiswahili na kazi hizi za nje zikija zikitafsiriwa kiswahili, watu wa nchi za Magharibi wanakuja kununua kwa sababu wanazungumza kiswahili. Kwa hiyo, kazi zetu sisi hazipati soko kwa sababu ya bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za ndani kutengeneza filamu moja inatumia zaidi ya shilingi milioni 18. Kuanza tu kuandika andiko kwenda kwenye Bodi ya Filamu ni shilingi 500,000, urudi *COSOTA*, sijui ikaguliwe, ukiigiza, maudhui, maadili, yote ni hela mpaka *COSOTA*, uende *TRA* ni hela. *Process* hii ni ndefu na ni hela nyingi, kwa hiyo, msanii huyu auze shilingi ngapi? Ndiyo maana unakuta soko za filamu hizi zinakuwa hazinunuliwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana, hizi kazi za nje wala hakuna haja ya kuwafungia watu. Wekeni utaratibu na wafuate taratibu wanazofuata hawa wa kazi za ndani. Wakishafuata, hakuna tatizo kwa sababu bei itakuwa ni moja na kazi zitanunuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie, Tanzania ni nchi ya pili kwa ubora wa kazi za filamu ikitanguliwa na Ghana, lakini kwa sababu ya gharama za uzalishaji, ndiyo maana unakuta kazi hizi hazipati wateja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumze suala la Sera ya Filamu. Sera ya Filamu kama tutaipitisha hapa itakwenda kurekebisha sheria na taratibu ambazo zitaweza kuwabana hata wale maharamia. Kwa sababu Sheria ya *COSOTA* sasa hivi ilivyo, mtu akikutwa na kazi haramu za shilingi bilioni moja, akipelekwa Mahakamani ni shilingi milioni tano, lakini kazi ni shilingi bilioni moja au jela miaka mitano. *Obviously* yule mtu yupo tayari kulipa gharama hizo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe namwamini sana kaka yangu, atakwenda kushughulikia hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nashauri, kwa sababu tuna chuo chetu cha Bagamoyo lakini hatuna Chuo cha Filamu, hebu naomba hilo, bado vijana hawa hawawezi kukopesheka. Nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri, wasanii hawa wapo takriban milioni tisa Tanzania. Afanye *research* ataona, ni ajira na ni kiwanda kikubwa sana kama tutawawekea mazingira mazuri ambayo Mheshimiwa Rais wetu amekusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Sera ya Filamu, Mheshimiwa Waziri aende BASATA akashirikiane nao wampeleke kwenye yale mashirikisho manne ambapo kuna Shirikisho la Filamu, Shirikisho la Kazi za Ufundi, Shirikisho la Muziki na Shirikisho la Sanaa za Jukwaani. Akienda kule kuna vyama, ndiko wasanii walipo ili wawawezeshe BASATA waweze kufanya kazi na mashirikisho haya kuwasaidia Watanzania wote. Maana tukisema kazi za ufundi; wapo vinyago, wapo akina tingatinga, wapo wachoraji, kuna waandishi na watu wengine, ni kiwanda kikubwa sana! Naomba sana Mheshimiwa Waziri aende BASATA akashirikiane nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba tu nimalizie kwa kusema kwamba, hebu niwapongeze wale wadau wote ambao wamekuwa wakiwasaidia wasanii. Nianze na *Ruge Clouds*, Msama; wote hawa ndio wamehangaika na wasanii kufika hapa. Nakumbuka wakati tunaanza sanaa, Ruge alianza na *Clouds FM* kwenye chumba kimoja; lakini wasanii tulikuwa tunaenda kujibanza pale. Ameendelea kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu Serikali iwe inawaangalia watu hawa ili muwasaidie waendelee kuwasaidia wasanii. Mwangalie Msama anavyohangaika kukamata kazi za wasanii, anaishia tu kuwapeleka Polisi, hakuna sheria, hakuna nini. Kwa hiyo, naomba washirikiane na wadau hawa ili waweze kuwasaidia wasanii. Kwa mfano,...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shangazi na Mheshimiwa Salum Rehani, ajiandae.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele ya Bunge lako Tukufu. Nami nianze kushukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri ambayo ameleta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba Wizara hii pamoja na ufinyu wa bajeti, lakini ni Wizara ambayo inaweza ikajitengenezea fedha katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwakyembe anao wajibu wa kuhakikisha kwamba anakuwa *celebrity* katika hii Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na Shirika la Utangazaji la Taifa *TBC*. Bajeti iliyopita *TBC* kupitia Wizara walituahidi kwamba Halmashauri 81 ambazo *TBC* ilikuwa haisikiki kwamba wanatafuta fedha na watahakisha kwamba katika bajeti ya mwaka huu maeneo hayo yatakuwa yamefikiwa; nasikitika kwamba mpaka sasa *TBC* haisikiki katika maeneo ya mbali hasa ya pembezoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejipa kazi ya kufanya utafiti, ukiondoa kule Mlalo ambako tunapakana na nchi jirani ya Kenya, lakini kule Rombo kwa Mheshimiwa Selasini pia haipatikani. Juzi nilikuwa Peramiho kwa Mheshimiwa Mhagama, nako huko wanapata redio za Msumbiji. Huko Nkasi kwa Mheshimiwa Keissy anapata redio za Kongo; ukienda Kakonko Kigoma, wanapata redio za Burundi. Sasa hii ni hatari sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema dhima na dira ya Wizara hii ni pamoja na kuwa na Taifa linalohabarishwa vizuri linaloshamirika na kiutamaduni lenye kazi bora za sanaa na lenye umahiri mkubwa katika michezo ifikapo 2025. Bila kuwa na chombo cha habari cha Taifa ambacho kinafikia hayo maeneo, hii itakuwa ni ndoto. Kwa hiyo, naomba sana Wizara ihakikishe kwamba *TBC* inafanya kazi kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mlata hapa alikuwa anaelezea namna ambavyo *Clouds FM* wameanza ambayo sasa hivi ni *Clouds Media.* Walianza kwenye chumba kimoja, lakini sasa hivi *Clouds* ipo nchi nzima, inasikika kwa mawimbi haya ya *FM*. Tatizo la *TBC* ni nini? Kama tatizo ni hii teknolojia mpya kwa nini tusirudi kwenye teknolojia ya zamani? Maana wakati ule wakati wa *short wave*, *medium wave* na *AM* ilikuwa inapatikana nchi nzima. Hawa wasanii akina Mzee Jangala, Majuto na wengineo wote tulikuwa tunawasikiliza kwenye vipindi, hatuwaoni lakini tuna-*enjoy*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunaona kabisa huu ndiyo utamaduni wa Kitanzania; walikuwa na vipindi vizuri vya kuelimisha wakati wa Kampeni za Malaria, Kampeni za Chaguzi na kampeni mbalimbali za nchi hii. *TBC* sasa hivi nao wanaigiza kwenye redio hizi za kizazi kipya. Nataka nitoe tahadhari kwamba tusipokuwa makini, hata *Millad Ayo* ambaye ameanza juzi juzi hapa, anaweza akaja akaizidi *TBC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala zima la michezo. Mheshimiwa Waziri ameeleza michezo kwa mapana, lakini nasikitika kwamba bado michezo inaonekana kwamba ni mpaka wadau washiriki. Hakuna jitihada Mahususi za Wizara yenyewe kutenga fedha kwa ajili ya kwenda kuhuisha michezo kwenye mashule, vyuo na hata huko mitaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana kuona kwamba wakati wa Mwalimu Nyerere vyanzo vyetu vya bajeti vilikuwa ni vichache sana, tena tulikuwa tunategemea zaidi mazao ya kilimo, yeye aliwezaje? Wale Marijendali wote uliowataja ni wa wakati wa Mwalimu. Inashindikana vipi sasa hivi wakati michezo hii imekuwa ni kama biashara? Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, aanze kuwatambua wadau lakini pia lazima Serikali na yenyewe iweke bajeti mahususi kwa ajili ya kuhuisha michezo mashuleni, vyuoni na katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Naibu Spika Tulia Ackson, yeye ameanzisha mashindano kule Mkoani Mbeya pamoja, Wilayani Kyela. Kwanza alianza na utamaduni na hili ndiyo eneo ambalo lipo katika Wizara ya Mheshimiwa Waziri. Pia kuna mashindano, anashindanisha ngoma za asili za makabila mbalimbali yaliyopo ukanda ule wa Mbeya. Mwaka huu kuna mpango wa kufanya mashindano haya yawe ya Kitaifa, tuone ngoma kutoka Pemba, kutoka Tanga na pengine popote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wadau kama hawa ni vizuri sana tukawaunga mkono ili angalau Watanzania hawa wa kizazi kipya ambao wanaanza kusahau mila na desturi zao waweze kujua kwamba nchi hii ina utamaduni na ina desturi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, mwaka huu pia kulikuwepo na mashindano ya *Tulia Marathon,*

yamefanyika katika Jiji la Mbeya. Haya ni mashindano ambayo nayo yanapaswa kuungwa mkono. Kwa sababu sasa hivi *Marathon* pekee tunayoitumia hapa Tanzania inayotambulika duniani ni hii ya *Kilimanjaro Marathon*. *Kilimanjaro Marathon* tayari imeshaanza kuzidiwa, sasa hivi washiriki wamekuwa ni wengi sana kiasi kwamba sasa wakati mwingine wanakosa nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuitumie fursa hii. Pamoja na jitihada nzuri pia za kutangaza Utalii wa Kusini, tunayo Mbuga yetu ile ya Kitulo, tunayo Ruaha, lakini hizi Mbuga hazijatangazwa vizuri. Kwa kutumia michezo hasa kutumia hii *Tulia Trust* tunaweza tukazitangaza vizuri kupitia *Marathon*, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, Wizara yake iweze kukaa na Mdau huyu kuona hii *Marathon* inaweza ikatambulika Kimataifa ili tupate washiriki mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala zima la michezo hasa mpira wa miguu. Mpira wa miguu sisi bado tumekuwa ni washindani wa kubahatisha. Hawa vijana wa *Serengeti Boys* ambao tunawapongeza sasa, huwezi ukaona *successful plan* ambayo inaandaa wengine. Inatokea tu kwamba ni bahati, vipaji vimekusanywa kwa wakati mmoja hasa kupitia wenzetu hawa wa *Airtel Rising Star*. Kwa hiyo, naomba kwamba lazima tuweke mkakati ambao utasaidia tuanze kuandaa vijana wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kuandaa vijana wengine, tuandae sasa hii ndio iwe dira yetu ya Timu ya Taifa inayokuja. Hawa vijana tutakapomaliza mashindano haya na tukawaacha wakaingia kwenye vilabu hivi vya Kitanzania ambavyo tunajua namna ambavyo wanawalea wachezaji, tutawaharibu. Kwa hiyo, nitoe rai kwa Mheshimiwa Waziri kwa kushirikiana na *TFF* tuhakikishe kwamba vijana hawa tunawatunza vizuri, tutafute Mawakala wazuri wa Kimataifa, vijana hawa waweze kupata *exposure* ya kwenda kucheza soka nje ya nchi ili baadaye waweze kuja kusaidia Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, uendeshaji wa mpira wa miguu bado una wasiwasi mwingi. Baada ya kuondoka Rais aliyepita, Leonard Chila Tenga sasa hivi *TFF* pameyumba sana. Maamuzi mengi yanafanyika kwa upendeleo, kwa hila; ni hivi juzi tu hapa timu ya Simba imenyang'anywa *points* zake tatu nzuri kabisa. Sasa sheria ziko wazi kwamba mchezaji akiwa na kadi za njano zaidi ya tatu, haruhusiwi kucheza mchezo unaofuata. Matokeo yake yametoka maamuzi mengine bila kugusia kwamba: Je, kadi ilikuwepo ama haikuwepo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, tuwaangalie *TFF* kwa jicho la karibu hasa ukizingatiwa kwamba *FIFA* ya wakati huu inaruhusu Serikali kuanza kuingilia kuangalia maendeleo katika nyanja hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, Mheshimiwa Waziri amezungumza hapa kwamba timu ya *Everton* inakuja kucheza na miongoni mwa timu moja ya Tanzania. Nataka niseme wazi kwamba *Simba Sport Club* ndiyo timu pekee inayoweza ikatoa uwakilishi mzuri. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Sawa! *(Makofi)*

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuishindanisha Simba na Timu ambayo imefungwa na *Mbao FC*.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo! *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Kwa hiyo, naombe sana Mheshimiwa Waziri kwamba hakuna haja ya kushindanisha, *Simba Sport Club* ndiyo wanatutoa kimasomaso kwenye mashindano ya Kimataifa, hii ni nafasi pekee. *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilikuwa nimejisahau kidogo, nilidhani bado una muda. Mheshimiwa Rehani, Mheshimiwa Bura hajarudi, Mheshimiwa Nyongo jiandae.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nashukuru kwa kupata nafasi hii adhimu ili niweze kuchangia katika taarifa hii ya bajeti ya Wizara ya Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kasi aliyoanza nayo katika Wizara hii na kuonesha nia kweli kuleta mabadiliko yaliyoachwa na mtangulia wake kwa Wizara hii ya Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ambayo nataka nitoe shukrani ya dhati kabisa kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanikisha Zanzibar kuweza kupata nafasi ya kuwa mwanachama wa *CUF* au Shirikisho la Mpira wa Miguu la Afrika (*CUF),* nafasi ambayo ilikuwa imetafutwa kwa miaka mingi na kilio kikubwa kwa Wazanzibari kuweza kupata nafasi hiyo, nao kushiriki kama nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kupata nafasi hiyo, bado naomba Wizara hii kwa kushirikiana na Chama cha Mpira wa Miguu Tanzania *TFF* na kile cha Zanzibar *ZFA* kuendelea na jitihada hizo katika kutafuta nafasi ya *FIFA* ili nayo iwe mwanachama kama ilivyo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine nilichokuwa nakiomba, ushirikiano uliokuwepo baina ya *ZFA*, *TFF* na Wizara zetu mbili hizi za Michezo za Tanzania Bara na ile ya Zanzibar uweze kuendelezwa katika mtazamo wa kuisaidia Zanzibar au *ZFA* ili nayo timu zake zinazoshiriki katika mashindano hayo ya Afrika ziweze kuwa na nguvu, kwani kwa hivi sasa timu nyingi zilizokuweko kule Zanzibar, kwa mfano, ndani ya Jimbo langu nina zaidi ya timu 60, lakini nina wachezaji ambao tumechukua Tanzania Bara wanaweza kufika hata 300. Kwa

hiyo hii fursa ya ushirikiano huu iliyokuwa imepatikana isikatikatishwe kwa vile Zanzibar sasa hivi imepata kuwa mwanachama wa *CUF. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ninachotaka nikione kwamba kinaendelezwa ni suala zima la michezo hasa kwa vijana wadogo. Tuna mashindano ya *Coca Cola* na kuna mashindano mengine mbalimbali ya *NSSF* ambayo yanashirikisha timu kutoka Zanzibar na hizi Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli timu hizi au mashindano haya yanaleta chachu ya ushindani na kuibua vipaji vingi vya wachezaji mbalimbali kuonekana wale wa Zanzibar wanapata nafasi ya kuja kucheza timu za Tanzania Bara, lakini na wale wa Bara wanapata nafasi ya kuja kucheza kule Zanzibar. Naomba fursa hii iweze kusimamiwa na Wizara na kuwe na mashindano ya ushindani kweli ambayo yataweza kuwanufaisha pande zote mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kulizungumza ni programu zima ya kuendeleza vijana wetu. Zanzibar miaka ijayo tunategemea nasi kuanza maandalizi ya vijana kwa ajili ya *AFCON* kama ilivyo *Serengeti Boys,* mkakati ambao unatakiwa uungwe mkono pande zote mbili na kuwe na programu za kushirikiana ambazo zitaziwezesha kuwa na timu ambayo itaweza kufanya vizuri na kupata nafasi kama ilivyopata nafasi *Serengeti Boys*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi hizi zinataka ziungwe mkono na wanachama wote, Wabunge, wadau mbalimbali wa ndani na nje ili leo hii tuione kwamba *Serengeti Boys* inavuka hapa tulipo na inatimiza lengo ambalo ilikuwa imetuahidi na iliyomwahidi Makamu wa Rais kwamba safari hii italeta kombe la Afrika la Vijana Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri akae na mwenzie, Mheshimiwa Waziri yule wa Zanzibar waangalie mkakati ukoje, kwa miaka

mingine mitatu ijayo timu zetu hizi tutaweza kuziinua na kutengeneza timu ambazo zitaweza kuonesha ushindani na kupandisha kiwango cha mpira hapa Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi hapa tarehe mosi kulikuwa na maadhimisho ya siku ya habari ambayo yalifanyika kule Mwanza. Waziri alitoa kauli kali kidogo, nami kama mdau wa habari vilevile niliguswa na ile kauli. Sasa sijui iko vipi? Kauli ambayo ilipiga marufuku uchambuzi wa magazeti katika vyombo vyetu vya habari. Sasa tunauliza; Mheshimiwa Waziri, siyo Watanzania wote ambao wanaweza kuwa na uwezo wa kununua gazeti, lakini siyo Mtanzania yeyote anaweza kufikishiwa magazeti haya. Leo tutakapopiga marufuku uchambuzi ule wa habari, wengi wao tumewanyima haki ya kupata habari Watanzania. Kwa sababu Magazeti yale au uchambuzi ule wengi wetu tulikuwa tunasikiliza kupitia redio, kwa hiyo, hata vile wengine kununua...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa. Huku nyuma!

**MWENYEKITI:** Taarifa.

## T A A R I F A

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba, pamoja na Watanzania wengi kutokuwa na uwezo wa kununua haya magazeti, lakini pia kuna kilio cha Watanzania wasioona, kwamba ile ilikuwa inawasaidia kupata habari. Ni hiyo tu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Rehani taarifa.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nimeipokea hiyo taarifa. Naomba kuishereheesha. Fursa hii ya uchambuzi wa magazeti ndiyo sauti ya Watanzania wengi, inaweza kuwaambia kwamba

ndani ya dunia hii au ndani ya Tanzania hii kuna taarifa hizi, hizi na hizi kwa leo; na kesho kuna taarifa hizi na hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri aweze kulitathimini agizo lake hili, kwa kweli linawakosesha fursa kubwa Watanzania kupata habari ambazo zinapita katika vyombo vyetu vya habari hivi hasa asubuhi kwa uchambuzi wa magazeti mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mwenzetu alivyosema, kundi hilo la wasioona na kuna makundi mengine mengi tu ambao uwezo wa kununua gazeti hawana, lakini wanazihitaji taarifa. Hili lipitiwe tena upya na Mheshimiwa Waziri atoe kauli ili kuweza kuwapa fursa Watanzania kupata habari kama walivyokuwa wanapata habari hivi sasa. Nitamsikiliza kwenye majibu yake ili tuone kitu gani ambacho ataweza kutuambia Watanzania katika hili eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nataka kuzungumza suala zima la Wasanii. Tanzania hii wanapozungumzwa Wasanii wanadhaniwa kwamba ni Wanamuziki na wale watu wa Filamu; lakini kuna kundi kubwa la wafinyanzi, wachongaji, waandishi wa vitabu mbalimbali, sijaona jicho la Mheshimiwa Waziri au Wizara yake kuweza kuangalia kundi hili na vipi wanavyoweza kuwasaidia kuinua vipaji vyao, lakini watu hawa wanaitangaza Tanzania katika Sanaa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Kisiwa cha Brunei ni mteja mkubwa wa bidhaa za vinyago ambazo zinachongwa Tanzania. Taarifa nilizonazo, kwa miaka mitano iliyopita wamenunua bidhaa hizi zaidi ya Dola milioni 600, zinanunuliwa katika maeneo mbalimbali na yeye kule wameweka ma-*shop mall* ya vinyago hivi ambavyo vinachongwa katika maeneo yetu mbalimbali.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, eneo hili nalo jicho lake liweze kuelekea. Wakurugenzi au Wizara iwe na mpango maalum wa kuwatambua kwanza, lakini siyo

kuwatambua tu kama ilivyokuwa wanatambuliwa wanamuziki ambao mpaka leo hawana walichokipa kutokana na mirahaba inayopatikana waweze kupewa *support* na Serikali na zile bidhaa zao zitangaze utalii wa nchi yetu na sanaa iliyokuwepo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba *BASATA,* bado haijafanya kazi ya kuwasaidia wanamuziki na wacheza filamu wa Tanzania.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Nyongo, Mheshimiwa Albeto na Mheshimiwa Ngwali wajiandae.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema. Nianze kwanza na ushauri kabla sijaongea mambo mengine. Ushauri wangu kuhusu Mwenge, leo ni mjadala ulikuwa umeendelea kuhusu Mwenge, watu wameongea sana na wanaongea hasa kuhusu gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba niungane na wenzangu kutetea umuhimu wa Mwenge. Tuendelee kukimbiza Mwenge, uendelee kuangaza hadi nje ya mipaka ulete upendo na amani katika nchi yetu. Ushauri wangu ni kwamba, kama tunaona kuna gharama kubwa, tusiwe na haja ya kuukimbiza Mwenge kila siku nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchague siku moja kama ni siku ya Uhuru tarehe 9 mwezi wa 12, tarehe 8 unawashwa katika Mkoa ambao wanaazimisha siku hiyo ya Kitaifa kama ni Mkoa wa Kilimanjaro mfano, unawashwa, tarehe 9 unazimwa na unafanya kazi zile zote ambazo Mwenge unafanya katika Mkoa husika. Mwaka unaofuata tunakwenda kwenye Mkoa mwingine tunafanya vile. Hayo

ni mawazo yangu, lakini tunaweza tuka-*discuss* zaidi katika *modarity* ya kuukimbiza Mwenge kama tunaona gharama ni kubwa. Huo ni ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili kuhusu *TBC. TBC* inavyoonekana kwa kweli, imewekwa pembeni. Tuangalie namna ya kuwasaidia *TBC*. Matangazo ya *TBC* yanakatika, *quality* ya picha ni mbovu, wakati mwingine unatazama sauti inakata na wakati mwingine unaona kabisa kwamba hapa kuna upungufu, teknolojia imeshawapita, wako nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri iangaliwe namna ya kuwasaidia hawa kupitia vile wanaita ving'amuzi. Wale wateja wa ving'amuzi waweze kulipa pesa na pesa zile zikilipwa *TBC* wapewe hela yao moja kwa moja kuliko kuanza kupeleka pesa Hazina, mara *process* zinafanyika za hapa na pale na matokeo yake wanachelewa kupata pesa. Wanahitaji mitambo mipya, wanahitaji teknolojia mpya. Wako nyuma, hawako kibiashara kabisa! Tunaomba muwaangalie kwa jicho la namna ya pekee ili kusudi muweze kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine natoa pongezi kwa *Serengeti Boys;* kazi wanayofanya ni nzuri kabisa, wametuletea heshima katika nchi hii. Tunaomba hiyo timu muilee vizuri, hiyo timu itatufikisha mbali. Nakumbuka kuna timu ya vijana ilienda hadi ikachukua ubingwa wa dunia, lakini baada ya pale kuja kurudi ile timu sijui imepotelea wapi. Tunaomba muiangalie hii *Serengeti Boys*, itatupeleka mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze kwa kina kidogo, naomba ku-*declare* mimi ni Mwenyekiti wa Chama cha Mpira katika Mkoa wa Simiyu. Kwa hiyo, mimi ni mdau mkubwa wa mpira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba katika timu ya Taifa ni lazima tuwe na utaratibu wa kutengeneza timu yetu ya Taifa. Watu tunadhani kwamba *premier league* ndiyo inayotengeneza timu ya Taifa. Hivi

vilabu, huwezi kutengeneza timu ya Taifa kutoka kwenye hivi vilabu. Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu inatengenezwa kutokana na *Football Academy.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwa na *Football Academy* nzuri za kutosha tutakuwa na vijana wengi ambao tutaweza kutengeneza kutengeneza timu ya Taifa. *Premier league* ni *typical commercial league.* Hiyo ni *commercial football,* pale ni biashara, siyo timu ya Taifa. Mshindi wa *Premier League* anapokwenda kwenye *Champions League* anakwenda kucheza kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sisi tunadhani kwamba kutengeneza Timu ya Taifa ni lazima wachezaji watoke kwenye *Premier League,* ni makosa. *Premier League* ni biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapotegemea *Premier League* kutengeneza Timu ya Taifa, utajikuta huyu mwenye timu, kwa mfano Azam tumchukulie, Azam ana uwezo wa kununua wachezaji kutoka nje hata 20; leo bingwa wa Tanzania akipatikana, anapokwenda kwenye *Champions League* ya Afrika anaenda kukutana na *TP* Mazembe, ambapo *TP* Mazembe yeye amenunua wachezaji karibu ya 20 kutoka nje, kwa sababu anafanya biashara. Sisi leo Azam unamzuia kwa mfano asinunue wachezaji zaidi ya watano kutoka nje, hii sheria haina maana yoyote. Hii muiondoe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachezaji wapatikane *first division* kushuka chini kutokana na zile *Football Academy* zetu. Nawapeni mfano, Zambia walipoteza wachezaji walikuwa wanaenda Gabon, walianguka na ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zambia wamepoteza wachezaji, makocha wakajiunga wakarudi kwenye *Football Academy* zao wakaangalia wachezaji wakatengeneza timu nyingine mpya ya watoto wadogo, wakaunda Timu ya Taifa ikaenda Gabon na ikacheza ikafika finali ikatolewa na Nigeria. Kila mtu anakumbuka hapa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Brazil, kuna wachezaji kama Romario alikataliwa asiingie Timu ya Taifa, kocha akasema tuna mchezaji anaitwa Gaucho kutoka kwenye *Football Academy.* Alivyoingia Gaucho wakachukua kombe la dunia. Sisi leo tunang'ang'ania wachezaji wa *Premier League* ndio wacheze Timu ya Taifa. Hatuwezi kufika popote! Undeni *Football Academies* za kutosha, fufueni vile Vyuo vya Michezo vya kutosha ili kusudi mpate watoto wa kutosha kwenda kucheza Timu ya Taifa. Kwa mtindo huu hatutafika. Kwanza *league* zenyewe hazina *quality, you cannot predict.* Ukienda kuangalia mpira, mara refa amekula mlungula, anaamua penati, anaamua kitu cha ajabu ajabu. Leo kuna *points* zinanyang'anywa mezani, hakuna! Tunafanya nini?

Mheshiiwa Mwenyekiti, nawashukuru *TFF,* wanafanya kazi nzuri. Hata ukitazama kalenda ya Kimataifa *TFF* wamefanya kazi nzuri. Ukitizama zile kalenda za michezo ya Kimataifa katika nchi 12 za *CECAFA, TFF* wamejitahidi badala ya mechi moja wanacheza mechi mbili, hilo nawapa pongezi, lakini waunde miundombinu ya kutafuta wachezaji wa Timu ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye *Bongo Movies;* hii ku-*burn* sinema za kutoka nje sijui imetoka wapi? Hivi una-*burn* sinema za kutoka nje mnatuuzia zile sinema zenu za jambazi ameingia na soksi! Eti jambazi ameingia na soksi kuvamia mtu, ulishawahi kuona wapi? Tuleteeni sinema; sisi tunamjua Rambo. Mimi nikiwa mdogo namjua James Bond. Kwenye miziki ya zamani tulikuwa tunamjua Bob Marley. Mbona wenye muziki wamejitahidi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilienda Kenya, kwenye *club* za Kenya unakuta watu wanapiga miziki ya Kenya. Sasa hivi ukienda unakuta wanapiga *Bongo Flava,* ina maana Bongo *Flava* wamejitahidi. Nyie Bongo Movie, mna-*burn* kuingiza sinema kutoka nje. Hii imetoka wapi? Naomba tusitafute kiki kwa *shortcut* ...

**MBUNGE FULANI:** Bashite huyo!

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO: ...**warudi nyuma, wajitahidi kutengeneza sinema vizuri, wataingia kwenye soko ndani na nje ya nchi. Sasa una-*burn* ku-*import* sinema kutoka nje: Je hao wa Kenya, Wanaigeria; sisi tunataka leo tuuze sinema Kenya na Uganda. Sasa tutaziuzaje kule? Tutaziuza iwapo tume-*improve quality* ya sinema zetu za Bongo. Warudi nyuma wajipange. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Kiswahili. Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, nilikwenda *South Africa* nikakuta kuna Wakalimani kwenye Mkutano. Mkalimani anaongea ki-*Portugal* na Kiingereza. Nikauliza, Mkalimani wa Kiswahili yuko wapi, kwa sababu nataka niongee Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnapokwenda kwenye mikutano, mwombe Wakalimani wa Kishwahili kule mnakokwenda. Kwa sababu mkiweka wakalimani wa Kiswahili, mtawapa soko wakalimani na watu watajifunza Kiswahili, wataona kwamba kina soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiswahili ni lugha kubwa, imekuwa ya pili kwa Afrika ikiongozwa na lugha ya Kiarabu. Lugha ya pili ni Kiswahili, ina maana lugha yetu ni kubwa, tusiibeze lugha yetu. Tuitukuze lugha yetu. Naomba tumjali, tumtetee na tumlinde na tumheshimu Mheshimiwa Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere kwa kukitukuza Kiswahili. Turudi tuendelee kuongea Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa hongera Mheshimiwa Magufuli kwa kwenda kuongea Kiswahili nje ya nchi. Ombeni siku zote mnapokwenda kwenye Mikutano mwombe Mkalimani wa Kiswahili. Semeni, hatujui Kiingereza. Tatizo la Sisi Wabongo, tunajifanya tunajua Kiingereza, hatujui. Unafika kule hata ukipewa muda wa kuongea, unaongea *point* mbili, tatu, baada ya hapo umetoka nje ya *line*. Tuongee Kiswahili. Tuweke Wakalimani wa Kiswahili, Kiswahili ziwe na soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hongera Mheshimiwa Magufuli kwa kwenda kuongea kiswahili nje ya nchi. Siku zote mnapokwenda kwenye mikutano ombeni mkalimani wa kiswahili, semeni hatujui kiingereza. Tatizo la sisi wabongo (watanzania) tunajifanya tunajua kiingereza, hatujui. Unafika kule hata ukipewa muda kuongea unaongea *point* mbili, tatu baada ya hapo umetoka nje ya *line.* Tuongee kiswahili, tuweke wakalimani wa kiswahili, ili kiswahili kiwe na soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoma za kienyeji, *tv* zetu, hawa *TCRA* mtu anayeomba leseni ya *tv* katika vipindi anavyoomba kwamba mimi nitaonyesha vipindi moja, mbili, tatu, kiwepo na kipindi cha ngoma za kienyeji kwenye *tv.* Iwe ni utaratibu kwa sababu sisi kwa mfano kule Usukumani tuna ngoma nyingi na nadhani hakuna kabila lenye ngoma nyingi kama Wasukuma. Tuna ngoma za gugobogobo, wigashe, bugoyangi na kadhalika kuna ngoma nyingi zionekane, mbona makirikiri tunaiona kutoka Zimbwabwe? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namuita Mheshimiwa Alberto ajiandae Mheshimiwa Ngwali.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nina mambo machache ya kuzungumza lakini kimoja nitakisema *in passing* tu juu ya mwenge. Tusipeane majina wala tusipunguziane uzalendo kwa sababu tu hatuukubali mwenge. Mimi kwa bahati nilikuwemo katika Tume ya Warioba na katika kitu Watanzania walichokikataa na wakasema waziwazi uende makumbusho ni Mwenge wa Uhuru. Kwa hiyo, wanaosema kwamba mwenge upumzike au kama msemaji wa sasa hivi aliyesema tutafute *modality* nyingine mimi ni mmojawapo na hii hainipunguzii uzalendo kwamba mimi ni Mtanzania na naipenda Tanzania yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, sisi kama Taifa tunaishi katika zama za sasa, hatuwezi kuishi sasa kisha tukabakia kizamani. Sasa hivi dunia imepanuka, kuna *technology* mbalimbali na kuna njia mbalimbali za kuwasiliana. Wakati njia za kuwasiliana zinapanuka na wakati sisi tunapimwa kwa ajili ya kuwa wawazi kwa wanachi wetu na sisi kuwa huru kujieleza, ndipo sisi tunapofunga milango ya uhuru wa habari na uhuru watu wetu kujieleza. Hii hai-*augur well* na vipimo ambavyo sisi tunapimwa kama nchi na ndiyo maana ripoti ya *Amnesty* juzi imetu-*condemn* na kutushusha sisi katika suala la uwazi na uhuru kwa waandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii katika upande wa habari, mimi maisha yangu yote ni mwandishi wa habari na nimepita wakati ambapo tulikuwa tunabanwa hata kusema tulikuwa hatuwezi. Wakati naripoti Zanzibar naweza kuiandika *story* leo nikaenda Dar es Salaam nikakaa siku tatu nasubiri mshindo kule Zanzibar utakuwa vipi, tusiishi tena hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii wakati tunapanua demokrasia mwaka mmoja tunapitisha sheria tatu za kubana uhuru na kubana watu namna ya kujieleza, nafikiri hii si sahihi. Hii ni dalili ya woga na dalili ya kuogopa watu wako wenyewe wasiseme. Kiongozi mzuri, Serikali nzuri ni ile ambayo inaruhusu watu wao watoe joto lao, wajieleze ili wajue kuna kitu gani katika Taifa. Kwa hiyo, mimi nafikiri tusijivunie kwamba tunazuia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine tu kwa mfano, leo tumezungumza vitu vingi sana kuhusu wasanii na utamaduni, lakini tumejifungia humu ndani. Tumezuia wananchi wetu wasisikilize na wasipate taarifa juu ya mijadala ya Bunge kwa hofu tu kwamba wakisikia watabadilika mawazo, tusiogope hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho nataka kuzungumzia ni suala la kiswahili, watu wengi wanazungumzia habari ya kiswahili. Kwa wale ambao

hawajui, mimi ni mpenzi sana wa Kiswahili na ni mwandishi wa mashairi lakini pia ni mwandishi wa vitabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, wakati tunajivuna kwamba Tanzania ndiyo mabingwa wa kiswahili lakini kusema kweli Kenya wametutangulia. *Graduates* wa Kenya kwa kiswahili hatufiki sisi hata *one third* yao kwa kila mwaka. Sasa hivi katika mashirika mengi ya kimataifa, *translators* wengi walioko nje, vyuo vingi vikuu, walimu ni kutoka Kenya na siyo Tanzania. Nchi hii ya Tanzania ambayo inajivuna ina kiswahili niambieni kuna *literature prize* gani ndani ya nchi hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya katika zawadi ambayo inaongoza duniani kwa kiswahili ni *Cornell-Mabati Kiswahili Prize* ambapo mimi mwaka huu nime-*submit* kitabu changu kinaitwa La Kuvunda. Wenzetu hawa wanatoa zawadi kila mwaka kwa miaka mitano sasa na kuna *commitment* ya kampuni ya Mabati na *Cornell University* kuendelea kwa muda wa miaka kumi ijayo, hata hili hatuwezi kubuni ku-*approach corporate world* ya Tanzania ikashirikiana na chuo kikuu kimojawapo kukawa na *literature prize* kwa kila mwaka? Hii itaibua waandishi, tutabaki tunaimba tu tulikuwa na Ibrahim Hussein, Profesa Lihamba, Profesa Penina, wako wapi watu kama hao, hakuna tena *caliber* kama hiyo kwa sababu hatuwatengenezi. Tusitarajie tu kwamba watuzuka bila kutengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ni suala zima la *culture* ya michezo ya kuigiza. Tunazungumza sana habari ya *bongo movie* lakini moja katika *culture* nzuri sana ni michezo ya kuigiza ambapo Tanzania imekufa. Nilipokuwa chuo kikuu ilikuwa wakija wale waigizaji *Nkurumah Hall* inajaa, sasa hivi hata sijui kama kuna michezo ya kuigiza ndani ya nchi hii kwa sababu hata waandishi wa michezo ya kuigiza hawapo tena na hawatengenezwi na hawatayarishwi. Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri alitizame hili, tuwe na *competition* za kila mara ili kuweza kukuza jambo hili. Sasa hivi tuna vyuo vikuu vinafika 50, jambo kama hilo linawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije katika *area* ya michezo ambayo naielewa vizuri sana kama ninavyoelewa suala la habari na hapa nitazungumza zaidi kidogo.

Mimi nafikiri ni katika wale ambao siamini kwamba Wizara au Serikali ndiyo yenye jukumu la michezo, mimi siamini. Mimi naamini Serikali kazi yake ni kutengeneza sera, lakini *corporate world* ndiyo ambayo inaweza kusimama na kukuza michezo na mfano mzuri ni huu wa Simbu hivi sasa. Niliwahi kuzungumza na Mheshimiwa Nape wakati akiwa Waziri kwamba tuache kumpa mzigo mtu mmoja kumwambia tunataka shilingi milioni 200 kwenda *Olympic* au shilingi milioni 500 kwenda *Commonwealth,* unakwenda kwa mtu mmoja mmoja, uache kila *corporate* imwambie wewe chukua dhamana ya mwanariadha huyu hapa, wewe chukua dhamana ya mwanariadha huyu hapa, tutafika mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini watu wanalalamika wanasema hatupati timu kubwa za nje kuja Tanzania, wanalalamika kwamba *rank* ya Tanzania haipandi kwa sababu hatuchezi na timu kubwa. Kucheza na timu kubwa ni gharama kubwa sana, kuileta Brazil mimi mwenyewe nilijaribu, *minimum* wanataka dola milioni moja za kucheza uwanjani, mbali ya gharama zao. Kuileta Argentina inahitajika kama dola 800,000 kuwaleta wakacheza uwanjani mbali ya gharama zao nyingine za ndege na kila kitu. Kwa hiyo, kama *corporate* Tanzania hatujaishirikisha vya kutosha ikaweza kuchangia, hatuwezi kuzileta timu kubwa na maisha yatabakia kule kule *zero.* Maana yake unataka ulete timu lakini kiingilio unataka uweke shilingi 5,000, unasema eti unawajali watu wadogo, haiwezekani, lazima kimojawapo utakikosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine watu wamezungumzia hapa habari ya vipaji, vipaji vinatengenezwa na tena siyo Serikali yenye jukumu la kutengeneza *academy,* ni mimi na wewe. Wabunge pia wana uwezo, wana haki na wajibu wa kutengeneza vipaji kwa sababu vipaji ni biashara, unaweza ukatumia shilingi

milioni 100 lakini wakati ukiuza mchezaji mmoja unaweza ukapata shilingi bilioni moja. Kesi ya Samata kwa mfano, mimi nilikuwa *involved* mara nyingi katika biashara zake, najua namna ambavyo amefikia pale.

Kwa hiyo, watu wajue kwamba kuwekeza kwenye riadha, soka, vipaji inalipa kwa mchezaji mmoja tu ukipata, siyo wawili au watatu, mmoja tu inalipa. Kwa hiyo, Wabunge hilo pia mnaweza kulichangamkia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sikubaliani na msemaji aliyepita hapa kwamba tuwalete wachezaji wengi wa nje wacheze ligi yetu ya ndani. Uingereza wana tatizo hivi sasa hawana timu ya Taifa nzuri kwa sababu wageni ni wengi. Cha kufanya sasa hivi *TFF* itengeneze kanuni kwamba klabu yoyote kwanza iwe na timu ndogo lakini ilazimike kama vile ambavyo kuna *limit* ya wachezaji wa nje kucheza watano basi lazima iwe na mchezaji *under 20* katika kila mechi yake ya ligi, mmoja, wawili au watatu, hiyo itatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine naogopa *time* yangu isiishe nataka nizungumzie juu ya mchezo wa *chess*. Mheshimiwa Waziri nisikilize vizuri. *Chess* ni mchezo ambao unaweza kututoa Tanzania kwa haraka sana, kwanza hauna gharama. Mimi ni mshabiki wa *chess* na nafundisha *chess*. Ni mchezo ambao ukishapata bao lako la kuchezea, mnakaa watu wawili, ukivaa bukta, kanga, seluni (msuli) unacheza tu. Ni mchezo ambao unaweza kufundishwa na kukuza vipaji vya watoto wetu. Kuna uwezekano pia wa kusaidia kupata *masters* wa *chess* wakacheza dunia nzima na tukajulikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nafikiri tusing'ang'anie tu michezo iliyopo na ndiyo maana hapa nataka kusema Mheshimiwa Waziri lazima hivi sasa tuamue tuwe na *priority,* iko michezo tumecheza miaka haijatupeleka popote, lakini iko michezo inayoweza kututoa. Kwa hiyo, hata kama utatangaza waziwazi kwamba *priority* itakuwa ni riadha, soka na kitu fulani na kitu fulani kwa sababu hatuwezi kucheza michezo yote kwa sababu hatuna fedha za

kuhudumia michezo yote, lakini lazima tuangalie na hii michezo mingine. Mheshimiwa Waziri tunaweza kushauriana zaidi ukinihitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ngwali, wajiandae Mheshimiwa Kadutu na Mheshimiwa Oscar Mukasa.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi nianze na ripoti ya ukaguzi wa fedha ambayo *TFF* wenyewe waliwataka *TAC* wafanye na waliwakabidhi tarehe 19 Januari, 2016 ripoti namba A/1/2015/2016. Ripoti hii ukifungua ukurasa wa 28 kuna fedha ambazo zimetumiwa na *TFF* kupitia Rais wake Jamal Malinzi ambazo haziko kwenye *document* na fedha hizo wamelipana wao wenyewe na pia wakakopeshana wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ambazo amelipwa Michael Richard Wambura bila kuwa na ushahidi wowote ni shilingi milioni sitini na saba mia tano na senti hamsini na nne. Fedha ambazo imelipwa kampuni ya *Panchline Tanzania Ltd.* ambazo hazina ushahidi wowote na hizi kampuni ni kampuni zao wenyewe tunajua, ni shilingi milioni mia moja na arobaini na saba laki moja hamsini na nne mia mbili ishirini na tisa. Fedha nyingine ambazo zimelipwa zikiwa hazina ushahidi ni fedha ambazo wamelipwa *Atriums Dar Hotel Ltd.* ambazo zilikuwa ni USD 28,000 sawasawa na shilingi milioni hamsini na tisa, ukifanya *grand total* pesa zote ambazo hazina mahesabu yoyote na zinaliwa ni shilingi milioni mia mbili sabini na nne na kitu kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni ripoti, ukitaka ushahidi Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe nitakukabidhi, ripoti ya ukaguzi ambayo Wizara kwa vyovyote mnajua, Baraza la Michezo linajua lakini pia TAKUKURU wanajua lakini Serikali imekaa kimya haijasema chochote. Kwa hiyo, naomba Wizara kwa jambo hili ilichukue ilifanyie utaratibu na wakati wa ku-*wind-up* nitataka majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti nyingine ya ukaguzi ni hii ya fedha za wadhamini, tarehe siioni vizuri lakini imefanywa na ma-*auditor* wa *Breweries.* Ukiipitia ripoti hii *TFF* wametafuna fedha za wadhamini zaidi ya shilingi bilioni 5.5 na hii ripoti nitakupa. Tena hii ni ripoti ya ukaguzi, haya maneno hayatoki kwenye kichwa tu kwa sababu ya mapenzi ama vipi. Tumalize jambo la *TFF* twende mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina masikitiko sana, mimi ni mpenzi mkubwa wa soka, lakini sidhani kwa mtindo huu inaweza kukua wala sifikirii, wala sina mawazo hayo mimi nina mawazo mengine ambayo nitapendekeza baadaye. Kwanza nionesha namna gani soka haiwezi kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ambazo wanakusanya *TFF* kwa ajili ya kukuza mpira wa miguu zinatoka *FIFA* ambazo ni fedha kidogo, ni dola 250,000 kwa mwaka. Fedha zinazopatikana Serikalini mnazijua hata kufika hazifiki lakini fedha zinazopatikana kutoka *CAF* ambazo sio nyingi ndiyo zinazotegewa lakini mpira hauwezi kuendeshwa na fedha hizo ni kidogo sana. Fedha nyingine ni za makusanyo za usajili wa kadi na fomu, wanasema *players transfer fee, players contract registration fee*, fedha kidogo sana hizo, *league participation fee, fine as appeal* maana yake hata ile *fine* ya timu ya Simba imo hapa, *sponsorship deals* na hizi ni mpaka zitokee na *sales market right. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nipendekeze na kwa mtindo huu tusifikirie kimaskini kama anavyofikiria Mheshimiwa Mwamoto kwamba twende zetu huko vijijini tukatafute wachezaji, hapana, tuiunganishe Wizara yako na Wizara ya Viwanda ili ile dhana ya Rais Magufuli kwamba tuwe na tuwe na uchumi wa viwanda iweze kufanya kazi. Tufanye kitu ambacho nchi nyingi wamefanya wamefanikiwa wanaita *sports industries* ambapo inakusanya michezo yote, *hockey* imo humo, mwendesha baiskeli yumo humo kila kitu kimo humo. Leo unataka kukuza michezo, unaletewa jezi kutoka China, unakwenda kununua mpira Pakistan, huo mpira unakuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina masikitiko makubwa sana, tunafanya vibaya sana katika *Olympic*, vibaya tena vibaya sana. Mheshimiwa nikuulize kitu kimoja, kuna Wanyamwezi wengi sana, samahani Wanyamwezi, pamoja na Wasukuma basi tunashindwa hata kupata mtu wa kurusha tufe? Mheshimiwa Waziri unashindwa hata mtu wa kurusha mkuki, vifua vyote vile, nguvu zote? Mheshimiwa Waziri tukienda kwenye ngumi kila siku tunapigwa, basi nguvu zote tulizonazo tupigwe siye tu kila siku? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ni kwamba hatujaandaa watu wetu, hatujaandaa sekta ya michezo. Kwa hiyo, mimi nipendekeze tena tunapokuwa na hiyo *sport industry* tunakuwa na michezo mingi ndani, tusifikiri kimaskini, lazima tupate *fund* kubwa, tutumie *PPP,* tupate ma-*expert,* tuwashawishi watu, Serikali iingilie kati pamoja na sekta binafsi ili tuwekeze tuwe na *Olympic Park,* tuweze kukuza hiyo michezo vinginevyo tutakuja kusema Jamal Malinzi kapiga hela, tutasema maneno ambayo hayawezi kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo cha msingi tupate hiyo *sport industry* inaweza kutusaidia sana. Maana yake ni kwamba tutajenga viwanda ambapo mipira ya michezo yote tutaweza kuzalisha sisi wenyewe, tutaweza kuzalisha jezi sisi wenyewe, viatu tutaweza kutoa sisi wenyewe, ngozi za ng'ombe tunazo tunaweza kufanya kila kitu sisi wenyewe, hapo hiyo soka inayozungumziwa ndiyo inaweza kukua, tusifikiria kimaskini. Tukishakuwa na hiyo *sport industry* ndiyo tunaweza kufanya kitu, lakini ukisema leo tukatafute watu sijui Shinyanga, sijui wapi tuunde timu ya Taifa, sio rahisi kabisa. Kwa hiyo, mimi napendekeza hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni muhimu sana, nirudi tena pale *TFF. TFF* ni *Tanzania Footbal Fedaration* maana yake ni kwamba Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tulitakiwa sisi tupate Makamu Mwenyekiti ama mbadilishe jina...

**MBUNGE FULANI:** *Yes.*

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** ...liwe jina lingine lakini mkisema ni chombo cha Tanzania halafu Zanzibar hawana ushiriki katika jambo hili inakuwa haliko sawa. Nafikiri tukae tuangalie upya namna gani tutawashirikisha Zanzibar katika hiyo *TFF* pamoja na kwamba Mheshimiwa Ally Saleh anasema siyo vizuri, lakini tutakaa pamoja tutalizungumza jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nizungumzie sanaa, sanaa imezidi imevuta mipaka sasa. Maana nyimbo sasa zinazoimbwa zilivyokuwa na matusi kama ninyi wenyewe Serikali hampo, sijui BASATA wanao-*control* wanafanya kazi gani? Michezo ya kuigiza *(bongo movie)* hizi, watu wanakaa wamevua mashati, wanabusiana, wanafanya mambo ya ajabu ajabu, huwezi kukaa na familia yako ukatizama, huwezi kukaa na mtu yeyote ukatizama na nyie mpo na nyie mnatizima, tatizo lenyewe na ninyi mnatizama. Hiyo ndiyo shida, utafikiri kama hatuna *control. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, japo dakika zangu hazijaisha lakini baada ya kusema hayo niseme kwamba siungi mkono hoja mpaka Mheshimiwa Waziri atakapojibu hoja zangu, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kadutu hayupo nafasi yake atachukua Mheshimiwa Kakunda, ajiandae Mheshimiwa Oscar Mukasa.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, sana kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi swali langu la kwanza kwenye Wizara hii ningependa kuuliza, hivi nchi hii tuna Chuo cha Waamuzi wa Michezo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza hivi kwa sababu uamuzi ni tatizo kubwa sana. Waamuzi wamekuwa wakilalamikiwa sana mpaka wakati mwingine mtu unafikiria hivi hawa waamuzi au wanahongwa rushwa au wanapewa maelekezo na mtu fulani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati alilalamikiwa sana Waziri wa Mambo ya Ndani kwamba labda anatoa maelekezo, pengine labda kweli au wanamsingizia, lakini inawezekana. Sasa mambo kama haya naomba sana Wizara hii ituambie hivi tuna Chuo cha Waamuzi ambapo kuna *curriculum* inafundisha uamuzi wa mpira wa miguu, mpira wa pete, *volleyball* na michezo mingine kwa ujumla?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza kwa Mheshimiwa Waziri atakaposimama atueleze uamuzi wa michezo katika nchi hii *curriculum* yake iko wapi? Kama hakuna basi kama Taifa inatakiwa tuanzishe *curriculum* ya uamuzi michezo au chuo maalum cha watu kujifunza uamuzi badala ya kutegemea mafunzo ya muda mfupi kutoka kwa waamuzi ambao wana-*experience* na watu wengine wanatoka nje ya nchi wanakuja hapa wanafundisha *brushing*, hilo ni tatizo kubwa sana kwenye michezo.

Suala hili Mheshimiwa Waziri atakaposimama alieleze vizuri na hata Waziri wa Mambo ya Ndani naye kwa sababu anatajwatajwa asimame maana timu zinakwenda zinafungwa hovyo hovyo kwa sababu inaaminika bingwa huwa hapatikani kwa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu programu za michezo mashuleni na vyuoni ni jambo la muhimu sana Wizara hii kwa kushirikiana na Waziri wa Elimu na TAMISEMI wasimamie programu hizi. Nchi nyingi zimefanikiwa sana katika michezo kwa kupitia programu za michezo mashuleni na vyuoni. Kuna wakati zilifutwa, lakini nashukuru Serikali wamerudisha tena lakini uratibu wake hauendi vizuri sana kwa sababu gharama ni kubwa, wanaogopa gharama. Mimi naomba sana kwa kushirikana ndani ya Serikali Wizara kama mbili au tatu wahakikishe programu za michezo mashuleni na vyuoni zinafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ambalo napenda kuzungumzia ni *academy* za michezo au vyuo vya michezo. Nasikia kule Mwanza kuna Chuo cha Michezo lakini hicho chuo kimoja tu hakitoshi kwa nchi nzima hii. Nchi hii ni kubwa

sana, mikoa yetu inahitaji angalau chuo kimoja kila mkoa, hicho kingefaa lakini sasa kwenye mpango wa maendeleo wa Wizara hii hakuna hata pendekezo. Mimi nadhani ili tuwe *serious* tutoe vijana ambao watashindana katika ngazi za kimataifa ni muhimu sana vyuo vya michezo vya watoto wadogo viwepo angalau kimoja kila mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kuzungumzia ni suala la utamaduni, mwenzetu mmoja nimemsikia amezungumzia ngoma za asili. Hili suala la ngoma za asili limeachwa nyuma kabisa, sio kwenye *television* tu peke yake hata kwenye redio, zamani *RTD* ilikuwa kuna programu maalum kabisa ya ngoma za asili siku hizi hamna. Watu wanacheza miziki ya Marekani labda wataishia kucheza *bongo fleva* lakini ile tumbuizo asilia hakuna. Hilo ni tatizo kubwa sana. Wale wanaotoa leseni kwenye vipengele vya maelekezo ndani ya leseni wanatakiwa wawaambie na wafuatilie vituo vya *television* na redio lazima wazingatie kucheza ngoma zetu za asili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kuhusu ngoma za asili ni kuhakikisha kunakuwa na programu maalum hasa wakati ambao ni wa mapumziko vijijini. Kuna wakati ambao wakulima wameshavuna, zamani kulikuwa na matamasha ya ngoma za asili katika kila Wilaya, angalau wakati ule hasa hasa mwezi wa sita au wa saba wakati watu wamevuna hawana kazi nyingi za shamba, kipindi kile kingekuwa sasa kila Wilaya inaratibu tamasha la ngoma za asili ili kuhakikisha kwamba tunaendeleza utamaduni wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu yalikuwa ni hayo naamini Mheshimiwa Waziri atatolea ufafanuzi na atazingatia kwenye kwenye hotuba yake.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Oscar Mukasa, ajiandae Mheshimiwa Kiteto Koshuma.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Na mimi niungane na wenzangu wote kumpongeza

Waziri na timu yake kwa kazi nzuri japo tuna maeneo ya kushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza, mwezi Februari sikumbuki tarehe nilikuwa na swali hapa kwa Wizara hii kuhusiana na kumomonyoka kwa matumizi ya lugha ya kiswahili ambako kwa kweli kunakithiri na pia hali ya kuchanganya lugha. Imefikia hatua hivi sasa kwenye vyombo vya habari msanii ama mtu yeyote ameitwa pale anazungumza Watanzania wote wanasikiliza, watoto wanaojifunza afadhali sisi tayari tulishapa misingi, unasikia anasema nyimbo hii niliitunga mwaka jana, mwingine anasema, tena watangazaji wa soka wale, kwa mfano anasema timu ya Lipuli imetoka sare na timu ya Polisi kwa hiyo wameshindwa kupata matokeo. Wakati tunafahamu kwamba matokeo ni ama kushinda ama kushindwa ama kutoka sare.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kuna maudhui yanabadilishwa ambayo kwa kiwango kikubwa kwa hawa watoto ambao wanakua sasa tunashindwa kujua tunawafundisha hii *version* mpya ya kiswahili ama tunaendelea na ile ya kwetu? Wakati huo huo Waziri kwenye ukurasa wa 25 anaongelea kiswahili kuwa bidhaa, ukurasa mwingine sikumbuki anasema ni lugha ya kumi katika lugha 6,000, hizo zote ni sifa ambazo zitakamilika endapo tutakuwa na jitihada za dhati za kutunza kiswahili.

Nafahamu kwamba kwenye kukua kwa kiswahili katika maeneno mapya yanayokuja nayo ni sehemu ya kukuza lakini iwe *guided.* Naamini kuna wataalamu wetu ambao wanaweza kutuongoza ili hata sisi ambao walau tunajua kile tulichofundishwa miaka hiyo tufahamishwe rasmi sasa kwamba imebadilishwa siku hizi ni nyimbo hii sio wimbo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri wakati ananijibu mwezi Februari alisema kuna sera inakuja nikafurahi sana. Nilitarajia hotuba hii isheheni hiyo mikakati ya sera na iongelee kwa uzito kwa sababu hili jambo linakera.

Tunaomba tuzungumze kiswahili fasaha ili hiyo habari kwamba ni bidhaa, ni lugha ya kumi kweli iwe na tija vinginevyo tutaishia kuiandika tu hapa, hiyo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, siku moja nilihudhuria mechi ya soka ya Simba na nafikiri ni Polisi Morogoro ilikuwa mwaka jana au mwaka juzi sikumbuki vizuri na mabadiliko hayajafanyika. Lile gori la uwanja wa Jamhuri Morogoro upande wa Polisi nafikiri ni Kaskazini, *goalkeeper* akidondoka kuna shimo pale unaweza usimuone tena refa anaweza akamtafuta. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapo ndipo tunatoa klabu bingwa ya Tanzania ikacheze na *National Al-Ahly,* tunajidanganya. *Core function* ya soka ni pale kwenye *pitch.* Tunazungumza habari ya *corporate,* ni sawa lakini *business* kubwa kabisa ya soka ni kwenye *pitch*. Hivi kwa nini msikae na hizo *corporate* tukatafuta namna ambavyo kila timu inavyopanda daraja tunaweka mkakati wa pamoja wa kibiashara na kijamii tunapata uwanja, *pitch* ile hata kama hakuna jukwaa. Huwezi kutoa klabu bingwa kwenye uwanja ule wa Morogoro ambao *goalkeeper* akidondoka humuoni ikaenda kucheza na *National* Al-Ahly au Zamalek, haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nampongeza sana Ndugu yetu Malinzi kwa mambo anayoyafanya, anafanya mazuri tu lakini yako ya msingi. Kwa mfano, amezuia hapa juzi, kuna watu walitaka kuleta fujo, mpira unachezwa uwanjani, ukishindikana mezani, ukishindikana maandamano, haiwezekani! Acha watu wacheze mpira uwanjani, wewe simamia, lakini Malinzi rudi kwenye *core function* mpira unachezwa kwenye *pitch* tukose majukwaa lakini pale tucheze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwenye hotuba sikumbuki ukurasa wa ngapi kuna vituo 56 vitaanza vya kukuza soka la watoto, tuondokane na hii Dar es Salaam, Mwanza na Arusha *syndrome*. Kuna wachezaji wa mpira kutoka maeneo mengine kwa mfano Biharamulo kuna vipaji.

Waziri atuhakikishie namna gani ata-*distribute* tupate kituo Biharamulo, Mtwara na sehemu nyingine habari ya Dar es Salaam, Arusha achana nayo, vipaji vipo vijijini. *(Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuja kwenye suala la sanaa, nimesoma ukurasa fulani hapa unasema kwenye kukuza sanaa lilifanyika kongamano/warsha Kisarawe kwenye shule moja. Jamani lazima tuangalie *coverage,* tukisema hili ni tukio moja Kisarawe halitatusaidia kuna mambo hayahitaji hata bajeti. Hivi tukihakikisha kwenye *curriculum* ya shule ya msingi kuna siku moja kwa wiki au kila baada ya wiki mbili, mwalimu mmoja ametengenezwa vizuri anawaandaa watoto wanacheza ngoma za kienyeji, anafanya tathmini, anawaelekeza, hakuna bajeti ni wale wale. Kwa hiyo, tutafute *coverage* kubwa siyo lazima kila wakati bajeti ni pesa kuna bajeti ya muda tu na bajeti ya kuandaa walimu kule chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari ya soka, pia kuna habari ya UMISETA. Wakati huo UMISETA ilikuwa inatengeneza watu kwa sababu nguvu kubwa ilikuwa inawekwa sasa hivi tunaisikia UMISETA *passively* yaani unaisikia juu juu tu. Ndiyo maana hata hawa akina Samatta wanatokea kwa ajali tu, hata hawa *Serengeti Boys* kama alivyosema msemaji mmoja aliyetangulia ni ajali. Kuna hatari ikawa wanatoka huko amepata sifa kubwa *TFF* kazi wameifanya, lakini baada ya hapo hutaona jambo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumalizia kwa habari ya kwenye ligi kuu ya soka kama alivyosema msemaji mmoja aliyetangulia. Tutafute namna gani ya kulinda vipaji vyetu, wazo limetolewa hapo, tuhakikishe kwa mfano kwenye *first eleven* katika dakika zote tisini kuna walau *under twenty* wa Tanzania kwenye kila mechi inayochezwa ya Ligi ya *Vodacom.* Amesema Mbunge mmoja hapa naomba kusisitiza, hiyo ndiyo namna ya kulinda. Pia tutafute namna ambavyo hata wale wachezaji saba waliosajiliwa kutoka nje ya nchi tuwalete ili watuongeze nguvu ligi yetu iwe na mvuto zaidi, lakini sio lazima wote watano wawe kwenye mechi

moja, uwa-*limit* kwamba wale wageni kuna *limit* fulani ili wa ndani nao wapate fursa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, mchango wangu ni huo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kiteto Koshuma ajiandae Mheshimiwa Lema.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nichangie kuhusiana na suala zima la *COSOTA*. *COSOTA* ni kitengo ambacho kilianzishwa makusudi kabisa kwa ajili ya kuwasaidia wasanii ili waweze kumiliki kazi zao ipasavyo, lakini pia kuondokana na wizi ambao unafanywa na watu kutokana na hizi kazi za wasanii. Cha kustaajabisha ni kwamba kitengo hichi cha *COSOTA* kimepelekwa katika Wizara ya Viwanda na Biashara. Niishauri Serikali kwamba kitengo hiki cha *COSOTA* kiondoke kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara na kuweza kurudi katika Wizara hii ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu ukiangalia *COSOTA* kazi yao ni kuwatetea wasanii, kulinda kazi zao na hizo hati miliki zao. Sasa unapokipeleka kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara yenyewe inajihusisha na mambo mengine kabisa. Sasa unapopeleka chombo hiki kwenye Wizara kama ile tusitegemee *accountability* ya chombo hiki. Nashauri Serikali iweze kurudisha chombo hiki cha *COSOTA* kwenye Wizara ya Habari na Utamaduni kwa ajili ya *accountability* yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia chombo hiki ni muhimu sana katika kulinda haki za wasanii. Tunaona kazi za wasanii zinaibiwa sana, lakini adhabu yake pia inayotolewa kutokana na ile sheria ambayo tulipitisha hapa Bungeni ya

hati miliki yaani *copy right* kwa kweli ni ndogo sana. Unakuta sheria inasema kwamba kazi za msanii zinapokuwa zimeibiwa mtu aliyeiba zile kazi anaadhibiwa kwa adhabu ya faini ya shilingi milioni tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni juzi tu hapa tuliona mtu ameiba kontena kubwa sana la kazi za wasanii na adhabu aliyopewa ni faini ya shilingi milioni tano. Hivi mimi nikiiba kazi ya msanii ambayo najua kabisa kwamba kazi hii inaenda kunipa pesa zaidi hata zaidi ya shilingi milioni 20 halafu leo unaniambia kwamba nilipe faini ya shilingi milioni tano, sitaacha kweli kuwaibiwa wasanii kazi zao? Hili liko wazi kabisa, kazi za wasanii zitaendelea kuibiwa endapo tutaacha *COSOTA* kutosimamia kazi hizi za wasanii na adhabu zake kuwa ni ndogo kiasi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri nini Serikali? Naishauri Serikali adhabu za kuiba kazi za wasanii ziwe sawa kabisa na adhabu za unyang'anyi, sijui kama niko sahihi lakini nazungumzia *piracy.* Kwenye *Penal Code* mtu akiwa amefanya unyang'anyi *(piracy)* anapelekwa jela kwa muda wa miaka saba, lakini sasa kazi za wasanii zinapoibiwa tunaona kama ni kitu cha kawaida tu. Nashauri kabisa Serikali iweze kuuchukulia huu wizi wa kazi za wasanii kuwa kama wizi mwingine tu wa aina ya *piracy*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni wasanii ambapo wanakuwa wanaibiwa kazi zao kwa namna ya kupigwa kwa mfano redioni. *Let's say* mwanamuziki ambapo nyimbo zake zinakuwa zinapigwa redioni, lakini huyu mwanamuziki hafaidiki na wimbo wake kupigwa redioni. Nitakupa mfano mzuri sana. Tuna wanamuziki maarufu sana hapa Tanzania nikimtaja King Kiki kila mtu anawaza kitambaa cheupe na ndani ya Bunge hili naamini kabisa hata leo hii nikisema mimi natoa *offer* kwa Waheshimiwa Wabunge kwenda kumsikiliza King Kiki wote mtakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukumbuke na kuweka kichwani kwamba tunapomsikiliza huyu mwanamuziki King Kiki pamoja na kupiga wimbo wake wa kitambaa cheupe,

tunashangilia kwenye sherehe kwenye harusi au popote pale ambapo mtu unakuwa na shughuli yako nzuri, unamaliza kushangilia pale lakini huyu mwanamuziki King Kiki ukienda kumuangalia na ile kazi ambayo wewe umekuwa ukiishangilia anafaidika vipi? Unamchukua huyu mwanamuziki unamuweka hapa haendani kabisa na muziki ambao unapigwa redioni na kushangiliwa na kila Mtanzania. Naomba sana Serikali iweze kusimamia na kuzilinda kazi za wasanii ili waweze kufaidika ili basi siku moja hawa wasanii tuwaone kwamba kweli wanaendana na muziki ambao sisi Watanzania tunapenda kuusikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusiana na suala la kurekebisha Sheria ya Hati Miliki. Nasema hivi kwa sababu gani? Sheria hii kwanza imeshapendekezwa katika kamati mbalimbali kwamba iweze kufanyiwa marekebisho. Mimi ni mjumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo ambao tuna-*deal* na hizi kanuni ambazo zinatungwa. Tuliipitia hii Sheria ya Hati Miliki tukaona upungufu uliomo katika sheria hiyo. Upungufu mmoja ambao tuliugundua ni kwamba wakati sheria hii inatungwa hakukuwepo na ushirikishwaji wa wadau ambao ni wasanii, wanamichezo na wadau wengine mbalimbali ambao wanahusika katika suala zima la utamaduni na sanaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatizo linakuja kwamba pale ambapo wale wadau ambao wanahusika na sheria inayotungwa hawajashirikishwa, utaona kabisa kunakuwa na *gap* ambalo limewekwa. Kwa hiyo, naomba sana pamoja na mambo mengine yote ambayo yanaitaka sheria hii kurekebishwa kama vile adhabu, kwa sababu katika sheria hii ndiyo pale tunaona ile adhabu ya kuwaadhibu wale ambao wameiba kazi za wasanii ndiyo hiyo ya shilingi milioni tano ambayo ni ndogo.

Kwa hiyo, kama ungeshirikisha wale wadau ambao wanahusika ungeona wangeweza kupendekeza jambo ambalo mimi leo nalisema na kulipendekeza mbele ya Serikali kwamba iwe ni adhabu sawa kabisa na wizi mwingine. Kwa hiyo, nashauri kabisa Serikali iweze kutuletea hii sheria ili

tuweze kuifanyia marekebisho lakini baada ya kuwa imewashirikisha wadau wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti jambo la mwisho ni suala la michezo. Suala la michezo hapa Tanzania hatulichukulii maanani kabisa. Ukiangalia enzi za zamani michezo ilikuwa ni kitu ambacho tunakitilia maanani sana. Kila mahali unakoenda hata mwanafunzi anafahamu kabisa kwamba mimi bila kushiriki michezo sitaweza kufaulu darasani kwa sababu darasani tulikuwa tunaambiwa hivyo na walimu wetu kwamba ili uweze kufanya vizuri lazima ushiriki michezo. Hiyo inaendana kabisa na usemi kwamba ili mtu uwe *active* kwenye akili zako lazima kwanza ushiriki michezo kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, suala la michezo hapa Tanzania tumekuwa tukilichukulia tu kama jambo la kawaida. Mimi naiomba Serikali ianze sasa kurudisha michezo mashuleni na kuweza kuweka mkazo huko mashuleni ili hawa akina Samatta watokee kule na hata kina Diamond hawa watokee kule kule kwa sababu hata kwenye kuhamasisha michezo kuna uimbaji pia huko mashuleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika kurahisisha suala hili ili liweze kufanyika vizuri ni kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wengine kwamba tuanzishe *sports academy*. Nchi kama Kenya tu msifikiri kwamba Kenya wanaposhinda kwenye *Olympics* mkadhani kwamba huwa wanaenda tu, wanaibuana *from no where* wanapelekwa kwenye michezo, hapana! Kenya wanachukua wachezaji kutoka kwenye *sports academy* zao na sasa hivi Kenya wanaenda mbali zaidi wanaleta *International Sports Academy* ambayo hiyo sasa itakuwa inawarahisishia kuweza kutoa wachezaji kutoka kwenye zile *sports academy* kuwapeleka kwenda kufanya mashindano lakini sisi hapa tunaibuana tu, mtu akisema anajua kuogelea anabebwa, anapelekwa, akifika kule ameshindwa. Tanzania hakuna mchezo ambao tumewahi kufanya vizuri hata siku moja. Nadhani hizo ni historia za nyuma kabisa labda hata nilikuwa sijazaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, baada ya mapendekezo hayo, naamini Serikali itachukua mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge wote na kuweza kuboresha Sekta hii ya Habari, Utamaduni na Michezo. Nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lema ajiandae Mheshimiwa Devotha Minja.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naif Abazeed alikuwa ni kijana mdogo sana kipindi hicho wa miaka isiyozidi 16 na ndiye alisababisha machafuko yanayoendelea Syria sasa hivi. Pia Mohamed Bouazizi yeye ndiye aliyesababisha machafuko yaliyotokea kule Tunisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mwanaharakati mmoja alisema maneno haya, naomba niyasome:-

*"Kitu kimoja tu cha hakika ni kuwa, damu ikimwagika hasa damu ya kimapinduzi hutoa mvuke utakaonyesha na kutiririsha mafuriko katika mito na vijito vya haki. Kama itanyesha mvua ya radi basi itaambatana na mwanga na cheche zitakazowamulika walaghai, watesaji, wakandamizaji wa haki na watetezi wa haki watapata mwanga katikati ya giza totoro la unyanyasaji." (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno haya ni *message* ya mwisho ya Ben Saanane ambaye hatujui kama ni marehemu ama ni hai, lakini hata kumjadili humu haturuhusiwi, nje mikutano ya hadhara hatufanyi. Kama kijana wa miaka 16 katika Taifa ambalo halina uhuru wa vyombo vya habari, halina chama cha siasa, aliandika maneno machache tu, *"Assad must go, Assad will be next,"* leo Syria haina amani. Kama kijana mmoja alijichoma moto Tunisia na Tunisia ikaingia kwenye machafuko, vyama vya siasa ni *alternative* ya amani, uhuru wa habari ni *alternative* ya amani siyo kikwazo cha amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanapoongea wanatema nyongo. Watu wanapoongea wana-*release tension,* leo tunapotaka kujadili mambo ya msingi mnatumia nguvu na uwezo mlionao, mtashinda. Kila jambo mnalotaka kulipitisha kwa wingi wenu mtashinda. Kila jambo mnalotaka kulifanya kwa wingi wenu mtatushinda. Kwenye mchango wangu uliopita nilisema Mungu hadhihakiwi, apandacho mtu ndicho avunacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa magereza, vijana waliokamatwa kwa makosa ya *cyber* walioko magereza, makosa ambayo ni *bailable offence* ni wengi. Wanakamatwa kimya kimya wanapelekwa mahakamani, wanasomewa mashtaka bila ndugu zao kuwepo, wanapelekwa magereza. Vijana wamejaa magereza kwa sababu ya ukosoaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimeona kwenye mitandao na mimi naomba nipaze sauti kabisa kwamba Kinana naye amefichwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nimtetee Kinana kama Waziri Kivuli wa Mambo ya Ndani. Kama ni kweli Kinana amefichwa, kwa mujibu wa mitandao kwa sababu hata Ben Saanane kupotea tuliona kwenye mitandao, tukapuuza. Hii ya Kinana kama ninyi mtapuuza, mimi sitaki kupuuza, ni mpiga kura wangu Arusha, naomba nimtetee. *(Makofi/Kicheko)*

*Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna mahali mmemficha Kinana, naomba Kinana aliko mumwachie mara moja aendelee na shughuli nyingine za kawaida za kila siku. (Makofi)* **[Maneno Haya Sio Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisome...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema subiri kidogo. Sasa Mheshimiwa Simbachene. Mheshimiwa Lissu kaa kidogo.

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Kuhusu utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu. Nataka nipitie kwenye Kanuni ya 64(2) ambayo inatoa nafasi kukumbusha Bunge na Waheshimiwa Wabunge endapo kuna Kanuni inayovunjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anayezungumza anasema jambo ambalo hana uhakika nalo na ni la mashaka. Sidhani kama ana uhakika na kama ana uhakika na jambo analolisema kwamba Kinana amefichwa alithibitishie Bunge hili na kama hawezi kulithibitishia Bunge hili kupitia Kanuni ya 72(2)...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Nisikilizeni basi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Kanuni ya 72(2), nakuomba umtake mzungumzaji anayezungumza afute maneno hayo.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu kwa dakika moja, umezoeleka utaratibu hapa wa kuomba utaratibu kupitia Kanuni moja tu ya 68 au kuomba kupitia Kanuni moja tu ya 64 au Kanuni ya 63, utaratibu unaombwa kwa *entries* nyingi sana. *Entry* niliyopitia hainitaki mimi nifanye hivyo, ninachotaka tu ni kukiomba Kiti ama anayezungumza athibitishe au umtake aondoe maneno hayo katika maelezo yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Mheshimiwa Simbachawene amezungumzia Kanuni ya 72(2), naomba niisome halafu uone kama alichozungumza...

**MWENYEKITI:** Amesema 64(2).

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema 72(2)...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Ngoja, ngoja, tuanze na Kanuni ya 64(2), inasema hivi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Simbachawene Kanuni ipi uliyoisema?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu kwa kumpunguzia kazi Mheshimiwa Mwanasheria mwenzangu...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hebu tulieni.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetumia Kanuni ya 72(2) kuomba utaratibu kupitia na inasema hivi...

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Lissu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Nisikilize.

**MWENYEKITI:** Basi kaa.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mheshimiwa Waziri Simbachawene hajui atendalo na Mwenyezi amsamehe.

**MBUNGE FULANI:** Amin.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 72(2) inasema:-

*"Mbunge atakayekiuka utaratibu uliowekwa na Kanuni hizi anaweza papo hapo kutakiwa na Spika afuate utaratibu na vilevile Mbunge mwingine yeyote anaweza kusimama na kumfahamisha Spika kuhusu ukiukwaji wa utaratibu huo na katika kufanya hivyo atalazimika kutaja Kanuni ya Bunge iliyoweka utaratibu uliokiukwa."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Simbachawene kama angekuwa anafahamu anataka nini asingetumia Kanuni ya 72(2) na kwa sababu amekitumia alitakiwa aseme ni Kanuni ipi ambayo imekiukwa. Ni kutokujua Kanuni tu...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Taarifa ya kitu gani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Simbachawene subiri kwanza.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Nataka nimpe taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa subiri kwanza.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Hebu akae.

**MBUNGE FULANI:** Sikiliza Kiti.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Lema amezungumza kauli ambayo ni ya uongo, ambayo sio ya kweli *then* utaratibu uliopo katika Kanuni ya 63 inayohusu kutokusema uongo Bungeni ingefuatwa. Utaratibu huo unasema hivi, huyo anayetuhumu

kwamba kuna uongo umezungumzwa yeye angetoa ukweli wake na baada ya kutoa ukweli wake basi huyo anayedai amesema uongo ndiyo angemwambia thibitisha kauli yako au ifute. Sasa kwa sababu Mheshimiwa huyu hajajiandaa amekwenda alikoenda. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lema amesema...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu umeshaeleweka, kaa chini.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumze hii ya Mheshimiwa Lema aliyoitumia.

**MWENYEKITI:** Eeh!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lema amesema amesoma kwenye mitandao kwamba Katibu Mkuu wa CCM Ndugu Abdulrahman Kinana amefichwa na anasema kama kweli amefichwa mambo haya ya mitandao ya Ben Saanane ndivyo yalivyoanza. Sasa amekosea wapi? Ame-*refer* taarifa za mitandao, ame-*refer to published information,* sasa shida iko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Mheshimiwa Lema aendelee na hoja yake. *(Makofi)*

**MHE. KAPT. MST. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Chief Whip.*

**MHE. KAPT. MST. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkuchika subiri *Chief Whip* kwanza.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunarudi pale pale Kuhusu Utaratibu na utaratibu ni jambo la kikanuni na nimshukuru sana Mheshimiwa Tundu Lissu ameelewa kwamba tulikuwa kwenye jambo la kiutaratibu la kikanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Simbachawene amesema Kanuni ya 64(1)...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Ngoja, amezitaja zote.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee. Nataka kuweka msisitizo kwenye Kanuni ya 64(1)(a) ambayo inakataza Mbunge kutokutoa taarifa ambazo hazina ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni hiyo ukienda kusoma na Kanuni nyingine, Mheshimiwa Lissu yuko sahihi kwamba inakupasa pia hata wewe unayesema hizo taarifa zinazosemwa ndani ya Bunge kwamba hazina ukweli lazima uzithibitishe. Mimi naomba nimthibitishie Mheshimiwa Lema, Mheshimiwa Kinana tumezungumza naye wakati wa maadhimisho ya Muungano, wakati wa maadhimisho ya Mei Mosi, Mheshimiwa Kinana ametoka matibabu na sasa anapumzika nyumbani kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Mheshimiwa Kinana mimi mwenyewe niliyekuwa nasimamia maadhimisho ya sherehe hizo na taarifa hizo ninazo, Mheshimiwa Lema afute maneno hayo, asiyazungumze. Maneno hayo anayoyachukua kwenye mtandao ambayo hayana ukweli na mimi hapa namthibitishia kwamba Mheshimiwa Kinana

hajafichwa, kwa mujibu wa utaratibu namuomba Mheshimiwa Lema aachane na maneno ya mtandao na ayafute ndani ya Bunge hili kwa sababu hayana ukweli. *(Makofi)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mkuchika.

**MHE. KAPT. MST. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako. Asubuhi leo Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo aliwasilisha mezani hotuba yake. Baada ya maswali ya majibu ukaanza mjadala na kweli kabla hatujaenda mapumziko watu wamejadili sana Wizara ya Habari, wametoa ushauri. Sasa hivi Mheshimiwa Lema amepewa nafasi kuchangia hotuba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, tangu ameanza hajazungumza habari yoyote inayohusu Wizara. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. KAPT. MST. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa umri huu hata ukinizomea siachi kusema. Mimi naomba mwongozo wako, Kanuni ya 64(1)(b) ya Kanuni zetu za Bunge inasema; *"Mbunge hatazungumzia jambo ambalo haliko kwenye mjadala."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Lema amezungumza mambo ya Wizara ya Mambo ya Ndani, amezungumza mambo ya wapi, naomba tu mwongozo wako kwa sababu wako Watendaji wa Wizara ya Habari wamejaa huko juu wanasubiri ushauri wa Bunge badala ya kupata ushauri unaowahusu Wizara ya Habari, watu wanazungumza habari ya *experience* ya kukaa jela, ilikuwaje jela, hapa hatuzungumzi mambo ya jela, tunazungumza Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, leo siku hii naomba tuimalize vizuri tu sababu tumeanza vizuri, tumalize vizuri.

**MBUNGE FULANI:** Amin.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni hizi, Kanuni ya 68(10), Spika ndiye mwenye maamuzi ya mwisho ya masuala yote ya Kanuni. Kwa hiyo, Mheshimiwa Lema, kwa *spirit* ile ya kifamilia tunayokubaliana nayo, nakuomba tu futa haya maneno, kwa sababu huyu mtu ana familia yake, watoto, ndugu zake na jamaa zake, unajenga kitu cha hofu ambacho hakipo. Kitu kama hicho hakijatokea na hatutegemei kitokee. Sasa ili kumpa heshima huyu mtu kama heshima ambayo Kiti kinakupa wewe na Bunge linakupa wewe futa haya maneno tuendelee na mjadala. *(Makofi)*

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuheshimu na Mheshimiwa Jenista nakuheshimu sana. Hivi viongozi wote wa CCM ninyi na Usalama wa Taifa mnashindwa kusema Kinana yupo? Si yupo Kinana? *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema...

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijenge hoja.

**MWEYEKITI:** *No, no, no,* Mheshimiwa Lema.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mitandao...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema, Bunge halifanyi kazi na mitandao. Nimekwambia kwa njia za kistaarabu sana, futa haya maneno uendelee na mjadala.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Usije ukawa...

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongee basi, nasema hivi...

**MWENYEKITI:** Ah, ah, mimi nimesimama kaa kwanza.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa.

**MWENYEKITI:** Sasa unataka kunikalisha mimi? Mimi nimesema, Mheshimiwa Lema nisikilize mimi sio Mheshimiwa Lissu. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 68(10) mwenye mamlaka ya Kanuni zote hizi ni Spika ambaye ndiye Kiti. Sasa *for the spirit* ya mjadala, futa hiyo kauli wala haikupeleki popote. Futa hiyo kauli endelea na mjadala wako.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa vile Waziri amesema Mheshimiwa Kinana yupo na mimi niwaambie wapiga kura wangu wa Arusha na familia yake kwamba Waziri ameniambia Kinana yupo. Nafuta maneno hayo kwa sababu Mheshimiwa Kinana yupo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetumia dakika mbili tu, nilikuwa naangalia, nina dakika nane. Kwa hiyo, hapo Makatibu Mezani naomba tafadhali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtoto mmoja alipewa shilingi 200,000 na baba yake akaambiwa akalipe ada. Alipokuwa njiani akaenda aka-*bet* mchezo kwa shilingi 30,000. Alipo-*bet* akapata shilingi 3,000,000. Akamtumia baba yake *message* akamwambia, baba ile pesa uliyonipa ya ada nimetumia shilingi 30,000 nime-*bet.* Sasa baba kabla hajajua mtoto alipata faida ya shilingi 3,000,000 akaanza kumtukana mtoto, mjinga wewe, kwa nini umetumia fedha kufanya mambo yako ya kitoto? Mtoto akamwambia, baba hapana, nime-*bet* shilingi 30,000 nimepata shilingi 3,000,000. Baba akageuka akamwambia si unge-*bet* yote upate nyingi? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko siku tutawabariki na mtakataa baraka. Yaani iko siku tutawatetea kabisa na mtakataa utetezi wetu kwa sababu kila mara tunapokuja na mambo ya msingi mnafikiri sisi ni maadui zenu. Ninyi sio maadui zetu, ninyi ni marafiki zetu, nyie ndiyo chama tawala. Leo tumeongea habari ya Ben Saanane mkakataa, nikaongea habari ya Katibu Mkuu wenu hata kama ni tetesi mlitakiwa mzichukulie maanani mseme huyu kijana ana roho nzuri, mmekataa, sasa nimeondoka huko. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhuru wa habari ni nini? Nimesema kwenye hoja zangu nilizojenga, hatuwezi kuwa na Taifa lenye amani bila kuwa na uhuru wa habari. Mheshimiwa Tundu Lissu amewaambia asubuhi hapa kwamba msifikiri mnatunga sheria ama msifikiri mnatumia wingi wenu kutukomoa sisi, mna watoto na wajukuu wanakua. Mheshimiwa Mkuchika hapa amesema yeye ana umri mkubwa, ni kweli ana umri mkubwa ndiyo maana kuna saa mambo mengine ya msingi yanaweza yakampita, lakini ninachosema ni kwamba Mheshimiwa Mkuchika ana watoto, ana wajukuu nawajua. Tunapopigania uhuru wa habari hatupiganii CHADEMA, tunapopigania uhuru wa habari hatupiganii CCM, tunapigania Taifa bora na Taifa huru. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndiyo tukasema leo ndani ya Bunge hatusemi na kwenye mitandao hawaongei. Sasa kama kwenye mitandao hawataongea, vyombo vya habari havitasema, huko mitaani mikutano ya hadhara imezuiwa ndiyo maana nikaanza kujenga hoja kwa wale vijana wawili, yule wa Syria na yule wa Tunisia kwamba iko siku watu wataingia barabarani kutafuta uhuru mnaowanyima. Watu hawa hawatakuwa wametumwa na CHADEMA wala hawatakuwa wametumwa na *CUF* na siku hiyo kila mtu atatafuta nyumba ya kujificha, iko siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu unapozuia haki, unapozuia uhuru, unapozuia kweli, unatengeneza balaa katika Taifa hili. Tunalalamika kwa sababu familia zetu zinaishi hapa, tunalalamika kwa sababu sisi tunaishi hapa tumejenga

Tanzania, tumeishi Tanzania, tumezaliwa Tanzania, tungekuwa na mpango wa kuondoka tungeenda kulalamikia Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisema miongozo ni mingi na sijui hata hotuba yangu itakuwaje sasa kama hotuba ya Waziri wa Michezo, Habari na Utamaduni mmeifanya hivi, hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani na uzoefu wa Lijualikali alivyokuwa Magereza, uzoefu wangu nilipokuwa magereza mtaanza kuizuia kuanzia kwenye salamu. *(Makofi)*

Waheshimwa Wabunge mko wengi tusaidieni, Mawaziri tusaidieni huku kuna madaktari, kuna maprofesa tusaidieni, taifa hili tukishamalizwa sisi, narudia tena, tukishamalizwa sisi, msumeno utakaofuatwa utakuwa ni kwenu. Ni nini mnachokipigania Waheshimiwa Wabunge mnakipigania mnafanya kila kitu kinakuwa hovyo, ni fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, utu wa mtu haupimwi kwa ghorofa, utu wa mtu haupimwi kwa cheo, utu wa mtu unapimwa kwa kazi na wajibu ulioufanya katika ulimwengu na wajibu huo ninyi kama Chama Tawala, mnaweza mkaufanya, sisi tutashindwa. Mimi nilikamatwa nje getini hapo, nikapelekwa Kondoa, nikawekwa *lockup* saa nne usiku mpaka saa nane usiku. Nikapelekwa Arusha nikatengwa chumba changu peke yangu, nikakaa jela nikatoka baada ya miezi minne. Mnaweza mkafanya hivyo leo, mimi mkitaka kuniua mnaniua leo, kesho ni mbali, mkitaka kumuua yeyote hapa mnamuua leo, kesho ni mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema hivi haya mambo mnayotuzuia kuyasema mnafikiri tunayasema kwa sababu tunapenda uanaharakati, mimi na watoto na mtoto wangu wa kwanza ana miaka 11 na wa mwisho ana miaka minne, ningependa kuona watoto wangu, ndoa, harusi na elimu ya watoto wangu kwa macho yangu. Hata hivyo, ikibidi nisione hiyo harusi kwa sababu ya kupigania ninachokipigania watakumbuka kwamba maisha yetu Bungeni hayakupigania *property* yalipigania haki na msingi wa Taifa hili kazi hii ambayo mmeishinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimwa Wabunge, Waheshimiwa Mawaziri, hapo alikaa Mzee Sitta leo ni marehemu, kila mtu atapita kwa wakati wake. Ni muhimu mkapita mkaacha faraja nyuma, ni muhimu mkapita mkaacha baraka nyuma, acheni kutumia wingi wenu vibaya.

Mheshimiwa Simbachawene wewe una historia, wewe ulikuwa kondakta, Mungu amekuweka hapo ulipo, tulitarajia tukuone wewe unapigania nchi hii, tulitarajia tukuone wewe unakumbukumbu ya haki na msingi, leo unaishi utafikiria umezaliwa kwenye familia *Warren Buffet* kila watu wakisimama kuongea ukweli ...*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Ya kwanza Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema ni ya pili.

**WABUNGE FULANI:** Ya kwanza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema ni kengele ya pili.

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Devotha Minja ajiandae Mheshimiwa Omari Kigua.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, niwapongeze waandishi wa habari ambao wanafanya kazi yao vizuri sana. Tuna kila sababu ya kuwapongeza waandishi kwa sababu tujiulize tu kama Taifa hili lingekuwa halina waandishi hakuna vyombo vya habari sijui tungekuwa kwenye giza la namna gani. Tunapenda tuwapongeze kwa kazi ambayo wanaifanya, japo tunajua wanafanya kazi katika mazingira magumu kuliko ilivyo kawaida. Tunaendelea kuwapa moyo

waendelee kupambana kuendelea kutoa elimu na kuelimisha taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata katika hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani (Waziri Kivuli) alikuwa ametoa pongezi nyingi kwa harakati mbalimbali ambazo Waandishi wa Habari wanaendelea kufanya katika kujaribu kujitetea na kuhakikisha kwamba wanaendelea kuifanya kazi yao. Pamoja na kwamba hotuba ile imechinjiwa baharini lakini mimi nawapa *comfort* kwamba tutaendelea kuwasemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza Waziri wakati wa hotuba yake, amewasifu wadau mbalimbali wakiwemo wanahabari, wanamichezo lakini sijasikia mahali akizungumza kuhusu habari ya mateso ya waandishi wa habari. Waandishi wa habari ambao walivamiwa na kuumizwa wakiwa katika *press conference* ya Chama cha Wananchi *(CUF)* ambao nao ni wadau muhimu nilitarajia angewapa pole. Hali kadhalika kwa wasanii, Ney wa Mitego na Roma Mkatoliki nao waliteswa ambao nao pia ni wadau wake, alipaswa nao awape pole kwa kazi kubwa ambayo wanafanya pamoja kupitia madhila mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Mheshimiwa Waziri amenukuliwa akisema kwamba yeye ni msikivu na yupo tayari kuhakikisha kwamba anaendelea kusaidia tasnia hii ya habari iendelee kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni zaidi ya waandishi 30 wamepitia manyanyaso makubwa, wengine wakiwekwa ndani na Wakuu wa Wilaya, vyombo vya habari vikivamiwa ikiwemo redio ya *Clouds*, tunamuomba Mheshimiwa Waziri wakati ana *windup* hapa atueleze ni nini hatma ya ripoti iliyoandaliwa na Mheshimiwa Nape Nnauye wakati akiwa Waziri kuhusu sakata la kuvamiwa *Clouds.* Si hiyo tu pia atuambie ni sheria ipi ambayo inamruhusu *DC* kumzuia mwandishi wa habari asiingie katika Wilaya eti apate kibali cha kuandika habari.

**MBUNGE FULANI:** Duh.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Tunaomba Mheshimiwa Waziri atueleze kwa hii sheria ambayo *RC, DC* ana uwezo wa kumuweka mtu rumande kwa saa 48 iletwe Bungeni irekebishwe kwa sababu imekuwa ikitumika kama kigezo cha kuwaumiza waandishi wa habari. Tumeona Ndugu Mnyeti ambaye ni *DC* wa Arumeru amewaweka Waandishi wa Habari ndani kisa wameingia katika eneo lake la kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 ambayo waandishi wa habari walitambuliwa rasmi kwa maana ya kuhakikisha *professional* hii ya waandishi wa habari inafanya vizuri. Tunashukuru hivi sasa Serikali inatambua kwamba tasnia ya habari ni muhimu na inafanya kazi. Hata hivyo, yapo mambo mengine ya msingi ambayo tunajiuliza, kama uandishi wa habari ni tasnia muhimu kama ilivyo *professional* zingine mfano za udaktari, wanasheria kuna mambo ya msingi sana ambapo yanatufanya tunashindwa kuielewa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikitokea mwandishi wa habari amefanya makosa ya kitaaluma sheria hii inasema akamatwe na polisi afikishwe mahakamani, lakini taaluma kama ya udaktari, endapo daktari atafanya makosa ya kitaaluma kuna sheria kwamba bodi inapitia, inamuajibisha lakini hakuna harakati za haraka haraka za kumpeleka polisi na kumfikisha mahakamani. Imewahi kutokea daktari ambaye alikuwa afanye operesheni ya kichwa akafanya ya mguu, lakini alifikishwa mahakamani? Kwa nini tunapokuja kwenye suala la uandishi wa habari wakamatwe na polisi wafikishwe mahakamani, tunaona hapa kuna *double standard*. Tunaomba kama kweli hii ni sheria na tumeamua kuitambua tasnia ya waandishi wa habari basi kama mtu atakuwa amefanya kosa la kitaaluma bodi zihakikishe zinamwadhibu kwa kuangalia taaluma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kuhusu ukata wa hivi sasa kwa vyombo vya habari, hii haijawahi kutokea. Hivi sasa waandishi wa habari hawana kazi za kufanya, kuna

poromoko kubwa la waandishi kuachishwa kazi. Kampuni za *The Guardian, Free Media,* Azam na *New Habari Cooperation* zimepunguza waandishi. Ni kwa nini waandishi hawa wanapunguzwa? Ni kwa sababu hali imekuwa ngumu, wanafanya kazi katika mazingira magumu. Gazeti ambalo lilikuwa linatengeneza nakala 26,000 sasa hivi linatengeneza nakala 5,000. Hali hii inakuwa ngumu zaidi kwa sababu Serikali haipeleki matangazo kwenye hivi vyombo vya habari hususani vya *private*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Rais akihitaji kufanya *press conference* anaita vyombo vyote, Mkuu wa Wilaya au *RC* wakitaka kufanya *press conference* anaita vyombo vyote lakini ikija kwenye suala la matangazo vyombo vya binafsi vinabaguliwa. Kwa nini tusitende haki tuwezeshe hizi *private sector* zifanye kazi zipate matangazo ziweze kuhudumia Taifa hili? Kama kuna mkakati wa kuhakikisha kwamba tunadumaza vyombo hivi tuelewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima Serikali iangalie imetoa mamlaka hivi hivi sasa kwa Idara ya Habari - Maelezo yenyewe ichuke jukumu la kuratibu matangazo yote. Katika matangazo ambayo yanakwenda kwenye vyombo vya habari, Idara ya Habari - Maelezo ambayo imepewa jukumu ya kuratibu matangazo inapata *commission* ya asilimia 10, kwa hiyo imeacha kazi yake ya msingi sasa hivi inahakikisha inatafuta matangazo. Hii ni kama ilivyo sasa hivi *traffic* ambapo wameacha kazi zao za msingi za kuhangaika na ajali inahangaika na tochi za kukusanya. Tunaomba tusaidiwe tujue kama kweli suala hili la kuratibu matangazo ambalo linakwenda kwa njia ambayo ni ya kibaguzi kupitia Idara ya Habari - Maelezo, ni kwa nini utaratibu wa zamani usitumike na vyombo vyote vipate haki katika kupata matangazo ili viweze ku–*retain* waandishi ambao wameajiriwa katika vyombo hivi vya habari. *(Makofi)*

Mheshimwa Mwenyekiti, tukitoka hapo tuzungumze kuhusu hofu iliyopo hivi sasa kwa vyombo vya habari. Hakuna uhuru kabisa wa vyombo vya habari hapa nchini. Tumemsikia Mheshimiwa Rais katika ziara zake Mkoani Shinyanga alisema

yapo magazeti matatu ambayo yupo karibuni kuyafungia, japo hakuyataja lakini hii moja kwa moja kama mkuu wa nchi inaleta hofu kwa waandishi wa habari na wamiliki wa vyombo vya habari kuona kwamba pengine ni mimi au yule. Kwa hiyo, waandike habari ya kuipendeza Serikali na kuacha kuandika habari za kukosoa Serikali pale ambapo inakwenda kinyume na utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sakata la Bashite kuvamia *Clouds*, Rais alinukuliwa kwamba vyombo vya habari haviko huru kwa kiasi hicho na kutoa karipio kali. Tulitegemea kwamba Rais angesaidia kwa mtu kama huyu ambaye amekiuka maadili ya utumishi wa umma kwa sheria ya mwaka 1995 mpaka sasa hivi asingekuwa kazini. Kwenda kuivamia *studio* na waandishi wa habari ambao wanafanya kazi zao kihalali na kuhakikisha waandishi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Omari Kigua, Mheshimiwa Mbogo na Mheshimiwa Mgumba.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo ili na mimi niweze kusema machache juu ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pale. Pengine nianze tu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanayoifanya katika Wizara yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa pongezi hizo, sitakuwa na maneno mengi sana, nitajikita kwenye maeneo matatu. Kwanza nitaanza na Shirika letu la Utangazaji *(TBC).* Inasikitisha sana kuona kwamba *TBC* haifanyi vizuri hata Kamati yetu imesema kwamba *TBC* waongezewe pesa, *TBC* haifiki maeneo mengi nchini hivi, tatizo liko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Waziri, *TBC* ndiyo wanatusaidia sisi hapa wakati wa kampeni

*TBC*, ndiyo inasikika kila eneo. Kuna baadhi ya *TV* hazifanyi *coverage* kabisa hasa kwa upande wetu wa Chama cha Mapinduzi, hebu tuone sasa wakati umefika tuwekeze *TBC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa kwenye kitabu hiki kwamba *Azam TV* wametumia dola milioni 40 takribani shilingi bilioni 90 tunashindwa nini kuwekeza kwenye *TBC?* Biashara ni ushindani kwa sababu hata ukipita mtaani unaona watu hawangalii *TBC* wanaangalia *tv* nyingine wakati hili ni Shirika kubwa la Taifa, tatizo liko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe wakati Mheshimiwa Waziri ana-*wind* tupeleke kwenye Kamati yetu ya Bajeti suala hili ili tuwawekee pesa *TBC*. Hili haliwezekani kwa sababu *TBC* ni shirika la wananchi, linatakiwa lifike kila kona ya Tanzania hii. Mimi nasikitika sana kwa sababu kama michango yetu haitazingatiwa maana yake *TBC* itakufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naomba nijikite kwenye *TFF* (Shirikisho la Mpira Tanzania). Sote tunakumbuka enzi ya Ndolanga wadau wa mpira ilikuwa kila siku ni mahakamani mpaka ikafika *FIFA.* Alipokuja Tenga nchi hii ilitulia na mpira ukaanza kwenda. Leo hii tunashuhudia Rais wa *TFF* kila siku ni migogoro. Tumeshuhudia migogoro imeanzia kwenye chaguzi za mikoa, kila siku unasikia huyu hana sifa, huyu hana *personality, TFF* imejaa Usimba na Uyanga. Tunashuhudia Kamati za *TFF* unakuta mtu ni Mwenyekiti/Rais wa Simba au Yanga huyo huyo unamkuta ni mshiriki wa *TFF*, tutafika wapi? Tunazungumzia mpira kwa sababu mpira ni biashara na ni ajira sasa tutafikaje kama tuna migogoro kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mzungumzaji wa mwanzo leo Mheshimiwa Juma Nkamia alisema kwamba *FIFA* wanaruhusu Serikali ku-*interfere,* mimi najua hairuhusiwi. Mimi naomba mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi tuhakikishe kwamba tunachagua viongozi ambao watasimamia maendeleo ya mpira ya nchi hii. Tuache habari ya Simba na

Yanga. Hebu Rais wa *TFF* nenda kajifunze kwa wenzetu wa *West Africa* wanafanya nini, kwa nini wanafika mbele? Inasikitisha leo Tanzania yenye zaidi ya watu milioni 50 tuna mchezaji mmoja ambaye anacheza *Europe,* Mbwana Samatta, hivi imefikia hapa? Hebu tujiulize tumekosea wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine hatuna viwanja vya kutosha. Uwanja mzuri upo Dar es Salaam mikoani kote hakuna viwanja, sisi Chama cha Mapinduzi tuna viwanja vingi tu. Tunaomba Wizara husika ianze kukarabati viwanja vile tusitegemee tu ufadhili. Tuangalie namna gani ambavyo tunaweza kukarabati viwanja vile ili mpira uweze kuchezwa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba nimeona kwamba Wizara itaanza kushirikiana na TAMISEMI kwa ajili ya kujenga vituo vya michezo mikoani. Ni jambo la kupongeza sana Mheshimiwa Waziri na mkashauri Waheshimiwa Wabunge pia waanzishe vituo katika majimbo yao, nadhani litakuwa ni jambo la busara sana. Nashauri Wahemishiwa Wabunge wachukue ushauri uliotolewa kwenye hotuba hii kwani una tija na manufaa kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 20 amezungumzia kwamba takribani asilimia 90 ya watumishi ambao wanafanya kazi katika vyombo vyetu vya habari hawana weledi au ujuzi wa mambo ya habari, hili jambo ni la kusikitisha sana. Hivi inawezekanaje mwandishi wa habari awe hana weledi wa kufanya kazi hii? Ndiyo maana yanazungumzwa mambo mengi kwamba hata utangazaji hauendi sawa, maneno yanayotamkwa siyo sahihi kwa sababu hawazingatii weledi. Nimwombe Mheshimiwa Waziri kupitia *TCRA* hebu angalieni weledi wa wafanyakazi hawa katika vyombo vyetu vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo maneno machache, naomba nikushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii. Kwanza nimshukuru Mungu na pia nimpongeze Waziri kwa uwasilishaji mzuri pamoja na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia suala la shule za msingi na sekondari kwa ujumla wake upande wa sanaa, michezo na utamaduni. Sijui kama ni sera imebadilika au ni kipi kilichotokea tofauti na miaka ya nyuma, shule zetu za msingi tulikuwa tunafundishwa michezo, sanaa, utamaduni na muziki. Hii ilikuwa inatujenga mpaka hata leo hii wengine tunaweza kuimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ilikuwa inasaidia kwa mtu ambaye anaendelea kusoma mpaka chuo kikuu anaenda kusomea muziki na kuna kozi zingine kwa mfano kama *physical education,* mtu anasomea muziki somo lingine la kufundishia. Kwa hiyo, atatoka ni mwanamuziki lakini pia anakuwa na somo la kufundishia. Msingi unakuwa umejengwa kuanzia shule ya msingi na tuna vyuo vingine ambavyo vilikuwa vinatoa *diploma* kwa mfano kule Mwanza (Butimba) watu wamesoma sanaa.

Kwa hiyo, tuombe Waziri atakavyokuja ajaribu kutuelekeza kwamba ni jinsi gani ataweza kurudisha kwenye shule zetu za msingi na sekondari jambo hili ambalo lilikuwa linatusaidia katika kukuza hivi vipaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Wizara hii tunaoanisha na utalii, kwa misingi ipi? Tunavyowakuza watu waka-*perfom* nje ya nchi, kama walivyokuwa akina Filbert Bayi na wengine, tukiangalia nchi za Kenya, Ethiopia watu ambao wanaweza kufanya hizi mbio za *marathon* kama akina Haile Gebrselassie wameingia mpaka kwenye matangazo, wanatangaza nchi yao, wameingiza mapato ya ndani katika nchi yao kwa kuleta fedha za kigeni. Sasa na sisi Wizara hii itakuwa ni moja ya Wizara ambazo zitaweza kuukuza utalii katika nchi yetu kwa watu kufanya kazi nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyikiti, kwa upande wa sanaa kwa mfano tulikuwa na Marehemu Kanumba aliweza kufanya *collaboration* na Wanaigeria, imeenda, sasa hizi tuna mwanamuziki Diamond anafanya *collaboration* na wanamuziki mbalimbali mpaka Marekani na huko kwingine. Kwa hiyo, Wizara hii inakuza utalii ni muhimu sana kwenye pato letu la nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine dunia sasa hivi imekuwa kwenye kiganja, teknolojia imekua. Ni jinsi gani Wizara inachukua ukuaji wa teknolojia katika kudhibiti mambo mbalimbali pamoja na kuongeza mapato. Kwa mfano, sasa kupitia simu zetu *(smart phone),* ukiingia *youtube* utaangalia wimbo umekuwa *viewed* labda mara milioni 900. Kwa mfano wimbo wa Diamond Mdogo mdogo ukiingia *youtube* sasa hivi *viewers* wame-*view* kwa milioni 900 karibuni na laki tatu. Je, kama Serikali kwa kupitia hii mitandao, tuna njia gani ya kuongeza mapato katika maeneo hayo? Sasa hivi watu wana-*create application* mbalimbali ambapo unaweza ukaingia uka-*download* na ukapata miziki mbalimbali, je, Serikali kupitia hizi *applications* tunaweza kufanyaje ili tuweze kuongeza mapato? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu ukuzaji wa mapato. Tukiangalia mchanganuo wa makusanyo ya maduhui, Baraza la Michezo la Taifa (BMT) ndio limeingiza shilingi 70,560,000 katika mapato ya kiujumla haya ya shilingi bilioni 36, kwa hiyo ni asilimia ndogo mno. Je, hawa viongozi wa Baraza la Michezo wana mkakati gani kuhakikisha kwamba wanapandisha mapato? Mapato haya ni madogo tatizo ni nini? Tuna *poor internal control* au vyanzo vingi vya mapato havifuatiliwi? Kwa hiyo, tutaomba Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha angalau awe na majibu ya jinsi gani BMT waweze kukuza mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni ukuzaji wa vipaji, hizi *academy.* Tunamshukuru Mheshimiwa Jakaya Kikwete pale Kidongo Chekundu Dar es Salaam aliweza kuweka ile *academy.* Je, kwa ujumla wake tukienda kikanda, tuna mkakati gani angalau kikanda tukawa na ukuzaji wa

vipaji ili vijana wetu katika michezo ya aina mbalimbali mfano riadha, tufe, mikuki, *netball*, *basketball* yote ili tuweze kwenda kimataifa. Leo hii mimi ukanipeleka nikawe mwanamchezo mzuri wa *football* siwezi kuwa lakini mtoto mdogo kuanzia miaka mitano diyo wanatakiwa wajifunze. Sasa hivi ukiangalia mtoto wa Ronaldo anacheza mpira mzuri, yuko kwenye shule na ni *academy,* mzazi wake anamlipia na atakuwa mchezaji mzuri, ataingiza pato lake binafsi na la nchi. Sasa hizi *academy* kama Wizara kwa kushirikiana na vyama mbalimbali vya michezo mje mtuambie mkakati gani ambao mnaolenga kuweza kukuza michezo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la sheria mbalimbali zilizoko katika Wizara. Mara ya mwisho ziliboreshwa lini ili kuendana na uhalisia wa hali halisi ya dunia ilivyo sasa hivi? Kwa hiyo, tutaomba Mheshimiwa Waziri upungufu wowote ulioko kwenye sheria mbalimbali hata hizi za haki miliki ambazo wasanii wengi wanalalamikia zije kwa ajili ya maboresho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikufuatilia kwa ukaribu, tutaomba kujua ile mikakati ya vazi la Taifa na tamaduni mbalimbali lilifikia wapi? Nakumbuka mwaka jana ilizungumziwa lakini imefikia wapi kwamba hili ndilo vazi la Mtanzania ambaye akivaa hivi unajua ametoka Tanzania. Wenzetu Wahindi ukiona tu lile vazi unajua hili la Kihindi, ukimwona Mnaigeria unajua vazi la Kinaigeria na nchi zingine sasa na sisi Tanzania *identity* yetu katika utamaduni ni ipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho lakini siyo dogo, ni jinsi gani tunavyo-*link* Wizara na Halmashauri zetu za Wilaya, Manispaa na Majiji kupitia Idara za Utamaduni. Nashauri wapewe vifaa angalau pikipiki kwa ajili ya kuzunguka katika maeneo mbalimbali ili wafanye kazi zao kiufanisi. Ukiangalia Maafisa Utamaduni ni moja ya idara ambazo katika Halmashauri hazina vifaa kabisa, Wabunge tukienda tunataka kuendesha ligi inabidi umtafutie usafiri ili ndio akazunguke huko vijijini na vijijini tuna vijana wanamichezo wengi kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hukitimisha tu naomba sana michezo upande wa shule za msingi na sekondari tuirudishe ili vijana wetu waweze kukuza vipaji na ni njia ya afya mojawapo, ukiangalia sasa hivi Makamu wa Rais Mama Samia Suluhu ametoa wito kwa watumishi kufanya mazoezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Richard Ndassa.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi niungane na wenzangu katika kuwapongeza Mawaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwangu la kwanza, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri wa Michezo, tunacho kiwanda cha kuzalisha wataalam wa michezo nchini, Chuo cha Michezo Malya. Wataalam hao ni walimu wanaotoka kwenye shule za misingi wanakwenda kujifunza namna ya kufundisha michezo mbalimbali kwenye shule zetu za misingi na sekondari, ndiyo maana nakiita ni kiwanda. Ili upate wachezaji wazuri wa fani zote, huwezi ukaanza na vijana wa sekondari wala vyuo, lazima uanze na shule za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri, chuo hiki malengo yake nafikiri anayafahamu na bahati nzuri juzi alifika akaona miundombinu yake, jinsi tulivyo-*invest* siku zote.

Sasa ni vizuri zaidi pale walipoishia wenzake hebu na yeye akanyage sasa huo moto ile *accelerator* asitoe mguu wake ili ipae zaidi, chuo kile ikiwezekana kiondoke na kutoa *certificate, diploma* kiende kwenye *degree* ya michezo. Tukifanya hivyo Mheshimiwa Waziri chuo kile tutakuwa tumekisaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nimuombe Katibu Mkuu, tuna upungufu kadhaa hasa upande wa maji, kipo kisima kikubwa tulitumia pesa zaidi ya shilingi milioni 230 kwa ajili ya kujenga kisima cha maji kwa ajili ya Malya ambayo mnufaika mmoja wapo ni Chuo cha Michezo Malya, tumepungukiwa mambo madogo madogo. Bahati nzuri kama sikosei Mkuu wa Chuo cha Malya yupo, nafikiri anaweza akamweleza Katibu Mkuu, hili tatizo la upungufu wa maji linaweza likaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niruhusu kwa sababu vinginevyo sitajitendea haki nimpongeze sana Naibu Spika kwa kuweza kuchukua baadhi ya wachezaji wa michezo ya ngoma za asili kwenda kupata mafunzo ya ziada kwenye chuo chetu cha Bagamoyo. Ni chuo kizuri na sisi Waheshimiwa Wabunge nafikiri si vibaya tukaiga utaratibu huo mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Baraza la Michezo la Taifa. Mimi sijui Bwana Malinzi ni Malinzi yupi sasa, Baraza hili ndilo linalosimamia michezo yote. Sijaona wala kusikia Baraza limekwenda limekemea eneo fulani penye mgogoro, lipo lipo tu. Nilisema kipindi kile na leo nasema tena kwa sababu Baraza hili ndiyo mlezi wa vyama hivi vya michezo. Sina uhakika kama Baraza hili linafanya kazi yake ile ambayo tuliitunga humu Bungeni. Mimi nasema kama upo upungufu kwenye utaratibu wetu hebu tuje hapa tubadilishe. Kwa sababu haiwezekani leo hii Baraza kila mnapoenda iwe kwenye vilabu, iwe kwenye riadha, kuna migogoro. Sasa kazi ya Baraza hili ni nini? Naomba Baraza hili hebu lijipange vizuri kwa sababu michezo hii ni mingi kama walivyosema wenzangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Uwanja wetu wa Taifa tubadilike sasa tuache kuutumia kwa ajili ya mechi za Simba na Yanga na hizi mechi la ligi. Uwanja ule tunaweza tukaugeuza ukawa ni uwanja wa kibiashara na ukawa ni uwanja wa kuleta watalii kutoka nje hasa michezo ya kimataifa. Nilisikia juzi juzi hapa Mheshimiwa Waziri sijui timu gani inakuja utasema, tuna uwanja mzuri, tuna mbuga za

wanyama, wachezaji hawa wa kigeni wakija kucheza michezo ya kimataifa Tanzania kwenye uwanja wetu wa Taifa baada au kabla ya michezo ile wanatembelea mbuga zetu za wanyama, tunapata watalii kupitia michezo na kupitia uwanja ule, ni jambo linalowezekana. Naomba Mheshimiwa Waziri akae na Katibu Mkuu wake na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii ili kusudi uwanja ule unufaishe pande zote mbili, kwenye upande wa michezo na kwa upande wa utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije upande wa timu zetu hasa hizi timu kubwa za Simba na Yanga lakini kuna mtu mmoja amechangia hapa anauliza kuhusu waamuzi. Mimi nishauri, tuwe wanasiasa au tuwe watu gani, tukitaka mpira wetu uendelee kwa timu zetu hizi Simba, Yanga na timu zingine sisi wanasiasa hebu tukae pembeni kidogo. Kwa sababu kama sisi wanasiasa tutaingia ndani tukajifanya sisi ndiyo waamuzi namba 12 au 13 kinachofuata ni kuharibu ile *test* ya mpira wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tunavurunda humu ndani kwa kutumia urafiki na wanasiasa tukienda huko nje hatufanikiwi. Watani zangu Yanga ndani humu wanacheza vizuri sana, lakini wakienda huko nje na bendera yetu ya Taifa wanarudi na rundo la magoli. *(Makofi)*

Sasa tujiulize hivi kwa nini humu wanaweza na kwa nini nje hawawezi? Ni kwa sababu ya mambo yetu ya siasa. Tukiacha siasa tukafanya mpira uwe mpira, wakacheza mpira bila kupendelewa na watu fulani fulani *whether* ni viongozi wa kisiasa au *linesman,* nina uhakika hata huku nje watashinda kwa sababu kule nje hamna kubebwa, mbeleko kule nje hakuna, ziko hapa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Baraza la Michezo tukiendelea kwa utaratibu huu wa kuzibeba timu zetu, tukienda nje ni aibu, tutaendelea kuwa wasindikizaji. Nirudie Baraza la Michezo hebu fanyeni kazi yenu. Hivi sisi kweli maandalizi yote hayo kwa timu zetu, tuna wachezaji wazuri lakini tukitoka hapa tukienda nje tunafungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata timu yetu hii ya vijana nina uhakika kama haitaingiliwa na wanasiasa kwenda kuwa-*lobby* wale wachezaji wazuri waliomo mle ndani, maana yake tutaanza wewe ni wa kwangu, wewe ni kwangu tutawapa vichwa watashindwa kufanya kazi yao ya kuchezea mpira uwanjani. Tuwaache wao na makocha wao na wataalam wao ili kusudi wacheze mpira, watuletee sifa Tanzania, kwamba Tanzania sasa sio Tanzania kama ile ya zamani. Tukianza sasa sisi wanasiasa kuingia ndani nina uhakika timu ile itarudia njiani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, wewe najua ni mpenzi mzuri wa mpira hasa wa miguu na ni kiongozi na humu tuko wapenzi wengi wa mpira wa miguu na michezo mingine, niwashauri sana Wabunge wenzangu pamoja na ushabiki wetu, pamoja na Mzee Mkuchika pale na Yanga yake tuache ushabiki usiokuwa na utaratibu kwa manufaa ya timu zetu. Nina uhakika hata timu ya sasa inayokuja kwenye ligi kuu ya *Singida United* mtakuja kuniambia na kukumbuka maneno yangu kwa sababu wanasiasa wanaingia kutafuta umaarufu, pesa zikishawaishia wanakaa pembeni ile timu inabaki peke yake. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kweli kabisa.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Wameshaanza kuingia wanasiasa kujipendekeza. Muda utakapofika wakikaa pembeni ile timu itabaki peke yake. Naomba *Singida United* ibaki kama ilivyoanzishwa kwa mapenzi yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, niwashukuru kwa shughuli ya leo, wachangiaji wetu wamekwisha na muda wetu umekwisha.

Kuna tangazo kutoka kwa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy, anaomba kuwatangazia Waheshimiwa

Wabunge kwa zoezi la kubadilisha vyeti vya homa ya manjano linaendelea kesho Jumamosi na Jumatatu. Kwa wale ambao hawana *passport* wanaweza kupewa vyeti hivyo endapo wana namba za *passport* zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo, nachukua tena nafasi hii kuwashukuru wote na naahirisha Bunge mpaka siku ya Jumatatu, saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.36 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 8 Mei, 2017 Saa Tatu Asubuhi)*